2008 Machi	177.3	172.0	160.0	253.9	135.2	130.2	142.4	125.8	124.5	178.7	185.1	79.3	174.6
Juni	184.2	171.4	173.3	260.0	135.3	133.8	146.7	128.2	129.5	181.5	185.1	86.1	179.1
Septemba	191.6	182.0	180.0	270.7	128.8	140.5	155.8	131.3	131.8	217.1	188.9	91.1	192.6
Desemba	198.3	192.3	186.7	301.4	130.9	149.4	164.2	135.8	135.4	214.2	190.9	91.8	198.0
2009 Machi	219.8	198.3	200.0	275.0	130.0	157.4	169.0	149.3	191.2	212.7	193.0	92.0	206.3
Juni	225.3	199.3	200.0	275.2	134.5	163.9	170.7	155.0	193.1	210.2	193.3	93.0	208.7
Septemba	237.8	237.8	200.0	293.0	139.7	176.4	180.1	172.5	190.8	225.0	193.5	94.9	220.2
Desemba	247.4	207.4	200.0	305.1	147.2	137.0	163.7	185.5	189.4	228.1	195.9	94.7	225.9
FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WATU WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM (Dec. 2015=100)													
Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE
2010 Robo ya kwanza	54.8	68.9	75.2	63.9	82.3	84.4	67.3	94.3	82.5	82.1	65.4	83.0	63.4
Robo ya pili	57.0	72.3	74.7	65.1	82.8	84.4	67.8	94.7	84.8	82.1	65.7	85.2	64.9
Robo ya tatu	56.8	72.4	78.6	68.2	85.5	84.4	68.5	94.9	87.1	82.1	66.3	86.7	65.8
Robo ya nne	57.7	72.6	81.1	67.7	84.6	84.4	69.1	94.9	88.2	82.1	65.9	87.1	66.3
2011 Robo ya kwanza	61.1	73.8	80.7	70.9	86.7	85.2	70.8	94.9	89.3	82.1	67.5	83.9	68.7
Robo ya pili	62.4	74.8	83.8	72.0	89.5	87.7	77.2	94.9	91.2	82.1	72.2	85.6	70.8
Robo ya tatu	64.5	76.7	84.2	74.4	88.9	87.7	80.5	95.2	91.8	82.5	76.4	86.9	72.8
Robo ya nne	68.8	77.3	85.7	76.4	90.3	89.5	82.9	95.4	92.0	82.7	77.2	88.4	75.7
2012 Robo ya kwanza	72.8	78.2	88.7	77.3	92.9	91.5	82.4	95.4	92.8	82.7	78.7	91.3	78.0
Robo ya pili	74.2	78.6	89.2	79.8	94.2	91.9	83.3	95.4	93.0	82.7	79.6	95.4	79.5
Robo ya tatu	74.9	80.5	91.0	81.8	95.0	92.0	83.3	95.5	93.3	82.7	81.5	95.7	80.4
Robo ya nne	77.3	81.4	93.0	83.1	95.7	93.3	85.2	95.6	93.4	82.7	82.9	96.1	82.2
2013 Robo ya kwanza	83.1	81.4	93.8	83.9	96.1	94.8	86.4	95.7	93.9	84.4	84.9	96.4	85.5
Robo ya pili	81.7	82.1	95.2	83.4	96.3	94.8	94.1	95.7	96.1	84.4	85.3	96.8	85.6
Robo ya tatu	82.8	87.7	96.3	84.3	97.1	94.8	95.6	95.7	96.3	84.4	85.8	97.2	86.6
Robo ya nne	84.2	90.4	96.4	86.4	97.7	94.8	96.2	95.7	96.0	84.7	87.4	97.2	87.9
2014 Robo ya kwanza	88.5	90.4	97.5	87.6	97.7	95.5	96.6	95.7	98.8	95.7	87.9	99.0	90.6
Robo ya pili	87.9	90.4	97.6	88.1	98.5	97.7	97.6	95.7	98.9	98.6	88.0	99.8	90.7
Robo ya tatu	88.0	92.9	97.5	92.7	97.8	97.5	98.7	95.7	99.3	98.6	90.4	101.2	91.8
Robo ya nne	89.7	95.6	97.3	95.1	98.2	97.3	99.3	95.6	99.8	98.6	92.5	99.9	93.3
2015* Robo ya kwanza	92.5	96.7	97.8	95.2	98.3	97.5	101.2	97.6	99.7	100.0	95.4	100.2	95.1
Robo ya pili	95.1	98.1	97.8	96.0	98.2	97.5	102.5	97.7	100.0	100.0	97.5	98.6	96.8
Robo ya tatu	97.6	99.0	98.5	97.1	98.7	98.4	102.6	98.5	100.2	100.0	97.5	98.7	98.3
Robo ya nne	100.0	99.6	99.3	101.1	99.6	99.3	99.9	100.0	100.1	100.0	98.4	99.6	100.0
2016 Robo ya kwanza	102.6	100.4	99.8	105.2	100.2	107.3	98.6	100.0	100.4	98.6	100.4	101.4	101.0
Robo ya pili	105.3	100.9	100.7	107.2	103.0	111.9	98.9	100.6	101.3	98.4	103.1	102.0	102.5
Robo ya tatu	106.0	102.3	99.7	104.3	100.1	114.0	99.7	101.2	101.0	98.4	102.9	102.7	102.4
Robo ya nne	104.4	102.8	100.2	106.9	104.4	115.0	99.8	101.3	101.9	98.4	102.4	105.0	102.8
2017 Robo ya kwanza	107.4	102.9	101.3	105.9	107.3	115.2	101.7	101.3	100.1	98.4	102.5	105.3	104.0
Robo ya pili	112.6	103.8	102.0	105.8	107.7	114.7	103.2	101.3	100.6	98.4	103.1	105.4	105.8
Robo ya tatu	116.9	104.1	102.1	107.7	107.3	114.2	104.8	101.3	99.4	98.4	103.4	106.3	107.4
Robo ya nne	119.9	104.1	102.4	110.0	107.2	115.2	106.8	101.5	99.8	98.4	103.0	107.3	108.9

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2004 hadi 2009 zilitumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi haziziwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WATU WENYE KIPATO
CHA JUU DAR-ES-SALAAM (Dec. 2015=100)**

Jedwali Na. 13

Mwaka	M I E Z I				Wastani	Badiliko Asilimia
	Machi	Juni	Sept.	Desemba		
2000	24.18	24.18	25.27	25.83	24.87	6.2
2001	30.87	28.15	27.03	25.83	27.97	12.5
2002	28.96	28.88	28.93	28.89	28.91	6.6
2003	29.92	30.22	30.19	30.24	30.14	4.2
2004	30.98	31.77	32.30	33.02	32.02	6.2
2005	33.62	33.88	34.76	36.80	34.77	8.6
2006	37.88	38.51	38.90	40.13	38.86	11.8
2007	42.19	43.45	44.68	45.76	44.02	13.3
2008	48.86	50.13	53.91	55.41	52.08	18.3
2009	57.72	58.40	61.62	63.21	60.24	15.7
2010	63.41	64.89	65.82	66.29	65.10	8.1
2011	68.73	70.77	72.83	75.67	72.00	10.6
2012	78.04	79.50	80.40	82.20	80.04	11.2
2013	85.48	85.58	86.64	87.93	86.41	8.0
2014	90.61	90.68	91.84	93.27	91.60	6.0
2015*	95.14	96.78	98.27	100.00	97.55	6.5
2016	101.02	102.52	102.43	102.81	102.20	4.8
2017	104.01	105.76	107.37	108.93	106.52	4.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (2001=100)

Jedwali Na.14

Mwaka	Chakula	Vinywaji na Sigara	Kodi ya Nyumba	Umeme, Mafuta ya Taa, Maji	Nguo na Viatu	Fenicha, Vyombo Vya Nyumbani	Huduma Mahitaji ya Nyumbani	Huduma za Afya	Michezo na Starehe	Usafiri	Elimu	Vinginevyo	Fahirisi Bidhaa Zote	
2008	Robo ya kwanza	163.4	146.8	138.9	161.6	105.3	116.6	115.1	113.6	110.0	132.9	106.2	103.4	149.2
	Robo ya pili	165.1	148.5	139.5	172.0	106.4	118.1	117.1	114.7	111.4	136.5	107.8	103.9	151.7
	Robo ya tatu	164.5	149.7	141.6	179.2	106.4	120.1	116.8	117.4	114.5	141.0	110.8	104.2	152.8
	Robo ya nne	175.0	152.1	141.6	172.5	108.6	122.1	119.1	120.3	117.6	139.6	112.7	105.2	158.4
2009	Robo ya kwanza	193.5	154.8	156.4	164.5	109.7	124.8	120.7	122.3	121.4	137.7	116.9	106.9	168.7
	Robo ya pili	194.0	158.2	156.5	158.7	112.5	126.1	122.7	125.9	121.4	135.3	122.4	108.6	168.9
	Robo ya tatu	193.6	165.7	159.4	168.9	115.7	128.0	123.0	126.1	124.6	140.3	122.4	108.3	170.6
	Robo ya nne	203.8	170.9	159.6	181.7	115.6	127.1	126.0	126.1	127.6	140.3	122.7	106.3	178.2

FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI - TANZANIA BARA (Dec. 2015=100)

Mwaka	Vyakula na vinywaji baridi	Vinywaji vyenye kilevi na bidhaa za tumbaku	Mavazi ya nguo na viatu	Nishati, Maji na Makazi	Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa nyumba	Gharama za Afya	Usafirishaji	Mawasiliano	Utamaduni na Burudani	Elimu	Hoteli na Migahawa	Bidhaa na huduma nyinginezo	FAHIRISI BIDHAA ZOTE	
2010	Robo ya kwanza	54.4	66.1	68.2	54.3	72.0	84.6	79.4	101.3	81.7	83.4	69.5	72.4	61.3
	Robo ya pili	55.2	64.8	68.4	57.2	72.9	84.8	79.2	102.0	82.7	83.4	69.5	72.9	62.1
	Robo ya tatu	54.2	66.2	70.2	58.1	74.1	84.9	78.9	102.2	84.2	81.9	69.8	74.6	61.9
	Robo ya nne	54.9	66.6	71.7	58.1	74.8	84.6	78.9	102.3	83.9	81.3	68.9	74.5	62.4
2011	Robo ya kwanza	59.0	67.7	73.6	61.9	80.5	85.7	80.4	100.2	84.7	85.6	72.4	74.6	65.8
	Robo ya pili	61.2	68.7	75.0	66.2	83.1	86.2	84.5	99.9	85.2	85.9	73.9	75.4	68.2
	Robo ya tatu	64.4	69.7	76.9	70.3	84.6	86.5	86.6	100.7	86.1	85.9	75.9	77.9	71.0
	Robo ya nne	69.0	70.3	79.5	71.8	86.1	87.6	88.1	100.7	86.3	85.9	78.0	80.3	74.2
2012	Robo ya kwanza	74.7	73.1	83.8	73.4	88.9	88.2	88.8	99.6	90.9	89.2	83.7	82.9	78.6
	Robo ya pili	76.3	75.5	86.5	76.3	90.7	89.0	90.4	99.1	93.7	90.0	87.3	85.2	80.5
	Robo ya tatu	76.3	83.3	87.8	80.4	91.8	89.4	90.5	99.1	96.0	90.0	88.5	85.9	81.4
	Robo ya nne	78.5	85.4	89.0	84.1	93.1	90.1	90.5	98.9	95.7	90.0	90.5	87.1	83.4
2013	Robo ya kwanza	83.4	87.6	90.5	86.1	94.4	91.0	90.7	98.7	95.6	91.7	91.8	88.6	86.7
	Robo ya pili	82.9	88.3	91.2	90.1	94.6	91.7	96.1	98.5	96.0	91.9	92.2	89.4	87.3
	Robo ya tatu	81.6	92.4	92.3	90.7	95.0	91.9	97.8	99.0	96.4	92.1	92.3	90.9	86.9
	Robo ya nne	83.7	93.5	92.8	92.0	95.6	92.0	98.4	99.1	96.4	92.1	92.9	91.7	88.4
2014	Robo ya kwanza	88.9	93.8	93.8	96.8	96.1	92.8	98.8	99.2	96.6	96.8	93.3	92.6	91.9
	Robo ya pili	89.7	93.8	94.1	98.7	96.8	95.2	99.4	99.5	96.7	96.8	94.5	96.6	92.9
	Robo ya tatu	88.6	96.8	94.5	100.5	96.9	95.8	100.0	99.9	96.9	96.8	95.2	96.6	92.7
	Robo ya nne	89.2	98.6	95.5	101.1	96.9	96.2	99.6	99.7	97.0	96.8	96.1	96.7	93.3
2015*	Robo ya kwanza	93.5	98.8	97.0	101.6	97.4	96.6	97.5	99.8	97.1	98.6	97.6	97.4	95.7
	Robo ya pili	97.3	98.8	97.8	99.8	97.4	97.1	97.6	99.8	97.5	100.0	98.9	97.8	97.8
	Robo ya tatu	97.5	99.4	99.1	101.1	98.7	98.4	100.3	99.7	98.9	100.0	99.8	98.5	98.5
	Robo ya nne	98.9	99.8	99.7	100.9	99.3	99.5	99.8	100.0	100.1	100.0	100.0	99.8	99.4
2016	Robo ya kwanza	102.1	100.4	101.0	103.8	100.5	101.6	99.1	99.5	100.4	101.8	100.5	100.8	101.4
	Robo ya pili	104.2	103.2	101.9	107.3	101.5	103.2	98.9	98.8	100.9	102.3	103.6	101.4	103.0
	Robo ya tatu	103.9	104.4	102.8	107.8	101.9	104.0	99.8	99.1	101.2	102.6	104.4	101.9	103.3
	Robo ya nne	105.1	104.9	103.3	110.1	103.1	104.6	100.0	99.1	101.7	102.6	104.1	102.6	104.2
2017	Robo ya kwanza	111.4	105.5	104.4	112.5	104.2	105.3	100.0	98.7	101.5	102.9	104.3	103.4	107.1
	Robo ya pili	115.7	106.5	105.8	113.6	104.7	105.8	100.1	98.1	102.0	103.1	104.4	105.5	109.1
	Robo ya tatu	113.2	107.0	106.4	116.7	104.8	106.2	99.5	98.1	102.7	103.4	104.4	105.7	108.6
	Robo ya nne	112.9	107.5	106.5	118.8	105.1	106.7	100.1	98.1	103.2	103.5	104.5	105.4	108.9

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

Fahirisi za Bei kuanzia mwaka 2005 hadi 2009 ziliumia mgawanyo wa makundi kwa tafsiri ya Kitaifa (National Classification) hivyo fahirisi hizi hazizwezi kuungwa na fahirisi zilizonzia mwaka 2010 zilizotumia mgawanyo wa makundi kwa mfumo wa kimataifa wa COICOP

**FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA (Dec 2015=100)**


Jedwali Na.15

Mwaka	R o b o y a M w a k a				Wastani wa Fahirisi	Badiliko Asilimia
	Robo ya Kwanza	Robo ya Pili	Robo ya Tatu	Robo ya Nne		
2000	33.2	33.0	31.8	32.3	32.6	6.0
2001	35.0	34.7	33.4	33.8	34.2	5.1
2002	35.4	35.6	35.5	36.3	35.7	4.3
2003	37.1	37.6	37.4	38.3	37.6	5.3
2004	39.0	39.0	39.1	40.4	39.4	4.7
2005	40.6	41.2	41.3	42.4	41.4	5.0
2006	43.8	44.9	43.7	45.1	44.4	7.3
2007	46.9	47.5	47.4	48.2	47.5	7.0
2008	51.1	51.9	52.3	54.2	52.4	10.3
2009	57.7	57.8	58.4	61.0	58.7	12.1
2010	61.3	62.1	61.9	62.4	61.9	5.5
2011	65.8	68.2	71.0	74.2	69.8	12.7
2012	78.6	80.5	81.4	83.4	81.0	16.0
2013	86.7	87.3	86.9	88.4	87.3	7.9
2014	91.9	92.9	92.7	93.3	92.7	6.1
2015*	95.7	97.8	98.5	99.4	97.9	5.6
2016	101.4	103.0	103.3	104.2	102.9	5.2
2017	107.1	109.1	108.6	108.9	108.4	5.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

MWENENDO WA KASI YA UPANDAJI BEI - Tanzania Bara



**FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO
NA WAKAZI WA MIJINI-TANZANIA BARA (Dec.2015=100)**

Jedwali Na.16

Mwaka	F A H I R I S I			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA	B A D I L I K O %			WAKAZI MIJINI TANZ. BARA
	K I P A T O C H A				K I P A T O C H A			
	CHINI	KATI	JUU		CHINI	KATI	JUU	
2000	23.8	27.9	24.9	32.6	1.7	2.5	6.2	6.0
2001	25.9	29.1	28.0	34.2	8.5	4.5	12.5	5.1
2002	26.9	30.2	28.9	35.7	3.8	3.5	3.3	4.3
2003	28.4	30.8	30.1	37.6	5.8	2.3	4.3	5.3
2004	30.2	33.4	32.0	39.4	6.4	8.2	6.2	4.7
2005	32.7	36.0	34.8	41.4	8.3	7.9	8.6	5.0
2006	36.5	39.3	38.9	44.4	11.5	9.2	11.8	7.3
2007	39.9	43.9	44.0	47.5	9.3	11.5	13.3	7.0
2008	46.8	50.6	52.1	52.4	17.3	15.3	18.3	10.3
2009	54.7	58.9	60.2	58.7	16.8	16.4	15.7	12.1
2010*	61.9	64.8	65.1	61.9	13.2	10.0	8.1	5.5
2011	66.5	69.9	72.0	69.8	7.4	7.9	10.6	12.7
2012	79.0	81.5	80.0	81.0	18.8	16.6	11.2	16.0
2013	86.3	88.3	86.4	87.3	9.3	8.3	8.0	7.9
2014	93.0	93.7	91.6	92.7	7.7	6.2	6.0	6.1
2015*	98.0	99.0	97.5	97.9	5.4	5.6	6.5	5.6
2016	102.2	103.5	102.2	102.9	4.3	4.5	4.8	5.2
2017	104.1	106.2	106.5	108.4	1.9	2.6	4.2	5.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

*Kizio cha Fahirisi kilibadilishwa na kuanza kutumika Dec. 2015=100

SURA YA 2

FEDHA NA TAASISI ZA FEDHA

Ujazi wa Fedha

32. Mwaka 2017, Benki Kuu ya Tanzania ilitekeleza sera ya fedha ya kuongeza ukwasi ili kusaidia kuboresha utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kusaidia ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika kipindi hicho, hatua mbalimbali za kuongeza ukwasi zilichukuliwa zikiwemo kupunguza kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu na benki za biashara, kushusha kiwango cha riba, kununua fedha za kigeni kutoka kwenye soka la jumla la fedha za kigeni na kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara. Hatua hizi zilisaidia kuongezeka kwa ukuaji wa ujazi wa fedha pamoja na kupungua kwa riba katika masoko ya fedha.

33. Hadi kufikia Desemba 2017, ujazi wa fedha kwa tafsiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 10.6 na kufika shilingi bilioni 11,155.5 kutoka shilingi bilioni 10,083.8. Vile vile, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) uliongezeka kutoka shilingi bilioni 16,620.3 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 18,346.9 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 10.4. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka na kufikia shilingi bilioni 24,711.3 mwaka 2017 kutoka shilingi bilioni 22,877.9 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.0, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 3.4 mwaka 2016. Ukuaji wa M2 na M3 ni chini ya lengo lililowekwa na Benki la asilimia 12.0 na 10.7 kwa mtiririko huo. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na kasi ya ukuaji wa rasilimali katika fedha za kigeni iliyozidi kasi ya kupungua kwa mikopo kwa Serikali kuu na sekta binafsi. Mwaka 2017, rasilimali halisi katika fedha za kigeni ziliongezeka kwa asilimia 41.7 ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 0.7 mwaka 2016. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa ukuaji wa rasilimali za Benki Kuu kutokana na upatikanaji wa mikopo ya kibiashara kutoka nje ya nchi na kuongeza manunuzi ya fedha za kigeni katika soko la ndani.

Mwenendo wa Mikopo kwa Serikali Kuu na Sekta Binafsi

34. Mwaka 2017, mikopo kwa Serikali kuu kutoka katika sekta ya benki ilipungua kwa asilimia 23.5 ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 12.3 mwaka 2016. Kupungua kwa mikopo kwa Serikali kuu kulitokana na

kuongezeka kwa mapato ya Serikali na kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya Serikali. Aidha, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 16,883.1 kutoka shilingi bilioni 16,608.9 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.7, ambalo ni la chini likilinganishwa na ongezeko la asilimia 7.2 kwa mwaka 2016. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kulichangiwa na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara katika kutoa mikopo kufuatia ongezeko la mikopo chechefu; na benki za biashara kupendelea zaidi kuwekeza katika dhamana za Serikali. Aidha, ukuaji wa mikopo kwenye shughuli za majengo na ujenzi, uzalishaji katika kilimo na shughuli za hoteli na migahawa uliimarika ikilinganishwa na mwaka 2016. Sehemu kubwa ya mikopo hiyo ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 19.6 ya mikopo yote ikifuatiwa na shughuli za watu binafsi zilizopata asilimia 19.3. Hata hivyo, ukuaji wa mikopo kwenye shughuli nyingine ulipungua zikiwemo shughuli za uchukuzi na mawasiliano, na biashara.

Amana Katika Benki za Biashara

35. Mwaka 2017, amana katika benki za biashara ziliongezeka hadi shilingi bilioni 20,381.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 18,766.5 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Ongezeko hili, lilitokana na jitihada za benki na Serikali kuhimiza wananchi kutumia huduma za benki katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi; na kuendelea kuongezeka kwa matawi ya benki nchini ikiwa ni pamoja na matumizi ya wakala wa benki (agent banking). Katika kipindi hicho, sekta binafsi ilikuwa na jumla ya shilingi bilioni 19,821.3 sawa na asilimia 97.2 kati ya amana zote. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni ukilinganishwa na amana zote ulipungua na kufikia asilimia 29.9 mwaka 2017 kutoka asilimia 31.1 mwaka 2016.

Mwenendo wa Viwango vya Riba

36. Mwaka 2017, mwenendo wa viwango vya riba uliongezeka, ambapo riba za mikopo zilifikia wastani wa asilimia 18.42 kutoka asilimia 15.66 mwaka 2016. Wakati huo huo, riba za mikopo ya mwaka mmoja ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 18.24 kutoka asilimia 12.87 mwaka 2016. Aidha, riba za amana za muda maalum ziliongezeka kufikia wastani wa asilimia 9.62 mwaka 2017 kutoka asilimia 8.78 mwishoni mwa mwaka 2016. Katika kipindi hicho, riba za amana za mwaka mmoja zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 10.86 kutoka asilimia 11.03 mwaka 2016. Kutokana na mwenendo huu, tofauti kati ya riba za amana na za mikopo za mwaka mmoja iliongezeka kufikia wastani wa

asilimia 7.38 mwishoni mwa mwaka 2017 kutoka asilimia 1.83 mwishoni mwa mwaka 2016. Kwa upande mwingine, riba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 3.26 mwishoni mwa mwaka 2017 kutoka asilimia 13.49 mwaka 2016. Vile vile, riba za dhamana za Serikali zilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.19 kutoka asilimia 15.12 mwaka 2016. Aidha, riba za mikopo inayotolewa na benki za biashara imebakia kuwa juu kutokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja wanaoshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati (risk premium).

MAENDELEO KATIKA SEKTA YA FEDHA

Huduma za Benki

37. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2017, Benki Kuu ya Tanzania ilifuta leseni za benki mbili (FBME Bank Limited na Mbinga Community Bank Limited) na kutoa leseni kwa benki moja (Yetu Microfinance bank Plc) na taasisi nyingine moja (First Housing Finance (T) Limited), hivyo kufanya idadi ya taasisi zinazosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania kubakia 67 (benki 58 na taasisi nyingine 9).

38. Katika kurahisisha upatikanaji wa huduma, benki ziliendelea kuongeza idadi ya matawi kutoka matawi 795 Desemba 2016 hadi kufikia matawi 821 Desemba 2017. Vile vile, hali ya ukwasi katika sekta ya benki iliimarika ikilinganishwa na mwaka 2016 na iliendelea kuwa juu ya ukomo unaokubalika kisheria. Uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslimu na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi (Liquid Assets to Demand Liabilities) iliongezeka na kufikia asilimia 40.3 Desemba 2017 kutoka asilimia 35.1 Desemba 2016, ikilinganishwa na uwiano wa chini wa asilimia 20 unaohitajika kisheria. Aidha, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki uliongezeka na kufikia asilimia 18.9 kutoka asilimia 17.8 ikilinganishwa na uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 10.

39. Mwaka 2017, utekelezaji wa Mpango wa Huduma za Fedha Jumuishi nchini uliendelea kuwa na mafanikio makubwa ambapo huduma hizo ziliendelea kupatikana kwa wingi mijini na vijijini, zikichangiwa kwa sehemu kubwa na matumizi ya simu za mikononi pamoja na Wakala wa Benki. Hadi kufikia Desemba 2017, benki 18 zilitoa huduma kwa njia ya uwakala kama ilivyokuwa mwaka ulioishia Desemba 2016. Aidha, idadi ya mawakala iliongezeka kwa

asilimia 87.9 kufikia mawakala 10,665 mwishoni mwa Desemba 2017 kutoka mawakala 5,676 mwishoni mwa Desemba 2016.

40. Miamala ya kuweka amana kupitia huduma za benki kwa njia ya uwakala ilikuwa 9,911,695 yenye thamani ya shilingi bilioni 4,638.6 mwishoni mwa Desemba 2017 ikilinganishwa na miamala 4,869,842 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,883.3 Desemba 2016, sawa na ongezeko la miamala la asilimia 103.5. Vile vile, idadi ya miamala ya kutoa fedha ilifikia 4,075,195 mwishoni mwa Desemba 2017 ikilinganishwa na miamala 1,657,092 Desemba 2016. Kutokana na miamala hiyo, fedha taslimu zilizotolewa kwa kipindi kilichoishia Desemba 2017 zilikuwa jumla ya shilingi bilioni 1,106.4 ikilinganishwa na shilingi bilioni 427.1 mwaka 2016.

Maendeleo ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

41. Mwaka 2017, idadi ya kampuni zilizo rodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam iliongezeka na kufikia kampuni 26 ikilinganishwa na kampuni 25 zilizo rodheshwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2016. Kampuni iliyoongezeka sokoni mwaka 2017 ni Vodacom Tanzania Plc ambayo ni moja kati ya kampuni za mawasiliano zinazotakiwa ku rodheshwa asilimia 25 ya hisa zake katika soko la Hisa la Dar es Salaam ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya marekebisho ya Sheria ya Kielektroniki na Mawasiliano ya Posta (EPOCA), ya mwaka 2017. Kati ya Kampuni hizo, kampuni za ndani zilikuwa 18 na kampuni za nje (kutoka masoko ya hisa ya Nairobi na Londoni) zilikuwa saba. Aidha, hadi kufikia Desemba 2017, idadi ya wawekezaji katika soko la hisa la Dar es Salaam iliongezeka na kufikia wawekezaji 524,277 ikilinganishwa na wawekezaji 472,514 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 11.0. Hii ilitokana na kuongezeka kwa fursa za kununua hisa kwenye soko kulikotokana na urodheshwaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc.

42. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2017, jumla ya hisa 328,552,495 zenye thamani ya shilingi bilioni 418.96 ziliuzwa na kununuliwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ikilinganishwa na hisa 189,962,928 zenye thamani ya shilingi bilioni 415.56 zilizouzwa na kununuliwa katika kipindi kilichoishia Desemba 2016, sawa na ongezeko la asilimia 73.0. Aidha, hatifungani za Serikali zenye thamani ya shilingi bilioni 683.17 zilinunuliwa na kuuzwa katika soko la pili, ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi bilioni 429.92 zilizouzwa na kununuliwa kwa kipindi kilichoishia Desemba 2016, sawa

na ongezeko la asilimia 58.9. Vile vile, katika kipindi hicho, Soko liliorodhesha hatifungani zenye thamani ya shilingi trilioni 7.71 ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya shilingi trilioni 5.34 zilizoorodheshwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 44.4. Kwa upande wa hatifungani za kampuni, katika kipindi kilichoishia Desemba 2017, hatifungani za kampuni zenye thamani ya shilingi bilioni 98.97 zilikuwa zimeorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam.

43. Mwaka 2017, thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja iliongezeka na kufikia shilingi milioni 256,480.40 ikilinganishwa na shilingi milioni 251,023.36 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 2.2. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya mifuko ya Ukwasi (asilimia 85.3), Watoto (asilimia 7.0) na Umoja (asilimia 2.0). Hata hivyo, thamani ya mfuko wa uwekezaji wa Jikimu ilipungua na kufikia shilingi milioni 21,687.04 mwaka 2017 ikilinganishwa na shilingi milioni 25,451.02 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 14.8. Kupungua kwa thamani kwa mfuko huu kulitokana na kutokufanya vizuri kwa uwekezaji wake kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ambapo mfuko uliwekeza asilimia 20.4 ya fedha zake. Aidha, thamani ya mfuko wa Wekeza Maisha ilipungua na kufikia shilingi milioni 1,488.96 mwaka 2017 ikilinganishwa na shilingi milioni 3,671.93 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 59.5. Upungufu huo ulitokana na mfuko huo kufikia ukomo wake wa miaka kumi na hivyo, kupelekea kuvunjwa kama taratibu za mfuko zinavyoelekeza.

Jedwali Na.2.1: Thamani ya Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja (Shs. Milioni)

Aina ya Uwekezaji	2016	2017	Ukuaji (%)
Umoja	210,443.15	214,658.83	2.0
Jikimu	25,451.02	21,687.04	-14.8
Wekeza	3,671.93	1,488.96	-59.5
Watoto	3,301.31	3,532.13	7.0
Ukwasi	8,155.95	15,113.44	85.3
Jumla	251,023.36	256,480.40	2.2

Chanzo: Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana

Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA)

44. Mwaka 2016/17, idadi ya wanachama wanaochangia katika mifuko ya pensheni ilifikia 2,409,303 ikilinganishwa na wanachama 2,234,246 waliokuwa wanachangia kufikia Juni 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.8. Mapato yatokanayo na michango ya wanachama yaliongezeka kwa asilimia 2.3 kutoka shilingi trilioni 2.61 mwaka ulioishia Juni 2016 hadi shilingi trilioni 2.67 mwaka ulioishia Juni 2017.

45. Mwaka 2016/2017, mali za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iliongezeka kwa asilimia 29.8 kutoka shilingi trilioni 9.42 mwaka 2015/16 hadi shilingi trilioni 12.23 mwaka ulioishia Juni 2017. Ongezeko hili lilitokana na kupanda kwa thamani ya uwekezaji na mapato yatokanayo na michango ya wanachama. Kwa upande mwingine, thamani ya uwekezaji wa Mifuko ya Pensheni iliongezeka kwa asilimia 21.0 kutoka shilingi trilioni 9.28 mwaka 2015/2016 hadi shilingi trilioni 11.23 mwaka 2016/2017. Aidha, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalipungua kwa asilimia 14.7 kutoka shilingi trilioni 1.96 mwaka 2015/16 hadi shilingi trilioni 1.67 mwaka 2016/17, hii ni kufuatia kuongezeka kwa udhibiti wa wanachama wanaojiotoa.

Jedwali Na. 2.2 : Taarifa ya Hali ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Mwaka	Idadi ya Wanachama	Michango (Shs.bilioni)	Mafao (Shs.bilioni)	Uwekezaji (Shs.bilioni)
2007/08	1,198,298	508.0	272.0	1,779.8
2008/09	1,275,993	754.0	308.0	2,476.9
2009/10	1,436,779	848.0	499.0	3,130.8
2010/11	1,599,208	1,178.0	565.0	3,757.4
2011/12	1,676,715	1,383.0	733.0	4,831.6
2012/13	1,856,245	1,635.0	1,068.0	5,866.5
2013/14	1,568,757	1,590.0	1,250.0	5,308.0
2014/15	1,887,000	2,314.0	1,546.0	7,619.6
2015/16	2,234,246	2,612.0	1,955.0	9,288.8
2016/17	2,409,303	2,669.0	1,668.0	11,235.0

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)

46. Mwaka 2016/17, wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii waliongezeka kwa asilimia 8.3 kufikia jumla ya wanachama 1,087,229 kutoka wanachama 1,003,563 mwaka 2015/16. Katika kipindi hicho, michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama wa Mfuko ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 736,405.01 ikilinganishwa na shilingi milioni 677,166.29 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Kuongezeka kwa idadi ya wanachama na makusanyo ya michango kulitokana na usajili wa wanachama wapya 107,764 na waajiri wapya 2,788 katika kipindi husika.

47. Mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalikuwa na thamani shilingi milioni 248,118.5 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi milioni 378,282.58 zilizolipwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 34.4. Aidha, wanachama waliolipwa mafao hayo walipungua kwa asilimia 52.0 na kufikia wanachama 45,143 ikilinganishwa na wanachama 94,103 waliolipwa mwaka 2015/16. Upungufu huu ulitokana na zuio lililowekwa na Mfuko kwa wanachama wanaotaka kujitoka uanachama bila kufuata sheria. Vile vile, Mfuko uliendesha jumla ya semina 4,180 nchini zenye lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa hifadhi ya jamii, ikilinganishwa na semina 4,412 zilizoendeshwa mwaka 2015/16.

48. Thamani ya uwekezaji katika vitega-uchumi iliongezeka kutoka shilingi milioni 2,328,732.22 mwaka 2015/16 hadi shilingi milioni 2,333,981.87 mwaka 2016/17. Kwa upande mwingine, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka na kufikia shilingi milioni 311,213.93 mwaka 2016/17, kutoka shilingi milioni 254,932.88 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 22.08. Aidha, mapato kutokana na uwekezaji katika vitega-uchumi yalipungua hadi shilingi milioni 205,077.38 mwaka 2016/17 kutoka shilingi milioni 262,693.78 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 21.9.

49. Mwaka 2016/17, thamani ya Mfuko iliongezeka na kufikia shilingi milioni 3,408,584.55 kutoka shilingi milioni 3,110,905.59 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 9.57. Aidha, rasilimali halisi za Mfuko zilikuwa na thamani ya shilingi milioni 3,119,622.60 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi milioni 2,943,369.11 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 6.0. Hii ilisababisha ongezeko halisi la rasilimali baada ya kodi kwa mwaka 2016/17

kuwa shilingi milioni 176,253.49 ikilinganishwa na shilingi milioni 167,249.48 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 5.4.

Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF)

50. Mwaka 2016/17, idadi ya wanachama katika Mfuko wa Pensheni wa GEPF iliongezeka kutoka wanachama 114,462 mwaka 2015/16 hadi wanachama 130,112, sawa na ongezeko la asilimia 13.7. Kwa upande mwingine, idadi ya wanachama waliosajiliwa kupitia mpango wa hiari unaolenga watu waliojijiri wenyewe katika sekta rasmi na isiyo rasmi ilikuwa 12,240 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na wanachama 14,429 waliosajiliwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 15.2. Michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama ilikuwa na thamani ya shilingi milioni 75,063.96 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi milioni 69,430.13 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Aidha, michango iliyokusanywa chini ya mpango wa hiari ilikuwa shilingi milioni 3,854.84 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi milioni 4,647.88 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 17.1.

51. Mwaka 2016/17, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yalikuwa na thamani ya shilingi milioni 20,066.68 ikilinganishwa na shilingi milioni 18,858.02 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 6.4. Hii ilitokana na kuongezeka kwa wanachama waliojitoa kwenye mpango wa hiari pamoja na kuongezeka kwa idadi ya wastaafu. Mwaka 2016/17, uwekezaji uliofanywa na Mfuko kwenye vitega uchumi mbalimbali uliongezeka kwa asilimia 24.7 kutoka shilingi milioni 403,315.82 mwaka 2015/16 hadi shilingi milioni 502,944.55. **Jedwali Na. 2.3** linaonesha mchanganuo wa uwekezaji uliofanywa na Mfuko.

Jedwali Na 2.3: Thamani ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi (Shs. Milioni)

Uwekezaji	2015/16	2016/17	Ukuaji (%)
Mali zenye faida inayojulikana kabla ya uwekezaji	333,555.96	414,967.23	24.4
Hisa za Makampuni	34,909.60	49,634.48	42.2
Majengo	28,269.04	30,033.97	6.2
Mfuko wa Pamoja	6,581	8,308.87	26.3
Jumla	403,315.60	502,944.55	24.7

Chanzo: Mfuko wa Mafao ya Kustaafu (GEPF)

52. Mapato yaliyotokana na uwekezaji wa rasilimali za Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 46.3 mwaka 2016/17 hadi shilingi milioni 53,312.03 kutoka shilingi milioni 36,435.16 mwaka 2015/16. Hii ilitokana na kuongezeka kwa riba iliyopatikana katika amana za Serikali, benki na vitega uchumi vingine. Aidha, hadi kufikia 2016/17, thamani ya Mfuko ilikuwa shilingi milioni 525,651.43 kutoka shilingi milioni 427,795.25 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 22.9.

Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (LAPF)

53. Mwaka 2016/17, idadi ya wanachama wa Mfuko wa Pensheni wa LAPF iliongezeka hadi kufikia 177,065 kutoka wanachama 166,260 mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Aidha, makusanyo ya michango kutoka kwa wanachama yaliongezeka kwa asilimia 4.2 hadi shilingi bilioni 291.29 mwaka 2016/17, ikilinganishwa na shilingi bilioni 279.68 mwaka 2015/16. Ongezeko la wanachama na makusanyo lilitokana na usajili wa wanachama wapya. Vile vile, mafao yaliyolipwa kwa wanachama yaliongezeka hadi shilingi bilioni 140.49 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi bilioni 107.25 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 30.9.

54. Mwaka 2016/17, uwekezaji uliofanywa na Mfuko katika vitega uchumi ulikuwa na thamani ya shilingi bilioni 1,397.35 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,098.37 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 27.2. Kwa upande mwingine, thamani ya uwekezaji katika dhamana za Serikali iliongezeka hadi shilingi bilioni 755.12 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 59.03 ikilinganishwa na shilingi bilioni 474.83 mwaka 2015/16. Aidha, mapato kutokana na uwekezaji uliofanywa na Mfuko kwenye vitega uchumi mbalimbali yalifikia shilingi bilioni 133.42 mwaka 2016/17 kutoka shilingi bilioni 93.88 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 42.1. Hii ilichangiwa na ongezeko la shughuli za uwekezaji katika dhamana za Serikali, kodi za majengo pamoja na mikopo ya muda mrefu. Vile vile, thamani halisi ya mali za Mfuko iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,397.35 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,169.06 mwaka 2015/16, ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.5.

Mfuko wa Pensheni wa PSPF

55. Mwaka 2017, idadi ya wanachama waliosajiliwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma walikuwa 22,884 ikiwa inajumuisha wanachama 4,350 katika Mfuko wa kisheria na wanachama 18,534 katika mpango wa hiari

ikilinganishwa na wanachama 47,238 waliosajiliwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 51.6. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa ushindani kutoka kwenye mifuko mingine pamoja na kupungua kwa ajira Serikalini. Usajili uliofanyika mwaka 2017, unafanya jumla ya idadi ya wanachama wa Mfuko hadi kufikia Desemba 2017 kuwa wanachama 427,856 kutoka wanachama 404,972 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 5.7.

56. Michango iliyokusanywa kutoka kwa wanachama iliongezeka kwa asilimia 2.5 kutoka shilingi bilioni 784.8 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 804.20 mwaka 2017. Ongezeko hilo lilichangiwa na ongezeko la wanachama na mabadiliko yaliyofanywa na Serikali kwenye mishahara ya watumishi. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2017, Mfuko ulilipa mafao yenye thamani ya shilingi bilioni 845.63 kwa wanachama 7,528, sawa na ongezeko la asilimia 7.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 786.36 zilizolipwa kwa wanachama 7,416 mwaka 2016. Mafao yaliyolipwa mwaka 2017 yalijumuisha: malipo ya kustaafu kwa umri shilingi bilioni 505.46; mafao ya kifo/mirathi shilingi bilioni 95.10; msaada wa mazishi shilingi bilioni 2.53; mafao ya kujitoa shilingi bilioni 10.57; pensheni kwa wastaafu shilingi bilioni 173.98; na pensheni ya wategemezi shilingi bilioni 57.99.

Jedwali Na.2.4: Malipo ya Mafao kwa Wanachama wa Mfuko (Shs. Bilioni)

Aina ya Mafao	2015	2016	2017	Ongezeko (%)
Malipo ya Kustaafu kwa Umri (Kiinua Mgongo)	354.6	497.0	505.46	1.7
Mafao ya Kifo/Mirathi	57.92	70.33	95.10	35.2
Msaada wa Mazishi	0.42	0.52	2.53	386.5
Mafao ya Kujitoa	1.61	2.62	10.57	303.4
Pensheni kwa Wastaafu	119.25	161.6	173.98	7.7
Pensheni ya Wategemezi	29.99	54.29	57.99	6.8
Jumla	563.79	786.36	845.63	7.5

Chanzo: Mfuko wa Pensheni wa PSPF

57. Mwaka 2017, Mfuko ulipata kiasi cha shilingi billioni 27.97 kutokana na uwekezaji ikilinganishwa na shilingi bilioni 75.59 mwaka 2016. Kushuka kwa mapato kulitokana na kupungua kwa fedha kwa ajili ya uwekezaji kulikosababishwa na ongezeko la malipo ya mafao kulinganisha na mapato ya Mfuko. Mapato mengineyo yaliongezeka hadi shilingi bilioni 4.09 kutoka

shilingi bilioni 2.4 kwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 70.4. Ongezeko hili lilitokana na mapato kutoka kwenye akaunti maalumu ya riba “*call account*”. Aidha, jumla ya mapato yote yaliyotokana na vitega uchumi mbalimbali yalifikia shilingi bilioni 32.06.

58. Thamani ya rasilimali na uwekezaji wa Mfuko ilipungua kwa asilimia 33.2 kutoka shilingi trilioni 1.38 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 921.33 mwaka 2017. Upungufu huo ulichangiwa na kutokuwepo kwa uwiano kati ya mafao yaliyolipwa na michango iliypokelewa kutokana na kuendelea kulipa wastaafu wa kabla ya Julai 1999 ambao hawakuchangia katika Mfuko. Aidha, mwaka 2017 Mfuko uliendelea kuimarisha huduma za mikopo mbalimbali ya muda mfupi ili kuwapatia fursa wanachama kunufaika na sekta ya hifadhi ya jamii. Hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya wanachama 3,203 walinufaika na mikopo iliyokuwa inatolewa na Mfuko kwenye makundi yafuatayo: mkopo wa elimu kwa wanachama 748; mkopo wa kuanzia maisha (wanachama 262); mkopo wa viwanja (wanachama 21); na mkopo kwa ajili ya wastaafu watarajiwa na wastaafu (wanachama 2,172).

Mfuko wa Pensheni wa PPF

59. Mwaka 2016/17, Mfuko wa Pensheni wa PPF uliandikisha wanachama wapya 104,207 na hivyo kufanya idadi ya wanachama kufikia 326,750. Idadi hiyo ya uandikishaji ni sawa na ongezeko la asilimia 46.9 ikilinganishwa na wanachama wapya 70,942 waliosajiliwa mwaka 2015/16. Lengo la kuandikisha wanachama 165,000 mwaka 2016/17 halikufikiwa kutokana na upungufu wa ajira mpya.

60. Mwaka 2016/17, mfuko ulikusanya shilingi bilioni 397.67 kutoka kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 378.4 zilizokusanywa mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Aidha, mafao ya jumla ya shilingi bilioni 223.3 yalilipwa kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 214.4 zilizolipwa mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 4.2. Ongezeko hilo lilitokana na kupandishwa kwa kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 50,000 hadi shilingi 100,000 kwa mwezi. Uwekezaji wa Mfuko uliongezeka kwa asilimia 11.9 kufikia shilingi trilioni 2.238 mwaka 2016/17 kutoka shilingi trilioni 2.0 mwaka 2015/16. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 154.6 mwaka 2015/16 hadi kufikia shilingi bilioni 200.65 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 29.8. Vile vile,

thamani ya Mfuko iliongezeka kwa asilimia 14.1 hadi shilingi trilioni 2.62 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.30 mwaka 2015/16.

Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF)

61. Hadi Desemba 2017, jumla ya waajiri 12,282 kutoka katika sekta binafsi na umma walisajiliwa na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi ikiwa ni ongezeko la asilimia 90.5 ya waajiri 6,448 waliosajiliwa mwaka 2016. Ongezeko hili ni matokeo ya elimu iliyotolewa kwa waajiri na wadau mbalimbali wa Mfuko. Kutokana na ongezeko hilo la waajiri, michango nayo iliongezeka na kufikia shilingi bilioni 81.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 59.1 mwaka 2016. Katika kipindi hicho, Mfuko ulitumia shilingi bilioni 1.76 kulipia matibabu na fidia kwa wafanyakazi walioumia, kuugua ama kufariki wakiwa kazini.

62. Mwaka 2017, Mfuko uliwekeza shilingi bilioni 70.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 53.90 zilizowekezwa mwaka 2016. Maeneo ambayo Mfuko umewekeza ni pamoja na amana za benki, soko la hisa na dhamana za Serikali. Hadi kufikia Desemba, 2017, shilingi bilioni 16.35 zilikusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya uwekezaji wa Mfuko na vyanzo vingine vya mapato. Aidha, thamani ya rasilimali halisi za Mfuko zilifikia shilingi bilioni 138.16 ikilinganishwa na shilingi bilioni 104.67 mwaka 2016.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

63. Mwaka 2016/17, idadi ya wanachama wachangiaji kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliongezeka kwa asilimia 7.3 na kufikia 753,892 ikilinganishwa na wanachama 702,598 mwaka 2015/16. Ongezeko hilo lilichangiwa na uandikishaji wa makundi mbalimbali ya wanachama kama vile wanafunzi, waajiriwa wa sekta binafsi, wanachama binafsi na watoto chini ya miaka 18 chini ya mpango wa TOTO AFYA KADI. Aidha, kaya zilizoandikishwa kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) kwa mwaka 2017 zilikuwa 577,811, na hivyo kufanya jumla ya kaya zilizoandikishwa kuongezeka kwa asilimia 39.8 kufikia kaya 2,030,666 kutoka kaya 1,452,855 mwaka 2015/16.

64. Mwaka 2016/17, Mfuko ulikuwa unahudumia jumla ya wanufaika 15,675,396 ikilinganishwa na wanufaika 12,094,153 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 29.6. Idadi hiyo ya wanufaika wa Mfuko ni sawa na asilimia 31 ya wananchi wote Tanzania Bara. Kati ya hao, wanufaika wa Mfuko

wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) walikuwa 3,491,400 na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) ulikuwa na wanufaika 12,183,996.

65. Mwaka 2016/17, kiasi kilichoombwa kama malipo kwa watoa huduma kilikuwa shilingi milioni 326,687.09 ambapo kiasi kilicholipwa kilikuwa ni shilingi milioni 303,818.99, sawa na asilimia 93.0 ya kiasi kilichoombwa. Tofauti kati ya madai yaliyoombwa na yaliyolipwa ilitokana na baadhi ya watoa huduma kutozingatia miongozo ya matibabu na mpangilio wa bei za Mfuko (NHIF), uandaaji usiofaa wa madai na kugushi madai.

66. Mwaka 2016/17, mapato ya Mfuko yaliongezeka na kufikia shilingi milioni 476,446.24 kutoka shilingi milioni 447,327.31 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 6.5. Kati ya mapato hayo, michango ya wanachama ilikuwa shilingi milioni 367,634.47 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na shilingi milioni 354,446.73 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Michango ya wanachama ilikuwa asilimia 79.2 ya mapato yote ikifuatiwa na mapato yatokanayo na vitega uchumi asilimia 20.4 na mapato mengineyo asilimia 0.4. Hadi kufikia mwaka 2016/17, rasilimali halisi za Mfuko zilifikia shilingi 1,315,802,747,000 ikilinganishwa na shilingi 1,192,666,840,000 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 10.3.

67. Mwaka 2016/17, jumla ya vituo vya afya vilivyosajiliwa na Mfuko vilifikia 7,140 ikilinganishwa na vituo 6,439 vilivyosajiliwa mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 10.9. Ongezeko hilo, lilitokana na usajili wa vituo vya uchunguzi wa magonjwa (asilimia 50) na kliniki maalum (asilimia 76.2). Kati ya hivyo, vituo 5,323 (asilimia 75) vilimilikiwa na Serikali, vituo 1,034 (asilimia 14) vilimilikiwa na sekta binafsi na vituo 783 (asilimia 11) vilimilikiwa na madhehebu ya dini.

Jedwali Na 2.5: Vituo vya Afya Vilivyosajiliwa na Mfuko

Aina ya vituo	2015/16				2016/17				Ukuaji (%)
	Serikali	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla	Serikali	Mashirika ya Dini	Binafsi	Jumla	
Hospitali	131	106	25	262	139	111	28	278	6.1
Vituo vya afya	449	142	37	628	474	177	54	705	12.3
Zahanati	4,509	319	103	4,931	4,702	490	168	5,360	8.7
Maduka ya dawa	2	5	586	593	8	4	742	754	27.2
Kliniki maalum	-	-	21	21	-	1	36	37	76.2
Vituo vya uchunguzi wa Magonjwa	-	-	4	4	-	-	6	6	50.0
Jumla	5,091	572	776	6,439	5,323	783	1,034	7,140	10.9%

Chanzo: Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania (TIRA)

68. Mwaka 2017, idadi ya kampuni zilizoandikishwa kufanya biashara ya bima nchini zilikuwa 31 (ikijumuisha kampuni 1 ya bima mtawanyo) kama ilivyokuwa mwaka 2016. Aidha, madalali waliosajiliwa kufanya biashara ya bima walikuwa 152 ikilinganishwa na madalali 136 mwaka 2016; mawakala wa bima 596 ikilinganishwa na mawakala 575 mwaka 2016; na wakadiriaji mali na hasara 55 ikilinganishwa na wakadiriaji 52 mwaka 2016.

69. Mauzo ya soko la bima kwa mwaka 2017 yalipungua kwa asilimia 3.6 kutoka mauzo ya shilingi bilioni 660.0 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 636.1 mwaka 2017. Bima za kawaida zilichangia asilimia 87.3 ya mauzo yote ya bima kwa mwaka 2017, wakati bima za maisha zilichangia asilimia 12.7 ya mauzo hayo. Mauzo ya bima za kawaida yalipungua kwa asilimia 5.2 kufikia shilingi bilioni 555.3 ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 585.8 mwaka 2016. Aidha, mauzo ya bima za maisha yaliongezeka kwa asilimia 8.8 kufikia shilingi bilioni 80.8, ikilinganishwa na mauzo ya shilingi bilioni 74.2 mwaka 2016.

Jedwali Na. 2.6: Mauzo ya Bima 2016 – 2017 (Shs. Milioni)

Mauzo	2016	2017	Ukuaji (%)
Mauzo - Bima za Kawaida	585,798	555,324	(5.2)
Mchango kwa jumla (%)	88.80	88.00	(0.9)
Mauzo - Bima za Maisha	74,249	80,812	8.8
Mchango kwa jumla (%)	11.25	12.70	12.9
Jumla ya Mauzo	660,047	636,136	(3.6)

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

70. Mwaka 2017, kampuni ya bima za kawaida zilipata faida yenye thamani ya shilingi bilioni 5.70, sawa na upungufu wa asilimia 68.6 ikilinganishwa na faida ya shilingi bilioni 18.2 mwaka 2016. Upungufu huu wa faida ulitokana na kupungua kwa mapato yatokanayo na uwekezaji hasa katika hisa na dhamana na mikopo.

71. Mwaka 2017, thamani ya mali za kampuni za bima ziliongezeka kwa asilimia 2.9 kufikia shilingi bilioni 859.3 kutoka mali za shilingi bilioni 835.3 mwaka 2016. Aidha, madeni ya kampuni za bima yaliongezeka hadi shilingi bilioni 569.8 mwaka 2017 kutoka shilingi bilioni 567.2 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.5. Hii ilifanya tofauti kati ya mali na madeni ya kampuni za bima kuongezeka kwa asilimia 8.0 kufikia shilingi bilioni 289.5 mwaka 2017 kutoka shilingi bilioni 268.1 mwaka 2016.

Jedwali Na. 2.7: Thamani ya Mali na Madeni

Mali na Madeni (Shs. Milioni)	2016	2017
Jumla ya Mali	835,310	859,331
Ukuaji (%)	14.50	2.90
Jumla ya Madeni	567,211	569,843
Ukuaji (%)	17.20	0.50
Ziada ya Mali	268,100	289,488
Ukuaji (%)	9.20	8.0

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania

Mwenendo wa Soko la Mikopo ya Nyumba Tanzania

72. Hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya mikopo iliyotolewa na sekta ya benki kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 344.8 ikilinganishwa na mikopo ya shilingi bilioni 416.94 iliyotolewa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 17.3. Hali hii ilitokana na kupungua kwa hali ya ukwasi kwenye benki za biashara iliyosababishwa na kuongezeka kwa mikopo chechefu.

73. Hadi kufikia Desemba 2017, taasisi zilizokuwa zinatoa mikopo ya nyumba ziliongezeka hadi 31 kutoka taasisi 28 mwaka 2016. Taasisi mpya zilizoingia sokoni ni Letshego Bank (T) Ltd, Yetu Microfinance Bank Plc na Mufindi Community Bank Ltd. Katika kipindi hicho, asilimia 60 ya soko ilimilikiwa na taasisi tano ambazo ni: Stanbic Bank (asilimia 18), Bank M (asilimia 16), CRDB (asilimia 11), Azania Bank (asilimia 8) na Commercial Bank of Africa (asilimia 7). Aidha, mwaka 2017, Benki Kuu iliipa leseni taasisi ya First Housing Finance (Tanzania) Limited (awali ikijulikana kama M Mortgage Finance) kama taasisi ya kwanza nchini ambayo imejikita (specialized) kufanya biashara ya kutoa mikopo ya nyumba pekee kwa wananchi. Taasisi hii inalenga kuboresha soko la nyumba kwa kutoa mikopo ya nyumba ya hadi miaka 20 kwa riba nafuu.

**Jedwali Na 2.8: Mchanganuo wa Utoaji wa Mikopo ya Nyumba hadi
Desemba 2017**

Mkopeshaji	Idadi ya Wateja	Thamani ya Mikopo (Shs.Bilioni)	Miliki ya Soko (%)
Stanbic Bank (T) Ltd	182	60.74	17.61
Bank M Tanzania Public Limited Company	30	53.79	15.60
Crdb Bank Plc	301	38.43	11.14
Azania Bank Limited	554	28.03	8.13
Commercial Bank Of Africa (T) Limited	161	23.94	6.94
Nic Bank Tanzania Limited	16	19.88	5.77
First National Bank Tanzania Limited	94	16.4	4.75
Bank Of Africa Tanzania Limited	113	11.9	3.45
Kcb Bank Tanzania Limited	57	9.37	2.72
Dcb Commercial Bank Plc	814	8.57	2.48
Nmb Bank Plc.	62	7.76	2.25
Barclays Bank (T) Limited	57	7.46	2.16
I & M Bank Tanzania Limited	37	7.13	2.07
Equity Bank Tanzania Limited	16	5.82	1.69
Letshego Bank (T) Limited	119	5.74	1.66
African Banking Corporation (T) Ltd	41	5.57	1.62
Nbc Limited	43	5.14	1.49
Standard Chartered Bank (T) Ltd	21	4.7	1.36
Exim Bank Tanzania Limited	37	4.28	1.24
Akiba Commercial Bank Ltd	600	3.85	1.12
Efc M.F.B Tanzania Limited	152	2.88	0.84
Amana Bank Limited	32	2.64	0.77
Peoples Bank Of Zanzibar	17	2.36	0.68
Tib Corporate Bank Limited	13	1.76	0.51
Diamond Trust Bank (T) Ltd.	3	1.73	0.50
Yetu Microfinance Plc	547	1.63	0.47
Citibank Tanzania Limited	11	1.55	0.45
Tib Development Bank Limited	10	1.03	0.30
International Commercial Bank (T) Ltd.	1	0.39	0.11
Mucoba Bank Plc	32	0.31	0.09
China Commercial Bank Limited	1	0.09	0.03
Jumla	4,174	344.87	100

Chanzo: Kampuni ya Mikopo ya Nyumba Nchini

74. Mwaka 2017, Kampuni ya Mikopo ya Nyumba nchini (Tanzania Mortgage Refinance Company- TMRC) ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 91.1 kwa benki 10 ambazo ni wanachama na benki nne ambazo sio wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 59.6 zilizotolewa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 52.9. Mikopo ya nyumba iliyotolewa na TMRC ilikuwa sawa na asilimia 26.4 ya mikopo yote ya nyumba nchini ikilinganishwa na asilimia 14.3 mwaka 2016. Aidha, mikopo iliyotolewa chini ya Mfuko wa Mikopo Midogo ya Nyumba unaotekelezwa na TMRC iliongezeka kwa asilimia 91.7 kutoka shilingi bilioni 6 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 11.5 mwaka 2017. Hii lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya fedha kwa benki za biashara kwa ajili ya mikopo ya nyumba.

Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania

75. Mwaka 2017, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania iliendelea kujiendesha kiufanisi kwa kukuza mtaji kupitia fedha za wanahisa na kupata faida. Benki ilipata faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 2.86 ikiwa ni ukuaji wa asilimia 23.8 kutoka faida ya shilingi bilioni 2.31 mwaka 2016. Aidha, mtaji wa benki uliongezeka kwa asilimia 3.0 kufikia shilingi bilioni 66.8 kutoka shilingi bilioni 64.9 mwaka 2016. Katika kipindi hicho, benki iliidhinisha mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 24.5 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 6.5 iliyoidhinishwa mwaka 2016. Mikopo hii ilitolewa kuendeleza mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Jumla ya wakulima 2,202 walinufaika na mikopo hii ambapo kati yao, asilimia 28.7 walikuwa wanawake ikilinganishwa na wakulima 857 walionufaika na mikopo mwaka 2016. Vile vile, kiasi cha shilingi bilioni 1.8 zilikopeshwa kwa miradi ya umwagiliaji wa mahindi, mpunga na mbogamboga inayofanywa na vyama vya wakulima wadogo katika mikoa ya Iringa, Morogoro, na Tanga ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.2 iliyotolewa mwaka 2016.

76. Mwaka 2017, benki ilitoa mafunzo kwa wakulima wadogo 4,795 katika mikoa mbalimbali nchini na hivyo kufikia jumla ya wakulima 15,646 tangu Benki ilipoanza rasmi kutoa mafunzo hayo mwishoni mwa mwaka 2015. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wakulima wadogo katika masuala ya usimamizi wa fedha, uendeshaji wa vikundi na vyama, utunzaji wa kumbukumbu na uandaaji wa andiko la mradi linalokidhi masharti ya mkopo.

Benki ya Posta

77. Mwaka 2017, Benki ya Posta Tanzania ilikuwa na matawi 30 kama ilivyokuwa mwaka 2016. Katika kipindi hicho, matawi madogo ya benki yaliongezeka na kufikia 37 kutoka matawi 24 yaliyokuwepo mwaka 2016. Ongezeko hili lilichangiwa na utekelezaji wa mkakati wa kupanua wigo wa biashara na kupeleka huduma za benki vijijini. Katika kipindi hicho, akaunti za utoaji huduma kwa njia ya simu za kiganjani zilizofunguliwa kupitia mpango wa “TPB Popote” zilikuwa 349,878 ikilinganishwa na akaunti 298,874 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 17.1. Aidha, benki iliendelea kutoa huduma zake kupitia mashine 238 za ATM ikilinganishwa na mashine 200 za ATM mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 19.0. Kati ya hizo, ATM 51 zilikuwa mali ya Benki ya Posta ikilinganishwa na ATM 44 mwaka 2016.

78. Amana za wateja katika benki ziliongezeka na kufikia shilingi milioni 317,645 mwaka 2017 kutoka shilingi milioni 292,200 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.7. Ongezeko hilo ni matokeo ya utekelezaji wa mikakati mipya ya kuwaendea wananchi katika maeneo yao kama vyuo, mashule na vikundi vya kuweka na kukopa na kuwaingiza katika mfumo wa kuweka amana na kupata mikopo midogo midogo.

Jedwali Na 2.9: Mchanganuo wa Akaunti za Benki ya Posta (Shs. Milioni)

Aina ya Akaunti	Desemba 2015	Desemba 2016	Desemba 2017	Ukuaji (%)
Akiba ya Kitabu	3,646	3,207	2,658	(17.1)
Akaunti ya Akiba (QA)	157,535	161,342	170,746	5.8
WADU	12,488	12,133	13,322	9.8
Amana ya muda maalum	107,615	93,848	105,194	12.1
Akaunti dada ya hundi	13,182	14,207	19,983	40.7
Akaunti Zilizolala	7,715	7,463	8,400	12.6
Jumla ya Amana	302,181	292,200	317,645	8.7

Chanzo: Benki ya Posta

79. Mwaka 2017, uwekezaji wa Benki ya Posta kwenye dhamana za Serikali uliongezeka kwa asilimia 45.5 kutoka shilingi bilioni 42.4 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 61.7 mwaka 2017. Kuongezeka kwa uwekezaji katika dhamana za Serikali kulitokana na kukua kwa thamani ya amana pamoja na hatua za kudhibiti ukuaji wa mikopo chechefu. Mwaka 2017, benki iliendelea kutoa

mikopo kwa wananchi ambapo thamani ya mikopo iliyotolewa ilikuwa shilingi milioni 336,802, sawa na ongezeko la asilimia 13.0 ikilinganishwa na shilingi milioni 298,057 mwaka 2016.

Jedwali Na 2.10: Mchanganuo wa Thamani ya Mikopo Iliyotolewa (Shs.Milioni)

Aina ya Mikopo	2014	2015	2016	2017	Ukuaji % (2016/17)
Mikopo ya Biashara	24,393	34,794	33,800	27,199	-19.5
Mikopo ya Watumishi	124,965	135,164	141,400	147,924	4.6
Mikopo ya Wastaafu	18,540	43,319	76,000	103,614	36.3
Mikopo midogo midogo	18,536	22,867	23,929	28,354	18.5
Mikopo ya Uwezeshaji	196	187	36	0	-100.0
Mikopo ya Vikundi (Group Lending)	2,297	5,831	4,600	5,979	30.0
PSL Loans	0	2,010	4,000	4,198	5.0
Mikopo ya VICOBA (NEEC Loans)	0	225	705	976	38.4
Mikopo ya Wafanyakazi	7,078	9,961	13,500	14,903	10.4
Jumla	196,005	254,358	298,057	336,802	13.0

Chanzo: Benki ya Posta Tanzania

80. Mwaka 2017, Benki ilizalisha pato ghafi la jumla ya shilingi milioni 107,964 sawa na ongezeko la asilimia 32.1 ikilinganishwa na mapato ya shilingi milioni 81,709 mwaka 2016. Ukuaji huu ulitokana na uongozi wa Benki kusimamia kwa uangalifu matumizi katika shughuli zake, kupanuka kwa uwekezaji katika mikopo na dhamana za Serikali pamoja na kuongezeka kwa wigo wa huduma na bidhaa zinazozalisha mapato. Aidha, faida ya benki baada ya kodi kwa mwaka 2017 ilikuwa ni shilingi milioni 12,815 kutoka shilingi milioni 10,808, sawa na ongezeko la asilimia 18.6.

Mfuko wa SELF

81. Mwaka 2017, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20.0 ikilinganishwa na shilingi bilioni 11.5 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 73.9. Hii ilichangiwa na utekelezaji wa mpango wa kufanya kazi na asasi zenye mitandao mikubwa ili kuwafikia walengwa wengi, hususan mikoa

ya pembezoni. Aidha, wajasiriamali wapatao 11,653 walinufaika na mikopo hiyo ikilinganishwa na wajasiriamali 5,130 mwaka 2016 ambapo wanawake walikuwa 6,733 (sawa na asilimia 58) na wanaume 4,920. Kwa upande mwingine, kiwango cha urejeshaji mikopo kilikuwa asilimia 88 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 91 mwaka 2016. Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na kiwango cha matarajio ya urejeshwaji mikopo katika sekta ndogo ya fedha cha asilimia 95.

82. Hadi kufikia Desemba 2017, thamani ya mtaji ya Mfuko wa SELF ilikuwa shilingi bilioni 58.87 ikilinganishwa na shilingi bilioni 57.09 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 3.1.

Jedwali Na.2.11: Mchanganuo wa Mtaji wa Mfuko wa SELF (Shs. Bilioni)

Eneo la Uwekezaji	Desemba 2016	Desemba 2017	Ukuaji (%)
Fedha Taslimu Benki	2.3	0.93	(59.6)
Kasma ya mikopo	11.09	17.95	61.9
Uwekezaji katika amana	43.7	39.99	(8.5)
Jumla	57.09	58.87	3.1

Chanzo: Mfuko wa SELF

83. Mwaka 2017, mapato ya Mfuko yaliongezeka kwa asilimia 3.4 kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 62.8 lililorekodiwa mwaka 2016. Ukuaji huu mdogo ulitokana na kushuka kwa uwekezaji kwenye amana za Serikali pamoja na kushuka kwa kiwango cha riba katika amana. Uwekezaji katika Amana za Serikali ulichukua sehemu kubwa ya uwekezaji uliofanywa na Mfuko (asilimia 61.2), ikifuatiwa na riba ya mikopo (asilimia 34.3) na mapato mengineyo ni asilimia 4.5.

Jedwali Na. 2.12: Vyanzo vya Mapato ya Mfuko wa SELF (Shs. Bilioni)

Vyanzo vya Mapato	2016	2017	Ukuaji (%)
Riba ya Mikopo	1.215	2.232	83.7
Uwekezaji katika Amana za Serikali	4.85	3.975	(18.0)
Mapato mengineyo	0.22	0.293	33.2
JUMLA	6.285	6.500	3.4

Chanzo: Mfuko wa SELF

MWENENDO WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 17

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba								Sh. Bilioni	
									Badiliko 2016/17	
	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Kiasi	%
Fedha ya msingi (M0)	1,897.1	2,235.8	2,414.8	2,764.0	3,244.7	3,678.5	3,608.7	3,831.8	223.1	6.2
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	4,521.4	5,572.0	6,538.6	7,218.1	8,284.2	9,575.7	10,083.8	11,155.5	1,071.7	10.6
Amana za Akiba na za muda maalum	3,520.7	3,676.0	4,186.0	4,672.4	5,632.9	6,204.4	6,536.5	7,191.4	654.9	10.0
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	8,042.2	9,247.9	10,724.5	11,890.6	13,917.0	15,780.1	16,620.3	18,346.9	1,726.6	10.4
Amana za fedha za kigeni	2,970.5	3,773.4	3,922.6	4,216.2	4,697.1	6,335.2	6,257.5	6,364.4	106.9	1.7
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	11,012.7	13,021.3	14,647.1	16,106.8	18,614.2	22,115.3	22,877.9	24,711.3	1,833.4	8.0
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	6,125.6	6,273.6	6,396.0	6,576.3	6,551.5	8,244.0	8,186.3	11,596.1	3,409.8	41.7
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	4,887.1	6,747.7	8,251.1	9,530.4	12,062.6	13,871.3	14,691.5	13,115.2	-1,576.3	-10.7
Karadha Nchini	9,522.8	10,958.1	13,719.0	16,293.0	18,863.7	22,505.5	23,775.8	24,949.7	1,173.9	4.9
Madai halisi kwa serikali kuu	806.7	1,471.3	2,019.4	2,554.6	3,651.6	4,881.6	4,282.0	3,275.7	-1,006.3	-23.5
Mikopo kwa serikali kuu	3,531.0	3,335.7	4,708.6	5,900.4	6,451.5	7,012.8	7,166.9	8,066.5	899.6	12.6
Mikopo kwa sekta binafsi	5,991.8	7,622.3	9,010.4	10,392.7	12,412.3	15,492.7	16,608.9	16,883.1	274.2	1.7
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	-1,911.4	-2,345.9	-2,778.7	-3,416.8	-4,001.3	-6,503.1	-6,199.3	-7,043.6	-844.3	13.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA - TANZANIA BARA

Jedwali Na. 18

	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba							
	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Fedha ya msingi (M0)	21.1%	17.9%	8.0%	14.5%	17.4%	13.4%	-1.9%	6.2%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1)	25.9%	23.2%	17.3%	10.4%	14.8%	15.6%	5.3%	10.6%
Amana za Akiba na za muda maalum	16.9%	4.4%	13.9%	11.6%	20.6%	10.1%	5.4%	10.0%
Ujazi wa fedha, kwa tafsiri pana (M2)	21.8%	15.0%	16.0%	10.9%	17.0%	13.4%	5.3%	10.4%
Amana za fedha za kigeni	36.5%	27.0%	4.0%	7.5%	11.4%	34.9%	-1.2%	1.7%
Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3)	25.4%	18.2%	12.5%	10.0%	15.6%	18.8%	3.4%	8.0%
Rasilimali halisi katika fedha za kigeni kwenye benki (Net foreign assets)	24.0%	2.4%	2.0%	2.8%	-0.4%	25.8%	-0.7%	41.7%
Rasilimali halisi katika fedha za ndani kwenye benki (Net domestic assets)	27.2%	38.1%	22.3%	15.5%	26.6%	15.0%	5.9%	-10.7%
Karadha Nchini	21.2%	15.1%	25.2%	18.8%	15.8%	19.3%	5.6%	4.9%
Madai halisi kwa serikali kuu	528.4%	82.4%	37.3%	26.5%	42.9%	33.7%	-12.3%	-23.5%
Mikopo kwa serikali kuu	23.2%	-5.5%	41.2%	25.3%	9.3%	8.7%	2.2%	12.6%
Mikopo kwa sekta isiyo serikali	20.0%	27.2%	18.2%	15.3%	19.4%	24.8%	7.2%	1.7%
Rasilimali nyinginezo (Other Items Net)	49.4%	22.7%	18.5%	23.0%	17.1%	62.5%	-4.7%	13.6%

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA VIWANGO VYA UBADILISHAJI KATI YA SHILINGI NA DOLA YA MAREKANI

Jedwali Na.19

	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Shs/Dola mwisho wa mwaka	1,132.09	1,280.30	1,313.29	1,453.54	1,605.35	1,578.41	1603.2067	1,723.69	2,148.52	2,172.62	2230.07
Badiliko la thamani ya shilingi (%)	11.4	-11.6	-2.5	-9.6	-9.5	1.7	-1.5	-7.0	-19.8	-1.1	-2.6
Shs/Dola wastani wa mwaka	1,239.04	1,206.32	1,307.23	1,401.79	1,557.43	1,571.71	1598.66	1,652.51	1985.39	2,177.07	2228.86
Badiliko la wastani wa thamani ya shilingi (%)	1.2	2.7	-7.7	7.2	-10.0	-0.9	-1.7	-3.3	-16.8	-8.8	-2.3

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MIKOPO YA BENKI ZA BIASHARA KWA SHUGHULI ZA KIUCHUMI

Jedwali Na. 20

Aina ya Shughuli	Kipindi kinachoishia mwezi Desemba (Sh. Milioni)					Ukuaji (%)	Mchango (%)
	2013	2014	2015	2016	2017		
Uzalishaji katika Kilimo	965,141	1,057,348	1,174,243	1,107,645	1,134,819	2.5	6.7
Huduma za Kifedha	251,255	310,712	404,606	388,745	292,128	-24.9	1.7
Madini na Uchimbaji Mawe	96,739	166,275	275,233	328,620	292,647	-10.9	1.7
Viwanda	1,160,594	1,386,237	1,695,767	1,627,766	1,777,573	9.2	10.5
Majengo na Ujenzi	514,408	660,148	741,401	740,727	837,159	13.0	5.0
Uchukuzi na Mawasiliano	727,538	925,724	1,231,806	1,180,905	975,551	-17.4	5.8
Biashara	2,162,191	2,652,057	3,077,683	3,349,329	3,306,914	-1.3	19.6
Utalii	113,395	129,478	176,626	198,482	176,349	-11.2	1.0
Mahoteli na Migahawa	371,008	436,101	514,642	526,390	594,968	13.0	3.5
Umeme	403,023	440,937	439,801	429,919	335,175	-22.0	2.0
Watu Binafsi	1,744,954	2,104,496	2,731,740	2,981,741	3,258,724	9.3	19.3
Sekta Nyinginezo	1,643,118	1,842,250	2,641,096	3,748,616	3,901,122	4.1	23.1
Jumla	10,153,364	12,111,763	15,104,644	16,608,885	16,883,129	10.0	100.0

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

MWENENDO WA AMANA KATIKA BENKI ZA BIASHARA

Jedwali Na.21

Sh. Bilioni

	Kipindi Kinachoishia mwezi Desemba										Badiliko 2016/17 (%)
	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	
Amana za Sekta Binafsi											
Amana za Hundi/Zinazaohamishika	1,715.7	2,019.4	2,624.3	3,336.2	4,123.8	4,454.2	5,039.4	5,897.2	5,941.5	6,685.3	12.5
Amana za Akiba na za Muda Maalum	2,307.9	3,011.9	3,520.7	3,676.0	4,186.0	4,672.4	5,632.9	6,204.4	6,415.6	7,049.0	9.9
Amana za fedha za kigeni	1,989.3	2,158.8	2,926.4	3,722.0	3,882.4	4,216.0	4,697.1	6,335.2	5,831.5	6,087.1	4.4
Jumla	6,012.9	7,190.1	9,071.5	10,734.2	12,192.2	13,342.6	15,369.4	18,436.8	18,188.7	19,821.3	9.0
Amana za Serikali	401.7	662.6	699.3	626.6	736.8	791.8	808.4	856.9	577.8	560.6	-3.0
Jumla za Amana zote	6,414.5	7,852.7	9,770.8	11,360.8	12,929.0	14,134.4	16,177.8	19,293.7	18,766.5	20,381.9	8.6

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

VIWANGO VYA WASTANI WA RIBA

Jedwali Na. 22

Asilimia

Aina ya Riba	Kipindi Kinachoishia Mwezi Desemba							
	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Riba ya Benki Kuu (Bank rate)	7.58	12.00	12.00	16.00	16.00	16.00	16.00	16.00
Riba za Amana								
Amana za akiba	2.43	2.90	2.94	3.11	3.12	3.42	3.08	2.83
Amana za muda maalum	6.09	7.12	8.82	8.87	8.76	9.30	8.78	9.62
Riba za mikopo								
Mikopo ya muda mfupi hadi mwaka mmoja	14.37	13.78	14.09	13.84	14.80	14.22	12.87	18.24
Mikopo ya muda wa kati na mrefu	14.92	14.21	15.68	16.13	15.75	16.39	15.66	18.42
Riba za Hawala za Hazina								
Siku 91	5.24	12.61	11.89	13.62	13.20	9.28	7.09	4.00
Siku 182	6.20	16.39	12.96	15.46	15.22	17.15	14.54	5.87
Siku 364	7.67	18.66	13.69	15.63	16.23	18.72	15.80	8.71

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

SURA YA 3

FEDHA ZA SERIKALI

Utangulizi

84. Bajeti ya mwaka 2017/18 ilikuwa na dhamira ya kuongeza kasi ya kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17-2020/21; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, dhima ya Bajeti ya mwaka 2017/18 ilikuwa ni **“kujenga uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii”**.

85. Katika bajeti ya mwaka 2017/18, Serikali ililenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: kuendeleza ukuaji wa uchumi na kujenga uchumi wa kipato cha kati; kuongeza mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kusimamia sheria ya ununuzi wa umma; na ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi (umeme, barabara, reli na usafiri wa anga na wa majini) ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje. Vipaumbele vingine ni pamoja na: kuhakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu; kuboresha kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi, hususan kuongeza thamani na kuzifanya shughuli hizi kuwa za kisasa zaidi kwa kutoa mafunzo, pembejeo, zana na wataalam; na kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wa huduma za afya na maji.

86. Shabaha za bajeti ya mwaka 2017/18 zililenga kuwa na ukuaji wa Pato halisi la Taifa wa asilimia 7.1 mwaka 2017; kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja kati ya asilimia 5.0 na asilimia 8.0 mwaka 2017; mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri kuwa asilimia 16.5 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18; mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18; matumizi ya Serikali kufikia asilimia 26.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18; na nakisi ya bajeti kupungua na kufikia asilimia 3.8 ya Pato la Taifa.

87. Katika mwaka 2017/18, Serikali ilitarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 31,712.0 kutoka vyanzo vya ndani na nje. Jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalitarajiwa kuwa shilingi bilioni 19,977.0, sawa na asilimia 63.0 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo ya ndani, mapato ya

kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 17,106.3, sawa na asilimia 14.2 ya Pato la Taifa. Mapato yasiyo ya kodi yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 2,183.4 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri shilingi bilioni 687.3.

Mwenendo wa Mapato

Mapato ya Ndani

88. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, makusanyo ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi bilioni 13,535.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12,469.9 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 9. Mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 11,546.9 sawa na asilimia 89 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 12,993.0. Kiasi kilichokusanywa ni sawa na ongezeko la asilimia 9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 10,626.3 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17.

89. Makusanyo ya maduhuli hadi Machi 2018 yalifikia shilingi bilioni 1,591.6 ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 1,455.4 sawa na asilimia 109.4 ya lengo la kipindi hicho. Serikali kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 na Waraka wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2017 ilizielekeza Wizara, Idara, Wakala na Taasisi za Serikali zinazokusanya maduhuli kujiunga na kukusanya mapato kwa kutumia mfumo wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato (Government Electronic Payment Gateway System – GePG). Hivyo, mwenendo huu mzuri wa makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi (maduhuli) ulitokana na jitihada za Serikali katika kuhakikisha Taasisi zake zote zinakusanya maduhuli kupitia mfumo huo. Aidha, makusanyo mazuri yalichangiwa na gawio la Benki Kuu (BOT) lililokuwa zaidi ya lengo. Mapato yaliyokusanywa na halmashauri yalifikia shilingi bilioni 397.2 sawa na asilimia 76 ya makadirio ya shilingi bilioni 521.2 kwa kipindi hicho.

90. Kwa ujumla, mapato ya ndani yalikuwa pungufu ya lengo kwa asilimia 10 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kupungua kwa usafirishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki; kupungua kwa matumizi (consumption) ya baadhi ya bidhaa zinazotozwa ushuru wa bidhaa hususan sigara, vinywaji vikali na vinywaji baridi kutokana na mabadiliko ya tabia za watumiaji (consumer behavior); kupungua kwa uzalishaji pamoja na bei za baadhi ya bidhaa zinazotozwa kodi ya ongezeko la thamani kutokana na kushuka kwa mauzo; na makampuni mengi ya utafutaji na uchimbaji wa madini na gesi asilia kupunguza

shughuli zao na hivyo, kusababisha kupungua kwa huduma zinazotolewa na wazabuni wao. Hali hii ilichangia kupunguza makusanyo ya kodi ya zuio.

Misaada na Mikopo Nafuu

91. Hadi Machi 2018, kiasi cha shilingi bilioni 1,637.9 kilipokelewa kama misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 61.2 ya ahadi za shilingi bilioni 2,675.5 kwa kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 70.2 zilipokelewa kama misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, sawa na asilimia 20.1 ya makadirio ya kipindi hicho ya shilingi bilioni 349.5; mifuko ya kissekta shilingi bilioni 180.5 ambayo ni asilimia 39.5 ya makadirio ya shilingi bilioni 457.0; na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,387.2 ikiwa ni asilimia 74.2 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,869.0.

92. Katika kuhakikisha misaada na mikopo nafuu inapatikana kama ilivyoahidiwa na kwa wakati, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo iliandaa na kupitisha Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Cooperation Framework-DCF). Aidha, Serikali iko kwenye mchakato wa kuandaa mpango kazi wa kutekeleza DCF ambao utakamilishwa mwishoni mwa Juni 2018. Mambo ya msingi yaliyokubalika katika Mwongozo huo ni pamoja na: kuweka misingi ya ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, ambapo msingi mkuu ni Serikali kumiliki na kuongoza michakato yote ya maendeleo; na kuweka mfumo mpya wa majadiliano ya kimkakati ya kitaifa, kissekta na yenye mwelekeo wa kisiasa.

93. Mwaka 2017/18, Serikali iliendelea kufanya majadiliano na Washirika wa Maendeleo kuhusu njia mpya za kutoa na kupokea misaada na mikopo (New Financing Instruments) na kufuatilia utekelezaji wa masharti ya makubaliano ya mikataba ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha fedha za Washirika wa Maendeleo zinapatikana kwa kiasi kama ilivyoahidiwa na kwa wakati. Aidha, Serikali iliendelea kufuatilia, kukagua na kufanya tathmini ya miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi (absorption rate). Kadhalika, Serikali iliendelea kuzihimiza sekta husika kukamilisha na kutimiza kwa wakati masharti na makubaliano yote yanayoweza kuathiri utoaji wa fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi na programu za maendeleo nchini.

Mikopo ya Ndani

94. Hadi kufikia Machi 2018, Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 4,560.9 kutoka soko la ndani sawa na asilimia 74 ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa mwaka 2017/18. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 3,806.0 zilikopwa kwa ajili ya kulipia hati fungani na dhamana za Serikali zilizoiva, na shilingi bilioni 754.9 zilikopwa ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, mikopo kutoka kwenye chanzo hiki ilielekezwa kulipia sehemu ya madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi wa barabara, maji na umeme.

Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara

95. Katika mwaka 2017/18, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 1,595.0 ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2018, Serikali iliweza kukopa kiasi cha shilingi bilioni 224.1 ikiwa ni asilimia 14 ya lengo la mwaka. Serikali haikuweza kukopa kiasi kilichopangwa kwa wakati kutoka kwenye chanzo hiki kutokana na hali ya soko la fedha la kimataifa kutokuwa nzuri. Hata hivyo, Serikali inaendelea kufanya majadiliano na taasisi mbalimbali za fedha ili kuweza kukopa kiasi kilichosalia.

Matumizi

96. Katika mwaka 2017/18, Serikali iliendelea kuhakikisha kuwa fedha zinaelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele ili kutekeleza kikamilifu Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/18. Katika kutekeleza hilo, Sera za matumizi zililenga kuhakikisha kuwa: Mashirika ya umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali; matumizi ya umeme, simu na maji yanadhibitiwa; mishahara inalipwa kwa watumishi wanaostahili; na Serikali inatumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika kufanikisha mawasiliano.

97. Mwaka 2017/18, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 31,712.0. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 19,712.4 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi bilioni 7,205.8 za mishahara na shilingi bilioni 9,461.4 kwa ajili ya kulipia deni la Serikali na huduma nyinginezo. Aidha, matumizi ya maendeleo yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 11,999.6, ambapo shilingi bilioni 8,969.7 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,029.8 ni fedha za nje.

98. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Serikali ilitoa jumla ya shilingi bilioni 20,254.9, sawa na asilimia 85.2 ya lengo la kipindi hicho kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 15,655.7 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 4,599.2 kwa ajili utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 4,193.0 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 406.2 ni fedha za nje.

99. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje yalifikia shilingi bilioni 1,479.3 ambayo ni asilimia 89 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,665.9 kwa kipindi hicho. Aidha, malipo ya mtaji yalifikia shilingi bilioni 4,845.6 ikiwa ni asilimia 101 ya lengo la shilingi bilioni 4,810.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,039.6 zilikuwa malipo ya mtaji kwa mkopo wa nje, sawa na asilimia 99.5 ya lengo la kulipa shilingi bilioni 1,044.6. Aidha, shilingi bilioni 3,806.0 zilikuwa ni malipo ya dhamana na hati fungani za Serikali zilizoiva ikiwa ni asilimia 101 ya lengo la shilingi bilioni 3,766.1 kwa kipindi hicho. Matumizi mengine ya Mfuko Mkuu yalikuwa shilingi bilioni 963.2 ikiwa ni asilimia 80 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,206.7 ya kipindi hicho.

100. Hadi Machi 2018, malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali yalikuwa shilingi bilioni 4,744.0, sawa na asilimia 89 ya lengo la shilingi bilioni 5,351.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1,493.3 zililipwa kwa watumishi wa Serikali Kuu, shilingi bilioni 107.4 zililipwa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na shilingi bilioni 2,557.0 kwa watumishi wa Halmashauri za majiji, manispaa, miji na wilaya. Aidha, Serikali ililipa mishahara ya taasisi na mashirika ya umma jumla ya shilingi bilioni 586.3. Ulipaji wa mishahara ulikuwa chini ya lengo kutokana na uhakiki unaoendelea wa kuhakikisha malipo ya mishahara yanafanyika kwa wanaostahili pamoja na kuchelewa kwa ajira mpya.


101. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Serikali ilipanga kutumia jumla ya shilingi bilioni 10,105.0 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali, ambapo shilingi bilioni 7,779.1 zilikuwa fedha za ndani na shilingi bilioni 2,325.9 fedha za nje. Hadi kufikia Machi, 2018, shilingi bilioni 4,599.2, sawa na asilimia 45.5 ya makadirio zilitolewa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 4,193.0 zilikuwa fedha za ndani, sawa na asilimia 53.9 na shilingi bilioni 406.2 fedha za nje, sawa na asilimia 17.5.

102. Baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele zaidi katika utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa kipindi cha Julai 2017 – Machi 2018 ni pamoja na: ujenzi wa miundombinu ya barabara zinazounganisha mikoa na nchi jirani, barabara zinazopunguza msongamano katika majiji, barabara za vijijini, reli, viwanja vya ndege, na bandari shilingi bilioni 1,722.8; kutekeleza azma ya kutoa elimu msingi bila ada na kugharamia mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu shilingi bilioni 581.2; uzalishaji na usambazaji wa umeme ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma hii muhimu kiasi cha shilingi bilioni 382.0; kutekeleza lengo la kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama shilingi bilioni 143.6; kuimarisha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi jumla ya shilingi bilioni 59.0 zimetolewa katika Halmashauri za wilaya 110 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya, ukarabati wa hospitali za mikoa 24 shilingi bilioni 24.1, ununuzi wa dawa, vifaa tiba shilingi bilioni 125.7; na kulipa malimbikizo ya madai ya watumishi umma, wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1,022.6

Deni la Serikali

103. Hadi Machi 2018, deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 49,728.03 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 16.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 42,883.59 Machi 2017. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 14,158.63 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12,073.68 na deni la nje ni shilingi bilioni 35,729.92 ikilinganishwa na shilingi bilioni 30,809.91, ongezeko hilo lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, malimbikizo ya riba na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani.

Kielelezo Na. 3.1: Mwenendo wa Deni la Serikali kwa kipindi cha Machi 2011 – Machi 2018 (Shs. Bilioni)



Deni la Nje

104. Deni la nje lilifikia dola za Marekani milioni 15,811.30 Machi 2018 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 13,783.90 Machi 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 14.7. Kuongezeka kwa deni kulitokana na mikopo mipya na malimbikizo ya riba hasa kutoka nchi za kundi lisilo la wanachama wa Paris ambazo hazijatoa misamaha ya madeni kulingana na makubaliano.

105. Mchanganuo wa deni la nje kwa wakopeshaji ulionesha kuwa, sehemu kubwa ya deni ni kutoka mashirika ya fedha ya kimataifa ambayo yalichangia asilimia 59.3 ya deni la nje, ikifuatiwa na mikopo yenye masharti ya kibiashara asilimia 28.6 na mikopo kutoka nchi wahisani iliyochangia asilimia 12.1. Serikali imekuwa ikikopa zaidi kutoka katika mashirika makubwa ya kifedha kwa sababu ya unafuu wa masharti katika mikopo na kutumia mikopo hiyo kugharamia miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi.

Jedwali Na.3.1: Mchanganuo wa Deni la Nje kwa Wakopeshaji


Taasisi	Machi 2015	Mchango kwa %	Machi 2016	Mchango kwa %	Machi 2017	Mchango kwa %	Machi 2018	Mchango kwa %
Mashirika ya Fedha	6,483.36	54.70	7,112.81	55.51	7,834.40	56.8	9,305.80	59.3
Washirika wa Maendeleo	1,028.40	8.68	1,652.80	12.90	1,905.30	13.8	1876.60	12.1
Benki za Kibiashara	4,341.70	36.63	4,048.30	31.59	4,044.20	29.3	4460.50	28.6

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Deni la Ndani

106. Hadi kufikia Machi 2018, deni la ndani la Serikali lilifikia kiasi cha shilingi bilioni 14,158.63 ikilinganishwa na shilingi bilioni 12,073.68 mwezi Machi 2017, sawa na ongezeko la asilimia 17.3. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya Serikali kugharamia miradi ya miundombinu na kukopa kwa ajili ya kulipia mikopo iliyoiva. Kiasi kikubwa cha deni la ndani kilitokana na: Hatifungani za Serikali ambazo zilikuwa sawa na asilimia 59.3; dhamana za Serikali za muda mfupi asilimia 20.6; hatifungani maalum asilimia 9.5 na madeni mengine asilimia 10.6.

Kielelezo Na. 3.2 Mwenendo wa Deni la Ndani



107. Mchanganuo wa deni la ndani la Serikali kwa makundi yaliyokopesha Serikali ulibainisha kuwa benki za biashara zilihodhi sehemu kubwa ya deni hilo. Hadi kufikia Machi 2018, benki za biashara zilikuwa zinahodhi asilimia 48.7 ya deni la ndani. Hii ilichangiwa na kukua kwa sekta ya benki nchini pamoja na athari ndogo ya kuikopesha Serikali ikilinganishwa na sekta binafsi. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ilihodhi asilimia 34.2, taasisi za fedha asilimia 1.2, kampuni za bima asilimia 10.1, mashirika madogo asilimia 2.2 na watu binafsi asilimia 3.6.

Jedwali Na. 3.2: Deni la Ndani kwa Wakopeshaji hadi Machi 2018

Taasisi	Machi 2015	Mchango kwa %	Machi 2016	Mchango kwa %	Machi 2017	Mchango kwa %	Machi 2018	Mchango kwa %
Benki za Biashara	4,446.27	64.81	4,859.48	64.60	4,578.83	49.1	5,417.34	48.7
Taasisi za Fedha	111.32	1.62	117.63	1.56	145.75	1.6	128.10	1.2
Mifuko ya Jamii	1,383.98	20.17	1,383.98	18.40	2995.30	32.1	3,805.40	34.2
Kampuni za Bima	676.49	9.86	798.75	10.62	1105.75	11.9	1,123.77	10.1
Mashirika Mdogo	106.56	1.55	187.13	2.49	193.83	2.1	245.82	2.2
Watu binafsi	136.04	1.98	175.55	2.33	297.70	3.2	397.92	3.6
Jumla	6,860.66	100.00	7,522.52	100.00	9,317.16	100.0	11,118.35	100.00

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Tathmini ya Uhimilivu wa Deni

108. Katika kuendelea kusimamia deni la Serikali, Tathmini ya Uhimilivu wa Deni ilifanyika mwezi Novemba, 2017 kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni:- uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa; uwiano wa deni halisi kwa mauzo ya nje; na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje. Matokeo ya uchambuzi yalionesha kuwa, deni la Serikali ni himilivu kwa kipindi cha muda wa kati na mrefu, kwa kuwa viashiria vyote vilionesha kuwa chini ya ukomo.

109. Katika Tathmini hiyo, viashiria vya deni vilionesha kuwa kwa mwaka 2017/18: thamani ya sasa ya deni la nje (Present Value) kwa Pato la Taifa ilikadiriwa kuwa asilimia 19.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya deni la nje kwa mauzo ya nje ilikuwa asilimia 81.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; thamani ya deni la nje kwa mapato ya ndani asilimia 117.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250; ulipaji wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na mauzo nje asilimia 9.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ulifikia asilimia 13.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Kwa kuzingatia hali hiyo, nchi bado ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili

kugharamia shughuli zake za maendeleo na ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo nje. Hata hivyo, Serikali inazingatia nidhamu ya matumizi ya mikopo na kukopa kutoka kwenye vyanzo vyenye masharti na gharama nafuu.

Jedwali Na.3.3: Tathmini ya Viashiria vya Deni la Taifa

VIASHIRIA VYA DENI LA NJE	Ukomo	2017/18	2018/19	2019/20	2027/28	2028/29	2036/37	2037/38
Deni (PV[1]) /Pato la Taifa	40	19.7	19.8	19.0	12.6	12.5	12.7	12.8
Deni (PV) / uuzaji wa bidhaa nje	150	81.8	83.2	80.7	56.7	56.3	57.4	57.8
Deni (PV) / Mapato ya ndani	250	117.1	117.3	110.1	67.3	66.7	64.5	64.7
Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje	20	9.3	8.2	10.1	6.6	6.5	5.9	6.0
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	20	13.3	11.6	13.8	7.7	7.5	6.6	6.7
VIASHIRIA VYA DENI LA NJE NA LA NDANI	Ukomo	2017/18	2018/19	2019/20	2027/28	2028/29	2036/37	2037/38
Deni (PV) /Pato la Taifa	56	34.4	33.0	31.2	20.5	20.2	19.7	19.0
Deni (PV) / Mapato ya ndani	N/A	194.5	183.9	170.7	107.8	105.9	99.2	95.0
Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani	N/A	26.3	23.0	25.2	13.8	13.6	11.6	11.7

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango


MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 23

Sh.milioni

	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17	2017/18	2017/18	2017/18
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Bajeti	Matokeo hadhi Machi	Matarajio hadhi Juni
A. MAPATO YA NDANI (yakijumuisha Halmashauri)	10,182,455	10,957,765	14,048,034	16,639,831	19,977,001	13,535,730	18,188,897
MAPATO YA NDANI	9,867,227	10,597,681	13,622,182	16,128,113	19,289,695	13,138,515	17,639,052
1. Mapato yatokanayo na Kodi	9,294,417	9,891,680	12,410,951	14,055,173	17,106,336	11,546,889	15,455,693
Ushuru wa Forodha na Excise Duty	2,243,413	2,495,082	3,090,110	3,116,298	3,885,921	2,462,238	3,497,329
Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)	2,647,665	3,031,828	3,553,637	3,979,473	5,100,232	3,405,479	4,430,404
Bidhaa toka nje	1,329,477	1,519,939	1,717,902	1,803,667	2,181,743	1,500,685	1,745,394
Bidhaa za ndani	1,318,188	1,511,889	1,835,735	2,175,806	2,918,489	1,904,795	2,685,010
Kodi ya Mapato	3,791,713	3,727,934	4,608,245	4,832,759	5,817,928	3,909,722	5,352,494
Kodi nyingine	1,123,779	1,278,648	1,921,459	2,216,357	2,538,682	1,809,749	2,335,588
Marejesho (Refunds Accounts)	(512,153)	(641,811)	(762,499)	(89,714)	(236,427)	(40,299)	(160,121)
2. Mapato yasiyotokana na Kodi	572,810	706,001	1,211,231	2,072,941	2,183,359	1,591,626	2,183,359
3. Mapato ya Halmashauri	315,228	360,084	425,852	511,718	687,306	397,215	549,845
B. JUMLA YA MATUMIZI	13,958,162	14,603,714	17,759,598	18,898,690	25,581,106	20,254,863	24,775,032
1. Matumizi ya Kawaida	10,032,120	10,893,486	13,420,045	11,625,866	13,581,514	15,655,660	13,120,250
2. Matumizi ya Maendeleo	3,926,042	3,710,228	4,339,553	7,272,824	11,999,592	4,599,203	11,654,782
Fedha za ndani	2,121,212	2,264,506	2,904,530	5,141,451	8,969,747	4,193,018	9,316,866
Fedha za nje	1,804,831	1,445,722	1,435,023	2,131,374	3,029,845	406,186	2,337,916
C. NAKISI/SALIO (A-B)	(3,775,707)	(3,645,949)	(3,711,564)	(2,258,859)	(5,604,105)	(6,719,133)	(6,586,136)
D. KUZIBA NAKISI	3,775,707	3,645,949	3,711,564	2,258,859	5,604,105	6,719,133	6,586,136
1. Fedha kutoka nje	3,858,785	3,030,875	3,982,100	2,797,488	4,125,815	946,134	2,542,981
Ruzuku	1,399,025	896,496	1,349,799	923,512	843,217	600,507	797,713
Basket support	188,623	127,637	81,073	168,984	200,621	109,444	177,799
Mikopo ya uagizaji bidhaa/OGL	733,822	537,881	546,846	257,473	849,068	71,078	343,202
Mikopo ya miradi	524,019	640,724	344,800	1,124,190	1,820,576	856,862	1,197,563
Mikopo ya masharti ya kibiashara	1,194,516	1,054,803	2,142,469	1,226,760	1,594,985	347,856	1,374,000
Kulipia madeni ya nje (Amortization Foreign)	(181,220)	(226,667)	(482,887)	(903,431)	(1,182,651)	(1,039,613)	(1,347,296)
2. Fedha za Ndani	(83,078)	615,075	(270,536)	(538,629)	1,478,290	5,772,999	4,043,155
Mikopo isiyo ya mabenki	21,216	-	776,945	989,283	122,067	400,957	119,937
Mikopo ya mabenki	205,526	799,776	1,522,207	(1,100,145)	1,098,601	(897,018)	1,079,436
Mikopo ya ndani (Rollover)	1,528,153	2,064,756	2,600,000	4,615,670	4,948,229	3,805,964	4,835,199
Mapato ya Ubinafsishaji	-	-	-	-	-	-	-
Marekebisho (Adjustment to Cash)	300,810	62,959	(2,500,270)	(368,120)	257,622	6,340,827	2,843,782
Kulipia madeni ya ndani (amortization)	(1,528,153)	(2,064,756)	(2,600,000)	(4,615,670)	(4,948,229)	(3,805,964)	(4,835,199)
Expenditure float	(610,630)	(247,661)	(69,418)	(59,647)	-	(71,768)	-

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango



MGAWANYO WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA HUDUMA ZA SERIKALI										
Shs Milioni										
Jedwali Na. 24										
Fungu	Maelezo	2015/2016 (Bajeti)			2016/2017 (Bajeti)			2017/2018 (Makadirio)		
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
701	Huduma za Kawaida	8019045	365537	8384582	9380484	591420	9971904	11002231	2269530	13271761
70111	Utawala na Shughuli za Bunge	722497	121329	843826	663043	240438	903482	636255	419169	1057424
70112	Fedha na Masuala ya Kodi	220012	16867	236879	261846	22568	284415	446213	1380668	1826882
70113	Mambo ya Nje	155709	1484	157193	102571	4476	107047	131033	8000	139033
70121	Misaada ya Kiuchumi kutoka Nje	1081	0	1081	0	0	0	0	0	0
70122	Misaada ya Kiuchumi kupitia Mashirika ya Kimataifa	130	0	130	265	0	265	507	0	507
70131	Huduma za Umma	106836	1166	108002	125847	11257	137104	132391	33767	166158
70132	Huduma za Mipango na Takwimu	49963	24065	74028	26467	9847	36315	122732	8523	131254
70133	Huduma nyingine za Kawaida	18979	198403	217382	34522	292082	326605	30239	388577	418816
70140	Utafiti wa Msingi	14	0	14	9	0	9	25	0	25
70150	Utafiti na Maendeleo Huduma za Umma	0	0	0	549	0	549	289	0	289
70160	Huduma za Umma zisizotajwa hapo juu	284059	0	284059	36450	8872	45322	24761	25965	50726
70170	Deni la Taifa	6456800	0	6456800	8126330	0	8126330	9472122	0	9472122
70180	Uhamishaji Fedha Ndani ya Serikali	2963	2223	5186	2584	1879	4463	3664	4860	8525
702	Ulinzi	1379250	279094	1658344	1413575	154311	1567887	1505662	218750	1724412
70210	Huduma za Ulinzi wa Kijeshi	1379250	279094	1658344	1412904	154311	1567216	1504956	218750	1723706
70220	Huduma za Ulinzi wa Kiraia	0	0	0	192	0	192	229	0	229
70230	Misaada ya Nje ya Ulinzi	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70240	Utafiti na Maendeleo ya Ulinzi	0	0	0	479	0	479	477	0	477
70250	Huduma za Ulinzi zisizotajwa hapo juu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
703	Usalama wa Raia	734684	17029	751713	709985	52002	761987	856199	59430	915628
70310	Huduma za Polisi	648956	4066	653022	627535	31098	658633	663307	12754	676061
70320	Huduma za Zimamoto	11373	0	11373	8830	0	8830	10407	0	10407
70330	Mahakama	58991	12963	71954	48230	15713	63943	137275	19476	156751
70340	Magereza	13999	0	13999	23786	5191	28977	32162	7200	39362
70350	Huduma za utafiti na Maendeleo Usalama wa Raia	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70360	Huduma Usalama wa Raia zisizotajwa hapo juu	1365	0	1365	1605	0	1605	13048	20000	33048
704	Shughuli za Kiuchumi	4189694	2483691	6673385	4162196	4452471	8614667	4776429	6948700	11725129
70411	Shughuli za Kiuchumi na Biashara	29929	3894	33823	35944	1152	37096	21439	6043	27482
70412	Masuala ya Kazi	10714	1455	12169	11125	13878	25003	14623	20846	35469
70421	Kilimo	3850951	319530	4170481	3804050	434551	4238601	4378418	1417520	5795938
70422	Misitu	14508	1162	15670	20137	2200	22337	52048	7591	59639
70423	Uvuvi na Uwindaji	6709	92	6801	5499	682	6181	14793	2000	16793
70431	Makaa ya Mawe na Nishati nyingine	4744	0	4744	5841	0	5841	5078	2380	7458
70432	Petroli na Gesi Asilia	14178	784752	798930	13674	726568	740242	18776	916849	935625
70433	Nishati ya Nyukilia	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70434	Nishati nyingine	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70435	Umeme	236	0	236	0	0	0	0	0	0
70436	Nishati isiyo ya umeme	6974	0	6974	23130	0	23130	6068	0	6068
70441	Uchimbaji Madini yasiyo Nishati	30429	1921	32350	22428	445	22873	28535	24047	52582
70442	Uzalishaji Viwandani	3097	3389	6486	3189	8663	11851	1222	71460	72682
70443	Ujenzi	73018	11428	84446	38867	42948	81814	28880	33713	62594
70451	Usafiri wa Barabara	114539	1295553	1410092	104044	1787428	1891472	106593	2275810	2382403
70452	Usafiri wa Majini	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70453	Usafiri wa Reli	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70454	Usafiri wa Anga	282	40287	40569	108	1411334	1411443	334	2064219	2064553
70455	Usafirishaji kwa njia ya Bomba na njia nyingine za usafiri	2180	4231	6411	1090	0	1090	1537	8285	9822
70460	Mawasiliano	3917	300	4217	13043	417	13460	8734	10900	19634
70471	Huduma za Biashara na Utunzaji Mizigo	2849	3435	6284	5523	8808	14331	31642	26350	57992
70472	Hoteli na Migahawa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70473	Utalii	8986	0	8986	12438	0	12438	14260	0	14260
70474	Miradi ya Maendeleo	4132	6597	10729	35544	10763	46307	36385	43870	80254
70481	Utafiti katika shughuli za Kiuchumi, Biashara na Kazi	204	522	727	4	7	11	41	250	291
70482	Utafiti na Maendeleo ya Kilimo, Misitu, Uvuvi na Uwindaji	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70483	Utafiti na Maendeleo ya Mafuta na Nishati	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70484	Utafiti na Maendeleo ya Uchimbaji Madini, Uzalishaji	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70484	Viwandani na Ujenzi	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70485	Utafiti na Maendeleo ya Usafiri	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70486	Utafiti na Maendeleo ya Mawasiliano	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70487	Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Vingine	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70490	Shughuli nyingine za Kiuchumi zisizotajwa hapo juu	7117	5142	12259	6518	2628	9146	7024	16567	23590

Jedwali Na. 24 linaendelea										
Fungu	Maelezo	2015/2016 (Bajeti)			2016/2017 (Bajeti)			2017/2018 (Makadirio)		
		Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla	Matumizi ya kawaida	Matumizi ya Maendeleo	Jumla
705	Hifadhi ya Mazingira	28921	7583	36503	28331	6611	34942	33481	66608	100089
70510	Hifadhi ya Taka	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70520	Hifadhi ya Maji Taka	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70530	Kupunguza Uharibifu wa Mazingira	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70540	Hifadhi ya Viumbehai na Mazingira	20571	0	20571	19854	0	19854	23652	42712	66363
70550	Utafiti na Maendeleo ya Hifadhi ya Mazingira	268	0	268	249	0	249	302	2500	2802
	Huduma nyingine za Hifadhi ya Mazingira zisizotajwa hapo juu	8082	7583	15664	8228	6611	14840	9528	21396	30924
706	Nyumba na Huduma za Jamii	48518	159204	207722	55316	233966	289281	52869	619953	672822
70610	Maendeleo ya Nyumba	15575	23132	38708	16351	7000	23351	15720	4400	20120
70620	Maendeleo ya Jamii	15512	1203	16715	15777	612	16389	17717	1566	19283
70630	Usambazaji Maji	16960	134868	151828	22765	226259	249024	18711	610187	628898
70640	Taa za Barabarani	471	0	471	423	95	518	722	3800	4522
70650	Utafiti wa Nyumba na Maendeleo ya Jamii	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70660	Nyumba na Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
707	Afya	357708	135579	493287	344363	370194	714557	370067	815910	1185977
70711	Madawa	29877	0	29877	45	142728	142773	167	236410	236577
70712	Bidhaa nyingine za madawa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70713	Huduma za Tiba na Vifaa vya Tiba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70721	Huduma za Tiba za Jumla	206826	7782	214608	192483	13530	206013	205977	62972	268949
70722	Huduma Maalumu za Tiba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70723	Huduma za Meno	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70724	Huduma za Wakunga Wasaidizi	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70731	Huduma za Hospitali	25357	279	25635	25207	1961	27168	26086	3342	29428
70732	Huduma za Hospitali Maalumu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70733	Huduma za Vifaa vya Kujifungulia Wajawazito	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70734	Huduma za Wakunga na Wakunga wa Jaji	74	0	74	75	0	75	321	0	321
70740	Huduma za Afya	40195	92257	132452	47228	158964	206192	73271	389506	462777
70750	Utafiti na Maendeleo ya Huduma za Afya	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70760	Huduma za Afya zisizotajwa hapo juu	55378	35262	90640	79325	53010	132335	64243	123681	187924
708	Burudani, Utamaduni na Dini	13011	1000	14011	15682	1061	16743	17746	5820	23566
70810	Huduma za Burudani na Michezo	1324	0	1324	1108	61	1169	1476	1820	3296
70820	Huduma za Utamaduni	3858	0	3858	3450	0	3450	4595	0	4595
70830	Huduma za Utangazaji na Uchapishaji	7559	1000	8559	10596	1000	11596	11375	3000	14375
70840	Dini na Huduma nyingine za Kijamii	0	0	0	250	0	250	300	1000	1300
70850	Utafiti na Maendeleo katika Burudani, Utamaduni na Dini	0	0	0	0	0	0	0	0	0
	Huduma nyingine za Burudani, Utamaduni na Dini zisizotajwa hapo juu	271	0	271	278	0	278	0	0	0
709	Elimu	674800	522648	1197449	697615	620438	1318053	748057	933047	1681104
70911	Elimu ya Awali	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70912	Elimu ya Msingi	18797	14987	33785	20037	16574	36611	24552	14965	39517
70921	Elimu ya Sekondari (Kidato cha I - IV)	312	7595	7908	289	5826	6115	352	0	352
70922	Elimu ya Sekondari (Kidato cha V - VI)	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70930	Elimu baada ya Sekondari isiyo ya Chuo Kikuu	424	188	612	393	0	393	502	2273	2775
70941	Daraja la Awali Elimu ya Chuo Kikuu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
70942	Daraja linalofuata Elimu ya Chuo Kikuu	2310	0	2310	1487	0	1487	2398	0	2398
70950	Elimu isiyopambanuliwa	225555	16270	241825	236424	18233	254656	309051	29638	338689
70960	Huduma za Ziada kwa Elimu	422008	483607	905615	426554	579805	1006359	389571	885671	1275242
70970	Utafiti na Maendeleo ya Elimu	0	0	0	6316	0	6316	12422	0	12422
70980	Huduma za Elimu zisizotajwa hapo juu	5393	0	5393	6115	0	6115	9209	500	9709
710	Kinga ya Jamii	303979	12978	316957	328700	15829	344530	335978	48246	384224
71011	Ugonjwa	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71012	Ulemavu	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71020	Wazee	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71030	Waathirika	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71040	Familia na Watoto	148158	9420	157577	147706	14474	162180	164743	45196	209939
71050	Ukosefu wa Ajira	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71060	Nyumba	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71070	Huduma za Jamii zisizotajwa hapo juu	499	1918	2418	528	0	528	697	0	697
71080	Utafiti na Maendeleo ya Kinga ya Jamii	0	0	0	0	0	0	0	0	0
71090	Huduma za Kinga ya Jamii zisizotajwa hapo juu	155323	1640	156962	180466	1355	181821	170538	3050	173588
Jumla Kuu		15749611	3984342	19733953	17136246	6498304	23634550	19698720	11985992	31684712

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
CS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni watu wote
IS: Huduma za umma zinazotolewa na serikali na wanufaika ni wanakaya

SURA YA 4

SEKTA YA NJE

Urari wa Malipo Yote

110. Mwaka 2017, urari wa malipo yote ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,649.5 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 mwaka 2016. Ongezeko hili la ziada lilitokana kwa sehemu kubwa na kupungua kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida pamoja na kuongezeka fedha kwa ajili ya misaada ya maendeleo pamoja na mikopo kutoka nje.


Akiba ya Fedha za Kigeni

111. Akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 5,906.2 mwezi Desemba 2017 ikilinganishwa na dola milioni 4,325.6 Desemba 2016. Kiasi hicho kilikuwa na uwezo wa kulipia bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.4. Aidha, akiba ya fedha za kigeni katika benki za biashara ilikuwa dola za Marekani milioni 726.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 768.2 zilizoripotiwa Desemba 2016.

Urari wa Biashara ya Huduma

112. Urari wa biashara ya huduma ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 1,909.7 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 38.8. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za huduma kama vile usafiri na usafirishaji hususan biashara ya utalii sambamba na kupungua kwa malipo ya usafirishaji kufuatia kupungua kwa uagizaji bidhaa kutoka nje. Mapato ya huduma yalikuwa kwa asilimia 8.9 hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,927.6 kutokana na kuongezeka kwa utalii na mapato ya usafirishaji. Mapato ya utalii yaliongezeka kwa dola za Marekani milioni 207.6 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,339.2 kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wanaoingia nchini ikiwa ni matokeo ya kuongezeka kwa juhudi za Serikali na sekta binafsi za kuutangaza utalii. Mapato yatokanayo na huduma za usafirishaji yaliongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 1,147.9 mwaka 2017 kutoka dola milioni 1,061.8 mwaka 2016 kufuatia kuongezeka kwa bidhaa zilizosafirishwa baina ya Tanzania na nchi jirani kulitokana na kuongezeka kwa ufanisi katika bandari ya Dar es salaam.


Kielelezo Na. 4.1: Mapato ya Huduma - Dola za Marekani (milioni)



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

113. Mwaka 2017, malipo ya huduma yalipungua kwa asilimia 9.6 hadi kufikia dola za Marekani milioni 2,017.9 ikilinganishwa na malipo yaliyofanywa mwaka 2016. Upungufu huu ulitokana kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa malipo nje ya nchi yanayohusiana na usafirishaji, hususan mizigo. Sambamba na kupungua kwa bidhaa zilizoagizwa nchini, malipo ya huduma za usafirishaji ambazo kwa kiasi kikubwa zinachangia huduma za malipo, zilipungua kwa asilimia 18.0 hadi kufikia dola za Marekani milioni 778.3

Kielelezo Na. 4.2: Malipo ya Huduma - Dola za Marekani (milioni)



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi

114. Urari wa mapato ya vitega uchumi ambayo yanajumuisha mapato ya uwekezaji na malipo kwa wafanyakazi uliongezeka hadi kufikia nakisi ya dola za Marekani milioni 1,206.8 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 1,109.7 mwaka 2016. Kuongezeka nakisi ya urari wa mapato ya vitega uchumi kulitokana na kuongezeka kwa malipo yaliyohusiana na uwekezaji wa moja kwa moja.

Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida

115. Urari wa uhamisho mali wa kawaida unaojumuisha uhamisho wa fedha baina ya wakazi na wasio wakazi nchini ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 402.0 ikilinganishwa na ziada ya dola milioni 381.5 katika mwaka uliotangulia. Hali hiyo ilitokana na kuongezeka uhamisho rasmi wa fedha ambao ulionesha ukuaji wa mwaka wa asilimia 50.1 kufikia dola za Marekani milioni 121.8 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa mwaka 2016.

Urari wa Malipo ya Kawaida

116. Mwaka 2017, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma, mapato ya vitega uchumi na uhamisho mali wa kawaida ilipungua kwa asilimia 43.8 na kufikia dola za Marekani milioni 1,210.5, ikilinganishwa na dola 2154.6 mwaka 2016. Upungufu huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kushuka kwa uagizaji bidhaa kutoka nje na malipo ya huduma pamoja na ongezeko la fedha za msaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Thamani ya Shilingi ya Tanzania

117. Katika mwaka 2017, thamani ya shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa imara. Katika kipindi hicho, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,228.86 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 2,177.07 katika mwaka 2016. Mwenendo huu unaashiria kuwa thamani ya shilingi ilipungua kwa kasi ndogo ya asilimia 2.4 ikilinganishwa na asilimia 9.7 mwaka 2016.

THAMANI YA BIDHAA ZA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.25

Shs. Milioni

Aina ya Bidhaa	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Zilizouzwa Nje	4,027,798	5,343,693	7,331,020	8,653,372	8,223,206	11,366,503	10,725,753	12,387,829	8,924,522
Bidhaa Halisi	3,872,289	5,165,013	7,175,377	8,363,496	7,012,100	9,429,219	9,959,761	11,342,534	8,638,133
Zilizouzwa Tena	155,509	178,680	155,643	289,875	1,211,106	1,937,284	765,992	1,045,294	286,388
Zilizoagizwa	8,619,837	11,131,917	17,112,779	18,275,893	19,904,472	20,977,104	21,475,090	20,660,282	17,380,607
Jumla	12,647,635	16,475,610	24,443,799	26,929,265	28,127,678	32,343,607	32,200,843	33,048,111	26,305,128
Urari	(4,592,039)	(5,788,224)	(9,781,759)	(9,622,521)	(11,681,266)	(9,610,601)	(10,749,337)	(8,272,453)	(8,456,085)
Thamani ya Fedha (Shs/US\$)	1,320.30	1,395.68	1,557.43	1,571.71	1,598.66	1,652.51	1,985.39	2,177.59	2,228.63

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Idara ya forodha na Benki Kuu ya Tanzania

KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 26

Bidhaa	Kiasi(000" Tani)						Thamani(sh. Milioni)					
	2013	2014	2015	206	2017	Badiliko(%) 2016/17	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%) 2016/17
Kahawa	59.5	44.1	51.9	60.3	42.1	-30.1	259,132	204,301	315,921	335,629	282,427	-15.9
Pamba	89.0	49.5	29.1	33.0	25.0	-24.2	137,663	558,404	62,959	101,816	80,259	-21.2
Katani	12.6	11.5	1.5	1.4	16.3	1064.4	25,396	111,323	53,927	37,524	57,703	53.8
Chai	28.8	29.2	27.5	26.4	27.5	4.3	86,810	72,784	86,285	97,381	108,990	11.9
Tumbaku	67.8	67.4	66.3	66.1	48.3	-27.0	159,454	319,295	568,812	680,453	434,456	-36.2
Korosho	147.3	172.2	171.7	169.2	331.1	95.7	301,212	647,936	430,023	587,849	1,200,450	104.2
Karafuu	4.1	4.7	2.8	4.9	6.9	40.8	68,429	50,880	48,912	85,454	121,237	41.9
Almasi (Carat)	173,464	241,709	185,873	235,951	282,032	19.5	63,584	166,107	65,636	186,254	142,998	-23.2
Dhahabu(gms)	35,100,000	41,813,100	48,394,953	81,561,000	54,660,377	-33.0	2,768,481	2,812,561	2,717,187	3,072,728	3,418,902	11.3

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA

- Takwimu hazikupatikana


KIASI NA THAMANI YA BIDHAA ZA ASILIA NA ZISIZO ZA ASILIA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 27


Bidhaa	Kiasi (000" Tani)						Badiliko(%)	Thamani (Milioni US\$)						Badiliko (%)	
	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2016/17	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2016/17	
Bidhaa Asilia:															
Kahawa	54.8	59.5	44.1	51.9	60.3	42.1	(30.1)	186.6	171.0	121.5	162.2	154.2	127.2	-17.5	
Pamba	132.0	89.0	49.5	29.1	33.0	25.0	(24.2)	164.9	111.7	54.7	30.2	46.8	36.0	-23.2	
Katani	13.5	12.6	11.5	1.5	1.4	16.3	1,064.4	18.4	16.9	16.8	26.5	17.2	25.7	49.7	
Chai	27.2	28.8	29.2	27.5	26.4	27.5	4.3	56.1	56.9	45.7	44.0	44.7	49.0	9.5	
Tumbaku	105.6	67.8	67.4	66.3	66.1	48.3	(27.0)	350.1	307.0	315.0	287.6	312.7	195.8	-37.4	
Koroshu	130.9	147.3	172.2	171.7	169.2	331.1	95.7	142.6	162.4	222.2	218.8	270.6	541.8	100.2	
Karafuu	3.4	4.1	4.7	2.8	4.9	6.9	146.4	38.1	43.0	52.9	24.1	39.3	54.4	38.4	
Jumla								956.8	868.9	828.8	793.4	885.5	1029.8	16.3	
Bidhaa zisizo asilia:															
Madini								2197.8	1782.1	1469.2	1285.4	1574.5	1629.5	3.5	
Bidhaa za Viwanda								1037.3	1072.1	1239.6	1364.5	1092.1	819.6	-25.0	
Samaki na Mazao ya Samaki								160.6	130.6	195.0	173.5	142.5	192.8	35.3	
Mazao ya Mboga na Maua								31.3	28.1	30.5	24.4	24.8	27.1	9.3	
Bidhaa zilizouzwa tena								181.7	172.8	177.0	385.8	480.0	237.6	-50.5	
Bidhaa nyinginezo								557.7	517.6	687.2	884.3	972.2	486.1	-50.0	
Jumla								4166.4	3703.3	3798.5	4117.9	4286.1	3392.7	-20.8	
Bidhaa Zisizorekodiwa								768.2	685.8	694.1	491.1	0.0	517.2	-	
JUMLA KUBWA								5891.4	5258.0	5321.4	5402.4	5171.6	4939.7	-4.5	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Idara ya forodha, TRA


I: BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA ZILZOUZWA NCHI ZA NJE
(US\$ Milioni)




II: PAMBA NA KAHAWA ILIYOUZWA NCHI ZA NJE
(Kiasi kwa Tani '000)



IIIA: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2016



III B: MCHANGO WA BIDHAA ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE - 2017



WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 28

Sh./Tani*

Bidhaa	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%) 2016/17
Kahawa	2,628,934	4,069,399	5,580,087	5,400,679	4,135,909	4,284,297	6,084,327	5,563,694	6,703,080	20.5
Pamba	1,462,236	1,775,008	1,431,997	1,724,164	2,016,331	4,196,444	2,164,592	3,080,982	3,210,269	4.2
Katani	1,951,011	1,986,211	2,091,121	2,102,332	2,129,059	2,052,892	3,554,124	2,473,086	3,539,730	43.1
Chai	2,373,683	2,501,897	2,664,933	3,144,333	3,392,989	2,617,376	3,139,968	3,543,747	3,956,329	11.6
Tumbaku	4,970,800	2,586,996	2,564,562	3,145,641	2,237,711	4,172,482	8,576,002	10,259,213	8,998,738	-12.3
Koroshu	950,656	1,284,308	1,636,560	1,695,963	1,943,340	3,255,142	2,503,867	3,422,830	3,625,943	5.9
Karafuu	4,008,131	4,390,290	20,972,246	9,783,616	16,735,615	17,997,878	17,576,080	17,439,592	17,570,634	0.8
Almasi (kwa carat)	157,319	38,695	40,709	99,809	353,966	317,548	353,123	789,375	507,027	-35.8
Dhahabu (kwa gramu)	40,826	60,038	85,738	89,993	78,874	64,709	56,146	37,674	62,548	66.0

Chanzo: Idara ya Forodha, Mamlaka ya Mapato Tanzania

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu

WASTANI WA BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE


Jedwali Na. 29

US\$/Tani*

Bidhaa	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	US\$/Tani*
										Badiliko(%) 2016/17
Kahawa	1,991	2,853	3,655	3,403	2,873	2,756	3,123	2,557	3,019	18.1
Pamba	1,108	1,242	1,529	1,250	1,256	1,105	1,038	1,416	1,438	1.6
Katani	980	940	1,224	1,357	3,142	1,460	1,749	2,002	1,579	-21.1
Chai	1,542	1,840	1,740	2,061	1,978	1,568	1,601	1,696	1,777	4.8
Tumbaku	3,762	4,337	3,839	3,316	4,526	4,673	4,336	4,732	4,056	-14.3
Korosho	720	963	1,110	1,089	1,103	1,291	1,274	1,599	1,636	2.3
Karafuu	3,036	3,450	13,163	11,189	10,563	11,231	8,653	7,976	7,884	-1.2
Almasi (kwa carat)	1,193	3,028	2,395	2,188	208	187	178	361	228	-37.0
Dhahabu (kwa gramu)	35	43	55	57	35	38	28	17	28	62.8

Chanzo: Idara ya forodha, TRA

* Isipokuwa kwa almasi na dhahabu



AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA TOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 31

Sh. Milioni

Mwaka	Bidhaa za Matumizi ya Kawaida	Bidhaa za Kati	Bidhaa za Viwanda	Jumla
2000	401612	222399	444427	1068438
2001	468173	386317	648361	1502851
2002	499346	408872	697209	1605426
2003	654630	705729	846251	2206610
2004	917953	1024705	1029389	2972046
2005	937031	1451062	1341462	3729555
2006	1068550	1977695	1799855	4846100
2007	1393799	2441781	2186910	6022490
2008	1703932	3217747	3537543	8459222
2009	1836142	2471066	3319331	7626538
2010	2385447	3825823	3789528	10000799
2011	3314193	6446217	5545242	15305652
2012	3634506	6790046	5794109	16218662
2013	3778395	8321394	5532070	17631859
2014	4389188	7706688	5945855	18041732
2015	4632916	7339405	7570108	19542430
2016	4870477	8536607	6603856	20010939

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


*Angalia: Kuanzia mwaka 1990, thamani ya bidhaa zilizoagizwa ni f.o.b. badala ya c.i.f.

MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na.32	US \$ milioni									
	2007	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Matarajio
Urari wa Biashara	-2634.1	-3433.5	-2536.1	-2841.2	-4729.6	-4429.9	-5771.1	-5723.7	-4440.7	-2774.8
Zilizouzwa nje (fob)	2226.6	3578.8	3298.1	4324.3	5097.9	5889.2	5258.1	5194.1	5402.3	5688.8
Zilizonunuliwa toka nje (fob)*	4860.6	7012.3	5834.1	7165.5	9827.5	10319.1	11029.1	10917.8	9843.1	8463.6
Urari wa Huduma	462.1	336.9	132.7	156.9	92.2	427.5	713.2	727.3	846.0	1455.5
Mapato	1875.7	1998.8	1854.6	2045.7	2300.3	2786.4	3201.7	3396.0	3515.8	3596.8
Malipo	1413.7	1661.9	1722.0	1888.9	2208.1	2358.9	2488.5	2668.7	2669.7	2141.3
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-282.1	-314.3	-297.8	-577.6	-645.8	-574.0	-705.7	-824.7	-900.2	-1066.7
Yaliyoingia	107.3	122.7	161.1	160.1	184.2	131.1	130.1	118.4	110.3	93.5
Yaliyotoka	389.4	437.0	458.9	737.651	830.0	705.1	835.8	943.1	1010.5	1160.2
Urari wa Uhamisho Mali wa Kawaida	651.5	833.8	891.2	1051.2	902.2	807.5	807.9	477.4	532.0	372.3
Iliyoingia	724.0	913.4	959.7	1130.2	994.9	913.0	869.6	535.6	612.2	443.5
Serikalini	626.9	588.5	658.4	798.1	609.7	544.3	517.9	178.0	246.9	63.3
Sekta nyingine	97.1	324.9	301.3	332.1	385.2	368.7	351.7	357.6	365.3	380.2
Iliyotoka	72.5	79.6	68.4	79.0	92.7	105.4	61.8	58.2	80.2	71.2
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali	-1802.6	-2577.1	-1809.9	-2210.8	-4381.0	-3768.9	-4955.7	-5343.7	-3962.9	-2013.8
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	938.5	524.2	442.2	537.9	690.9	777.2	658.8	522.2	354.4	327.8
Iliyoingia	938.5	524.2	442.2	537.9	690.9	777.2	658.8	522.2	354.4	327.8
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	873.0	2592.8	1984.4	3063.7	2843.3	3879.6	5021.0	3499.9	3157.7	2059.1
Uwekezaji katika miradi	581.5	1383.3	952.6	1813.2	1229.5	1799.6	2087.3	1672.6	1604.6	1365.4
Uwekezaji katika hisa	4.3	1.8	3.5	3.1	11.3	6.1	4.5	11.5	27.6	-5.0
Uwekezaji aina nyingine	287.1	1207.8	1028.3	1247.4	1602.5	2073.9	2929.3	1815.9	1525.5	698.8
Makosa na Masahihisho	307.8	-391.9	-250.5	-1282.3	-325.2	-561.8	-215.8	1069.5	251.8	-67.6
Urari wa Malipo yote	316.7	148.0	366.2	108.5	-1171.9	326.2	508.2	-252.2	-199.0	305.5

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

* Kuanzia mwaka 2006 bidhaa zilizouzwa nje zinajumuisha pia zile zisizorekodiwa (Unrecorded trade)



SURA YA 5

HALI YA UCHUMI WA DUNIA NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

HALI YA UCHUMI WA DUNIA

Ukuaji wa Uchumi

118. Ukuaji wa uchumi wa dunia uliimarika kutoka katika kusuasua kulikojitokeza mwaka 2016. Uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.1 kwa mwaka 2016. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia ilichangiwa na kuimarika kwa uwekezaji, biashara na uzalishaji viwandani na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ya bidhaa na huduma kwa nchi zilizoendelea na China. Aidha, ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea nao uliimarika.

119. Mwaka 2017, kasi ya ukuaji wa pato la nchi zilizoendelea iliongezeka na kufikia asilimia 2.3 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2016. Hali hii ilitokana na kukua kwa uwekezaji na shughuli za kibiashara kwa nchi ya Marekani, kuongezeka kwa tija kwenye uzalishaji na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ya bidhaa na huduma kutoka nje kwa nchi za Ulaya na Japan.

120. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 4.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 4.1 mwaka 2016. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mahitaji ya ndani ya bidhaa na huduma kutoka nje kwa nchi za Asia ya Mashariki na China na kuimarika kwa uchumi kwa nchi nyingine katika ukanda huo. Kwa upande wa India, kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutokana na athari za marekebisho yaliyofanyika kwenye mfumo wa ubadilishanaji wa fedha za kigeni na kuanzishwa kwa kodi ya huduma na bidhaa. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa pato la nchi za Asia zinazoendelea ikijumuisha China na India ilikuwa asilimia 6.5 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 6.3 mwaka 2016.

Jedwali Na 5.1: Pato la Dunia 2010 – 2017

	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
<i>Ukuaji kwa asilimia</i>								
Pato la Dunia	5.4	4.2	3.5	3.3	3.4	3.2	3.2	3.8
Nchi Zilizozendelea	3.1	1.7	1.2	1.2	1.9	2.1	1.7	2.3
Nchi Zinazozendelea	7.4	6.3	5.3	4.9	4.6	4.1	3.5	4.7
Nchi za Asia Zinazozendelea	9.6	7.8	6.9	6.9	6.8	6.7	6.5	6.5
Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara	6.6	5.0	4.3	5.2	5.1	3.4	1.4	2.8

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), WEO - Aprili, 2018

121. Ukuaji wa Pato la nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ulikuwa asilimia 2.8 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 1.4 mwaka 2016. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta kwa nchi ya Nigeria na Angola na uzalishaji katika sekta ya kilimo kutokana na upatikanaji wa mvua za kutosha. Sababu nyingine ni kuimarika kwa uchumi wa dunia, hususan kwa nchi za Ulaya na China ambazo ni washirika wa kibiashara na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini. Aidha, kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi nyingine kusini mwa Jangwa la Sahara uliongezeka kutokana na hali nzuri ya hewa na kuboreka kwa mazingira ya uchumi duniani. Kwa nchi za kipato cha kati, kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka na kufikia asilimia 1.9 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 0.4 mwaka 2016. Vile vile, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za kipato cha chini iliongezeka hadi asilimia 5.5 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2016.

**Jedwali Na.5.2: Mwenendo wa Baadhi ya Viashiria vya Uchumi kwa
Baadhi ya Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara: 2015 – 2017**

	Ukuaji kwa mwaka			Ukuaji kwa mwaka			Sehemu ya pato la taifa		
	2015	2016	2017	2015	2016	2017	2015	2016	2017
Nchi Kusini mwa Jangwa la Sahara	3.4	1.6	2.8	7.0	11.3	11.0	-5.9	-4.5	-0.1
Nchi zinazouza mafuta	2.6	-1.3	0.5	8.8	18.2	17.2	-4.7	-2.2	6.1
Nigeria	2.7	-1.7	0.8	9.0	15.4	16.5	-3.1	-16.6	2.6
Angola	3.0	0.0	0.7	10.3	33.7	31.7	-8.5	-5.4	13.8
Equatorial Guinea	-7.4	-9.9	-4.4	1.7	1.5	0.7	-16.8	-11.8	26.9
Gabon	4.0	3.2	0.8	0.2	2.5	3.0	-2.3	-5.3	18.7
Republic of Congo	2.3	1.7	-4.6	2.0	4.0	0.5	-21.0	-8.2	27.5
Chad	1.8	-1.1	-3.1	3.7	0.0	-0.9	-12.4	-8.7	3.1
Cameroon	5.8	4.8	3.2	2.7	2.2	0.6	-4.2	-4.2	-0.9
South Sudan	-0.2	-13.1	-11.1	52.8	476.0	187.9	-11.1	-0.5	11.7
Nchi za Kipato cha Kati	2.7	0.4	1.9	7.2	11.8	11.1	-4.5	-3.0	2.3
Botswana	-0.3	3.1	2.2	3.0	3.2	3.3	7.2	4.1	0.2
Cape Verde	1.5	3.6	4.0	0.1	0.1	0.8	-4.3	-7.7	-37.5
Ghana	3.9	3.3	8.4	17.2	17.0	12.4	-7.5	-6.3	2.3
Kenya	5.6	6.0	4.8	6.6	6.2	8.0	-6.8	-6.4	-12.1
Lesotho	2.8	2.4	3.1	5.3	8.6	5.6	-8.7	-8.0	-31.7
Mauritius	3.5	3.5	3.9	1.3	1.5	3.7	-4.9	-4.3	-21.4
Namibia	5.3	4.2	-1.2	3.4	6.6	6.1	-12.9	-12.4	-10.9
Senegal	6.5	6.6	7.2	0.1	1.0	1.4	-7.6	-8.4	-16.3
Seychelles	5.7	4.9	4.2	4.0	-0.8	2.9	-18.6	-18.7	-17.4
South Africa	1.3	0.1	1.3	4.6	6.4	5.3	-4.3	-3.3	1.5
Swaziland	1.7	0.5	0.2	5.0	7.0	6.3	9.2	-4.9	8.7
Zambia	3.0	3.0	3.6	10.1	19.1	6.6	-3.5	-4.5	0.4
Nchi za Kipato cha Chini	5.6	4.7	5.5	6.3	9.5	10.9	-10.7	-9.3	-7.9
Benin	5.0	4.6	5.6	0.3	0.6	2.9	-10.5	-10.0	-7.5
Burkina Faso	4.0	5.2	6.4	0.9	1.6	0.4	-6.4	-6.0	-3.1
Ethiopia	10.2	6.5	10.9	10.1	7.7	9.9	-12.0	-10.7	-15.9
Gambia	4.4	2.3	3.5	6.8	7.2	8.0	-15.2	-12.7	-31.6
Madagascar	3.1	4.1	4.1	7.4	6.7	8.1	-1.9	-2.3	-7.1
Malawi	2.9	2.7	4.0	21.9	19.8	11.5	-8.3	-15.8	-9.4
Mali	6.0	5.3	5.3	1.4	1.0	1.8	-5.1	-6.0	-3.9
Mozambique	6.6	4.5	2.9	2.4	16.7	15.3	-39.0	-33.5	-4.8
Niger	3.5	5.2	5.2	1.0	1.6	2.4	-17.2	-17.8	-8.5
Rwanda	6.9	6.0	6.1	2.5	5.3	4.8	-13.5	-16.6	-9.5
Sierra Leone	-21.1	4.3	3.5	9.0	9.7	18.0	-15.5	-16.2	-17.4
Tanzania	7.0	7.0	7.1	5.6	5.2	5.3	-8.8	-8.8	-5.7
Uganda	4.8	4.9	4.5	5.5	5.5	5.6	-9.4	-8.7	-6.5

Chanzo: Shirika la Fedha Duniani (REO) Aprili 2018

Chanzo: Shirika la Fedha Duniani (IMF), REO - Aprili 2018

Mwenendo wa Bei

122. Mwaka 2017, mfumuko wa bei wa dunia uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na kushuka kwa kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni, kuondolewa kwa ruzuku, kupanda kwa kodi ya ushuru wa bidhaa, kodi ya ongezeko la thamani, na kuongezeka kwa wastani wa bei za bidhaa mbalimbali ikiwemo nishati. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka na kuwa asilimia 1.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 0.8 mwaka 2016. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia ulipungua na kuwa asilimia 2.6 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2016. Kupungua kwa mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea za Asia kulitokana na kushuka kwa bei za vyakula na mafuta.

123. Mwaka 2017, kasi ya ukuaji wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 11.0 ikilinganishwa na asilimia 11.3 mwaka 2016. Kushuka kwa mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kulichangiwa zaidi na kuimarika kwa sera za fedha na kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni pamoja na upatikanaji wa chakula kutokana na hali nzuri ya hewa. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara zinazouza mafuta ulipungua na kufikia asilimia 17.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 18.2 mwaka 2016. Vile vile, mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara za kipato cha kati ulipungua na kufikia asilimia 11.1 ikilinganishwa na asilimia 11.8 mwaka 2016. Kwa upande wa nchi za kipato cha chini za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei uliongezeka hadi wastani wa asilimia 10.9 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 9.5 mwaka 2016.

Mwenendo wa Biashara Duniani

124. Ukuaji wa shughuli za biashara duniani uliimarika na kutoka katika hali ya kudhoofika ambapo kasi yake ilikuwa asilimia 4.7 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka 2016. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje na mahitaji ya huduma na bidhaa hususan kwa nchi za Asia na Marekani na kupanda kwa bei ya bidhaa ghafi zinazouzwa nje kwa nchi zinazoendelea. Aidha, ukuaji wa uchumi wa Marekani na China na kuongezeka kwa uwekezaji kwa nchi ya Marekani kulisababisha ongezeko la mahitaji ya huduma na bidhaa kutoka nje na hivyo kuimarisha shughuli za biashara duniani.

Jedwali Na.5.3: Mwenendo wa Biashara Duniani 2017 (USD Bilioni na Asilimia)

	Mauzo ya Nje					Manunuzi kutoka Nje				
	Thamani	Badiliko kwa mwaka (Asilimia)				Thamani	Badiliko kwa mwaka (Asilimia)			
	2017	2010-17	2015	2016	2017	2017	2010-17	2015	2016	2017
Dunia	17,198	2.1	-13.2	-3.0	10.7	17,572	2.1	-12.5	-2.9	10.7
Amerika ya Kaskazini	2,377	2.8	-0.8	-3.4	7.3	3,285	2.9	-4.5	-2.8	7.3
Marekani	1,547	2.8	-7.3	-3.4	6.6	2,409	2.9	-4.0	-2.8	7.1
Canada	421	1.2	-13.9	-4.8	7.8	442	1.3	-9.6	-3.7	7.0
Mexico	409	4.6	-4.1	-1.7	9.5	432	4.9	-1.5	-1.9	8.7
Amerika ya Kusini na Kati	583	-0.2	-21.0	-4.9	13.0	579	-0.2	-16.3	-14.2	7.8
Brazil	218	1.1	-15.1	-3.1	17.5	157	-2.8	-25.2	-19.8	9.7
Nchi nyingine za Amerika ya Kusini na Kati	365	-1.0	-23.9	-5.8	10.5	421	1.0	-12.0	-11.9	7.0
Ulaya	6,501	2.0	-12.5	-0.2	9.3	6,521	1.4	-13.2	0.4	9.9
Umoja wa Nchi za Ulaya	5,904	1.9	-12.5	-0.2	9.7	5,878	1.2	-13.3	0.4	10.0
Ujerumani	1,448	2.0	-11.2	0.6	8.5	1,167	1.5	-12.9	0.4	10.5
Ufaransa	652	1.8	-15.2	0.1	14.1	574	1.5	-13.1	-1.4	13.7
Uholanzi	535	0.3	-12.9	-0.9	6.7	625	0.3	-15.5	-0.2	9.2
Uingereza	445	1.0	-8.9	-11.0	8.6	644	1.2	-9.3	-1.6	12.0
Italia	506	1.8	-13.7	1.0	9.6	453	-1.0	-13.3	-1.0	11.2
Jumuiya ya Madola ya Nchi huru (CIS)	518	-1.8	-32.3	-16.5	24.4	402	-0.5	-32.4	-2.5	20.8
Shirikisho la Urusi	353	-1.8	-31.3	-17.4	25.3	238	-0.6	-37.3	-0.7	24.1
Afrika	417	-3.2	-29.3	-9.6	18.3	534	1.6	-13.9	-10.7	7.8
Afrika ya Kusini	89	-0.4	-11.7	-7.6	18.4	101	0.7	-14.2	12.5	10.6
Afrika bila Afrika ya Kusini	328	-3.8	-32.8	-10.1	18.2	432	1.8	-13.8	-10.3	7.1
Wauza mafuta Nje	154	-8.5	-44.1	-23.2	29.0	144	-0.5	-19.2	17.9	6.4
Wasiouza Mafuta Nje	173	2.8	-15.4	3.3	10.1	289	3.1	-10.4	-6.0	1.1
Mashariki ya Kati	961	0.8	-30.3	-7.0	18.0	712	2.9	-7.4	-4.5	15.3
Asia	5,842	3.2	-7.9	-3.4	10.7	5,541	2.9	-14.4	-4.4	16.0
China	2,263	5.3	-2.9	-7.7	7.9	1,842	-0.5	-14.3	-5.5	10.6
Japan	698	-1.4	-9.5	3.2	8.3	672	3.6	-20.2	-6.5	23.8
India	298	4.0	-17.1	-1.2	13.0	447	1.3	-15.1	-8.1	13.7
Nchi zinazochipukia kiviwanda	1,283	2.1	-11.1	-2.8	12.6	1,203	0.5	-16.6	-4.2	10.6

Chanzo: Shirika la Biashara Duniani (WTO), *Trade Statistics and Outlook* - Aprili 2018

125. Mwaka 2017, thamani ya mauzo ya bidhaa nje kwa nchi za Afrika iliongezeka hadi dola za Marekani bilioni 417 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 346 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 20.5. Aidha, thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka hadi dola za Marekani bilioni 534 mwaka 2017 kutoka dola za Marekani bilioni 501 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.6. Kulingana na mwenendo huo wa biashara, nakisi kwenye urari wa biashara ya bidhaa nje ilipungua na kufikia dola za Marekani bilioni 117 mwaka 2017 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani bilioni 155 mwaka 2016.

USHIRIKIANO WA UCHUMI KIMATAIFA

Jumuiya ya Afrika Mashariki

126. Mwaka 2017, Vituo vya Ushuru wa Forodha 10 vilianzishwa katika nchi wanachama kwa lengo la kutekeleza Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa upande wa Soko la Pamoja, jumla ya viwango vya ubora 106 vilitangazwa na kuchapishwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa bidhaa za nguo, ngozi na mazao yake, vyakula vya nafaka, na vifungashio vya vyakula vya lishe. Aidha, katika kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha, nchi wanachama ziliridhia Sheria ya Kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiforodha ya Mwaka 2017. Vile vile, mwaka 2017 Ripoti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Viwanda ilizinduliwa ambayo inatoa mwelekeo katika kuongeza fursa za masoko na ushindani kikanda na kimataifa.

127. Kikao cha Kawaida cha 18 cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilifanyika mwezi Mei 2017 katika Jiji la Dar es Salaam, Tanzania. Pamoja na mambo mengine, kikao hicho kilipokea taarifa ya mwaka ya Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kwa kipindi cha Disemba 2015 hadi Mei 2017 na kuridhishwa na utekelezaji wa programu za Jumuiya. Aidha, kikao kilimteua Mheshimiwa Rais Yoweri Kaguta Museveni kuwa mwenyekiti wa Jumuiya baada ya Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli kumaliza muda wake. Vile vile, kikao kilijadili Ripoti ya Utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Wakuu wa Nchi na kuagiza nchi wanachama kuwasilisha hati za kiitifaki za kuridhia maamuzi hayo kwa Katibu Mkuu wa Jumuiya.

128. Kwa upande mwingine, kikao hakikuridhishwa na utekelezaji wa malengo ya kukuza biashara kati ya nchi wanachama na kuliagiza Baraza la Mawaziri na Sekretarieti kutatua tatizo la muda mrefu la kuwepo vikwazo visivyo vya kiforodha kati ya nchi wanachama na kuwasilisha ripoti ya utekelezaji kwenye kikao cha Wakuu wa Nchi kitakachofuata. Aidha, kikao cha Wakuu wa Nchi kilijadili hatua za nchi wanachama kutoridhia Mkataba wa Ushirikiano wa Kiuchumi kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Nchi za Umoja wa Ulaya kutokana na baadhi ya vipengele ambavyo havina maslahi kwa nchi zao. Vile vile, kikao kiliishauri nchi ya Kenya kuendelea na maamuzi yake baada ya kusaini Mkataba huo bila kuathiriwa na nchi wanachama ambazo hazikusaini Mkataba huo. Kikao kilipokea ripoti ya mkakati endelevu wa kugharamia shughuli za Jumuiya na kuagiza mawaziri wa fedha wa nchi wanachama kuandaa mpango endelevu wa kugharamia shughuli za Jumuiya. Kuhusu uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa, Kikao cha Wakuu wa Nchi kiliridhia pendekezo la kipindi cha mpito cha kufikia Shirikisho la Kisiasa kwa kuagiza Sekretarieti kuunda timu ya wataalam wa mambo ya katiba kuandaa katiba ya Shirikisho.

Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

129. Kikao cha Dharura cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mfalme Mswati III kilifanyika tarehe 18 Machi, 2017 katika Mji wa Mbabane-Swaziland. Pamoja na mambo mengine, kikao kilipokea ripoti ya Kikosi Kazi cha Mawaziri kuhusu Mtangamano wa Kiuchumi na kiliridhia Mpango Kazi wa Jumuiya wa kutekeleza Mkakati na Mwelekeo wa Viwanda 2015-2063. Katika kutekeleza Mkakati huo, Wakuu wa Nchi walihimiza ufuatiliaji wa ushiriki wa sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa agenda ya viwanda ya Jumuiya.

130. Kwa upande mwingine, kikao kiliridhia mapendekezo ya Kikosi Kazi Maalum cha Mawaziri kilichofanyika tarehe 12-14 Machi, 2017 kilichokuwa na kaulimbiu *Utangamano wa Kikanda - Jumuiya ya Maendeleo Tunayoitaka*. Kikosi Kazi kilipitia utekelezaji wa majukumu ya Jumuiya tangu kuanzishwa kwake mwaka 1980, changamoto zilizojitokeza na mambo muhimu ya kutekelezwa ili kuongeza kasi ya agenda ya utangamano. Kikao kilipokea mapendekezo yaliyotolewa na Kikosi Kazi cha Mawaziri na kuagiza Sekretarieti kuandaa mpango na mwelekeo wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.

131. Kikao cha 37 cha Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Mfalme Mswati III kilifanyika tarehe 19-20 Agosti, 2017 katika Mji wa Pretoria Afrika ya Kusini. Pamoja na mambo mengine, kikao kilimchagua Mheshimiwa Rais Jacob Zuma kuwa mwenyekiti wa Jumuiya na Mheshimiwa Rais Jose Eduardo dos Santos kuwa mwenyekiti wa Kamati ya Siasa, Ulinzi na Usalama. Aidha, kikao kiliridhia Mpango wa 37 wa Jumuiya wa kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza viwanda na biashara. Nchi wanachama zilihimizwa kutekeleza Mpango huu katika maeneo ya kuongeza thamani mazao ya kilimo, kuongeza thamani ya madini, nishati, na uzalishaji wa dawa za binadamu.

132. Kikao cha Wakuu wa Nchi kilijadili hatua iliyofikiwa ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Kuleta Mabadiliko na kuhimiza mawaziri wenye dhamana ya elimu, sayansi na teknolojia kukamilisha mpango kazi wa kuanzishwa kwa Chuo hicho. Kwa upande mwingine, kikao kilipokea taarifa kuhusu mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Kikanda kwa lengo la kuendeleza agenda ya viwanda. Aidha, kikao kilipokea Ripoti ya Utekelezaji wa Mkakati na Mwelekeo wa Viwanda 2015-2063 na kuhimiza nchi wanachama kutekeleza maeneo matatu ya kipaumbele ya Mkakati huo ambayo ni kuongeza thamani mazao ya kilimo, kuongeza thamani ya madini, na uzalishaji wa dawa za binadamu. Vile vile, kikao kilipokea na kujadili taarifa ya Jopo la Mapitio ya Viashiria vya Uchumi Jumla kwa nchi wanachama ambapo ilibainika kuwa nchi nyingi zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazofanya kushindwa kufikia malengo ya vigezo vya kiuchumi na kibajeti.

Umoja wa Afrika

133. Kikao cha 28 cha Wakuu wa Umoja wa Afrika chini ya uenyekiti wa Mheshimiwa Rais Alpha Conde wa Guinea kilifanyika tarehe 31 Januari, 2017 katika jiji la Addis Ababa, Ethiopia. Kikao hiki kilimchagua Mheshimiwa Oussa Faki Mahamat kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika kuchukua nafasi ya Mheshimiwa Nkosazana Dlamini-Zuma ambaye alimaliza muda wake. Aidha kikao hicho kiliridhia ombi la nchi ya Morocco kujiunga tena katika Umoja huo.

SURA YA 6

RASILIMALI WATU

Idadi ya Watu

134. Idadi ya watu Tanzania ilikadiriwa kuwa 52,554,628 mwaka 2017 ikilinganishwa na watu 50,941,672 mwaka 2016. Katika mwaka 2017, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 51,020,337, sawa na asilimia 97.1 ya watu wote na Tanzania Zanzibar watu 1,531,291, sawa na asilimia 2.9. Aidha, mchanganuo wa watu kwa jinsia unaonesha kuwa wanawake walikadiriwa kuwa 26,867,474 sawa na asilimia 51.1 ya watu wote na wanaume 25,687,154 sawa na asilimia 48.9. Makadirio haya yalitokana na maoteo ya idadi ya watu kwa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 na viashiria muhimu vya mabadiliko ya idadi ya watu vikijumuisha uzazi, vifo na uhamiaji.

Mgawanyiko wa Watu Kimkoa

135. Mgawanyo wa watu kimkoa unaonesha kuwa, Mkoa wa Dar es salaam ulikuwa na watu wengi zaidi wapatao 5,017,294, sawa na asilimia 9.8 ya watu wote Tanzania Bara ikilinganishwa na watu 4,885,865 mwaka 2016. Mkoa wa Mwanza ulifuatia kwa kuwa na takribani watu 3,393,620, sawa na asilimia 6.7; na Kagera watu 2,919,942, sawa na asilimia 5.7. Idadi kubwa ya watu katika mkoa wa Dar es salaam ilitokana na upatikanaji wa huduma muhimu za kijamii na za kiuchumi na hivyo, kusababisha ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohamia kutoka mikoa mingine. Aidha, mkoa wa Katavi ulikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu ikilinganishwa na mikoa mingine ya Tanzania Bara, ukikadiriwa kuwa na watu 706,472, sawa na asilimia 1.4. Kwa upande wa Zanzibar, mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na watu wengi zaidi ikilinganishwa na mikoa mingine, ukiwa na watu takribani 683,833, sawa na asilimia 44.6 ya watu wote Tanzania Zanzibar ukifuatiwa na mkoa wa Kaskazini Pemba uliokadiriwa kuwa na watu 260,884, sawa na asilimia 17.0 na mkoa wa Kusini Unguja ukiwa na idadi ndogo zaidi ya watu 131,162, sawa na asilimia 8.5.

136. Mwaka 2017, msongamano wa watu kwa kila kilometa moja ya mraba kwa Tanzania ulikuwa na wastani wa watu 59. Aidha, kwa upande wa Tanzania Bara msongamano ulikuwa na wastani wa watu 58 kwa kila kilometa moja ya

mraba. Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na msongamano mkubwa zaidi wa watu kwa upande wa Tanzania Bara, ukiwa na watu 3,601 kwa kila kilometa moja ya mraba, ukifuatiwa na Mwanza (watu 356), Kilimanjaro (watu 138) na Kagera (watu 116). Mikoa ya Lindi na Katavi ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya watu kwa kila kilometa moja ya mraba ikiwa na wastani wa watu 15, ikifuatiwa na mkoa wa Ruvuma wastani wa watu 24 kwa kila kilometa moja ya mraba. Kwa upande wa Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi ulikuwa na msongamano mkubwa wa wastani wa watu 2,973 kwa kila kilometa moja ya mraba wakati Mkoa wa Kusini Unguja ulikuwa na wastani wa watu 154 kwa kila kilometa moja ya mraba.

137. Mchanganuo wa watu kwa makundi ya umri kwa mwaka 2017, ulionyesha kuwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano walikuwa 9,185,466, sawa na asilimia 17.5 ya idadi ya watu wote Tanzania. Idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka 5 hadi 14 ilikuwa 13,717,980, sawa na asilimia 26.1 ya watu wote Tanzania. Mchanganuo unaonesha kuwa watu wenye umri wa miaka 15 – 24 walikuwa 10,312,774, sawa na asilimia 19.6 ya watu wote Tanzania. Vile vile, idadi ya watu wenye umri kuanzia miaka 25 hadi 64 ilikuwa 17,579,467, sawa na asilimia 33.4 ya watu wote Tanzania. Wazee wenye umri zaidi ya miaka 64 walikuwa 1,758,941, sawa na asilimia 3.3 ya watu wote Tanzania. Aidha, idadi ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 ambayo ni nguvukazi ya Taifa ilikuwa 27,892,241, sawa na asilimia 53.1 ya watu wote Tanzania.

Jedwali Na: 6.1 Mchanganuo wa Idadi ya Watu kwa Makundi ya Umri na Jinsi kwa mwaka 2017

Umri	Jinsi			Asilimia
	ME	KE	Jumla	
5<	4,635,867	4,549,599	9,185,466	17.5
5 - 14	6,860,623	6,857,357	13,717,980	26.1
15 - 24	5,083,330	5,229,444	10,312,774	19.6
25 - 64	8,286,949	9,292,518	17,579,467	33.4
65+	820,385	938,556	1,758,941	3.3
Jumla	25,687,154	26,867,474	52,554,628	

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Nguvu kazi na Ajira

138. Taarifa ya matokeo ya Utafiti wa Ajira na Mapato katika sekta rasmi uliofanyika mwaka 2016 (Employment and Earning Survey, 2016) ilionesha kuwa ajira katika sekta rasmi ziliongezeka kutoka 2,334,969 mwaka 2015 hadi kufikia ajira 2,599,311 mwaka 2016, sawa na ongezeko la ajira 264,342. Kati ya ajira hizo, 83,812 zilikuwa ajira za sekta ya umma na ajira 180,530 zilikuwa za sekta binafsi. Aidha, sekta binafsi ilitoa ajira 1,748,695, sawa na asilimia 67.3 ya ajira zote na sekta ya umma ilichangia asilimia 32.7. Matokeo ya utafiti huo yalibainisha kuwa mchango wa ajira za masharti ya muda mrefu uliongezeka kutoka asilimia 88.2 mwaka 2015 hadi asilimia 92.9 mwaka 2016. Kwa upande mwingine, ajira za muda mfupi zilipungua kutoka asilimia 11.8 ya ajira zote mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 7.1 mwaka 2016.

Jedwali Na: 6.2 Mchanganuo wa Jumla ya Ajira kwa Aina za Ajira na Sekta

Aina za Ajira	2015				2016			
	Umma	Binafsi	Jumla	Mchango kwa Jumla ya Ajira (%)	Umma	Binafsi	Jumla	Mchango kwa Jumla ya Ajira (%)
Ajira za Masharti ya Muda Mrefu	755,360	1,304,653	2,060,013	88.2	848,010	1,568,022	2,416,032	92.9
Ajira za Muda Mfupi	11,444	263,512	274,956	11.8	2,605	180,673	183,278	7.1
Jumla	766,804	1,568,165	2,334,969	100.0	850,616	1,748,695	2,599,311	100.0

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

139. Uwiano wa ajira kwa jinsia ulionesha kuwa wanawake walikuwa asilimia 38.7 na wanaume asilimia 62.2. Aidha, matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa, idadi ya vijana wenye umri wa miaka 15-35 walioajiriwa kwa masharti ya muda mrefu iliongezeka kutoka asilimia 31.3 mwaka 2015 hadi asilimia 36.8 mwaka 2016. Aidha, idadi ya ajira za muda mrefu kwa wenye umri wa miaka 36 na kuendelea ilipungua kutoka asilimia 68.7 mwaka 2015 hadi asilimia 63.2 mwaka 2016. Sekta binafsi ilichangia asilimia 64.9 ya ajira za kudumu wakati sekta ya umma ikichangia asilimia 35.1. Kwa upande wa ajira za muda mfupi, sekta binafsi ilitoa ajira nyingi (asilimia 98.6) ikilinganishwa na sekta ya umma iliyotoa asilimia 1.4.

140. Idadi ya waajiriwa wenye ulemavu mwaka 2016 ilikuwa 3,935, sawa na asilimia 0.2 ya waajiriwa katika sekta rasmi. Kati ya hao, wanaume walikuwa 2,321 (sawa na asilimia 59) na wanawake 1,614 (sawa na asilimia 41). Sekta binafsi iliajiri sehemu kubwa ya waajiriwa wenye ulemavu (asilimia 61.6) na asilimia 38.4 walijajiriwa katika sekta ya umma.

141. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo, Mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kutoa ajira nyingi, ukichangia asilimia 31.2 ya waajiriwa wote mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 30.6 mwaka 2015. Mikoa iliyofuatia ni Morogoro uliochangia asilimia 10.9; Arusha (asilimia 6.8); na Mwanza (asilimia 5.9). Mikoa ya Katavi na Njombe iliajiri watu wachache zaidi kuliko mikoa mingine yote ambapo kila mkoa ulitoa ajira kwa kiwango kisichozidi asilimia moja ya waajiriwa wote. Aidha, mchanganuo wa ajira kissekta ulionesha kuwa sekta ya elimu iliendelea kutoa mchango mkubwa katika ajira ambapo ilichangia asilimia 18.5 ya ajira zote ikifuatiwa na sekta ya viwanda (asilimia 18.1) na utawala (asilimia 13.6). Sekta ya upangishaji majengo ilitoa mchango mdogo zaidi wa asilimia 0.2 ya ajira zote.

Jedwali Na. 6.3: Mchanganuo wa Ajira Kimkoa na Kisekta

Mkoa	Binafsi		Umma		Jumla	
	2015	2016	2015	2016	2015	2016
Dodoma	22,368	24,914	39,513	43,311	61,880	68,225
Arusha	138,099	147,497	26,595	28,079	164,693	175,576
Knjaro	87,953	90,508	40,105	44,680	128,057	135,188
Tanga	72,166	80,867	37,897	39,696	110,063	120,562
Morogoro	194,037	207,475	74,834	75,586	268,871	283,061
Pwani	20,587	23,765	27,566	28,969	48,153	52,734
DSM	614,445	706,159	100,784	105,388	715,229	811,547
Lindi	5,855	7,379	22,563	25,320	28,417	32,699
Mtwara	12,161	15,321	16,087	19,654	28,249	34,975
Ruvuma	22,519	32,464	23,065	23,652	45,585	56,116
Iringa	35,527	38,543	27,746	31,374	63,273	69,917
Mbeya	65,548	69,448	54,037	58,721	119,586	128,169
Singida	15,337	19,131	22,864	25,450	38,201	44,581
Tabora	14,090	14,127	23,767	29,890	37,857	44,017
Rukwa	8,998	9,240	16,104	19,500	25,102	28,740
Kigoma	14,601	17,504	26,689	28,075	41,290	45,580
Shinyanga	26,492	26,795	28,174	33,933	54,666	60,728
Kagera	19,897	23,551	27,794	30,322	47,691	53,873
Mwanza	102,992	105,145	40,644	47,274	143,635	152,420
Mara	17,922	19,120	29,038	33,738	46,959	52,858
Manyara	15,811	25,209	17,133	20,519	32,944	45,728
Njombe	8,924	10,551	10,523	15,108	19,448	25,659
Katavi	821	1,930	7,104	9,086	7,925	11,016
Simiyu	4,741	5,602	17,469	21,714	22,210	27,317
Geita	26,275	26,449	8,709	11,575	34,984	38,024
Jumla	1,568,165	1,748,695	766,803	850,616	2,334,969	2,599,311

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

142. Matokeo ya utafiti huo pia yalionesha kuwa ajira mpya mwaka 2016 zilipungua kutoka ajira 102,672 mwaka 2015 hadi ajira mpya 69,639. Kati ya ajira hizo mpya, wanaume walikuwa 34,975 na wanawake 34,664. Aidha, kwa majibu wa utafiti huo, sekta ya umma ilichangia ajira mpya 18,388 ikilinganishwa na ajira mpya 51,251 katika sekta binafsi. Kati ya idadi ya ajira

mpya zilizotolewa, kada za wahudumu na wafanyakazi wa madukani ilitoa waajiriwa wengi ambao walikuwa 15,515 ikifuatiwa mafundi na wataalam washiriki 15,346 na kazi za msingi (elementary occupation) waajiriwa 13,747.

143. Mwaka 2017, Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA) ulisajili na kutoa ushauri kwa watafutakazi 1,344 juu ya uchaguzi wa fani, mafunzo na kazi stahiki kulingana na sifa zao na mahitaji ya soko la ajira ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri na kuajirika. Idadi hiyo ni pungufu kwa asilimia 11.3 ikilinganishwa na watafutakazi 1,516 waliosajiliwa na kupewa ushauri mwaka 2016. Aidha, watafutakazi 339 waliunganishwa kwa waajiri wenye fursa za ajira ndani ya nchi ikilinganishwa na watafutakazi 624 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 45.7. Vile vile, Wakala ulitoa mafunzo kwa watafutakazi 448 ya kuwajengea uwezo wa kushindania fursa za ajira ikilinganishwa na watafutakazi 629 waliopewa mafunzo mwaka 2016. Mafunzo hayo pia yalitolewa kwa wanafunzi 520 wa vyuo mbalimbali vya elimu ya juu ikilinganishwa na wanafunzi 1,255 mwaka 2016.

144. Mwaka 2017, Wakala kwa kushirikiana na taasisi binafsi za ajira na Balozzi za Tanzania katika nchi husika ulipitia na kuridhia mikataba ya watanzania 2,882 ikilinganishwa na mikataba ya watanzania 914 waliopata ajira mwaka 2016. Watanzania hao walipata ajira katika nchi za Oman (wanaume 58, wanawake 2,650), Saudi Arabia (wanaume 109), Dubai (wanaume 26, wanawake 15), Qatar (wanaume nane, mwanamke mmoja), Abu Dhabi (wanaume watano, wanawake wawili), Japan (wanaume wanne), India (wanaume wawili), Kuwait (mwanume mmoja) na Bahrain (mwanume mmoja). Hii ilitokana na kuongezeka kwa elimu juu ya huduma za ajira nje ya nchi. Aidha, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji na Balozzi za Tanzania katika nchi husika ilihakikisha kuwa watanzania hao wanaajiriwa bila kuwepo kwa aina yoyote ya unyanyasaji wala ubaguzi, kwa kuweka utaratibu madhubuti unaozingatia sheria za nchi na miongozo ya Shirika la Kazi Duniani (ILO).

IDADI YA WATU NCHINI TANZANIA KIMKOA: 2009-2017

Jedwali Na.33

Mkoa	2009	2010	2011	2012**	2013	2014	2015	2016	2017
Dodoma	2058630	2111764	2163817	2083588	2127416	2172165	2217856	2264508	2419941
Arusha	1617728	1664780	1711624	1694310	1741396	1789791	1839531	1890653	1948219
Kilimanjaro	1602530	1635870	1669174	1640087	1669051	1698526	1728522	1759048	1823151
Tanga	1923468	1966908	2010480	2045205	2091341	2138517	2186757	2236086	2284712
Morogoro	2068426	2115275	2162197	2218492	2271310	2325386	2380750	2437431	2531268
Pwani	1038654	1062574	1086658	1098668	1122685	1147227	1172306	1197933	1236481
Dar es Salaam	3040118	3118132	3194903	4364541	4617000	4884061	5166570	5465420	5017294
Lindi	905480	923607	941884	864652	872758	880939	889197	897533	963465
Mtwara	1297751	1323568	1349235	1270854	1286501	1302340	1318374	1334606	1397723
Ruvuma	1338800	1375017	1412084	1376891	1406411	1436563	1467362	1498821	1543869
Iringa	1709225	1737382	1764285	941238	951964	962813	973784	984882	1068695
Mbeya	2581792	2662156	2743084	2707410	2781971	2858585	2937310	1883024	2006072
Singida	1330931	1367481	1404065	1370637	1402820	1435758	1469469	1503972	1569304
Tabora	2258664	2349374	2443049	2291623	2359642	2429679	2501796	2576053	2769093
Rukwa	1450118	1503184	1558200	1004539	1037259	1071044	1105931	1141953	1160568
Kigoma	1740111	1814158	1891173	2127930	2179598	2232520	2286727	2342250	2528708
Shinyanga	3692941	3841787	3998664	1534808	1566734	1599325	1632593	1666554	1816316
Kagera	2469904	2563870	2661671	2458023	2537021	2618558	2702715	2789577	2919942
Mwanza	3464566	3566263	3669380	2772509	2856258	2942537	3031422	3122992	3393620
Mara	1756442	1822866	1891907	1743830	1787279	1831810	1877451	1924230	2123683
Manyara	1337015	1388295	1441771	1425131	1471083	1518516	1567479	1618020	1692667
Njombe	-	-	-	702097	707698	713345	719036	724772	786347
Katavi	-	-	-	564604	583160	602325	622121	642567	706472
Simiyu	-	-	-	1584157	1613580	1643549	1674075	1705168	1998224
Geita	-	-	-	1739530	1785824	1833350	1882141	1932230	2148409
Songwe	-	-	-	-	-	-	-	1136415	1166094
Tanzania Bara	40683294	41914311	43169305	43625354	44827757	#####	#####	48676698	51020337
Kaskazini Unguja	1711150	177095	183209	187455	193551	199844	206343	213053	216697
Kusini Unguja	110183	112612	115035	115588	117923	120305	122736	125215	131162
Mjini Magharibi	471341	483205	495054	593678	619144	645701	673398	702283	683833
Kaskazini Pemba	243759	253999	264677	211732	214502	217309	220153	223033	260884
Kusini Pemba	236072	246601	257577	195116	197274	199456	201662	203893	241715
Zanzibar	1232505	1273512	1315552	1303569	1342394	1382616	1424292	1467477	1534291
Tanzania	41915799	43187823	44484857	44928923	46170151	#####	#####	50144175	52554628

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Takwimu za matokeo ya sensa mwaka 2012

- Takwimu Hazipo, Mkoa Mipya

SEHEMU YA PILI

UENDELEZAJI SEKTA BINAFSI

SURA YA 7

UENDELEZAJI WA SEKTA BINAFSI

Uwekezaji Vitega Uchumi Nchini

145. Mwaka 2017, Kituo cha Uwekezaji kilisajili jumla ya miradi 337 ikilinganishwa na miradi 345 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 2.3. Kati ya miradi iliyosajiliwa, miradi mipya ilikuwa 336 na mradi wa upanuzi ulikuwa mmoja. Aidha, miradi 84, sawa na asilimia 25.0 ilimilikiwa na watazania, miradi 168, sawa na asilimia 50.0 ilimilikiwa na wageni na miradi 85, sawa na asilimia 25.2 ilimilikiwa kwa ubia kati ya watazania na wageni. Katika kipindi hicho, miradi iliyomilikiwa na wageni iliongezeka kwa asilimia 17.5 ikilinganishwa na miradi 143 iliyomilikiwa mwaka 2016. Hata hivyo, miradi iliyomilikiwa na watazania ilipungua kwa asilimia 18.4 ikilinganishwa na miradi 103 iliyomilikiwa mwaka 2016 na miradi iliyomilikiwa kwa ubia kati ya watazania na wageni ilipungua kwa asilimia 19.0 ikilinganishwa na miradi 105 iliyomilikiwa mwaka 2016.

146. Thamani ya miradi iliyosajiliwa mwaka 2017 ilipungua kwa asilimia 14.4 hadi kufikia dola za Marekani bilioni 5.07 kutoka dola za Marekani bilioni 5.92 mwaka 2016. Aidha, usajili wa mwaka 2017 ulitengeneza fursa za ajira 30,728 ikilinganishwa na fursa za ajira 49,711 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 38.27.5.

Mgawanyiko wa Miradi Kisekta

147. Mwaka 2017, sekta ya viwanda iliongoza kwa kusajili miradi yenye thamani ya dola za Marekani bilioni 2.55, sawa na asilimia 50.3 ya thamani ya miradi yote iliyosajiliwa ikifuatiwa na usafirishaji mizigo dola za Marekani bilioni 1.44 (asilimia 28.4), kilimo dola bilioni 0.37 (asilimia 7.3), nishati dola bilioni 0.29 (asilimia 5.7), majengo ya biashara dola bilioni 0.20 (asilimia 3.9), utalii dola bilioni 0.06 (asilimia 1.2), huduma dola bilioni 0.05 (asilimia 1.0), taasisi za fedha dola bilioni 0.04 (asilimia 0.8) na miundombinu dola bilioni 0.03 (asilimia 0.6).

148. Aidha, sekta ya uzalishaji viwandani iliongoza kwa kuvutia idadi kubwa ya miradi kwa kuwa na asilimia 55.7 ya miradi mipya iliyosajiliwa ikifuatiwa na utalii asilimia 8.6, usafirishaji mizigo asilimia 8.3, majengo ya biashara asilimia

8.0, kilimo asilimia 6.8, huduma asilimia 5.7, taasisi za fedha asilimia 1.8, nishati na maliasili asilimia 1.5 kwa kila sekta, miundombinu na rasilimali watu asilimia 0.9 kwa kila sekta, mawasiliano asilimia 0.3 na sekta za utangazaji na kompyuta hazikuvutia miradi yoyote.

Mgawanyiko wa Miradi Kimkoa

149. Mgawanyiko wa miradi iliyosajiliwa katika mwaka 2017 unaonesha kuwa mkoa wa Dar es Salaam uliendelea kuongoza kwa kuvutia miradi ya uwekezaji kwa kuwa na asilimia 48.5 ya miradi mipya, ikifuatiwa na Pwani asilimia 14.3; Mwanza asilimia 8.3; Arusha asilimia 4.5; Morogoro na Dodoma asilimia 3.3 kila mmoja; Tanga na Iringa asilimia 2.7 kila mmoja; Lindi asilimia 2.1; Geita asilimia 1.8; Manyara na Mtwara asilimia 1.2 kila mmoja; Kilimanjaro, Mbeya, Mara na Shinyanga asilimia 0.9 kila mmoja; Kagera na Singida asilimia 0.6 kila mmoja; Kigoma, Njombe, Ruvuma, Simiyu na Tabora asilimia 0.3 kila mmoja; na mkoa wa Katavi haukusajili mradi mipya wowote.

Jedwali Na. 7.1: Mtawanyiko wa Miradi ya Uwekezaji Kimkoa Iliyosajiriwa na Kituo Cha Uwekezaji Tanzania katika mwaka 2017

Sekta	Arusha	Pwani	Dar	Dodoma	Geita	Iringa	Kagera	Katavi	Kigoma	Kilimanjaro	Lindi	Manyara	Mbeya	Morogoro	Mtwara	Mwanza	Njombe	Mara	Ruvuma	Shinyanga	Simiyu	Singida	Tabora	Tanga	Jumla
Kilimo		5	6	1		1	1							4	1									4	23
Utangazaji																									
Kompyuta																									
Majengo ya Bihashara	1	2	19											1	1	1						1		1	27
Miundo Mbinu		1																1			1				3
Nishati	1		2	1											1										5
Taasisi za Kifedha			6																						6
Rasilimali Watu			3																						3
Uzalishaji Viwandani	7	37	77	7	5	7	1		1	2	3	4	3	4	1	21			1	2		1	1	2	187
Maliasiri		1	1								1					1	1								5
huduma			13	1	1								1		3										19
Mawasiliano			1																						1
Utarii	6	2	11	1						1	3			1				2						2	29
Usafirishaji			24			1										2				1					28
Jumla	15	48	163	11	6	9	2		1	3	7	4	3	11	4	28	1	3	1	3	1	2	1	9	336

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania

Urahisi wa Kuwekeza na Kufanya Biashara Nchini

150. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, kupunguza urasimu, kuharakisha maamuzi, kuimarisha ulinzi na usalama, kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu sahihi na imara, kutoa huduma bora zikiwemo upatikanaji wa umeme wa uhakika na hivyo, kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza nchini. Taarifa ya Mazingira ya Biashara ya mwaka 2018 ilionyesha kuwa mwaka 2017, Tanzania ilifanya vizuri kati ya nchi 190 zilizofanyiwa tathimini katika baadhi ya vipengele ambapo ilishika nafasi ya 58 katika utekelezaji wa mikataba, nafasi ya 55 katika kupata mikopo, na nafasi 82 katika kuunganisha umeme. Hata hivyo, Tanzania haikufanya vizuri katika baadhi ya vipengele ambapo ilishika nafasi ya 182 katika biashara za mipakani, nafasi ya 162 kuanzisha biashara na nafasi ya 156 katika vibali vya ujenzi. Serikali inaendelea na juhudi za kuboresha mazingira ya kufanyia biashara kwa lengo la kuhakikisha nchi inafanya vizuri zaidi.

151. Utafiti uliofanywa na *Deloitte Africa Private Equity Confidence Survey* 2017, ulionyesha kuwa asilimia 67 ya wawekezaji waliohojiwa, waliitaja Tanzania kuwa ni mojawapo ya nchi ambazo wangependa kuwekeza miradi mipya ikilinganishwa na asilimia 52 katika utafiti uliofanywa mwaka 2016. Vile vile, ripoti ya *Africa Attractiveness Index (AAI)* ya mwaka 2017, ilionyesha kuwa Tanzania ilishika nafasi ya 5 kati ya nchi 46 ikilinganishwa na nafasi ya 12 mwaka 2016 kwa kuwa na mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji. Halikadhalika, Ripoti ya Mwaka 2018 ya Maendeleo Shirikishi (*The Inclusive Development Index Report 2018*), ilionyesha kuwa mwaka 2017, Tanzania ilishika nafasi ya 48 miongoni mwa nchi za uchumi unaoinukia na hivyo kuwa nchi ya Tatu kwa nchi za Afrika. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, nafasi hiyo ilitokana na jitihada za Serikali za kuboresha sera na kuimarisha taasisi mbali mbali nchini. Aidha, ripoti iliyotolewa na *Rand Merchant Bank (RMB)* ya mwaka 2018 inayoangalia nchi zinazovutia uwekezaji Afrika, ilionyesha kuwa Tanzania ilishika nafasi ya 7 kati ya nchi 53 mwaka 2017 ikilinganishwa na nafasi ya 9 mwaka 2016. Hii ilitokana na juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuboresha na kuimarisha mazingira ya uwekezaji nchini.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

152. Mwaka 2017, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliendelea kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004. Katika kuboresha uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa mipango ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, kisekta na katika halmashauri, Baraza lilitoa mafunzo kuhusu uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa watendaji 133 wa mikoa na halmashauri. Mafunzo hayo yalilenga: kujenga uelewa wa mkakati wa Taifa wa kuwezesha wananchi kiuchumi; na kuongeza ushiriki wa watanzania katika uwekezaji, mitaji na fursa mbalimbali za uwekezaji zilizopo nchini. Aidha, kupitia mifuko ya uwezeshaji watanzania 478 (wanaume 357 na wanawake 121) walipata mikopo yenye masharti nafuu katika benki na taasisi za fedha. Aidha, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ulitoa dhamana ya mikopo yenye jumla ya shilingi 373,636,000 kwa vikundi 42 vya VICOBA. Vile vile, Mfuko ulifanya maonesho ya mifuko ya uwezeshaji yaliyolenga kuwawezesha watanzania kupata fursa za mitaji iliyopo katika mifuko hiyo na taasisi mbalimbali za fedha ambapo mifuko ya uwezeshaji 13 na wajasiliamali 115 walishiriki.

Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

153. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kupokea maandiko ya miradi inayokusudiwa kuendelezwa kwa utaratibu wa ubia katika wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, taasisi na mashirika ya umma. Maandiko hayo yalihusu ujenzi wa kituo cha biashara Kurasini; ujenzi wa reli ya Mtwara-Mchuchuma/Liganga kwa kiwango cha *Standard Gauge*; ujenzi wa reli ya Tanga–Arusha-Musoma kwa kiwango cha *Standard Gauge*; ujenzi wa miundombinu ya reli katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya treni ya abiria; mradi wa kusambaza gesi asilia nchini; mradi wa Bandari ya Mwambani; na ujenzi wa vituo vya kupumzikia katika barabara kuu zote nchini.

154. Serikali iliendelea kutoa mafunzo ya ubia kwa maofisa zaidi ya 360 kutoka katika wizara, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mashirika na taasisi za umma. Aidha, Serikali iliendelea kusimamia mradi wa ubia wa mabasi yaendayo haraka katika Jiji la Dar es Salaam na kufanya uchambuzi kwa miradi ya barabara ya tozo ya Dar es Salaam-Chalinze; mradi wa kuzalisha madawa muhimu wa Bohari Kuu ya Madawa; mradi wa kukagua na kusajili magari kwa njia ya kielektroniki; na mradi wa kujenga na kuendesha vyuo 10 vya VETA.

KITUO CHA UWEKEZAJI TANZANIA (TIC): MIRADI YA UWEKEZAJI ILIYOSAJILIWA

Jedwali Na.34

Sekta	2016								2017							
	A	B	C	D	E	F	G	H	A	B	C	D	E	F	G	H
Kilimo	24	24	0	7	8	9	25547	496.1	23	23	0	9	11	3	2535	371.6
Maliasili	2	2	0	0	0	2	235	264.9	5	5	0	1	2	2	286	5.3
Utafiti	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Uzalishaji Viwandani	178	178	0	48	86	44	12455	615.1	187	187	1	42	102	44	18389	2552.4
Majengo ya biashara	48	48	0	16	16	16	4812	1133.7	27	27	0	5	13	9	2284	204.3
Usafirishaji Mizigo	21	21	0	12	9	6	2605	384.9	28	28	0	13	11	4	2953	1443.8
Huduma	16	16	0	1	6	9	670	48.0	19	19	0	3	12	4	1061	50.8
Komputa	1	1	0	1	0	0	37	0.1	0	0	0	0	0	0	0	0
Taasisi za fedha	4	4	0	0	1	3	140	9.0	6	6	0	0	2	4	520	40.1
Mawasiliano	2	2	0	1	0	1	58	282.3	1	1	0	0	1	0	18	4.1
Nishati	8	8	0	3	3	2	627	2457.7	5	5	0	0	5	0	407	299.6
Rasilimali watu	8	8	0	3	1	4	362	33.3	3	3	0	1	1	1	202	4.5
Utalii	33	33	0	11	13	9	2163	194.4	29	29	0	9	8	12	1581	64.4
miundombinu	0	0	0	0	0	0	0	0.0	3	3	0	1	0	2	492	30.63
Utangazaji	0	0	0	0	0	0	0	0.0	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla	345	345	0	103	143	105	49711	5919.4	336	336	1	84	168	85	30728	5071.5

Chanzo: Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC)

- A Jumla ya Miradi Iliyosajiliwa
- B Miradi Mipya
- C Miradi ya Upanuzi
- D Miradi ya Wazawa
- E Miradi ya Wageni
- F Miradi ya Ubia
- G Jumla ya Ajira
- H Jumla ya Thamani ya Uwekezaji (USD. Milioni)
- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 8

MASUALA MTAMBUKA

UKIMWI

155. Mwaka 2017, Serikali iliendelea na juhudi za kupunguza maambukizi mapya katika jamii, hususan kwa vijana kwa kuhakikisha kuwa walioambukizwa na VVU wanaendelea kuishi. Katika kipindi hicho, Serikali ilianzisha Mfuko Maalumu wa UKIMWI (AIDS Trust Fund) kwa lengo la kuongeza rasilimali endelevu kwa ajili ya kuboresha huduma za UKIMWI zinazotolewa nchini na kupunguza utegemezi wa fedha za wafadhili. Aidha, mwaka 2017, jumla ya watu wapatao 5,164,297 walipimwa VVU ambapo kati yao, watu 145,104 (asilimia 2.8) waligundulika kuwa na maambukizi na kuanzishiwa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI. Hadi Desemba 2017, jumla ya watu 965,081 wenye virusi vya UKIMWI walikuwa wanatumia dawa za ARV, sawa na asilimia 69 ya watu 1,400,000 wanaokadiriwa kuishi na virusi vya UKIMWI nchini kote.

156. Matokeo ya utafiti wa nne wa viashiria vya UKIMWI uliofanyika katika ngazi ya kaya mwaka 2016/17 ulibainisha kuwa wastani wa kitaifa wa maambukizi ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 49 ulikuwa asilimia 4.7. Hii inamaanisha kuwa kati ya watu 1000, takribani watu 47 walikuwa wameambukizwa VVU. Aidha, utafiti huo ulionesha kuwa kiwango cha maambukizi kwa wanawake kilikuwa asilimia 6.2 na wanaume asilimia 3.1. Vile vile, mikoa iliyokuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi juu ya wastani wa kitaifa wa asilimia 4.7 ilikuwa Njombe asilimia 11.4, Iringa (asilimia 11.3), Mbeya (asilimia 9.3), Mwanza (asilimia 7.2), Kagera (asilimia 6.5), Katavi (asilimia 5.9), Shinyanga (asilimia 5.9), Songwe (asilimia 5.8), Ruvuma (asilimia 5.6), Pwani (asilimia 5.5), Tabora (asilimia 5.1), Tanga (asilimia 5.0), Dodoma (asilimia 5.0) na Geita (asilimia 5.0). Halikadhalika, utafiti huo ulibainisha kuwepo na idadi ya maambukizi mapya 81 ya VVU kwa mwaka, sawa na asilimia 0.27.

Mazingira

157. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuwahimiza wawekezaji kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika uwekezaji kwa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla ya kutekeleza miradi yao. Katika kipindi hicho, miradi 1,176 ilisajiliwa kwa ajili ya kuandaa TAM ikilinganishwa na miradi 1,058 iliyosajiliwa mwaka 2016. Kati ya hiyo, miradi 425, sawa na

asilimia 36 ilipata hati ya kukidhi vigezo vya TAM ikilinganishwa na miradi 475 iliyosajiliwa na kupata hati ya kukidhi vigezo mwaka 2016. Aidha, wataalam elekezi wa TAM 757, wakaguzi wa Mazingira 357, kampuni 152 za ushauri wa TAM na kampuni 74 za ukaguzi wa Mazingira zilisajiliwa ili kuboresha uwezo wa ukaguzi wa mazingira.

158. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ambapo miradi 627 ilikaguliwa katika maeneo ya viwanda, migodi, majengo, mabwawa, machinjio, masoko, mifumo ya majitaka, mifumo ya maji ya mvua, vituo vya mafuta, hoteli, na vyanzo vya maji. Aidha, hatua stahiki za kisheria ikiwemo kulipa faini zilichukuliwa kwa miradi 179 iliyokiuka Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

159. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza miradi miwili ya kujenga uwezo wa jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Pwani ambayo ni mradi wa kujenga uwezo wa jamii za pwani kuhimili mabadiliko ya tabianchi na mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jiji la Dar es Salaam. Aidha, miradi hiyo ilitekelezwa kwa kushirikiana na Wilaya za Pangani, Rufiji, Bagamoyo na Zanzibar (Pemba na Unguja) ili kunusuru maeneo hayo na athari za kuongezeka kwa usawa wa bahari. Halikadhalika, kupitia miradi hiyo kulifanyika ujenzi wa kuta za pembeni mwa bahari katika eneo la Pangani (mita 600) kwa upande wa kaskazini, kisiwa Panza-Pemba (mita 50) na Kilimani-Unguja (mita 538). Vile vile, mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika jiji la Dar es Salaam unatekelezwa kwa kujenga kuta katika maeneo ya Barabara ya Barack Obama (mita 920), Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (mita 500); ukarabati wa mitaro ya maji ya mvua Bungoni-Ilala (mita 475) na Mtoni-Temeke (mita 950) ili kupunguza athari za mafuriko.

Jinsia

160. Matokeo ya uchambuzi wa fahirisi ya maendeleo watu kwa jinsia (Gender Development Index – GDI) na fahirisi ya usawa wa kijinsia (Gender Inequality Index – GII) zote zilionesha kuwa wanawake wana uwezekano mkubwa wa kutokuwa na maendeleo kutokana na kuwa na nafasi finyu za kupata huduma za elimu, afya, na fursa za kiuchumi. Taarifa ya maendeleo ya watu ya mwaka 2017 ilionesha kuwa fahirisi ya maendeleo ya watu kwa jinsia Tanzania ilikuwa alama 0.864. Fahirisi hiyo inamaanisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kupunguza tofauti ya jinsia, hususan katika kipengele cha umri wa kuishi na elimu ya awali. Matalani, wastani wa umri wa kuishi kwa wanawake ni

mkubwa (miaka 63.7) ikilinganishwa na umri wa wanaume (miaka 59.7). Hata hivyo, kuna tofauti kubwa kwa upande wa kipato (wastani wa pato kwa mtu) ambapo kipato cha wanawake ni kidogo kuliko cha wanaume.

161. Kuhusiana na fahirisi ya usawa wa kijinsia, Tanzania ilipata alama 0.544 na kushuka kwa nafasi nne hadi kuwa nchi ya 129 kati ya nchi 188 duniani kulingana na taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP) ya mwaka 2016. Changamoto kubwa ilikuwa ushiriki wa wanawake katika vyombo vya maamuzi ambapo asilimia 82.6 ya nafasi hizo zilichukuliwa na wanaume na wanawake walikuwa asilimia 17.4. Aidha, changamoto nyingine iliyoongeza ukubwa wa tofauti ya kijinsia ni usimamizi na umiliki wa rasilimali za uzalishaji na rasilimali fedha na mimba za utotoni. Takwimu za TDHS-MIS 2015/16 zinaonesha kuwa asilimia 27 ya wanawake wa umri wa miaka 15 – 19 walipata mimba ikiwa ni ongezeko kutoka asilimia 23 mwaka 2010. Hata hivyo, mafanikio makubwa yalikuwepo katika vipengele vya ongezeko la nafasi za wanawake bungeni ambapo asilimia 37 ya nafasi hizo zinashikiliwa na wanawake bungeni. Aidha, ushiriki wa wanawake katika soko la ajira uliongezeka kufikia asilimia 69.2 ya wanawake wote ikilinganishwa na asilimia 81.4 ya wanaume.

Usalama wa Raia

162. Mwaka 2017, jumla ya makosa makubwa ya jinai 67,140 yaliripotiwa ikilinganishwa na makosa 74,659 yaliyoripotiwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 10.1. Aidha, makosa 12,578 dhidi ya binadamu yakiwemo mauaji, ubakaji, ulawati, utupaji wa watoto, wizi wa watoto, unajisi na usafirishaji wa binadamu yaliripotiwa mwaka 2017 ikilinganishwa na makosa 12,567 yaliyoripotiwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Makosa 32,175 ya kuwania mali yanayohusisha unyanganyi, uvunjaji, wizi, kuchoma nyumba moto, kugushi na noti bandia yaliripotiwa mwaka 2017 ikilinganishwa na makosa 37,882 yaliyoripotiwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 15.1. Makosa 1,640 dhidi ya uhalifu wa kifedha yanayojumuisha wizi kwenye benki, ATM na mitandao ya simu yaliripotiwa mwaka 2017 ikilinganishwa na makosa 1,990 yaliyoripotiwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 17.6. Makosa 20,747 kinyume na sheria yalijumuisha rushwa, kupatikana na pombe ya moshi, nyara za Serikali, silaha, risasi, bangi na magendo, yaliripotiwa mwaka 2017 ikilinganishwa na makosa 22,220 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 6.6.

163. Mwaka 2017, matukio ya usalama barabarani yalipungua kwa asilimia 41.5 na kufikia matukio 6,022 kutoka matukio 10,297 mwaka 2016. Hali hii ilitokana na kuimarika kwa uzingatiaji wa sheria za usalama barabarani. Aidha, ajali zilisobababisha vifo zilipungua kutoka 2,840 mwaka 2016 hadi ajali 2,254 mwaka 2017, sawa upungufu wa asilimia 20.6. Upungufu huu ulitokana na uboreshwaji wa miundombinu, elimu kwa umma na kuimarishwa kwa ukaguzi wa vyombo vya usafiri. Vile vile, vifo vilivyotokana na ajali hizo vilipungua kutoka 3,381 mwaka 2016 hadi vifo 2,705 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 20.0. Halikadhalika, majeruhi 6,169 waliotokana na ajali hizo ikilinganishwa na majeruhi 9,549 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 35.4.

164. Mwaka 2017, jumla ya wakimbizi na waomba hifadhi 358,520 kutoka mataifa mbalimbali walipokelewa na kupewa hifadhi ikilinganishwa na wakimbizi na waomba hifadhi 299,074 mwaka 2016. Kati ya hao, wakimbizi walikuwa 315,073 na waomba hifadhi 43,447, waliotoka katika mataifa ya Burundi (275,687), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (82,315), Somalia (150) na 368 walitoka mataifa ya Rwanda, Kenya, Uganda, Sudan Kusini na Ethiopia. Wakimbizi hao walihifadhiwa katika kambi na makazi yaliyoko mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora na Tanga na wengine wenye uwezo wa kujitegemea waliruhusiwa kuishi nje ya kambi. Katika kipindi hicho, wakimbizi 1,620 walihamishiwa katika nchi ya tatu (resettlement) ikilinganishwa na wakimbizi 8,905 waliohamishiwa mwaka 2016. Kati ya hao, wakimbizi 16 walihamishiwa Australia, Canada (457), Finland (3), Marekani (1,129), Sweden (11) na Uingereza (4). Kwa upande mwingine, wakimbizi 16,130 walirejeshwa kwa hiari katika nchi zao za asili mwaka 2017.

Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa

165. Mwaka 2016/17, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika wilaya zote nchini ilisajili na kutambua jumla ya wananchi 14,048,493. Aidha, Mamlaka ilifanikiwa kufungua ofisi usajili na utambuzi kwenye wilaya zote nchini pamoja na kuajiri watumishi 437. Vile vile, Mamlaka ilikamilisha uwekaji mtandao wa mawasiliano katika ofisi za wilaya 117 ili kurahisisha utumaji wa taarifa za wananchi kwenda makao makuu.

166. Mwaka 2016/17, Mamlaka ilijenga majengo ya ofisi za usajili katika wilaya 13 nchini na kukamilisha ujenzi wa kituo cha kuchakata, kuzalisha na kutunza kumbukumbu pamoja na kituo cha urejeshaji kumbukumbu wakati wa

majanga (Disaster Recovery Site). Aidha, taasisi 35 ziliunganishwa katika mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili kusaidia upatikanaji na utambuzi wa taarifa za watu kwa jamii kulingana na uhitaji.

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini

167. Mwaka 2017, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini uliendelea na shughuli za usajili ambapo, jumla ya vizazi 1,764,494; vifo 52,323; ndoa 23,444; talaka 109 na hati 37 za watoto wa kuasili zilisajiliwa ikilinganishwa na usajili wa vizazi 980,012; vifo 24,061; ndoa 18,339; talaka 110 na watoto wa kuasili 24 mwaka 2016.

168. Mwaka 2017, jumla ya watoto 1,132,566 wenye umri wa chini ya miaka mitano walisajiliwa kupitia Mpango wa Usajili kwa Watoto Walio na Umri wa Chini ya Miaka Mitano ikilinganishwa na watoto 365,433 waliosajiliwa mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kusimikwa kwa mfumo wa usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Mtwara na Lindi. Kiwango cha usajili kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kitaifa kiliongezeka hadi kufikia asilimia 28 mwaka 2017 kutoka asilimia 13 ya kiwango kilichotajwa katika Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012. Aidha, Mfumo wa Usajili wa Kizazi- Toleo la Nne ulianza kufanya kazi ambapo jumla ya vizazi 5,525 na vifo 231 vilisajiliwa katika vituo 60 vya majaribio vilivyopo mikoa ya Shinyanga, Geita na Dar es Salaam. Mfumo huu umesaidia kubadilishana taarifa na mifumo mingine ya Serikali kama NIDA na wadau wengine.

169. Mwaka 2017, Wakala ulitoa na kusajili hati 121 za miunganisho ya wadhamini ikilinganishwa na hati 155 mwaka 2016. Aidha, jumla ya wosia 57 ziliandikwa na kuhifadhiwa ikilinganishwa na wosia 49 mwaka 2016. Katika kipindi hicho, elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuandika na kutunza wosia ilitolewa kupitia vipindi vya redio, luninga na makala katika magazeti ili kusaidia kuepusha migogoro kwa wanafamilia pindi mwenye mali anapofariki.

SURA YA 9

HALI YA UMASKINI NA MAENDELEO YA WATU

UTANGULIZI

170. Mwaka 2017, Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha maisha ya watanzania pamoja na ustawi wao kwa kuboresha huduma za kijamii, hususan katika sekta za elimu, afya na maji. Aidha, Serikali imeendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha nchi inafikia uchumi wa kati na hatimaye kutokomeza umaskini uliokithiri ifikapo mwaka 2025. Katika kuhakikisha ukuaji wa uchumi jumuishi na kupunguza umaskini, Serikali iliendelea na juhudi za utekelezaji wa ujenzi wa uchumi wa viwanda unaotumia malighafi za ndani hususan za kilimo (Agro-processing) na kuongeza fursa za ajira.

HALI YA UMASKINI KWA KUTUMIA VIASHIRIA VINGI

171. Hali ya umaskini nchini imeendelea kupungua miongoni mwa watanzania japokuwa kasi ya kupungua ni ndogo ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa uchumi. Hali hii inatokana na kuwa sekta zinazokua kwa kasi ni zile ambazo hazina mchango mkubwa katika kupunguza umaskini kama vile madini, mawasiliano na usafirishaji. Sekta ya kilimo ambayo inategemewa na asilimia 66.3 ya wananchi kama chanzo cha kipato na kuchangia wastani wa asilimia 30 katika Pato la Taifa imeendelea kuwa na kasi ndogo ya ukuaji wa wastani wa chini ya asilimia 3.0 kwa mwaka, hivyo kuathiri kasi ya kupungua kwa umaskini. Kwa kuzingatia hali hiyo, Serikali inakusudia kuelekeza mikakati yake kwa kiasi kikubwa kupambana na umaskini katika maeneo ya vijijini.

172. Hali ya umaskini inaweza kupimwa kwa kuzingatia kigezo zaidi ya kimoja (Multidimensional Poverty). Nchi nyingi duniani ikiwemo Tanzania zinatafsiri umaskini kwa kigezo kimoja cha viwango vya mapato au matumizi, ijapokuwa umaskini una sura zaidi ya moja. Umaskini unaweza kupimwa kwa kutumia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na elimu, afya, makazi, uwezeshaji, ajira na usalama. Taarifa ya Maendeleo ya watu Tanzania ya mwaka 2017 imetumia vigezo vitatu katika kupima umaskini ambavyo ni elimu, afya na hali ya maisha. Vigezo hivi vitatu vinahusisha viashiria kumi (10) vya umaskini ambavyo ni: lishe; vifo vya watoto; miaka inayotumika shule; mahudhurio ya shule; nishati ya kupikia; usafi wa mazingira; upatikanaji wa maji safi na salama; upatikanaji wa umeme; aina ya sakafu; na umiliki wa mali.

173. Katika kutafuta Fahirisi ya Umaskini kwa kuzingatia kigezo zaidi ya kimoja (MPI), takwimu za Utafiti wa Afya na Demografia Tanzania (THDS) kwa mwaka 2010 na 2015/2016 zilitumika. Fahirisi ya Umaskini kwa kuzingatia kigezo zaidi ya kimoja inaonesha kwamba umaskini umepungua kutoka asilimia 64 mwaka 2010 na kufikia asilimia 47.4 mwaka 2015/2016. Aidha, umaskini uliokithiri umepungua kutoka asilimia 31.3 mwaka 2010 na kufikia asilimia 17.7 mwaka 2015/2016. Kuongezeka kwa hali ya upatikanaji wa umeme, kuongezeka kwa kiwango cha umiliki wa mali kama vile, simu za viganjani, pikipiki, redio na kuimarika kwa utoaji wa huduma za kijamii kama vile elimu, afya na maji ni miongoni mwa sababu zilizochangia kupungua kwa umaskini. Vile vile, kwa mujibu wa fahirisi hiyo, mkoa wa Rukwa ulikuwa na kiwango kikubwa cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini cha asilimia 65.5 ikilinganishwa na mkoa wa Dar es Salaam uliokuwa na kiwango kidogo cha asilimia 12.2. Mikoa mingine iliyokuwa na kiwango kikubwa cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini ni Tabora, Shinyanga, Geita, Dodoma na Simiyu, wakati iliyokuwa na kiwango kidogo ni Kilimanjaro, Njombe, Morogoro, Ruvuma na Iringa.

MAENDELEO YA WATU

174. Mwaka 2017, Serikali imeendelea kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi, hususan elimu na afya ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, malengo ya Ajenda ya Afrika ya mwaka 2063, na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030. Kwa mujibu wa taarifa ya dunia ya maendeleo ya watu ya mwaka 2016 (UNDP Global Report), Tanzania ilishika nafasi ya 151 kati ya nchi 185 katika maendeleo ya watu mwaka 2015 sawa na nafasi iliyoshika mwaka 2014. Aidha, Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (HDI) iliongezeka hadi kufikia 0.531 mwaka 2015 ikilinganishwa na 0.519 mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 2.3. Kwa takwimu hizo, Tanzania iko juu ya kiwango cha wastani kwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara cha 0.518. Licha ya kuimarika kwa kiwango cha maendeleo ya watu. Ongezeko hilo, linaonesha Tanzania bado ipo katika kundi la chini katika maendeleo ya watu. Taarifa ya maendeleo ya watu huzipanga nchi katika makundi manne; kundi la juu zaidi kwenye maendeleo ya watu, kundi la juu, kundi la kati na kundi la chini.

Jedwali Na. 9.1: Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu Kitaifa na Kimkoa katika Mwaka 2017

SNo.	Mkoa	Maendeleo ya Watu ¹	Hali ya umaskini kwa kipimo cha MPI	Umaskini wa Kipato
1	Kagera	0.44	53%	39.3%
2	Singida	0.47	51%	38.2%
3	Tabora	0.47	65%	32.6%
4	Kigoma	0.47	56%	48.9%
5	Dodoma	0.48	60%	27.1%
6	Katavi	0.52	58%	23.9%
7	Shinyanga	0.53	64%	34.2%
8	Pwani	0.53	47%	14.7%
9	Geita	0.55	62%	43.7%
10	Simiyu	0.56	60%	28.8%
11	Rukwa	0.56	66%	27.1%
12	Mtwara	0.60	49%	33.9%
13	Morogoro	0.60	39%	23.1%
14	Mara	0.61	50%	26.2%
15	Tanzania Bara	0.61²	47%	28.8%
16	Lindi	0.62	47%	30%
17	Manyara	0.63	50%	18.3%
18	Mwanza	0.65	49%	35.3%
19	Tanga	0.65	46%	32.7%
20	Ruvuma	0.66	39%	34.9%
21	Songwe	0.66	43%	
22	Mbeya	0.66	43%	24.3%
23	Njombe	0.67	31%	25.7%
24	Iringa	0.70	40%	26.7%
25	Arusha	0.70	48%	14.7%
26	Dar es Salaam	0.72	12%	5.2%
27	Kilimanjaro	0.75	22%	14.3%

Chanzo: Tanzania HDR 2017

175. Mwaka 2017, Serikali iliendelea na juhudi za kuboresha hali za maisha ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri na kulinda mtaji-watu wa watoto

¹ Kadiri tarakimu inavyokaribia 1 (moja), kiwango cha maendeleo ya watu kinazidi kuongeka

² Inatofautiana na takwimu za UNDP Kutokana na tofauti ya njia iliyotumika kufanya ukokotoaji

wanaoishi katika mazingira hatarishi kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (Productive Social Safety Net - PSSN) unaotekelezwa na TASAF. Mpango huu unatekelezwa kupitia maeneo matatu ambayo ni uhawilishaji fedha, miradi ya ajira za muda na mradi wa kukuza akiba ya jamii (Community Savings Promotion).

176. Hadi kufikia mwaka 2017, fedha zilizotolewa kwa njia ya uhawilishaji na ajira za muda zilikuwa shilingi bilioni 715.9 ikilinganishwa na bilioni 455.8 zilizotolewa kufikia mwaka 2016. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 668.3 zilitolewa kupitia uhawilishaji fedha ikilinganishwa na shilingi bilioni 435.4 zilizotolewa kufikia mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 53.5. Kwa upande wa mradi wa ajira za muda (Public Works Programme - PWP), hadi kufikia Desemba 2017, ujira wenye thamani ya shilingi bilioni 47.6 ulilipwa kwa kaya maskini zilizoshiriki katika miradi iliyoibuliwa kwenye maeneo yao ikilinganishwa na ujira wenye thamani ya shilingi bilioni 20.4 uliolipwa kufikia mwaka 2016.

177. Hadi kufikia Desemba 2017, uhawilishaji fedha kwa kaya maskini ulifikia asilimia 70 ya kaya zilizoainishwa katika Mpango huo. Aidha, hadi Desemba 2017, jumla ya wanufaika milioni 5.1 walijumuishwa katika Mpango ikilinganishwa na wanufaika milioni 5 kufikia Desemba 2016. Mchanganuo wa wanufaika ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 9.2.**

Jedwali Na. 9.2: Wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini hadi Mwaka 2017


Makundi	Miaka 0-2	Miaka 2-5	Miaka 6-18	Miaka 19-60	Zaidi ya 60	Jumla
Idadi ya Wanufaika	343,558	487,134	1,994,687	1,697,279	605,072	5,127,730
Asilimia (%)	6.7	9.5	38.9	33.1	11.8	100.0

Chanzo: TASAF

178. Rushwa huathiri juhudi za kupambana na umaskini na kuboresha maendeleo ya watu kutokana na kudumaza hali ya upatikanaji wa huduma za msingi zikiwemo afya, elimu na maji. Kwa kutambua hilo, Mwaka 2017 Serikali iliendelea kudhibiti vitendo vya rushwa katika sekta na mashirika ya umma ili kuhakikisha kuwa jamii maskini inapata huduma stahiki. Kutokana na jitihada hizo, Tanzania ilipata alama 36 ya fahirisi ya rushwa katika kupambana na

vitendo vya rushwa katika sekta ya umma ikilinganishwa na alama 32 iliyopata mwaka 2016, sawa na ongezeko la alama 4. Alama hii ni ya juu kufikiwa kwa zaidi ya muongo mmoja uliopita na ipo juu ya wastani wa alama 32.02 ambayo nchi za kusini mwa jangwa la Sahara zimepata. Taarifa hii ni kwa mujibu wa takwimu za rushwa zilizotolewa mwaka 2017 na Shirika la *Transparency International*. Aidha, kutokana na juhudi za kupambana na rushwa kuimarika kwa mwaka 2017, Tanzania ilishika nafasi ya 103 kati ya nchi 180 katika kupambana na rushwa ikilinganishwa na nafasi ya 116 kati ya nchi 176 mwaka 2016. **Kielelezo Na. 9.1** kinaonesha fahirisi ya rushwa katika sekta za umma.

Kielelezo Na. 9.1: Fahirisi ya Rushwa katika Sekta za Umma



SEHEMU YA TATU

SUALA MAALUMU KIMAENDELEO

SURA YA 10

SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TANZANIA MERCANTILE EXCHANGE)

Utangulizi

179. Soko la Bidhaa ni mahali ambapo wauzaji na wanunuzi hukutana kwa kuwakilishwa na mawakala walioidhinishwa kufanya biashara ya mikataba ya bidhaa. Mawakala hawa wanapaswa kuwa na leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na kuidhinishwa na Bodi ya Soko la Bidhaa kufanya kazi hiyo. Mawakala hao huendesha shughuli zao kwa kuzingatia taratibu za soko na sheria zilizopo za usimamizi wa Soko ili kuhakikisha kuwa biashara inaendeshwa kwa ufanisi ili kuepusha mambo yanayoweza kuyumbisha bei katika soko (market manipulations). Aidha, Soko la Bidhaa huwaleta pamoja wanunuzi wengi wa ndani na nje ya nchi ambao sio lazima wafike kwenye soko la bidhaa au nchini, kwa kuwa miamala hufanyika kwa njia za kielektroniki. Vile vile, mfumo huu unasimamiwa kisheria na hivyo hulinda wanunuzi na wauzaji. Katika utaratibu huo, muuzaji huwa na uhakika wa kupata malipo yake baada ya mauzo na hivyo, mnunuzi huwa na uhakika wa kupata mazao aliyoyanunua yakiwa katika ubora na uzito uliokubalika kwenye mkataba wa mauzo.

180. Kwa kutambua hilo, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ilianzisha Kampuni ya Soko la Bidhaa Tanzania ambayo ilisajiliwa mwaka 2014 chini ya Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002. Aidha, Kampuni hiyo ilipewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Desemba 2016 kwa mujibu wa Sheria ya Masoko ya Bidhaa ya mwaka 2015 na Kanuni zake za mwaka 2016. Uanzishwaji wa Soko la Bidhaa, upanuzi na uimarishaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni moja ya hatua zinazochukuliwa katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21) na Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP-2) ili kutatua tatizo la masoko linalowakabili wakulima nchini.

181. Hadi kufikia Machi 2018, Kampuni ya Soko la Bidhaa ilikuwa na wanahisa watatu waliowekeza mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 4.5 ili kuliwezesha Soko la Bidhaa kuanza kazi. Serikali kwa kupitia Msajili wa Hazina imewekeza jumla ya shilingi bilioni tatu, Mfuko wa Pensheni wa PSPF shilingi bilioni moja, na Benki ya Maendeleo TIB shilingi milioni 500. Aidha, wanahisa

wa Kampuni ya Soko la Bidhaa Tanzania wameteua Bodi inayoundwa na wajumbe nane kutoka Serikalini na taasisi za umma. Bodi hiyo, imechukua nafasi ya Bodi ya mpito ambayo ilifanya kazi tangu Kampuni iliposajiliwa mwaka 2014.

Uendeshaji wa Soko la Bidhaa Nchini

182. Kampuni ya Soko la Bidhaa inategemea kuanza na mauzo ya papo kwa papo ili kuwezesha wakulima kupata bei zinazotokana na ushindani wa haki, kufanya biashara kwa uwazi na gharama nafuu. Ili kuwawezesha wakulima na wenye viwanda kujikinga na mabadiliko ya bei yanayoathiri kipato chao na gharama za uzalishaji, Soko la Bidhaa linatarajia kuwa na mikataba ya bidhaa ambayo makubaliano ya bei na kiasi cha bidhaa hukubaliwa mwanzoni lakini utekelezaji wake hufanyika baada ya kipindi kilichokubaliwa. Mikataba hii itawawezesha wakulima kuwa na uhakika wa bei na kipato na kuwawezesha wenye viwanda kuwa na uhakika au kujikinga na mabadiliko ya bei. Aidha, Kampuni ya Soko la Bidhaa inaazimia kuwezesha mauzo ya bidhaa za aina mbalimbali na kutoa huduma zake kwa uwazi, uhakika, uadilifu, usalama na kwa gharama nafuu ili kuwanufaisha wadau wote katika sekta ya kilimo na maliasili kama madini. Juhudi zimeanza kuchukuliwa ili kuwezesha mfumo huu utekelezwe kwenye mazao ya ufuta, pamba, alizeti, mahindi, mbaazi, na mchele. Kutokana na kuboreshwa kwa masoko ya bidhaa nchini, kutakuwa na ongezeko la fursa katika soko la bidhaa na sekta zinazohusiana nazo kama viwanda vya kuchakata mazao, sekta ya usafiri, huduma za maghala, benki, bima na kadhalika.

Mfumo wa Kielektroniki wa Soko la Bidhaa

183. Soko la Bidhaa litaanza na mfumo wa utamkaji wa bei hadharani (Public Open Outcry) wakati mfumo wa mauzo wa kielektroniki unafanyiwa kazi. Mfumo huo wa kielektroniki utawezesha wadau wote muhimu kuelewa kinachofanyika katika Soko la Bidhaa. Aidha, andiko la mfumo wa kielektroniki wa mauzo na Stakabadhi za Ghala limetayarishwa na kuwasilishwa Benki Kuu ambayo inaratibu mchakato wa ununuzi wa mfumo huo. Mfumo huo utahusisha mfumo wa mauzo (trade matching engine), mfumo wa uhawilishaji bidhaa na malipo (Clearing and Settlement System), mfumo wa hifadhi ya milki ya bidhaa (Central Depository System) na mfumo wa utoaji wa taarifa za masoko (Market Information Dissemination System). Ufanisi wa masoko ya bidhaa hutegemea ufanisi wa mifumo ya kielektroniki katika mauzo ya bidhaa na utolewaji wa taarifa za bei na bidhaa kwa umma mara mauzo yanapofanyika


Mfumo wa Stakabadhi za Ghala

184. Mfumo wa stakabadhi za ghala ni utaratibu wa kibiashara unaotumika nchini ambapo bidhaa zinahifadhiwa ndani ya ghala lenye leseni maalum na mmiliki wa bidhaa husika kupewa stakabadhi inayothibitisha kuwa bidhaa zilizowekwa zinamilikiwa kihalali. Stakabadhi inayotolewa huweza kutumika kama dhamana ili kumwezesha mkulima kupata mkopo kwenye taasisi za fedha. Stakabadhi hizo huipa Benki uhakika wa marejesho ya mkopo pindi mazao yatakaponunuliwa. Mfumo kama huu pia unatekelezwa katika nchi nyingine duniani zikiwemo Ethiopia, Uingereza, Afrika ya Kusini na Rwanda. Kwa kufuata mfumo huu, wakulima wadogo na wa kati wakiwa katika ushirika au vikundi wanakuwa na nguvu ya soko na kuingia katika soko la ushindani ambalo ingekuwa vigumu kutokana na kukosekana kwa mitaji. Aidha mfumo huu unasaidia kuzuia upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi dhaifu wa mazao ili kusubiri kuuza wakati muafaka ambapo bei inakuwa ya kuridhisha.

185. Stakabadhi za ghala ni mfumo unaotumika chini ya Sheria ya Stakabadhi za Ghala Namba 10 ya mwaka 2005 ambayo ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria namba 3 ya Mwaka 2015 (Sura 339) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2006. Mfumo huu unasimamiwa na Bodi ya Usimamizi wa stakabadhi za ghala inayofanya kazi chini ya Wizara ya Viwanda Biashara na Uwekezaji. Aidha, mfumo huu kwa sasa unatumika katika maeneo mbalimbali nchini kwa mazao ya kahawa, pamba, korosho, mahindi na mpunga/mchele.


186. Kwa kuwa uhifadhi wa bidhaa kwenye maghala unazingatia viwango vya ubora, Mfumo huu umewezesha wakulima kuzingatia ubora kwenye upandaji, utunzaji na uvunaji wa mazao shambani na hivyo kuwezesha wanunuzi kupata mazao yenye ubora, kwa wingi, na mkulima kupata bei nzuri pale bidhaa husika inapouzwa. Aidha, uwepo wa Mfumo huu umekuwa msingi wa Serikali kuanzisha Soko la Bidhaa nchini.

Kielelezo Na. 10.1: Namna Mfumo Unavyofanya Kazi



187. Tangu kuanzishwa kwa mfumo wa stakabadhi za ghala, kumekuwa na mafanikio makubwa kwa wakulima nchini. Kwa mfano, zao la korosho lilianza kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala katika msimu wa mwaka 2007/08 katika mkoa wa Mtwara. Hadi kufikia Desemba 2017, sehemu kubwa ya wakulima wanaolima zao hili katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani walikuwa wamejumuishwa kwenye Mfumo huu. Aidha, Mfumo huu umeleta manufaa makubwa katika bei ya zao la korosho ambayo imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 17.8 kwa mwaka kutoka shilingi 720 kwa kilo mwaka 2007/08 hadi shilingi 2,350 kwa kilo mwaka 2016/17. **Kielelezo Na. 10.2** kinaonyesha mwenendo wa bei ya zao la korosho kwa kipindi kabla na baada ya kutumia mfumo wa stakabadhi za ghala.

Kielelezo Na. 10.2: Mwenendo wa Bei ya Zao la Korosho



Chanzo: Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

Mawakala wa Soko la Bidhaa

188. Jumla ya mawakala watano (5) wameidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana baada ya kukidhi vigezo vya kuwa wanachama wa Soko la Bidhaa. Kampuni ya Soko la Bidhaa inaendelea kushawishi washiriki katika biashara ya mazao waweze kuomba leseni toka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na uwanachama katika Soko la Bidhaa ambalo linahitaji washiriki wanaoelewa vyema biashara ya mazao.

Uhawilishaji wa Malipo Kupitia Benki

189. Mwaka 2017, Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Soko la Bidhaa iliidhinisha benki tano za CRDB, NMB, Standard Chartered, TIB Corporate na Azania kutoa huduma ya malipo kwenye Soko la Bidhaa. Uteuzi wa benki hizo ulizingatia miongozo ya malipo na mifumo ya ulipaji iliyotolewa na kamati ya pamoja ya ufundi ya Jumuiya ya Kimataifa ya Mamlaka za Masoko ya Dhamana na Umoja wa Benki (Bank for International Settlement). Mawakala wa Soko la Bidhaa watatakiwa kufungua akaunti mbili katika mojawapo ya benki hizo; akaunti ya kutunza fedha za wateja na akaunti ya uendeshaji ya wakala. Fedha za wateja na fedha za wakala hazitaruhusiwa kuchanganywa, na akaunti hizo

zitakuwa zikikaguliwa mara kwa mara ili kuhakikisha usalama wa fedha za wateja.

Mikataba Mahsusi ya Bidhaa

190. Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Kampuni ya Soko la Bidhaa, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Bodi ya Mazao Mchanganyiko iliandaa na kuidhinisha mikataba mahsusi ya bidhaa zitakazouzwa sokoni. Mazao ambayo mikataba yake imeandaliwa na kuidhinishwa ni ufuta, alizeti, korosho, mahindi, mbaazi, njugu mawe, soya, na mchele. Aidha, mikataba ya uuzaji wa madini kama vile dhahabu na shaba imeanza kuandaliwa kwa ushirikiano kati ya Wizara na taasisi husika. Lengo la mikataba hii ni kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa kwa kiasi kilichokubaliwa na kwa kiwango stahiki, sambamba na kumlinda mteja kutokana na mabadiliko ya bei.

Changamoto

191. Soko la bidhaa limeanzishwa ili kuwezesha mfumo wenye ufanisi wa upatikanaji wa bei kwa njia ya ushindani unaozingatia mahitaji na ugavi wa bidhaa. Aidha, Soko la bidhaa litaongeza uwazi katika biashara ya bidhaa na kupunguza gharama za miamala katika biashara ya mazao. Vile vile, soko la bidhaa linatarajia kuwa na utaratibu wa kuingia mikataba ya bidhaa itakayowasaidia wakulima na wenye viwanda kujikinga na athari za mabadiliko ya bei. Pamoja na faida hizo, uendeshaji wa Soko la Bidhaa nchini unakabiliwa na changamoto kadhaa ambazo zinapaswa kufanyiwa kazi na wadau husika kwenye sekta hii. Changamoto hizo ni pamoja na:

a) Kutoeleweka vyema kwa tofauti na kutegemeana kati ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa

192. Baadhi ya wadau bado hawajaelewa tofauti na uhusiano uliopo kati ya Soko la Bidhaa na Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, jambo ambalo limekuwa likikwamisha juhudi za kuzindua mauzo katika Soko la Bidhaa. Bado kuna wadau wanaona kuwa Soko la Bidhaa ni mshindani wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala wakati ambapo Soko la Bidhaa na Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ni mifumo inayotegemeana katika utendaji wao. Soko la Bidhaa litauimarisha zaidi Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwani litatatua tatizo la masoko kwa mazao yanayohifadhiwa ghalani na kupatiwa stakabadhi za ghala kwa kuweka mfumo wa mauzo wenye ushindani, uwazi, ufanisi, gharama nafuu na wenye uhakika

wa malipo kwa wakulima. Soko la Bidhaa huhusika na mauzo ya bidhaa baada ya mazao kukusanywa na kuhifadhiwa kwenye ghala na stakabadhi za ghala kutolewa. Kwa hiyo Soko la Bidhaa halitachukua nafasi ya mifumo mingine iliyopo yaani mfumo wa ukusanyaji mazao kwa kutumia vyama vya ushirika na vikundi vya wakulima na usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, vyama vya ushirika, wafanyabiashara na wabunge ili kujenga uelewa wa pamoja wa namna mifumo hiyo inavyofanya kazi.

b) Ushirikiano Hafifu kutoka kwa Wadau Mbalimbali

193. Pamoja na faida nyingi zinazotarajiwa kutoka kwenye mfumo wa Soko la Bidhaa, bado kumekosekana ushirikiano wa dhati kutoka kwa wadau mbalimbali, hususan Bodi za Mazao. Kampuni ya Soko la Bidhaa kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuhamasisha ushiriki wa wadau wote kuunga mkono Soko la Bidhaa kwa kuleta mazao wanayoyasimamia katika Soko la Bidhaa. Aidha, Serikali imeanzisha mchakato wa kuhuisha sheria zinazohusiana na biashara ya mazao.

Hitimisho

194. Ufanisi wa Soko la Bidhaa unategemea ushirikiano wa wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa ngazi za juu kitaifa. Soko hili litakuwa na mchango mkubwa katika kubadili mfumo wa kilimo kutoka kilimo cha kujikimu na kuwa cha biashara kutokana na uwepo wa masoko ya uhakika. Kwa kuzingatia ukubwa wa nchi na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, Tanzania ina nafasi kubwa ya kuongeza uzalishaji wa mazao na hivyo kupunguza umaskini.

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALIMBALI

SURA YA 11
KILIMO NA USHIRIKA

KILIMO

Uzalishaji wa Mazao ya Chakula

195. Mwaka 2017, uzalishaji wa mazao makuu ya chakula hususan mahindi, viazi, mimea jamii ya mikunde na mtama uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2016 kutokana na kuwepo kwa mvua za kutosha katika maeneo yanayozalisha mazao hayo. Hata hivyo, uzalishaji wa mazao ya mchele, mihogo na ndizi ulishuka kutokana na mvua zilizozidi kwa upande wa mchele, na magonjwa kwa upande wa mihogo na ndizi. Mwenendo wa uzalishaji umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 11.1.**

Jedwali Na. 11.1: Uzalishaji wa Mazao ya Chakula (Tani' 000)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%)
Mahindi	4,341	5,104	5,288	6,734	5,908	6,149	6,681	8.7
Mchele	1,461	1,170	1,342	1,681	1,937	2,229	1,594	(28.5)
Ngano	113	109	102	167	72	76	50	(34.2)
Mtama/Ulezi	1,119	1,052	1,074	1,246	1,007	1,003	1,064	6.1
Mihogo	1,549	1,821	1,878	1,664	1,962	2,205	1,342	(39.1)
Maharage/Mikunde	1,632	1,827	1,871	1,697	1,808	1,959	2,318	18.3
Ndizi	1,048	842	1,317	1,064	1,195	1,061	845	(20.4)
Viazi vitamu	1,710	1,418	1,808	1,761	1,645	1,491	2,008	34.7

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uzalishaji wa Mazao ya Biashara

196. Mwaka 2017, uzalishaji wa mazao makuu ya biashara uliongezeka kwa asilimia 14.2 kufikia tani 909,287 ikilinganishwa na upungufu wa asilimia 13.0 mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na uzingatiaji wa kanuni bora za kilimo, matumizi ya teknolojia na zana za kisasa, kuimarika kwa bei ya mazao katika soko la dunia na hali nzuri ya hewa. Mazao yaliyokuwa na ongezeko la uzalishaji ni pamoja na korosho, tumbaku, sukari na pareto. Hata hivyo, uzalishaji wa Pamba, chai, mkonge na kahawa ulishuka mwaka 2017 kutokana na uhaba wa mvua katika maeneo ya uzalishaji na matumizi hafifu ya pembejeo hususan mbegu bora na mbolea. Mwenendo wa uzalishaji mazao ya biashara umeainishwa katika **Jedwali Na. 11.2.**

Jedwali Na. 11.2: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara (Tani)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%)
Pamba	225,938	225,938	357,130	246,767	203,312	149,455	121,639	-18.6
Tumbaku	126,624	126,624	86,359	100,000	87,737	60,691	81,976	35.1
Sukari	260,055	262,880	296,697	294,421	304,007	293,075	326,447	11.4
Chai	33,000	32,810	33,700	33,000	35,750	32,629	26,975	-17.3
Pareto	5,700	5,700	6,100	7,090	6,050	2,011	2,150	6.9
Kahawa	33,219	33,219	71,200	47,301	41,674	60,921	48,329	-20.7
Mkonge	33,406	25,690	34,875	37,571	39,204	42,314	36,533	-13.7
Koroshho	160,000	160,000	127,947	123,449	197,933	155,416	265,238	70.7
Jumla	877,942	872,861	1,014,008	889,599	915,667	796,512	909,287	14.2

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta

197. Mwaka 2017, uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ya alizeti, karanga, ufuta, mawese na soya uliongezeka hadi tani 6,667,893 kutoka tani 6,301,147 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta kulichangiwa na kuendelea kuwepo kwa soko la uhakika pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati. Uzalishaji wa mazao hayo ni kama unavyoainishwa katika **Jedwali Na.11.3**.

Jedwali Na. 11.3: Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani)

Zao	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%)
Alizeti	786,902	1,125,000	2,625,000	2,755,000	2,878,500	2,995,500	3,112,500	3.9
Karanga	651,397	810,000	1,425,000	1,635,735	1,835,933	2,025,595	2,215,257	9.4
Ufuta	357,162	456,000	1,050,000	1,113,892	1,174,589	1,232,092	1,291,724	4.8
Mawese	17000	24880	40500	41000	41475	41925	42,277	0.8
Soya	2500	5620	5830	6025	6030	6035	6,135	1.7
Jumla	1,814,961	2,421,500	5,146,330	5,551,652	5,936,527	6,301,147	6,667,893	5.8

Chanzo: Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uzalishaji wa Mazao ya Bustani

198. Mwaka 2017, uzalishaji wa mazao ya bustani yakiwemo matunda, mboga, maua na viungo uliongezeka kwa asilimia 10.7 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2016. Hii ilitokana na kuhamasika kwa wakulima kuongeza uzalishaji kufuatia uwepo wa soko la uhakika, kuongezeka kwa usindikaji wa mazao hayo

na kuongezeka kwa ulaji wa matunda na mboga. **Jedwali Na. 11.4** linaonesha uzalishaji wa mazao ya bustani.

Jedwali Na.11. 4: Uzalishaji wa mazao ya Bustani (Tani)

Zao	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%)
Matunda	3,938,730	4,096,280	4,416,690	4,574,240	4,711,000	5,243,343	11.3
Mboga	901,680	937,750	1,005,305	1,041,375	1,189,000	1,298,388	9.2
Maua	9,850	10,200	10,790	11,140	11,500	11,615	1.0
Viungo	7,370	8,125	8,377	8,609	20,400	22,062	8.1
Jumla	4,857,630	5,052,355	5,441,162	5,635,364	5,931,900	6,563,793	10.7

Chanzo: Wizara ya Kilimo

Uwekezaji katika Shughuli za Kiuchumi za Kilimo

199. Mwaka 2017, jumla ya matrekta makubwa mapya 1,604, madogo 378 na mashine 27 za kuvunia mpunga (combine harvester) yaliingizwa nchini ikilinganishwa na matrekta makubwa 900 na madogo 260 yaliyoingizwa nchini mwaka 2016. Matrekta makubwa 870 yaliyoingizwa nchini mwaka 2017 yalikuwa kamili na yaliyobaki yalikuwa vipande vipande. Idadi ya matrekta yaliyoingizwa nchini iliongezeka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya zana bora za kilimo na juhudi za Serikali kuboresha kiwanda cha kuunganisha matrekta kilichoko Kibaha mkoani Pwani ambacho kilianza kuunganisha matrekta. Aidha, kati ya matrekta makubwa yaliyoingizwa nchini mwaka 2017, matrekta 734 aina ya URSUS yalitoka nchini Poland yakiwa hayajaunganishwa. Hadi Desemba 2017, idadi ya matrekta ya URSUS yaliyounganishwa katika kiwanda cha Kibaha (fully assembled) yalikuwa 420.

Mwenendo wa Bei na Masoko ya Mazao ya Kilimo

200. Mwaka 2017, bei ya zao la pareto ilipanda kutoka kati ya shilingi 1,500 hadi shilingi 2,700 mwaka 2016 na kufikia shilingi 2,000 hadi shilingi 3,000 kwa kilo. Bei ya zao la majani mabichi ya chai iliongezeka kutoka shilingi 176 kwa kilo mwaka 2016 hadi kufikia shilingi 285 kwa kilo. Aidha, kwa upande wa mkoa wa Njombe, kampuni ya chai ya Unilever ilitoa bei ya shilingi 305 kwa kilo kwa wakulima wadogo kama bei ya awali. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji katika viwanda vya kusindika chai nchini hususan viwanda vipya vya chai vya Unilever, Chai leo Ltd, Rift Valley Tea Solutions, Tea Plus Investment na TEAZANIA. Vile vile, bei elekezi ya pamba ilipanda kutoka shilingi 1,000 mwaka 2016 hadi shilingi 1,300 kwa kilo mwaka 2017. Bei ya zao la korosho ilipanda kutoka shilingi 1,820 hadi 2,900 mwaka 2016 na kufikia kati ya shilingi

1,877 hadi 4,000 kwa kilo mwaka 2017. Vile vile, bei elekezi ya korosho ilibaki kuwa shilingi 1,200 kwa kilo kutoka mwaka 2016 hadi 2017. Kuimarika kwa bei za mazao kulitokana na juhudi za bodi za mazao kumlinda mkulima kwa kuhakikisha kuwa wakulima wanapata bei stahiki.

Huduma za Ugani

201. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kupeleka teknolojia za kisasa za kilimo bora kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji na tija. Wakulima wawezeshaji 100 kutoka skimu za umwagiliaji za Njange, Mbogo, Komtonga, Mvumi, Kigugu na Msolwa Ujamaa walipewa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga kupitia mfumo wa kilimo shadidi. Wakulima waliopata mafunzo walifundisha wakulima 454 kupitia mashamba darasa. Aidha, wataalam 70 kutoka ngazi ya mkoa na halmashauri walipewa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga kupitia mfumo wa kilimo shadidi.

Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo

202. Mwaka 2017, Serikali ilitoa ufadhili kwa wanachuo 1,956 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala ikilinganishwa na ufadhili wa wanachuo 2,000 mwaka 2016. Aidha, wanachuo 246 wanaojilipia wenyewe walidahiliwa katika ngazi ya Astashahada na Stashahada ikilinganishwa na wanachuo 456 waliodahiliwa mwaka 2016. Mwaka 2017 vyuo sita vya kilimo vya KATC, Mtwara, Ukiriguru, Igurusi, Ilonga na Tumbi, kupitia mradi wa TANRICE2 vilitoa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji mpunga kwa wakulima 4,781 ikilinganishwa na wakulima 4,247 mwaka 2016.

Utafiti

203. Mwaka 2017, Serikali kwa kushirikiana na taasisi za kilimo 35 (21 Serikali na 14 Taasisi Binafsi) kupitia vituo vya utafiti iligundua na kuidhinisha aina ya mbegu bora mpya 14 na kuendeleza mbegu 29 zilizogunduliwa mwaka 2016 za mazao ya maharage, viazi vitamu, mahindi, korosho na viazi mviringo. Aidha, zilizalishwa mbegu mama na za awali (Breeder and Pre- basic seeds) za mazao mbalimbali ambapo mbegu mama zilizozalishwa ni pamba kilo 2,600 na viazi mviringo miche 60,000. Mbegu za awali zilizozalishwa ni pamba kilo 21,600; muhogo pingili 2,008,000; viazi vitamu vipando 3,476,750; viazi mviringo kilo 5,150; mpunga kilo 2940; mahindi kilo 11,300; ngano kilo 1,560;

soya kilo1,900; maharage kilo 43,900; migomba miche 1,830; na parachichi miche 3,390. Vile vile, vizazi (germplasm) 1,228 vya mbegu za mpunga na 172 vya ulezi vilikusanywa na kutunzwa vituoni.

Ruzuku ya Pembejeo

204. Mwaka 2017, Serikali iliwezesha upatikanaji wa mbolea kufikia tani 277,935 sawa na asilimia 57.3 ya mahitaji ya tani 485,000. Kutofikiwa kwa lengo kulitokana na uwezo mdogo wa wananchi kununua pembejeo za kilimo zinazohitajika. Aidha, jumla ya kaya 378,900 zilinufaika na ruzuku ya mbolea mwaka 2017 ikilinganishwa na kaya 99,926 mwaka 2016 kufuatia kuimarishwa kwa utaratibu wa ugawaji mbolea. Kwa upande mwingine, Serikali kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania ilitoa ruzuku ya mbolea tani 32,394 kwa wakulima wa zao la mahindi na mpunga nchini ikilinganishwa na tani 99,993 zilizotolewa mwaka 2016. Kati ya mbolea ya ruzuku iliyotolewa mwaka 2017, mbolea ya kupandia ilikuwa tani 14,421 na mbolea ya kukuzia tani 17,973. Katika kuongeza upatikanaji na kupunguza bei za mbolea kwa wakulima, Serikali iliandaa Kanuni za Ununuzi wa Mbolea kwa Pamoja za Mwaka 2017 na mwongozo wa utekelezaji.

205. Mwaka 2017, upatikanaji wa mbegu bora ulifikia tani 28,278.2 sawa na asilimia 47.13 ya mahitaji ya tani 60,000 kwa mwaka. Kati ya kiasi hicho cha mbegu bora, tani 11,802.44 zilizalishwa nchini na tani 16,475.76 zilingizwa kutoka nje ya nchi. Wakala wa Mbegu za Kilimo uliongeza uzalishaji wa mbegu bora za nafaka na mikunde kutoka tani 2,804 mwaka 2015/16 hadi tani 2,884 mwaka 2016/17. Aidha, Wakala ulizalisha miche bora ya matunda 20,435 na vipando bora vya muhogo pingili 12,772,210.

206. Mwaka 2017, Serikali ilitoa ruzuku ya mbegu bora tani 3,731.5 kwa wakulima wa mazao ya mahindi na mpunga kwa kaya 378,900 nchini ikilinganishwa na tani 10,270.86 kwa kaya 999,926 mwaka 2016. Kati ya mbegu zilizosambazwa kwa wakulima, tani 3,407 zilikuwa za mahindi na tani 333.5 za mpunga. Aidha, Serikali ilitoa ruzuku katika vituo vya Lyamungo, Mbimba, Ugano, Mwayaya, Maruku na Sirari ambapo miche bora ya kahawa 2,412,805 ilizalishwa na kusambazwa katika mikoa mbalimbali nchini. Vile vile, miche bora ya chai 7,100,000 ilizalishwa kupitia Wakala wa Kuendeleza Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) katika eneo la Igominyi - Njombe. Kwa upande mwingine, Serikali ilitoa ruzuku kwa ajili ya viuatilifu vya zao la korosho na ekapaki 1,803,586 za viuatilifu vya zao la pamba.

Mfuko wa Pembejeo

207. Mwaka 2017, Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo ilitoa mikopo ya matrekta makubwa 46 ikilinganishwa na matrekta 65 yaliyotolewa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 29.2. Aidha, mwaka 2017, mikopo 23 ilitolewa kwa ajili ya pembejeo mchanganyiko kama vile mbolea za viwandani, mbegu bora na madawa ya mifugo ikilinganishwa na mikopo 28 iliyotolewa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 17.9. Vile vile, katika kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kuepukana na utegemezi wa mvua, Mfuko ulitoa mikopo 13 ya zana za umwagiliaji ikilinganishwa na mikopo 6 mwaka 2016. Kadhalika, Mfuko ulitoa mikopo miwili ya mashine za usindikaji mwaka 2017 ikilinganishwa na mikopo mmoja mwaka 2016.

MIFUGO

Uzalishaji wa Mifugo na Mazao yake

208. Mwaka 2017, idadi ya mifugo ilifikia ng'ombe milioni 28.4, mbuzi milioni 17.7 na kondoo milioni 5.1 ikilinganishwa na ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 17.1 na kondoo milioni 9.2 mwaka 2016. Aidha, mwaka 2017 kulikuwa na kuku wa asili milioni 37.4 na nguruwe milioni 1.85 ikilinganishwa na kuku wa asili milioni 42.0 na nguruwe milioni 2.67 mwaka 2016.

209. Mwaka 2017, uzalishaji wa nyama ulipungua kwa asilimia 14.0 kutoka tani 648,810 mwaka 2016 hadi tani 558,164. Kati ya hizo, uzalishaji wa nyama ya ng'ombe ulikuwa tani 394,604; nyama ya mbuzi na kondoo tani 81,064; nyama ya kuku tani 63,597; na nyama ya nguruwe tani 18,899 ikilinganishwa na nyama ya ng'ombe tani 323,775; nyama ya mbuzi na kondoo tani 129,292; nyama ya kuku tani 104,292; na nyama ya nguruwe tani 91,451 mwaka 2016. Hali hiyo ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya nyama nchini. Kwa upande wa mauzo ya nyama nje ya nchi, jumla ya tani 3,162.65 za nyama ziliuzwa katika nchi za Dubai, Iraq na Vietnam. Kati ya hizo, nyama ya mbuzi ilikuwa tani 711.82, nyama ya ng'ombe tani 439.03, nyama ya kondoo tani 222.74 na nyama ya punda tani 1,789.06. Vile vile, jumla ya tani 890.67 za nyama zilingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini na Uingereza ikijumuisha nyama ya nguruwe tani 366.34, nyama ya ng'ombe tani 512.06 na nyama ya kondoo tani 12.27.

210. Mwaka 2017, uzalishaji wa maziwa nchini ulipungua kwa asilimia 2.3 kutoka lita bilioni 2.13 mwaka 2016 hadi lita bilioni 2.09. Kati ya kiasi kilichozaishwa, lita milioni 626.1 zilitokana na ng'ombe wa kisasa na lita

bilioni 1.46 zilitokana na ng'ombe wa asili. Kupungua kwa uzalishaji wa maziwa kulitokana na upungufu wa malisho kulikosababishwa na ukame katika maeneo mengi ya ufugaji. Hali hiyo ya ukame iliathiri viwanda vya kusindika maziwa, hivyo kusababisha baadhi ya viwanda kusitisha usindikaji na vilivyobaki kuzalisha chini ya uwezo. Kiwango cha usindikaji kilipungua kwa asilimia 34.4 kutoka lita milioni 61.18 kwenye viwanda 82 mwaka 2016 kufikia lita milioni 40.13 kwenye viwanda 65 vinavyofanya kazi mwaka 2017.

Jedwali Na.11.5: Uzalishaji wa Mazao Yatokanayo na Mifugo

Aina ya Zao	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Uzalishaji wa Maziwa katika lita '000								
Ng'ombe wa Asili	997,261	1,135,422	1,297,775	1,339,613	1,381,451	1,381,451	1,423,288	1,460,900
Ngombe wa Kisasa	652,596	608,800	597,161	623,865	650,570	677,275	703,979	626,100
Jumla	1,649,857	1,744,222	1,894,936	1,963,478	2,032,021	2,058,726	2,127,267	2,087,000
Uzalishaji Nyama katika kilo'000								
Ng'ombe	243,943	262,606		299,581	309,086	319,112	323,775	394,604
Mbuzi/Kondoo	86,634	103,709		115,652	120,199	124,745	129,292	81,064
Nguruwe	38,180	43,647		50,814	74,174	54,360	91,451	18,899
Kuku	80,916	93,534		87,408	95,292	99,540	104,292	63,597
Jumla	449,673	503,496		553,455	598,751	597,757	648,810	558,164
Uzalishaji Mayai katika '000								
Mayai	2,917,875	3,339,566		3,725,200	3,899,569	4,153,800	4,353,182	2,758,000

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

211. Mwaka 2017, uzalishaji wa mayai ulipungua hadi mayai milioni 2,758.0 kutoka mayai milioni 4,353.2 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 36.6. Hali hii ilitokana na kupungua kwa mahitaji ya ulaji wa mayai pamoja na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na hivyo kulazimika kwa baadhi ya wadau kupunguza uzalishaji pamoja na idadi ya kuku. Aidha, uzalishaji wa vifaranga wa mayai na wa nyama ulipungua kutoka vifaranga milioni 68.3 vilivyozalishwa mwaka 2016 na kufikia vifaranga milioni 64.3 mwaka 2017.

Uzalishaji na Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo

212. Mwaka 2017, mbegu bora za aina mbalimbali za malisho zenye ujazo wa tani 3.9 zilizalishwa ikilinganishwa na tani 49.96 zilizozalishwa mwaka 2016. Aidha, uzalishaji wa majani ya hei ulikuwa marobota 1,120,246 mwaka 2017 ikilinganishwa na marobota 1,140,266 yaliyozalishwa mwaka 2016. Kati ya kiasi hicho, marobota 467,104 yalizalishwa katika mashamba ya Serikali na

marobota 653,142 yalizalishwa katika mashamba ya sekta binafsi na kuuzwa kwa wafugaji. Kupungua kwa uzalishaji kulitokana na ukame katika maeneo ya uzalishaji wa malisho.

213. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuratibu usindikaji na kusimamia ubora wa vyakula vya mifugo ambapo maeneo 35 ya vyakula vya mifugo yalikaguliwa na kusajiliwa. Aidha, mwaka 2017 sekta binafsi ilizalisha tani 1,100,000 za vyakula vya mifugo ikilinganishwa na tani 1,903,000 zilizozalishwa mwaka 2016. Kupungua kwa usindikaji wa vyakula kulitokana na kupungua kwa mahitaji ya vyakula vya mifugo kulikotokana na kuongezeka kwa bei ya vyakula hivyo.

Biashara ya Mifugo na Mazao Yake

214. Mwaka 2017, jumla ya mifugo hai iliyojumuisha ng'ombe 1,618,047; mbuzi 1,278,182; na kondoo 278,595 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.36 iliuzwa katika minada ya ndani ikilinganishwa na ng'ombe 1,337,095; mbuzi 1,056,218; na kondoo 230,221 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.03 waliouzwa mwaka 2016. Aidha, idadi ya mifugo hai iliyouzwa nje ya nchi iliongezeka kutoka ng'ombe 2,139 mwaka 2016 hadi ng'ombe 26,515 na mbuzi 11,553 mwaka 2017. Ongezeko la biashara ya mifugo hai ndani na nje ya nchi lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya masoko ikiwemo kukarabati na kusimika mizani katika minada, hususan katika minada ya upili na ya mipakani.

215. Mwaka 2017, ngozi za ng'ombe zilizouzwa nje ya nchi zilipungua kufikia vipande 1,215,030 kutoka vipande 1,575,139 mwaka 2016 na vipande vya ngozi ya mbuzi na kondoo vilipungua kutoka vipande 1,124,000 mwaka 2016 hadi kufikia vipande 928,115 mwaka 2017. Aidha, jumla ya tani 6,482 za ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zilizosindikwa zenye thamani ya bilioni 9.45 ziliuzwa nje ya nchi kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na tani 2,592 za ngozi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zilizosindikwa zenye thamani ya shilingi bilioni 5.10 zilizouzwa mwaka 2016. Vile vile, jumla ya tani 4,835 za ngozi ghafi za ng'ombe, mbuzi na kondoo zenye thamani ya bilioni 6.6 ziliuzwa nje ya nchi kwa mwaka 2017 ikilinganishwa na tani 1,758 za ngozi ghafi zenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 zilizouzwa mwaka 2016.

Jedwali Na. 11.6: Ukusanyaji na Uuzaji wa Ngozi Ndani na Nje ya Nchi

UKUSANYAJI NGOZI			
Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi /Kondoo	Thamani shilingi'000'
2002	1,400,0000	1,050,000	4,500,000
2003	1,400,000	1,260,000	5,500,000
2004	1,600,000	1,850,000	6,500,000
2005	1,600,000	2,250,160	5,500,000
2006	1,660,000	2,350,000	6,800,000
2007	1,980,000	2,720,000	8,700,000
2008	2,500,000	3,400,000	13,500,000
2009	1,650,000	4,240,000	10,900,000
2010	1,500,000	3,050,000	8,500,000
2011	2,500,000	2,600,000	16,100,000
2012	2,800,000	4,050,000	32,988,000
2013	2,900,000	4,300,000	34,673,500
2014	3,100,000	3,350,000	32,000,000
2015	4,050,000	4,640,000	85,165,000
2016	4,620,000	4,220,000	22,962,000
2017	4,100,000	5,6000,000	32,600,000
B. UUZAJI NGOZI NJE			
Mwaka	Ngozi za Ng'ombe	Ngozi za Mbuzi /Kondoo	Thamani shilingi'000'
2002	1,200,000	676,700	4,000,000
2003	1,300,000	900,000	4,600,000
2004	1,774,000	1,919,000	5,712,000
2005	1,400,000	1,797,155	4,025,400
2006	1,363,721	2,078,510	7,500,000
2007	1,700,000	1,980,530	16,200,000
2008	2,300,000	2,700,000	21,500,000
2009	982,668	3,469,936	12,800,000
2010	739,315	2,088,582	8,191,803
2011	1,719,506	1,561,000	17,400,000
2012	2,000,000	3,600,000	17,500,000
2013	1,269,060	2,582,525	63,600,000
2014	1,263,472	2,716,436	76,300,000
2015	1,388,139	1,020,000	39,200,000
2016	1,575,139	1,124,000	52,500,000
2017	1,215,030	928,115	42,790,000

Chanzo: Wizara ya Mifugo na Uvuvi

Jedwali Na. 11.7: Mwenendo wa Mauzo ya Ngozi Nje

Mwaka	Ngozi ghafi		Ngozi zilizoongezwa thamani		Jumla ya Thamani (Shilingi milioni)	Ngozi zilizoongezwa thamani (%)
	Kiasi kg ('000')	Thamani (shilingi Milioni)	Kiasi kg ('000')	Thamani (shilingi Milioni)		
2007	10,569	8,571	5,566	16,036	24,607	65.2
2008	5,482	5,107	6,749	12,093	17,200	70.3
2009	1,666	1,433	5,026	6,797	8,230	82.6
2010	3,241	2,438	7,217	8,672	11,110	78.1
2011	8,141	6,831	7,904	17,005	23,836	71.3
2012	2,887	3,445	5,011	17,375	20,820	83.5
2013	2	3	7,061	22,686	22,689	99.9
2014	1,559	2,231	11,186	33,372	35,603	93.7
2015	372	1,185	6,594	20,878	22,063	94.6
2016	1,758	2,397	2,592	5,097	7,494	68.0
2017	4,835	6,592	6,482	9,452	160,044	58.9

Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2017

MAENDELEO YA USHIRIKA

216. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza majukumu yake ya usimamizi, udhibiti na uhamasishaji wa sekta ya ushirika. Katika kipindi hicho, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vilitoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 1,007 kwa wanachama ikilinganishwa na shilingi bilioni 900 zilizotolewa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 11.9. Aidha, akiba za wanachama katika ushirika wa akiba na mikopo iliongezeka hadi shilingi bilioni 561 ikilinganishwa na shilingi bilioni 331 mwaka 2016. Vile vile, thamani ya amana iliongezeka kutoka shilingi bilioni 47 mwaka 2016 hadi shilingi bilioni 53 mwaka 2017.

217. Mwaka 2017, Serikali kupitia Bodi ya Leseni za Maghala, Bodi ya Korosho, Vyama Vikuu vya Ushirika ilisimamia minada 57 na biashara ya zao la korosho inayoendeshwa kupitia Vyama vya Ushirika chini ya Mfumo wa Stakabadi Ghalani katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Ruvuma. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa ushirika iliratibu na kuwezesha kufanyika kwa majukwaa ya ushirika kwa mikoa 23 ya Manyara, Pwani, Arusha, Tanga, Njombe, Mbeya, Katavi, Rukwa, Lindi, Mwanza, Kagera, Singida, Tabora, Kigoma, Songwe, Iringa, Shinyanga, Simiyu, Ruvuma, Dar es Salaam, Mara, Geita na Dodoma ambapo Jukwaa la Ushirika la kitaifa lilifanyika. Majukwaa hayo yaliwezesha kuundwa na kufufuliwa kwa Kamati za

Ushirika za mikoa husika zitakazosimamia shughuli mbalimbali za ushirika katika mikoa hiyo. Vile vile, Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ilifanya uhamasishaji kwa wakulima wanachama 9,188 wa vyama vya ushirika katika mikoa ya Lindi na Mtwara kujiunga na huduma za Bima ya Afya kwa hiari ijulikanayo kama Ushirika Afya. Wakulima 345 wa mikoa hiyo walihamasishwa kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa GEPF kampeni zinazojulikana kama Ushirika Akiba.

218. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini changamoto katika sekta ya ushirika na kuainisha maeneo ya kiutafiti na mahitaji ya mafunzo ndani ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika na vyama vya ushirika nchini. Katika kipindi hicho, zilifanyika pembuzi yakinifu tatu (3) kwenye vyama vya ushirika vya mazao vya mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara na Lindi pamoja na kuandaa Mpango Mkakati mmoja (1) wa chama cha wachimbaji wadogo cha Mafurungu. Aidha, tafiti za namna ya kuimarisha vyama vya ushirika vya Kilimo na Masoko vya mazao zilifanyika katika zao la zabibu kwa mkoa wa Dodoma; na kahawa kwa mikoa ya kanda ya ziwa pamoja na mkoa wa Kilimanjaro. Vile vile, mafunzo yalitolewa kwa watendaji 46 wa vyama vikuu na miradi ya pamoja na wa vyama 15 vya akiba na mikopo.

UZALISHAJI WA MIWA NA SUKARI NCHINI

Jedwali Na. 35

Msimu ¹	Miwa				Sukari		
mwaka 2017 kutoka dola za Marekani milioni 60.5 mwaka 2016. Katika kipindi hicho, Serikali ilifanya mnada wa tatu wa kimataifa wa Tanzanite ghafi ambapo jumla ya makampuni 60 kutoka nchi saba zilijisajili na kushiriki mnada huo. Nchi hizo zilikuwa ni Tanzania, Sri-Lanka, Hong Kong, India, Thailand, China na Marekani. Katika mnada huo, jumla ya gramu 47,201.00 za Tanzanite ghafi ziliuzwa kwa dola za Marekani 820,744.00 sawa na shilingi 1,839,476,075.13. Kutokana na mauzo hayo, Serikali inatarajia kupata mrabaha na ada ya ukaguzi dola za Marekani 57,452.08 sawa na shilingi 128,673,325.26. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro inatarajia kupata shilingi 5,518,428.23 kama tozo ya huduma. Vile vile, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha sheria na kanuni za kusimamia minada ya madini ili kuongeza mapato, ufanisi na tija katika minada itakayofuata.

Makaa ya Mawe

236. Mwaka 2017, kulikuwa na ongezeko kubwa la uzalishaji wa makaa ya mawe lililotokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kuimarika kwa uzalishaji wa makaa ya mawe katika mgodi wa TANCOAL na Magamba; kuanza kwa uzalishaji kwenye migodi ya Edenville International (T) Ltd na Kabulo unaomilikiwa na STAMICO; na kuongezeka kwa wanunuzi kutoka nje na ndani ya nchi kutokana na Serikali kuzuia uagizaji wa makaa ya mawe kutoka nje ya nchi. Uzalishaji wa makaa ya mawe uliongezeka kwa asilimia 102.4 na kufikia tani 558,553.14 mwaka 2017 kutoka tani 276,030 mwaka 2016. Aidha, thamani ya mauzo ya makaa ya mawe iliongezeka kwa asilimia 92.1 hadi kufikia dola za Marekani milioni 22.25 mwaka 2017, kutoka dola za Marekani milioni 11.58 mwaka 2016.

Madini Mengine

237. Uzalishaji wa kaolin uliongezeka na kufikia tani 13,815.62 mwaka 2017 kutoka tani 656.31 zilizozalishwa mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kwa uchimbaji wa kaolin katika wilaya ya Kisarawe, ambapo madini haya yanatumika kwenye viwanda vipya vya marumaru vilivyopo Kibaha na Mkuranga. Aidha, thamani ya mauzo ya kaolin iliongezeka kwa asilimia 105.2 hadi dola za Marekani 62,380.38 mwaka 2017 kutoka dola za Marekani 30,400.89 mwaka 2016. Uzalishaji wa jasi ulikuwa tani 123,644.69 mwaka 2017 ikilinganishwa na tani 213,743.57 mwaka 2016. Mauzo ya jasi yalikuwa dola za

Marekani milioni 3.19 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 6.28 mwaka 2016.

238. Mwaka 2017, uzalishaji wa madini ya chumvi ulikuwa tani 100,017.07 ikilinganishwa na tani 145,718 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 31.4. Thamani ya mauzo ya chumvi ilikuwa dola za Marekani milioni 3.80 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola milioni 4.8 mwaka 2016, ambao ni upungufu wa asilimia 20.8. Uzalishaji wa madini ya bati ulikuwa tani 91.42 ikilinganishwa na tani 138.22 mwaka 2016. Mauzo ya bati yalikuwa dola za Marekani milioni 1.04 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1.5 mwaka 2016. Aidha, uzalishaji wa chokaa ulikuwa tani 3,300,898.66 ikilinganishwa na tani 4,170,056.87 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 20.8. Thamani ya mauzo ya chokaa iliongezeka kwa asilimia 21.6 hadi kufikia dola za Marekani milioni 27.61 mwaka 2017 kutoka dola za Marekani milioni 22.71 mwaka 2016.

Uongezaji Thamani Madini

239. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuhamasisha uwekezaji katika uongezaji thamani wa madini kupitia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017. Katika kipindi hicho, jumla ya wafanyabiashara 103 wa madini ya vito walisajiliwa na kuwekeza mashine 357 za kukata, kusanifu na kung'arisha madini ya vito. Aidha, Kituo cha Uongezaji Thamani Madini Arusha kiliendelea kutoa mafunzo ya usanifu wa madini ya vito ambapo wanafunzi 18 walidahiliwa mwaka 2017 na hivyo kufanya Kituo hicho kuwa na jumla ya wahitimu 83 tangu kuanzishwa kwa mafunzo hayo mwaka 2014.

UCHIMBAJI WA MADINI: KIASI KILICHOPATIKANA

Jedwali Na.56

MADINI	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Almasi	Carat	237676	181874	80498	28378	127174	179633	252875	216491	237685	304456
Dhahabu	Kg	36434	39112	39448	37085	39012	42534	40481	43293	45155	43490
Gemstones	Kg	1858287	1068481	2646109	1241581	1237625	1692436	3083765	1872915	2554932	1186237
Chumvi	Tani	25897	27393	34455	32297	34016	36032	54757	92158	145718	100017
Phosphate	Tani	28684	752	17180	848512	570626	397020	738000	222800	23658	1351
Limestone	000 Tani	1282	1284	1437	202	1224	35529	873	2945	4170	3301
Tin Ore	Tani	-	-	3	-	-	2	79	179	138	91
Gypsum	Tani	55730	8105	26918	9288	91610	171567	200179	239302	213744	123645
Makaa ya mawe	Tani	15242	1	179	80710	78672	84772	246128	257321	276030	563053
Pozolana	Tani	260403	61501	60320	113489	75193	79452	68925	342628	230045	79085
Kaolin	Tani	13926	18624	58	178	1422	907	3809	1953	656	13816
Madini ya fedha	Kg	10388	8231	12470	10399	11227	12159	14493	15569	17984	10911
Shaba	Pound	6288503	4451697	11741898	7531164	12426025	12749548	14027008	14252341	15762430	2933941
Bauxite	Tani	20601	122920	39326000	29520000	28433930	39977300	25641201	204956	72779	12090

Chanzo: Wizara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

Carat = 0.205 gm

MADINI YALIYOUZWA NCHI ZA NJE 2013 - 2017

Jedwali Na. 57

Aina ya madini	Kipimo	Kiasi kilichouzwa					Thamani ('000 US \$)				
		2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017
Almasi (Rough)	'000 Carats	179633	252875	216491	239305	304456	46013	82053	56003	85090	67510
Almasi (iliyokatwa)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Almasi (Construct goods)	'000 Carats	-	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Dhahabu	'000 Gramu	42534	40481	43358	45155	43490	1735708	1640072	1609392	1824815	1636575
Mawe ya thamani	'000 Gramu	1086532	3083765	1872915	2944107	1185697	62453	49146	46067	60483	53596
Chumvi	Tani	33210	54757	92158	145718	100017	3785	5275	5071	4806	3803
Phosphate	Tani	397020	738000	222800	23658	1351	225	140	126	721	585
Bati	Tani	-	79	179	138	91	-	907	959	1499	1037
Jasi	Tani	-	200179	235920	213744	123645	231	2518	4445	6279	3187
Grafiti	Tani	-	25	30	1180	128	-	3	5	2132	18
Fedha	000Grams	11013	14493	15569	17984	10911	17214	10283	7626	9901	5850
Shaba	0001b	12654045	14027008	14252	16247	2934	42134	43675	35658	35421	7741
Madini ya viwandani	Tani	-	98	151297	4769577	708047	-	9	3254	78491	29896
Bauxite	Tani	39977300	25641201	204956	74660	12090	35827	20014	325	1242	898
Jumla ('000 US \$)							1943590	1854095	1768930	2110877	1810697

Chanzo: Wizara ya Nishati na Madini, Idara ya Madini

- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 14

VIWANDA NA BIASHARA

Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo

240. Katika uendelezaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo, Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF) ulitoa mafunzo kwa wajasiriamali 54,894 mwaka 2017 ikilinganishwa na wajasiriamali 39,319 waliopatiwa mafunzo mwaka 2016. Mafunzo hayo yalihusu kilimo bora, kuzalisha mizinga ya nyuki ya kisasa, kubuni mavazi na ushonaji, usindikaji wa vyakula, utengenezaji wa mitambo na mashine za aina mbalimbali, matumizi ya mbegu bora, ukamuaji wa mafuta na utengenezaji wa bidhaa mbalimbali. Ongezeko hili la ushiriki ni ishara ya mwamko wa wajasiriamali katika fursa za kiuchumi zinazojitokeza kwa lengo la kujiongezea kipato na kujikwamua kiuchumi. Aidha, Mfuko ulitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 61,374.2 kwa wajasiriamali 87,315 ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 49,073.8 kwa wajasiriamali 66,253 mwaka 2016. Mikopo hiyo iliwezesha upatikanaji wa fursa za ajira 178,438 ikilinganishwa na fursa za ajira 133,506 mwaka 2016.

241. Mwaka 2017, Serikali kupitia TanTrade ilitoa mafunzo kwa wazalishaji na wafanyabiashara 410 katika mikoa ya Kigoma, Kagera, Shinyanga, Mwanza, Lindi, Mtwara na Dar es Salaam ili kuwawezesha kufanya biashara kiushindani kwa kuzingatia ubora katika mnyororo wa thamani ya bidhaa za alizeti, asali na bidhaa za ngozi. Wajasiriamali hao walifundishwa mbinu bora za uzalishaji, ufungashaji, uongezaji ubora wa bidhaa na namna ya kutafuta masoko ya bidhaa hizo. Aidha, Serikali kupitia TanTrade ilitoa ushauri kwa wajasiriamali 20,036 ili kuwawezesha kujiendesha kiushindani. Ushauri huo ni pamoja na: namna ya kubuni, kuanzisha na kuendesha biashara kwa njia ya vikundi; kuandaa maandiko ya miradi; kutengeneza rajamu (brand) za bidhaa; kutengeneza nembo za kampuni; machapisho mbalimbali yanayotumika kutangaza bidhaa; na umuhimu wa kushiriki maonesho kwa lengo la kutangaza biashara.

242. Mwaka 2017, makampuni 1,577 yanayojishughulisha na uuzaji wa viungo, asali, maharage, mbaazi, soya, mboga na matunda, chai, kahawa, korosho, miwa, katani, chakula cha mifugo, ufugaji na usindikaji wa samaki, bidhaa za ngozi na vifaa vya ujenzi yaliunganishwa na wanunuzi wa bidhaa hizo katika

masoko ya ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha mauzo ya bidhaa nje yanaongezeka.

243. Mwaka 2017, teknolojia 312 zilibuniwa na machine ndogondogo 775 zilitengenezwa chini ya uangalizi wa SIDO kupitia vituo saba vya kuendeleza teknolojia ikilinganishwa na teknolojia 252 na mashine ndogondogo 659 zilizotengenezwa mwaka 2016. Sambamba na hilo, idadi ya mashine mpya zilizotengenezwa kutokana na teknolojia mpya zinazosambazwa kwa wajasiriamali wadogo zilikuwa 40 ikilinganishwa na mashine 33 mwaka 2016. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya teknolojia mpya na mashine mpya. Aidha, idadi ya wajasiriamali waliopatiwa huduma ya ushauri wa mashine mpya zilizoanzishwa ilikuwa 1,592 ikilinganishwa na wajasiriamali 1,253 mwaka 2016. Vile vile, jumla ya wajasiriamali 23,376 walirasimisha biashara zao ikilinganishwa na wajasiriamali 13,249 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 76.4. Ongezeko hilo lilitokana na kutolewa kwa mafunzo juu ya umuhimu wa kurasimisha biashara nchini.

Uzalishaji katika Baadhi ya Viwanda Nchini

244. Mwaka 2017, uzalishaji wa baadhi ya bidhaa za viwandani uliongezeka kama ifuatavyo: betri asilimia 76.81; unga wa ngano asilimia 21.54; rangi asilimia 14.39; dawa za pareto asilimia 6.65; tabaka za mbao asilimia 6.63; biskuti na tambu asilimia 4.81; na bia asilimia 3.55. Kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo kulitokana na ongezeko la mahitaji ya bidhaa za viwandani katika soko la ndani na nje. Hata hivyo, uzalishaji ulipungua kwa bidhaa za kamba za katani (asilimia 49.17); nyavu za uvuvi (asilimia 37.10); nguo (asilimia 31.90); chibuku (asilimia 14.67); chuma (asilimia 11.40); konyagi (asilimia 11.12); sigara (asilimia 8.39); saruji (asilimia 7.63); na bati (asilimia 7.53).

245. Mwaka 2017, kwa ujumla gharama za uzalishaji bidhaa ziliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 6,029,305 kutoka shilingi milioni 5,963,094 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa gharama za wafanyakazi pamoja na bei za malighafi za viwandani zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa

246. Mwaka 2017, Serikali kupitia TanTrade iliratibu na kuendesha maonesho ya 41 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo jumla ya kampuni za ndani 2,520 zilishiriki ikilinganishwa na kampuni 2,500 zilizoshiriki katika maonesho ya 40 mwaka 2016, ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.8. Aidha mwaka 2017, kampuni za nje ya nchi zilizoshiriki maonesho ya 41 zilikuwa 515 ikilinganishwa na kampuni za nje 501 zilizoshiriki maonesho ya 40 ya mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 2.8. Kadhalika, Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali zilishiriki maonesho hayo na kutoa fursa kwa watu kufahamu na kupata huduma zinazotolewa. Aidha, jumla ya nchi 30 zilishiriki maonesho hayo ikiwa ni idadi sawa na nchi zilizoshiriki Maonesho ya 40 ya mwaka 2016. Nchi zilizoshiriki katika maonyesho hayo ni pamoja na: Afrika ya Kusini, Burundi, China, Ghana, India, Indonesia, Iran, Italia, Japan, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Kenya, Lebanoni, Malawi, Malaysia, Morocco, Misri, Msumbiji, Namibia, Pakistan, Rwanda, Singapore, Sudani ya Kusini, Syria, Uganda, Jamhuri ya Falme za Kiarabu, Marekani, Uingereza, Uturuki, Ujerumani na Vietnam.

247. Mwaka 2017, Serikali kupitia TanTrade iliandaa Maonesho ya Pili ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania ambapo jumla ya makampuni 506 yalishiriki na kutangaza bidhaa na shughuli wanazozifanya. Katika maonesho hayo, jumla ya viwanda vikubwa na vya kati 150, viwanda vidogo 333, taasisi 21 na wizara mbili zilishiriki. Maonesho hayo yalikuwa na kauli mbiu “Tanzania Sasa Tunajenga Viwanda” ambayo yalilenga kujenga uzalendo kwa watazania kupenda bidhaa zinazozalishwa nchini. Aidha, mwaka 2017, Tanzania ilishiriki katika Maonesho mbalimbali ya Biashara ya Kimataifa yaliyofanyika Kigali-Rwanda ambapo kampuni 18 kutoka Tanzania zilishiriki; Manzini-Swaziland (kampuni 11); Uganda (wajasiriamali 10); Nairobi- Kenya (wajasiriamali 28); na Mauritius (wajasirimali watano). Maonesho hayo yalilenga kutafuta fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania katika nchi husika na baadhi ya kampuni ziliweza kupata oda ya kuuza bidhaa zao katika nchi hizo.

MATUMIZI YA SARUJI NCHINI

Jedwali Na. 58

Mwaka	Kutoka Nje	Uuzaji nje	Uzalishaji wa Ndani	Tani	
				Matumizi Tani	Badiliko, %
2000	7281	30497	833092	809876	-0.6%
2001	56395	53517	900430	903308	11.5%
2002	149079	37203	1026082	1137958	26.0%
2003	166446	34396	1186434	1318484	15.9%
2004	125007	37655	1280851	1368203	3.8%
2005	120200	40430	1375222	1454992	6.3%
2006	92711	98	1421460	1514073	4.1%
2007	101827	52170	1629890	1679547	10.9%
2008	356468	99688	1755862	2012642	19.8%
2009	516182	57569	1940845	2399458	19.2%
2010	566828	189321	2312055	2689562	12.1%
2011	768343	217944	2408765	2959164	10.0%
2012	1013986	145793	2557798	3425991	15.8%
2013	1218453	154481	2369819	3433791	0.2%
2014	1428995	142001	2795687	4082681	18.9%
2015	1257578	126391	3273000	4404187	7.9%
2016	1306732	194338	4916400	6028794	36.9%
2017	188067	226588	4222764	4184243	-30.6%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Jedwali Na.59

Aina ya Bidhaa	Kipimo											Badiliko(%)
		2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	2016/17
Biskuti & tamba	Tani	15435	15200	7435	12053	16423	17440	18225	19204	15890	16654	4.8
Unga wa ngano	Tani	287925	368885	444242	439926	442345	516778	529797	533257	498940	606432	21.5
Konyagi	000 Lita	4049	10201	11186	15432	16229	20680	31963	29491	28754	25555	-11.1
Bia	000 Lita	291178	284906	242689	323393	338041	374238	379913	386310	383251	396864	3.6
Chibuku	000 Lita	10235	16141	21037	23474	22359	19935	20301	23028	26513	22624	-14.7
Sigara	Milioni	6101	5831	6181	6630	7723	7710	8028	7837	8091	7412	-8.4
Nguo	000 M ²	140531	91501	103177	101820	81437	97522	119458	100491	76436	52052	-31.9
Kamba za katani	Tani	7783	7913	6872	6976	7927	7542	7871	8851	9216	4685	-49.2
Nyavu za uvuvi	Tani	-	64	247	164	272	297	279	311	312	196	-37.1
Mazulia	000 M ²	-	37152	-	-	-	-	-	0	0	-	
Tabaka za mbao	M ²	44547	266	-	30589	38871	36935	38913	36317	34983	37302	6.6
Dawa za pareto	Tani	73	-	49	53	70	83	136	118	126	134	6.7
Mbolea	Tani	-	25762	-	11200	-	-	-	0	0	-	
Rangi	000 Lita	24857	-	28201	31211	35025	36623	38308	38372	35096	40146	14.4
Bidhaa za petrol	000 Tani	-	1941	-	-	-	-	-	0	0	-	
Saruji	000 Tani	1756	34793	2313	2409	2558	2369	2795	3135	4572	4223	-7.6
Chuma	Tani	39969	34793	33384	39955	46690	48500	56752	62612	65686	58199	-11.4
Bati	Tani	31743	50664	71276	76912	81427	85314	86825	91385	91421	84541	-7.5
Aluminium	Tani	105	58	59	33	23	37	27	32	14	-	
Radio	000 namba	-	-	-	-	-	-	-	0	0	-	
Betri	Milioni	53	78	93	89	68	75	93	87	69	122	76.8

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

- Hakuna uzalishaji

VIWANDA - IDADI YA WATU WALIOAJIRIWA

Jedwali Na. 60

ISIC (Rev 3)	Shughuli															
		2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017
151-4	Vyakula	63863	67056	70409	73929	77625	21466	22540	23667	24850	26092	85330	89596	94076	98779	103718
155	Vinywaji	6919	7265	7629	8010	8410	85	89	93	98	103	7004	7354	7722	8108	8513
160	Tumbaku na Sigara	5103	5358	5626	5908	6203	6	6	7	7	7	5109	5365	5633	5915	6210
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	27102	28457	29880	31374	32942	21151	22209	23319	24485	25709	48253	50666	53199	55859	58651
191	Ngozi, bidhaa za ngozi	1410	1480	1554	1632	1713	316	332	348	366	384	1726	1812	1902	1998	2097
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	7209	7570	7948	8346	8763	2209	2319	2435	2557	2685	9418	9889	10383	10903	11448
210-221- 222	Karatasi, Uchapishaji	5391	5661	5944	6241	6553	201	211	222	233	244	5592	5872	6165	6473	6797
241-2	Utengenezaji wa Kemikali na Madawa ya serikali	7209	7569	7948	8345	8762	227	238	250	263	276	7436	7808	8198	8608	9038
251	Bidhaa za mpira na Plastiki	4286	4500	4725	4961	5209	57	59	62	65	69	4342	4559	4787	5027	5278
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	8093	8497	8922	9368	9837	1292	1357	1424	1496	1570	9385	9854	10347	10864	11407
271-369	Nyinginezo	30303	31818	33409	35079	36833	17201	18061	18964	19912	20908	47503	49879	52373	54992	57741
	Jumla	166889	175233	183994	193193	202852	64210	67421	70792	74331	78047	231098	242654	254786	267524	280899

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

Viwanda viliyohusika ni wenyewe ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA - GHARAMA ZA KAZI

Jedwali Na. 61

(Sh.milioni)

ISIC (Rev 3)	Shughuli	Mishahara					Malipo Mengine					Jumla				
		2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017
151-4	Vyakula	165024	166675	168341	170025	171725	48796	49284	49777	50275	50778	213821	215959	218119	220300	222503
155	Vinywaji	101137	102148	103169	104201	105243	69423	70117	70818	71526	72241	170559	172265	173987	175727	177484
160	Tumbaku na Sigara	45051	45501	45956	46416	46880	20349	20553	20758	20966	21176	65400	66054	66715	67382	68056
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	50198	50700	51207	51719	52236	42794	43222	43654	44090	44531	92992	93922	94861	95810	96768
191	Ngozi, Bidhaa za ngozi	2852	2881	2910	2939	2968	466	470	475	480	485	3318	3351	3385	3419	3453
201- 202	Mbao, Bidhaa za Mbao	13279	13412	13546	13681	13818	3037	3067	3098	3129	3160	16316	16479	16644	16810	16978
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji	24130	24371	24615	24861	25110	8641	8728	8815	8903	8992	32771	33099	33430	33764	34102
241-2	Utengenezaji wa Kemikali na Mada	32758	33086	33417	33751	34088	8268	8351	8434	8519	8604	41026	41437	41851	42269	42692
251	Bidhaa za Mpira na Plastiki	16834	17002	17172	17344	17517	3998	4038	4079	4119	4161	20832	21041	21251	21463	21678
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	44344	44788	45236	45688	46145	21708	21925	22144	22366	22589	66052	66713	67380	68054	68734
271-369	Nyinginezo	73154	73886	74625	75371	76125	24588	24834	25082	25333	25586	97742	98720	99707	100704	101711
	Jumla	568762	574449	580194	585996	591856	252068	254589	257135	259706	262303	820830	829038	837329	845702	854159

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO

Jedwali Na. 62

ISIC (Rev 3)	Shughuli	PATO					GHARAMA					Thamani Iliyoongezeka (Value Added)				
		2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017
151-4	Vyakula	4231129	4273440	4316175	4359336	4446523	2322611	2345838	2350020	2296401	2321700	1908518	1927603	1966155	2062936	2124824
155	Vinywaji	1744910	1762360	1779983	1797783	1833739	724600	731846	728859	694919	697789	1020310	1030514	1051124	1102864	1135950
160	Tumbaku na Sigara	655707	662264	668886	675575	689087	245768	248226	246568	232469	232687	409938	414038	422318	443106	456400
171-2, 181	Ufumaji na Ushonaji	512018	517138	522309	527532	538083	280298	283101	283592	277064	280101	231720	234037	238718	250468	257982
191	Ngozi, bidhaa za ngozi	57467	58042	58623	59209	60393	42063	42484	42753	42558	43242	15405	15559	15870	16651	17150
201-202	Mbao, Bidhaa za Mbao	155563	157119	158690	160277	163483	68791	69479	69297	66484	66876	86772	87640	89393	93793	96607
210-221-222	Karatasi, Uchapishaji	281228	284040	286881	289750	295545	191843	193761	194796	193132	196029	89385	90279	92085	96617	99516
241-2	Utengenezaji wa Kemikali na madawa ya Binadamu	615973	622133	628354	634638	647331	423562	427798	430133	426659	433112	192411	194335	198222	207979	214218
251	Bidhaa za mpira na Plastiki	632722	639049	645440	651894	664932	446088	450549	453169	450160	457145	186634	188500	192270	201734	207786
261-9	Bidhaa za Madini yasiyo Chuma	807924	816003	824163	832405	849053	475805	480563	482015	473415	479293	332119	335440	342149	358990	369760
271-369	Nyinginezo	1242153	1254575	1267121	1279792	1305388	807373	815447	819210	809834	821331	434780	439128	447910	469958	484057
	Jumla	10936795	11046163	11156625	11268191	11493555	6028804	6089092	6100412	5963094	6029305	4907992	4957072	5056213	5305097	5464250

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

Viwanda viliyohusika ni wenyewe ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VIWANDA - MUHTASARI WA MATOKEO KIMKOA *

Jedwali Na. 63

Jina la mkoa	Idadi ya Wafanyakazi					Idadi ya Waajiriwa					Mishahara (TShs. Milioni)					Thamani Iliyoongezeka (TShs. Milioni)				
	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017	2013	2014	2015	2016	2017
Dodoma	5032	5284	5548	5825	6116	3239	3401	3571	3749	3937	3848	3886	3925	3964	4004	22501	22726	23181	24322	25052
Arusha	15482	16257	17069	17923	18819	13015	13665	14349	15066	15819	36788	37156	37527	37903	38282	222748	224976	229475	240771	247994
Kilimanjaro	9034	9485	9960	10458	10980	7073	7426	7798	8188	8597	43613	44049	44489	44934	45384	148593	150079	153080	160615	165434
Tanga	12785	13425	14096	14801	15541	10603	11133	11689	12274	12887	22653	22880	23108	23339	23573	165283	166936	170275	178656	184016
Morogoro	20992	22042	23144	24301	25516	16739	17576	18455	19378	20347	44971	45421	45875	46334	46797	619838	626036	638557	669989	690089
Pwani,	5137	5394	5664	5947	6245	3271	3435	3607	3787	3976	6862	6930	7000	7070	7140	19648	19845	20242	21238	21875
Dar es Salaam	53137	55794	58584	61513	64588	43688	45872	48165	50573	53102	163138	164770	166418	168082	169762	1354652	1368198	1395562	1464257	1508184
Lindi	2756	2894	3039	3191	3350	1476	1550	1627	1708	1794	925	934	943	953	962	4700	4747	4842	5081	5233
Mtwara	3231	3392	3562	3740	3927	1680	1764	1852	1945	2042	2464	2489	2514	2539	2564	27969	28248	28813	30232	31139
Ruvuma	7015	7366	7734	8121	8527	2520	2646	2778	2917	3063	2159	2180	2202	2224	2246	12690	12817	13073	13717	14128
Iringa	9453	9926	10422	10943	11491	6844	7186	7546	7923	8319	11438	11553	11668	11785	11903	64853	65502	66812	70101	72204
Mbeya	9576	10055	10557	11085	11639	6246	6558	6886	7231	7592	27089	27360	27633	27910	28189	184137	185979	189698	199036	205007
Singida	5281	5545	5823	6114	6419	3480	3654	3836	4028	4230	1686	1703	1720	1737	1754	20053	20254	20659	21676	22326
Tabora	2728	2865	3008	3158	3316	1778	1867	1960	2058	2161	7078	7149	7220	7293	7366	49174	49666	50659	53153	54748
Rukwa	2088	2192	2302	2417	2538	806	846	889	933	980	722	729	736	744	751	34757	35105	35807	37569	38696
Kigoma	2652	2785	2924	3070	3224	1321	1387	1456	1529	1605	1470	1485	1500	1515	1530	18215	18397	18765	19688	20279
Shinyanga	8966	9415	9886	10380	10899	7201	7561	7939	8336	8752	109752	110849	111958	113077	114208	535417	540771	551587	578738	596100
Kagera	12654	13287	13951	14649	15381	9005	9455	9928	10424	10945	8332	8415	8499	8584	8670	52448	52973	54032	56692	58392
Mwanza	9133	9589	10069	10572	11101	7317	7683	8067	8470	8894	20983	21193	21405	21619	21835	169923	171623	175055	183672	189182
Mara	12611	13241	13904	14599	15328	5969	6267	6581	6910	7255	18615	18801	18989	19179	19370	614399	620543	632954	664110	684033
Manyara	10515	11040	11592	12172	12781	7653	8036	8437	8859	9302	9479	9574	9670	9767	9864	45947	46407	47335	49665	51155
Njombe	4931	5177	5436	5708	5993	2427	2549	2676	2810	2950	1542	1557	1573	1588	1604	14689	14836	15133	15878	16354
Katavi	460	483	508	533	560	294	309	324	341	358	32	32	33	33	33	1514	1530	1560	1637	1686
Simiyu	1988	2087	2191	2301	2416	928	974	1023	1074	1128	237	239	242	244	246	4078	4119	4201	4408	4540
Geita	3459	3632	3814	4005	4205	2318	2434	2555	2683	2817	22887	23116	23347	23581	23817	499762	504759	514855	540198	556404
Jumla	231098	242654	254786	267524	280899	166889	175233	183994	193193	202852	568762	574449	580194	585996	591856	4907992	4957072	5056213	5305097	5464250

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

* Takwimu zimekadiriwa kutokana na utafiti wa sensa ya viwanda ya mwaka 2013

Viwanda vilivyohusika ni vyenye ajira ya mtu mmoja na kuendelea (1+)

VICEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWANDA (%)

Jedwali Na. 65

Mwaka	Mchango katika Pato la Taifa (Bei za miaka husika)	Ukuaji wa Sekta (Bei za 2007)	Mchango katika mauzo nje	Mchango katika mauzo nje yasiyo asilia	Ongezeko la mauzo nje ya bidhaa za viwanda
2005	7.29		9.3	11.81	
2006	7.50	8.4	11.2	13.81	25.4
2007	7.02	11.5	15.3	18.14	57.9
2008	6.97	11.4	20.7	28.48	139.9
2009	6.88	4.7	15.4	21.35	-31.7
2010	6.89	8.9	22.3	30.34	90.3
2011	7.64	6.9	16.9	22.99	-10.6
2012	7.49	4.1	17.6	24.91	20.4
2013	6.45	6.5	20.4	28.95	3.3
2014	5.58	6.8	23.3	32.63	15.6
2015	5.25	6.5	25.3	33.14	10.1
2016	4.92	7.8	21.1	25.48	-20.0
2017	5.52	7.1	16.6	24.16	-25.0

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

SURA YA 15

UJENZI NA MAENDELEO YA ARDHI

UJENZI

Mtandao wa Barabara

248. Mtandao wa barabara nchini una urefu wa kilometa 86,472. Mtandao huo unajumuisha kilometa 12,786 za barabara kuu zinazounganisha mikoa na nchi jirani, kilometa 22,214 za barabara za mikoa zinazounganisha wilaya na miji mikuu na kilometa 51,472 za barabara zinazounganisha wilaya na vijiji.

249. Mwaka 2017, barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za wilaya za kiwango cha lami na changarawe/udongo zilikuwa na urefu wa kilometa 32,170 ikilinganishwa na kilometa 30,265 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.3. Ongezeko hilo lilitokana na baadhi ya barabara za wilaya kupandishwa hadhi na kuwa barabara za mikoa. Aidha, barabara zingine zilizokuwa chini ya halmashauri zilikasimiwa kwa TANROADS. Kati ya kilometa 32,170, kilometa 11,681 za barabara kuu sawa na asilimia 36.3 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 12,388 mwaka 2016. Barabara zenye hali nzuri zilipungua kutokana na kuongezeka kwa barabara za wilaya zenye hali mbaya ambazo zilihamishiwa TANROADS ili ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami/changarawe. Aidha, kilometa 16,639 sawa na asilimia 51.7 zilikuwa katika kiwango cha wastani ikilinganishwa na kilometa 13,643 mwaka 2016; na kilometa 3,849 sawa na asilimia 12.0 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 4,235 mwaka 2016.

250. Hadi kufikia Desemba 2017, barabara kuu zilizokuwa na kiwango cha lami na changarawe zilikuwa na urefu wa kilometa 10,065 ikilinganishwa na kilometa 9,953 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.1. Kati ya hizo, kilometa 6,351.9 sawa na asilimia 63.1 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 6,672 mwaka 2016. Barabara zenye hali nzuri zilipungua kutokana na barabara nyingi kutofanyiwa ukarabati kwa wakati mara zinapoharibika. Aidha, kilometa 2,734.9, sawa na asilimia 27.2 zilikuwa na hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 2,386 mwaka 2016. Barabara zenye hali ya wastani ziliongezeka kutokana na kuendelea kufanyiwa matengenezo kwa wakati kutokana na kutokuwa na gharama kubwa za ukarabati. Vile vile, kilometa 977 za barabara kuu, sawa na asilimia 9.7 zilikuwa na hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 896 mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na barabara nyingi zenye hali nzuri kutofanyiwa ukarabati kwa wakati.

251. Barabara za mikoa zilizokuwa na kiwango cha lami na changarawe mwaka 2017 zilikuwa kilometa 21,660 ikilinganishwa na kilometa 20,312 mwaka 2016. Kati ya hizo, kilometa 5,285 sawa na asilimia 24.4 zilikuwa katika hali nzuri ikilinganishwa na kilometa 5,716 mwaka 2016. Barabara zenye hali nzuri zilipungua kutokana na barabara za wilaya zenye hali mbaya kuhamishiwa kwenye mtandao wa barabara za TANROADS ili ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami na changarawe. Aidha, kilometa 13,663, sawa na asilimia 63.1 zilikuwa katika hali ya wastani ikilinganishwa na kilometa 11,256 mwaka 2016. Barabara zenye hali ya wastani ziliongezeka kutokana na kuendelea kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara. Vile vile, kilometa 2,712 sawa na asilimia 12.5 zilikuwa katika hali mbaya ikilinganishwa na kilometa 3,339 mwaka 2016. Barabara zenye hali mbaya zilipungua kutokana na kuendelea kujengwa kwa kiwango cha lami/changarawe.

252. Barabara za wilaya zilizokuwa katika kiwango cha lami na changarawe zilikuwa kilometa 445 hadi kufikia Desemba 2017. Kati ya hizo, kilometa 44.2 sawa na asilimia 10.0 zilikuwa katika hali nzuri; kilometa 240.9, sawa na asilimia 54.1 zilikuwa katika hali ya wastani; na kilometa 159.9, sawa na asilimia 35.9 zilikuwa katika hali mbaya. **Jedwali Na. 15.1** linaonesha mchanganuo wa mtandao wa barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za wilaya kwa kiwango cha lami na changarawe.

Jedwali Na.15.1: Hali ya Mtandao wa Barabara Hadi Desemba 2017

Aina ya Barabara	Hali ya Mtandao wa Barabara						Jumla Kuu
	Nzuri		Wastani		Mbaya		
	Km	%	Km	%	Km	%	
Barabara Kuu za Lami	5,648	79.0	994	13.9	509	7.1	7,152
Barabara Kuu za Changarawe / Udongo	703.9	24.2	1,740.9	59.8	468	16.1	2,913
Jumla Ndogo-Barabara Kuu	6,351.9	63.1	2,734.9	27.2	977	9.7	10,065
Barabara za Mikoa za Lami	719	56.2	331	25.9	230	18.0	1,280
Barabara za Mikoa za Changarawe / Udongo	4,566	22.4	13,332	65.4	2,482	12.2	20,380
Jumla Ndogo - Barabara za Mikoa	5,285	24.4	13,663	63.1	2,712	12.5	21,660
Barabara za Wilaya za Lami	5	23.8	3.3	15.7	13.3	63.3	21
Barabara za Wilaya za Changarawe/Odongo	39.2	9.3	237.6	56.2	146.6	34.7	423
Jumla Ndogo-Barabara za Wilaya	44.2	10.0	240.9	54.1	159.9	35.9	445
Jumla Kuu	11,681	36.3	16,639	51.7	3,849	12.0	32,170

Chanzo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

Matengenezo ya Barabara, Magari, Madaraja na Vivuko

253. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kufanya matengenezo ya barabara kuu na madaraja kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha ili kuzuia uzalishaji wa madai mapya. Katika kipindi hicho, jumla ya kilometa 26,712 za barabara kuu na za mikoza zilifanyiwa matengenezo ikilinganishwa na kilometa 33,058 zilizofanyiwa matengenezo mwaka 2016. Aidha, madaraja 2,742 yalifanyiwa matengenezo mwaka 2017 ikilinganishwa na madaraja 2,934 mwaka 2016.

254. Mwaka 2017, Serikali ilikamilisha ujenzi wa kivuko kipya cha MV Kazi chenye uwezo wa kubeba tani 170 (sawa na abiria 800 na magari madogo 22) kinachotoa huduma katika kituo cha magogoni-Kigamboni, Dar es Salaam. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) ilitengeneza magari 14,380 ikilinganishwa na magari 11,417 mwaka 2016. Kuongezeka kwa matengenezo ya magari kulitokana na kuboreshwa kwa huduma na vifaa vya karakana pamoja na kutolewa kwa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwa mafundi. Vile vile, Serikali iliendelea kutoa ajira mpya kwa wahandisi na mafundi wasaidizi kwa ajili ya karakana hivyo kuongeza nguvukazi na kufanya kazi kwa weledi na ufanisi.

Bodi ya Mfuko wa Barabara

255. Mwaka 2017, Bodi ya Mfuko wa Barabara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 793 ikilinganishwa na shilingi bilioni 819 zilizokusanywa mwaka 2016. Mapato hayo yalipungua kwa asilimia 3.2 kutokana na kupungua kwa kiasi cha dizeli na petroli (kinachotozwa tozo hiyo) kilichoagizwa. Fedha zilizopelekwa kwenye Taasisi zinazotekeleza miradi ya barabara inayofadhiliwa na Mfuko zilikuwa shilingi bilioni 758 mwaka 2017 ikilinganishwa na shilingi bilioni 637 mwaka 2016. Aidha, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi ya barabara 762 ikilinganishwa na miradi 692 iliyokaguliwa mwaka 2016.

Wakala wa Nyumba na Majengo ya Serikali

256. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza miradi 292 ya ujenzi na ukarabati wa nyumba ikilinganishwa na miradi 110 mwaka 2016. Hadi Desemba 2017, jumla ya miradi 128 ya ukarabati wa nyumba na majengo ilitekelezwa ikilinganishwa na miradi 63 mwaka 2016. Kuongezeka kwa ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali kulitokana na Wakala wa Majengo kutumia teknolojia mpya ya ujenzi na ukarabati wa majengo, mitambo mipya ya kisasa ikiwemo mitambo ya kuchanganya zege yenye uwezo wa kukoroga mita 60 za zege kwa saa moja, ununuzi wa vifaa vya kupima ubora wa majengo bila ya kuyaharibu pamoja na ununuzi wa malighafi za ujenzi kutoka viwandani na kutoza ada ndogo ya usimamizi wa ujenzi na ukarabati. Aidha, hadi Desemba

2017, idadi ya nyumba zilizopangishwa kwa watumishi wa Serikali na nyumba za biashara zilizopangishwa kwa watu mbalimbali zilifikia 5,941 ikilinganishwa na nyumba 2,518 mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba.

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi

257. Mwaka 2017, Bodi ya Wakandarasi ilisajili jumla ya wakandarasi wapya 875 ikilinganishwa na wakandarasi 774 mwaka 2016. Usajili huu unafanya jumla ya wakandarasi waliosajiliwa hadi Desemba 2017, kufikia 9,065 ikilinganishwa na wakandarasi 8,418 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Aidha, wakandarasi 10 walifutiwa usajili ikilinganishwa na wakandarasi 7 waliofutiwa usajili mwaka 2016 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutozingatia taratibu za kazi na taaluma zao na kushindwa kulipa ada ya mwaka. Vile vile, Bodi ilisajili miradi ya ujenzi 3,600 ikilinganishwa na miradi 3,556 iliyosajiliwa mwaka 2016. Kati ya miradi iliyosajiliwa, Bodi ilifanya ukaguzi wa miradi 3,256 ikilinganishwa na ukaguzi wa miradi 2,934 mwaka 2016. Kati ya miradi iliyokaguliwa, miradi 2,213 sawa na asilimia 68.0 haikuwa na mapungufu na miradi 1,043 sawa na asilimia 32.0 ilikuwa na kasoro mbalimbali zikiwemo: miradi kufanywa na watu wasiosajiliwa; miradi kutosajiliwa; kutokuweka bango la mradi; na kutozingatia sheria ya afya na usalama wa wafanyakazi. Hatua za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wahusika wa miradi iliyokutwa na kasoro zikiwemo kutozwa faini, kusimamishwa kwa muda au kushtakiwa mahakamani pale ambapo mradi unatekelezwa na watu wasio wakandarasi.

Bodi ya Usajili ya Wahandisi

258. Mwaka 2017, Bodi ya Usajili wa Wahandisi ilisajili wahandisi 20,138 wa fani mbalimbali ikilinganishwa na wahandisi 1,892 waliosajiliwa mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu wengi kujisajili kutokana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi zinazohusu taaluma ya uhandisi hasa viwanda vya uzalishaji, ujenzi wa miundombinu ya reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kati ya wahandisi waliosajiliwa, wahandisi 18,405 walikuwa watanzania na wahandisi 1,733 walikuwa wageni. Aidha, Bodi ilisajili kampuni za ushauri 318 ambapo kampuni 224 zilikuwa za kitanzania na 94 za kigeni ikilinganishwa na kampuni 14 zilizosajiliwa mwaka 2016, ambapo kampuni 8 zilikuwa za kitanzania na 6 za kigeni. Vile vile, jumla ya wahandisi 4,692 walipata mafunzo ikilinganishwa na wahandisi 459 mwaka 2016. Ongezeko la wahandisi kupata mafunzo lilitokana na wahandisi kutambua umuhimu wa kusajili taaluma zao. Bodi pia ilisajili miradi ya ujenzi 723 na kukagua miradi 97 ikilinganishwa na usajili wa miradi 847 na ukaguzi wa miradi 210 mwaka 2016. Usajili wa miradi

ulipungua kutokana na wadau kutojitokeza na kutotambua umuhimu wa kusajili miradi yao.

Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi

259. Mwaka 2017, Bodi ya Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilisajili jumla ya wataalam 907 ikilinganishwa na wataalam 830 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilinia 9.3. Ongezeko hilo lilitokana na wahitimu wengi kujitokeza kufanya mitihani ya Bodi kwa mwaka husika kwa kuhamasishwa na Bodi kwa lengo la kutambulika katika shughuli zao binafsi na pia kupata ajira ya uhakika katika sekta binafsi na ya umma. Aidha, katika kipindi hicho, kampuni 363 za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi zilikuwa zimesajiliwa ikilinganishwa na kampuni 346 mwaka 2016, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.9. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za Bodi kuhamasisha Waendelezaji wa Majengo kutumia huduma za wataalamu waliosajiliwa kwa mujibu wa Sheria Na. 4 ya mwaka 2010. Kati ya kampuni zilizosajiliwa, kampuni 353 zilikuwa za kitanzania na kampuni 10 zilikuwa za kigeni.

260. Mwaka 2017, jumla ya miradi 1,943 ilikaguliwa ikilinganishwa na miradi 2,153 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 10.8. Upungufu huo ulitokana na waendelezaji wengi kuwa na uelewa mdogo wa kutumia huduma za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika kuendeleza miradi yao wakiwemo waendelezaji wa makazi binafsi (ghorofa moja na miradi midogo ya kijamii). Aidha, miradi 800 ya ujenzi ilisajiliwa ikilinganishwa na miradi 780 iliyosajiliwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 2.6. Ongezeko hilo lilitokana na juhudi za kuelimisha jamii na waendelezaji kuhusu umuhimu wa kutumia huduma za ushauri za Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi katika miradi ya ujenzi.

Baraza la Taifa la Ujenzi

261. Mwaka 2017, Baraza la Taifa la Ujenzi lilifanya ukaguzi wa kiufundi katika miradi 190 ikilinganishwa na miradi 151 iliyokaguliwa mwaka 2016. Aidha, Baraza lilisuluhisha migogoro mipya 46 ya ujenzi ikilinganishwa na migogoro 23 mwaka 2016. Ongezeko la usuluhishi wa migogoro lilitokana na wadau wengi kuelewa haki zao kisheria na kimkataba. Vile vile, Baraza lilitoa mafunzo kwa wadau 8 wa sekta ya ujenzi ikilinganishwa na wadau 119 mwaka 2016. Wadau wote waliopata mafunzo mwaka 2017 walikuwa wa fani ya ukaguzi wa miradi ya ujenzi. Upungufu wa wadau waliopata mafunzo, ulitokana na kutojitokeza kwa wadau wa fani nyingine kutokana na uhaba wa fedha.

MAENDELEO YA ARDHI

Utayarishaji wa Hatimiliki, Ukaguzi, na Uhakiki Milki

262. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kufanya ukaguzi wa milki katika kanda nane za ardhi, ambapo jumla ya milki 39,418 zilikaguliwa, kuhakikiwa na kuandaliwa hatimiliki ikilinganishwa na milki 32,230 mwaka 2016. Aidha, ilani 1,242 za ubatilisho zilitumwa kwa wapangaji waliokiuka masharti ya upangaji wa ardhi ikilinganishwa na ilani 5,016 za ubatilisho zilizotumwa mwaka 2016. Vile vile, jumla ya migogoro ya ardhi 6,811 ilitatuliwa kiutawala ikilinganishwa na migogoro 820 iliyotatuliwa mwaka 2016. Hii ilitokana na hamasa ya viongozi wa juu wa Serikali ya Awamu ya Tano kufuatilia kwa karibu migogoro ya ardhi nchini. Kwa upande mwingine, jumla ya hatimiliki za kimila 87,703 zilitolewa kwa wananchi nchini mwaka 2017 ikilinganishwa na hatimiliki za kimila 7,833 zilizotolewa mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) sambamba na kuanza kwa utekelezaji wa programu ya kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi (Land Tenure Support Program).

Usajili wa Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria

263. Mwaka 2017, jumla ya hatimiliki na nyaraka za kisheria 49,728 zilizajiliwa ikilinganishwa na hatimiliki na nyaraka za kisheria 91,187 zilizosajiliwa mwaka 2016. Kati ya hizo, hati za kumiliki ardhi zilikuwa 21,743; hati za umiliki wa sehemu ya jengo zilikuwa 827; na nyaraka nyingine za kisheria zilikuwa 27,158.

Jedwali Na.15.2: Usajili wa Hati Miliki na Nyaraka za Kisheria

Hati na Nyaraka zilizosajiliwa	2014	2015	2016	2017
Hati za kumiliki Ardhi zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati	29,951	31,254	33,257	21,743
Hati ya sehemu ya jengo zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati 'Unit Title Act No. 17/2008'	1,027	1,541	1,410	827
Nyaraka za kisheria zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Hati Sura Na. 334	39,540	29,546	34,682	13,821
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Nyaraka Sura Na. 117	13,403	13,041	20,525	13,027
Nyaraka zilizosajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Rehani ya mali zinazohamishika Sura na. 210	3,100	2,082	1,313	310
Jumla	87,021	77,464	91,187	49,728

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Uthamini wa Mali kwa Madhumuni Mbalimbali

264. Mwaka 2017, Serikali iliidhinisha taarifa 14,483 za uthamini ikilinganishwa na taarifa 9,047 zilizoidhinishwa mwaka 2016. Idadi hii ilijumuisha taarifa zilizopokelewa kutoka katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kampuni binafsi za uthamini pamoja na zilizofanywa na Serikali Kuu. Uthamini ulifanyika kwa madhumuni mbalimbali yakiwemo kupisha miradi, kukadiria malipo ya fidia, kodi ya majengo na kodi ya ardhi na viwanja.

Upimaji wa Mashamba na Viwanja

265. Mwaka 2017, ramani zenye viwanja 170,442 na mashamba 445 ziliidhinishwa katika mikoa ya Tanzania Bara ikilinganishwa na viwanja 123,727 na mashamba 391 yaliyoidhinishwa mwaka 2016. Mchanganuo wa viwanja na mashamba yaliyoidhinishwa unaoneshwa katika **Jedwali Na 15.3**.

Jedwali Na.15.3: Upimaji wa Viwanja na Mashamba

Mikoa	Milki zilizoidhinishwa mwaka 2015		Milki zilizoidhinishwa mwaka 2016		Milki zilizoidhinishwa mwaka 2017	
	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba	Viwanja	Mashamba
Arusha	1,209	58	1769	19	1392	18
Pwani	20,227	241	21539	190	36974	107
DSM	22,178	0	29985	1	28079	0
Dodoma	2,512	0	1653	0	3622	5
Geita	2,688	0	1808	0	5279	0
Iringa	2,606	9	1893	38	4531	26
Kagera	804	14	1211	9	2959	2
Katavi	5936	0	767	0	2858	1
Kigoma	3120	0	4773	0	1893	2
Kilimanjaro	833	144	1284	58	1532	36
Lindi	2786	0	3000	4	7253	0
Manyara	192	7	1198	14	1668	86
Mara	4983	17	4998	0	2326	16
Mbeya	2735	11	2093	15	3473	17
Morogoro	4877	80	6538	4	5298	73
Mtwara	1825	2	4847	2	4737	1
Mwanza	7369	4	6042	0	22910	0
Njombe	1955	3	1829	11	2870	6
Ruvuma	1700	0	2368	0	1112	0
Rukwa	659	0	248	8	2388	9
Simiyu	1232	0	832	0	2720	14
Singida	9282	1	4101	1	8934	8
Songwe	0	0	1022	0	98	1
Shinyanga	9230	1	4690	0	5028	0
Tabora	16248	0	11524	0	4265	1
Tanga	8247	44	1715	17	6223	26
Jumla	135,433	636	123,727	391	170,422	455

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mipango ya Matumizi ya Ardhi

266. Mwaka 2017, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 47 iliandaliwa katika wilaya 15 nchini ikilinganishwa na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 79 iliyoandaliwa mwaka 2016. Lengo la mipango hii ni kuepusha migogoro ya ardhi na kuhakikisha uwepo wa matumizi sahihi ya ardhi kwa ajili ya kilimo, ufugaji na matumizi mengine.

Jedwali Na.15.4: Orodha ya Vijiji Vilivyoandaliwa Mipango ya Matumizi ya Ardhi Mwaka 2017

Mkoa	Wilaya	Jina la kijiji	Idadi ya vijiji
Mara	Tarime	Matongo, Bisarwi, Weigita, Keisaka	4
	Serengeti	Motukeri, Nyamisingisi, Nyibereketa, Marasomote	4
Katavi	Tanganyika	Songambebe, Kapalamsenga, Kapanga, Bujombe, Nkungwi, Mnyagala	6
	Mpanda	Igongwe	1
Morogoro	Ulanga	Isyaga, Kituti, Mbangayao, Lyandu, Minepa, Kivukoni, Mbuyuni, Nakafulu, Idunda, Ikungua	10
Iringa	Kilolo	Lyamko	1
	Mufindi	Kiyowela, Lugolofu, Lugema, Isaula	4
Lindi	Liwale	Darajani	1
Mtwara	Newala	Kadengwa, Mandala, Mitema, Mtongwela,	4
Rukwa	Kalambo	Samazi, Kisala.	2
Tanga	Muheza	Mbomole, Sakale, Mkwini, Mlesa	4
	Handeni	Ngojolo	1
Ruvuma	Mbinga	Lipilipili, Ukimo	2
Kagera	Misenyi	Kabingo, Buchurago	2
Pwani	Kibaha	Minazimikindani	1
Jumla			47

Chanzo: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya

267. Mwaka 2017, jumla ya mashauri mapya 21,183 yalifunguliwa katika mabaraza ya ardhi na nyumba ya wilaya ikilinganishwa na mashauri 18,546 yaliyofunguliwa mwaka 2016. Idadi ya mashauri yaliyofunguliwa mwaka 2017 inafanya kuwa na jumla ya mashauri 45,375. Kati ya hayo, mashauri 21,561

yaliamuliwa na mashauri 23,814 yaliendelea kusikilizwa ikilinganishwa na mashauri 20,667 yaliyoamuliwa na mashauri 24,192 yaliyoendelea kusikilizwa mwaka 2016.

MAENDELEO YA MAKAZI

Ujenzi wa Nyumba za Makazi na Biashara

268. Mwaka 2017 Shirika la Nyumba la Taifa lilijenga nyumba za biashara na makazi 2,738 ikilinganishwa na nyumba za biashara na makazi 2,033 zilizojengwa mwaka 2016. Kati ya hizo, nyumba za makazi zilikuwa 1,804 na za biashara 934 ikilinganishwa na nyumba za makazi 1,410, za biashara 342 na za matumizi mengineyo 281 mwaka 2016. Kati ya nyumba za makazi, nyumba 616 zilikuwa za gharama nafuu na nyumba 1,188 za gharama ya kati na juu ikilinganishwa na nyumba 492 za gharama nafuu na nyumba 918 za gharama ya kati na juu mwaka 2016. Aidha, Watumishi Housing Company (WHC) iliendelea na ujenzi wa nyumba 186 katika mikoa mbalimbali nchini mwaka 2017 ikilinganishwa na nyumba 592 mwaka 2016. Kati ya hizo, ujenzi wa nyumba 134 za makazi na nyumba 12 za biashara ulikamilika na nyumba 40 za makazi ujenzi wake uliendelea mwaka 2017.

SURA YA 16

MAWASILIANO NA UCHUKUZI

UCHUKUZI

Usafiri wa Barabara

269. Mwaka 2017, leseni za vyombo vya usafirishaji zilizotolewa ziliongezeka kwa asilimia 9.5 hadi leseni 160,915 kutoka leseni 146,974 mwaka 2016. Kati ya hizo, leseni 46,612 zilitolewa kwa mabasi ya abiria ya masafa marefu na mijini, leseni 99,484 kwa magari ya mizigo yenye uwezo wa kubeba shehena kuanzia tani tatu na kuendelea na leseni 14,819 zilitolewa kwa pikipiki/bajaji zilizojihusisha na ubebaji wa abiria kibiashara. Mchanganuo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 16.1**.

Jedwali Na. 16.1: Mchanganuo wa Leseni za Usafirishaji Zilizotolewa

Leseni	2015	2016	2017	Badiliko (%)
Mabasi ya Abiria	47,451	46,691	46,612	- 0.2
Magari ya Mizigo	81,567	87,383	99,484	13.8
Bajaj/Pikipiki	6,054	12,900	14,819	14.9
Jumla	135,072	146,974	160,915	9.5
Ratiba za mabasi	6,077	6,637		

Chanzo: SUMATRA

Kampuni ya Reli Tanzania (TRL)

270. Mwaka 2017, Kampuni ya Reli Tanzania ilisafirisha shehena tani 351,758 kwa umbali wa kilometa 360,955,000 ikilinganishwa na tani 209,203 zilizosafirishwa kwa umbali wa kilometa 230,204,000 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 68.1. Ongezeko hilo lilitokana na ukarabati wa mabehewa ya mizigo pamoja na baadhi ya maeneo korofi ya reli na madaraja. Aidha, abiria 566,135 walisafirishwa kwa umbali wa kilometa 386,442,000 mwaka 2017 ikilinganishwa na abiria 517,358 waliosafirishwa kwa umbali wa kilometa 353,245,000 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuelimisha wafanyakazi wanaotoa huduma kwa wateja pamoja na kusogeza huduma za kistesheni katika kituo kipya cha kuuzia tiketi cha Kasulu - Kigoma.

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

271. Mwaka 2016/17, TAZARA ilisafirisha shehena ya tani 171,405 ikilinganishwa na tani 128,105 zilizosafirishwa mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la asilimia 33.8. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya reli pamoja na ukarabati wa mabehewa ya abiria na mizigo. Katika kipindi hicho, shehena zilizosafirishwa na TAZARA ziliongezeka, ambapo shehena ya mizigo kwenda nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 48.7, shehena kutoka nje ya nchi asilimia 19.6 na shehena iliyosafirishwa ndani ya TAZARA iliongezeka kwa asilimia 23.7.

Jedwali Na.16.2: Shehena ya Tani za Mizigo Iliyosafirishwa

Aina ya mizigo	2015/2016	2016/2017	Badiliko (%)
Kwenda nje ya Nchi	57,063	84,864	48.72
Kutoka nje ya Nchi	33,050	39,541	19.64
Ndani ya TAZARA	37,992	47,000	23.71
Jumla	128,105	171,405	33.80

Chanzo: TAZARA

272. Mwaka 2016/2017 abiria 483,856 wa njia kuu walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 414,776 waliosafirishwa 2015/2016, sawa na ongezeko la asilimia 16.7. Aidha, treni ya Udzungwa inayofanya safari zake kati ya stesheni ya Kidatu na Makambako (km 365) ilisafirisha abiria 294,031 mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na abiria 225,540 waliosafirishwa mwaka 2015/2016, sawa na ongezeko la asilimia 30.4. Ongezeko hilo lilitokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya reli pamoja na ukarabati wa mabehewa ya abiria na mizigo. Vilevile, treni ya usafiri wa mjini ilisafirisha abiria 2,375,436 mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na abiria 2,516,202 waliosafirishwa mwaka 2015/2016, sawa na upungufu wa asilimia 5.6. Upungufu huo ulitokana na kampuni ya Reli ya Tanzania (TRL) kuanza kutoa huduma ya usafiri kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Pugu.


Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

273. Mwaka 2017, jumla ya kampuni 45 za usafiri wa ndege zilikuwa zinatoa huduma ya usafiri wa anga ikilinganishwa na kampuni 61 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 26.2. Hadi Desemba 2017, mashirika ya ndege ya kimataifa (ya ndani na nje) yaliyokuwa yanatoa huduma kwa utaratibu wa *Bilateral Air Service Agreement* (BASA) yalikuwa 30 ikilinganishwa na makampuni 29 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Aidha, idadi ya abiria waliowasili na kuondoka katika viwanja vya ndege nchini iliongezeka

kutoka abiria 4,959,652 mwaka 2016 hadi abiria 5,013,430 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 2.1. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa miruko ya ndege kwa wiki kwa watoa huduma wafuatao: Kenya Airways, Qatar Airways, Air Tanzania, Precision Air na Rwanda Air.


Kielelezo Na. 16.1: Idadi ya Abiria Waliowasili na Kuondoka Nchini



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)


274. Mwaka 2017, safari za ndege ziliongezeka kwa asilimia 1.8 hadi safari 237,382 kutoka safari 233,260 mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kuendelea kutolewa kwa huduma za mashirika ya ndege ya Air Mauritius na Air Zimbabwe. Aidha, mizigo iliyosafirishwa iliongezeka kutoka tani 24,030 hadi tani 27,448.6 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 14.2. Ongezeko hili lilitokana na uingizaji wa mitambo ya uwekezaji na ujenzi wa miundombinu kama vile reli ya kisasa (Standard Gauge).

Kielelezo Na. 16.2: Idadi ya Safari za Ndege



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

Kielelezo Na.16.3: Tani za Mizigo Zilizosafirishwa



Chanzo: Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA)

Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

275. Mwaka 2016/17, Kampuni ya Ndege Tanzania ilifanikiwa kusafirisha abiria 107,207 ikilinganishwa na abiria 49,173 mwaka 2015/2016 sawa na ongezeko la asilimia 118. Hii ilitokana na Serikali kuongeza idadi ya ndege, kuboresha mazingira ya kazi na usimamizi mzuri wa Kampuni.

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

276. Mwaka 2016/17, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ilihudumia shehena tani milioni 14.733 ikilinganishwa na tani milioni 15.293 zilizohudumiwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 3.7. Aidha, katika kipindi hicho, shehena iliongezeka katika bandari za Mtwara, Mwanza na Kyela wakati bandari za Dar es Salaam, Tanga, Kilwa, Lindi, Mafia na Kigoma shehena ilipungua. Upungufu huo ulitokana na uchache wa meli za kubeba mizigo na kuharibika mara kwa mara kwa meli, ambapo kwa sasa shehena hii inasafirishwa kwa njia ya barabara na kuendelea kutumika kwa magati binafsi kwa bandari za Ziwa.

Jedwali Na. 16.3: Shehena Zilizosafirishwa (Tani, Milioni)

Kituo (Bandari)	2014/2015	2015/16	2016/17	Badiliko (%)
Bandari Kuu za Mwambao				
Dar es Salaam	14.803	14.033	13.561	-3.4
Tanga	0.645	0.677	0.486	-28.2
Mtwara	0.2966	0.273	0.378	38.5
Jumla ndogo	15.745	14.983	14.425	-3.7
Bandari Ndogo na Bandari za Maziwa Makuu				
Kilwa, Lindi na Mafia	0.026	0.046	0.041	-10.9
Mwanza	0.129	0.123	0.124	0.8
Kigoma	0.099	0.139	0.137	-1.4
Kyela	0.002	0.0004	0.006	
Jumla ndogo	0.231	0.264	0.308	0
Jumla Kuu	16.001	15.293	14.733	-3.7

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

277. Mwaka 2016/17, idadi ya kontena iliyohudumiwa na kitengo cha mizigo ya kawaida kinachosimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilipungua kutoka kontena (TEUs) 130,893 mwaka 2015/16 hadi kontena (TEUs) 108,088, sawa na upungufu wa asilimia 17.4. Aidha, kitengo cha kontena cha TICTS kilihudumia kontena (TEUs) 445,493 ikilinganishwa na kontena (TEUs) 497,769 zilizohudumiwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 10.5.

Jedwali Na. 16.4: Shehena ya Kontena (TEUs) - Bandari ya Dar es Salaam

	2015/2016	2016/17
TICTS	497,769	445,493
General Cargo	130,893	108,088
Jumla Ndogo	628,662	553,581
Tanga	8,118	8,048
Mtwara	14,337	30,371
Jumla Ndogo	22,455	38,419
Jumla Kuu	651,117	592,000

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

278. Mwaka 2016/17, jumla ya abiria 2,037,853 walihudumiwa na Mamlaka ikilinganishwa na abiria 1,827,666 waliohudumiwa mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 11.5. Katika kipindi hicho, abiria waliohudumiwa na Mamlaka waliongezeka katika bandari za Dar es Salaam, Kigoma na Kyela wakati abiria waliohudumiwa katika bandari ya Mwanza walipungua.

Jedwali Na. 16.5: Idadi ya Abiria Waliohudumiwa

Bandari	2012/13	2013/14	2014/15	2015/2016	2016/17
DSM	1,373,146	1,412,357	1,569,053	1,614,831	1,848,937
Tanga	23,287	12,747	-	-	10,508
Mwanza	395,808	735,794	340,125	206,763	165,098
Kigoma	20,063	15,239	38,749	4,700	9,895
Kyela	13,759	12,325	15,541	1,372	3,415
Jumla	1,826,063	2,188,462	1,963,468	1,827,666	2,037,853

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Muda wa Meli Kukaa Bandarini

279. Muda wa meli kukaa bandarini kwa kitengo cha kontena uliongezeka hadi kufikia siku 2.1 mwaka 2016/17 kutoka siku 2.0 mwaka 2015/16. Kwa upande wa mizigo ya kawaida, muda wa meli kukaa bandarini uliongezeka na kufikia siku 2.7 kutoka siku 2.5 mwaka 2015/16. Vile vile, kwa mizigo ya kontena, muda wa kukaa bandarini baada ya kupakuliwa kutoka melini na kabla ya mteja

kuchukua ulikuwa wastani wa siku 11.5 ikilinganishwa na siku 10.2 mwaka 2015/16. Aidha, katika kitengo cha mafuta muda ulipungua na kufikia siku 3.0 kutoka siku 3.2 mwaka 2015/16.

Shehena za Nchi Jirani

280. Mwaka 2016/17, jumla ya tani 4,785,219 za mizigo ya kwenda nchi jirani zilihudumiwa katika bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na tani 4,839,467 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 1.1. Shehena za mizigo kwenda nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zambia ambazo ndizo zenye kiwango kikubwa cha mizigo zilipungua kwa asilimia 22.1 na 6.2 kwa mtiririko huo. Upungufu huo ulitokana na ushindani katika bandari za nchi jirani. Hata hivyo, shehena za mizigo kwenda nchi jirani za Malawi ziliongezeka kwa asilimia 103.8, Uganda (asilimia 53.7), Rwanda (asilimia 20.6) na Burundi (asilimia 3.4).

Jedwali Na.16.6 : Shehena za Nchi Jirani

Nchi	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17
Zambia	1,858,718	1,818,141	1,737,650	1,819,069	1,705,659
J.D. Kongo	965,377	1,352,457	1,677,527	1,464,847	1,141,611
Burundi	308,180	346,159	332,263	351,044	363,060
Rwanda	636,998	670,634	724,683	839,826	1,012,889
Malawi	93,411	141,536	94,294	106,883	217,852
Uganda	190,876	122,318	127,737	156,105	239,953
Nyinginezo	70,148	118,206	319,298	101,693	104,195
Jumla	4,123,708	4,569,451	5,013,452	4,839,467	4,785,219

Chanzo: Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)

Uchukuzi Kwenye Maziwa

Kampuni ya Huduma za Meli

281. Mwaka 2017, jumla ya abiria 49,885 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 101,103 mwaka 2016, sawa upungufu wa asilimia 50.7. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 12,773 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 18,419 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 30.7. Vile vile, utendaji katika huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo ulishuka kutokana na kusimama kwa meli za MV. Clarias, MV. Serengeti, MV. Liemba, MV. Songea na MV. Sangara kwa nyakati tofauti kulikotokana na uchakavu wa mitambo ya meli hizo. Aidha, meli ya mizigo ya MV. Umoja ilisimama kwa muda mrefu kutokana na kukosekana kwa biashara ya kusafirisha shehena ya mizigo kati ya Mwanza na Portbel-Uganda.

Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP)

282. Mwaka 2017, shehena zilizosafirishwa na kampuni ya SINOTASHIP ziliongezeka kwa asilimia 48.7 hadi kufikia tani 580,000 ikilinganishwa na tani 390,000 mwaka 2016. Ongezeko hilo lilitokana na kampuni kukodisha kwa mkataba meli ya MV. Changshun II yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa wakati mmoja kwa Kampuni ya COSCO Container Line. Aidha, idadi ya makasha yaliyohudumiwa na kampuni katika bandari ya Dar es Salaam iliongezeka kutoka makasha 8,800 mwaka 2016 hadi kufikia makasha 20,880. Ongezeko hilo lilitokana na Kampuni ya COSCO Container Line kuongeza idadi ya njia za kusafirishia mizigo kutoka njia mbili hadi kufikia njia nne kutoka Asia.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

283. Mwaka 2017, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilitoa huduma za hali ya hewa katika Bahari ya Hindi kwa meli na boti 3,100 ikilinganishwa na meli na boti 2,586 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Hii ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za hali ya hewa. Katika kipindi hicho, idadi ya wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa kwa sekta ya usafiri wa anga iliongezeka na kufikia 42,000 ikilinganishwa na wateja 40,082 mwaka 2016. Vile vile, kiwango cha usahihi wa utabiri wa hali ya hewa kiliongezeka kutoka asilimia 84.0 mwaka 2016 hadi asilimia 87.1 mwaka 2017. Hii ilitokana na Mamlaka kuongeza uwezo wa kitalaam na vifaa vya kisasa katika utabiri wa hali ya hewa.

Jedwali Na. 16.7: Viashiria vya Ufanisi wa Utendaji katika Sekta ya Hali ya Hewa

Kipimo cha Utendaji (KPI)	Maelezo	2015	2016	2017
Kiwango cha usahihi wa utabiri wa siku na msimu (Asilimia)	Usahihi wa Utabiri	81.0	84.0	87.1
Idadi ya wateja na watumiaji wa huduma za hali ya hewa	Sekta ya Usafiri wa Anga	38,761	40,082	42,000
	Meli na Boti	2,651	2,586	3,100
	Huduma mahsusi	193	268	530
Kiwango cha watumiaji na wateja wanaoridhika na huduma za hali ya hewa (Asilimia)	Kiwango cha kuridhika	85.0	86.0	88.7

Chanzo: Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

HUDUMA ZA MAWASILIANO

Huduma za Posta

284. Mwaka, jumla ya barua 6,750,443 zilisafirishwa na Shirika la Posta Tanzania ndani ya nchi ikilinganishwa na barua 24,445,425 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 72.4. Katika kipindi hicho, barua zilizotumwa nje ya nchi zilikuwa 1,852,600 ikilinganishwa na barua 3,405,317 mwaka 2016. Upungufu huu ulitokana na kuongezeka kwa ushindani na teknolojia ya mawasiliano.

285. Vifurushi vilivyosafirishwa ndani ya nchi vilikuwa 68,214 mwaka 2017 ikilinganishwa na vifurushi 86,902 vilivyosafirishwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 21.5. Vile vile, vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi vilipungua kwa asilimia 18.6 kufikia vifurushi 3,455 mwaka 2017 kutoka vifurushi 4,242 vilivyotumwa mwaka 2016. Upungufu wa idadi ya vifurushi vya kwenda nje ya nchi ulitokana na mabadiliko ya taratibu kwa watumaji kutakiwa kuwa na vibali mbalimbali.

286. Rejesta 347,879 zilisafirishwa nchini mwaka 2017 ikilinganishwa na rejesta 578,731 zilizosafirishwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 39.9. Vile vile, rejesta zilizotumwa nje ya nchi zilipungua kwa asilimia 50.9 hadi kufikia rejesta 22,605 mwaka 2017 kutoka rejesta 46,069 zilizotumwa mwaka 2016. Hii ilitokana na kupungua kwa rejesta zilizotumwa nje ya nchi hasa kutoka asasi za kijamii.

287. Kwa upande wa nyaraka na vipeto vilivyotumwa kwa njia ya haraka (EMS) nchini, vilipungua kwa asilimia 12.9 kufikia 719,390 mwaka 2017 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 825,479 vilivyotumwa mwaka 2016. Aidha, idadi ya nyaraka na vipeto vilivyotumwa nje ya nchi kwa njia ya haraka mwaka 2017 vilikuwa 13,220 ikilinganishwa na nyaraka na vipeto 54,755 vilivyotumwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 75.9. Upungufu huo ulitokana na mabadiliko ya taratibu kwa watumaji kutakiwa kuwa na vibali mbalimbali.

288. Barua na nyaraka 10,944 zilipokelewa na kusambazwa kwa njia ya huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji mwaka 2017 ikilinganishwa na barua na nyaraka 72,327 zilizopokelewa na kusambazwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 84.9. Upungufu huo, ulitokana na taasisi kuanzisha mitandao yao ya usambazaji na kujitoa katika huduma ya usambazaji wa barua za haraka ndani ya miji kupitia Posta.

289. Miamala ya fedha 531 ilihaulishwa kwa njia ya kielektroniki (Electronic Money Transfer) mwaka 2017 ikilinganishwa na miamala 516 mwaka 2016,

sawa na ongezeko la asilimia 2.9. Huduma ya Money Gram iliendelea kutolewa ambapo ilikuwa na jumla ya vituo 57 mwaka 2017 sawa na ilivyokuwa mwaka 2016. Aidha, mwaka 2017, miamala ya fedha 448 ilitumwa kupitia mfumo wa kimataifa wa utumaji fedha ikilinganishwa na miamala 7,039 iliyotumwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 93.6. Upungufu huo ulitokana na kufungwa kwa huduma ya miamala ya kimataifa kwa baadhi ya nchi zilizokuwa na madeni makubwa ya fedha za wateja na baadhi ya benki za biashara zenye matawi yake hapa nchini kufungua matawi yake katika nchi zilizokuwa zinatumia huduma ya miamala ya fedha kupitia mfumo wa kimataifa. Hatua hii ilisababisha wateja wengi kutumia huduma za benki badala ya Posta. Katika kipindi hicho, jumla ya wateja 151,980 walihudumiwa kwa kupitia huduma ya kufanya malipo kwa uwakala ya Post Giro ndani ya nchi ikilinganishwa na wateja 168,867 mwaka 2016. Huduma hii hutumika kulipa pensheni za wastaafu kupitia mifuko ya hifadhi za jamii na gawio la hisa za makampuni yaliyoorodheshwa katika soko la Hisa la Dar es Salaam.

Huduma za Simu

290. Hadi kufikia Desemba 2017, mitandao ya simu za viganjani ilikuwa na jumla ya kadi za simu 39,953,860 ikilinganishwa na kadi 40,173,783 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 0.6. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa umakini wa usajili wa kadi za simu unaofanywa na kampuni za simu kwa usimamizi wa Mamlaka ya Mawasilino Tanzania, na kupungua kwa gharama za mawasiliano ndani na nje ya mtandao kutokana na upangaji bei wa vifurushi na hivyo kupunguza ulazima wa watumaji wa huduma za mawasiliano kuwa na kadi za simu zaidi ya moja. Kati ya kadi hizo, zilizosajiliwa rasmi zilikuwa 39,498,921, sawa na asilimia 99.0 ya kadi zote. Aidha, kati ya kadi zote, kampuni ya simu ya Vodacom ilikuwa na asilimia 32.2 ya kadi zote; kampuni ya Tigo (asilimia 27.7); Airtel (asilimia 27.2); Halotel (asilimia 9.5); Zantel (asilimia 2.3); TTCL (asilimia 0.8) na Smart (asilimia 0.3). Kwa upande mwingine, watumiaji wa simu za mezani walipungua kwa asilimia 1.9 hadi kufikia watumiaji 127,094 mwaka 2017 kutoka watumiaji 129,597 mwaka 2016.

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

291. Hadi Desemba, 2017 jumla ya kilometa 28,560 za miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zilijengwa, zikijumuisha kilometa 7,560 zilizojengwa na Serikali na kilometa 21,000 zilizojengwa na watoa huduma za mawasiliano. Aidha, hadi Desemba 2017, kata 451 zenye vijiji 1,954 zilifikishiwa huduma ya mawasiliano kwa kupitia ruzuku ya Serikali kwa watoa huduma za mawasiliano. Vile vile, jumla ya vijiji 3,712 vilifikishiwa huduma ya mawasiliano kwa kupitia ushirikiano wa Serikali na Kampuni ya Viettel.

Kadhalika, miundombinu ya mawasiliano ilifikishwa katika ofisi za halmashauri 119; vituo vya posta 55; vituo vya polisi 121; hospitali za wilaya 95; mahakama 25; na shule 425 za sekondari.

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Uendelezaji wa Rasilimali Watu

292. Mwaka 2017, Serikali ilindelea na juhudi za kuongeza rasilimali watu katika teknolojia na tasnia ya ubunifu nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 4,180 walidahiliwa katika Chuo Kikuu cha Ardhi. Aidha, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 4,218, ambapo wanaume walikuwa 3,509 na wanawake 709. Vile vile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 2,089 ambapo wanaume walikuwa 1,648 na wanawake 441.

Udhibiti wa Mionzi

293. Mwaka 2017, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania ilipokea na kutathmini maombi 237 ya leseni za matumizi na umiliki wa vyanzo vya mionzi ikilinganishwa na maombi 273 ya mwaka 2016, ambapo maombi yote yalipata vibali baada ya kukidhi matakwa na vigezo vya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya mwaka 2003. Vigezo hivyo vinahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji na mpango wa uhifadhi wa kudumu wa mabaki ya chanzo cha mionzi. Aidha, mwaka 2017 Tume ilipima kiasi cha mionzi kwa wafanyakazi 423 kutoka katika vituo 68 ikilinganishwa na wafanyakazi 317 kutoka vituo 51 mwaka 2016. Kiwango cha mionzi kwa wafanyakazi ndani ya miezi mitatu kilikuwa chini ya 5 mSv ambacho kinakubalika kimataifa. Vile vile, Tume ilikagua vituo 23 vinavyotumia mionzi na kutoa ushauri wa maboresho ya usalama wa watumiaji na mazingira ikilinganishwa na vituo 131 vilivyokaguliwa mwaka 2016. Mwaka 2017, kulikuwa na vituo vipya 70 vya watumiaji wa vyanzo vya mionzi na hivyo kufikia jumla ya vituo 788 vinavyotumia mionzi nchini.

294. Mwaka 2017, Tume ilikagua vituo vya mionzi katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Tanga na Mtwara pamoja na Mipaka ya Namanga, Tarakea, Sirari, Holili, Horohoro, Mtukula, na Tunduma ili kutathmini hali ya vifaa vinavyotumika iwapo vinakidhi mahitaji ya sheria. Katika maeneo yaliyokaguliwa, Tume ilifanya upimaji wa viwango vya mionzi kwa sampuli 2,012 ikilinganishwa na sampuli 1,806 za mwaka 2016. Kati ya hizo, sampuli 1,002 zilikuwa za vyakula vilivyoingia nchini, sampuli 602 za vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi, sampuli 238 za vyakula vya wanyama na sampuli 58 za sigara. Aidha, mwaka 2017 Tume ilikarabati vifaa 43 vya elektroniki, vifaa tisa (9) vya ukaguzi na uhakiki wa vifaa vya ujenzi wa barabara (troxler

gauges) pamoja na mashine ya uhakiki wa mionzi (calibration irradiation machine).

HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Sekta ya Habari

295. Mwaka 2017, jumla ya magazeti na majarida 161 yalisajiliwa ikilinganishwa na magazeti na majarida 26 mwaka 2016. Kuongezeka kwa usajili kulitokana na mwitikio wa kutekeleza matakwa ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na kanuni zake za mwaka 2017 ambapo magazeti na majarida yalitakiwa kusajiliwa upya baada ya sheria kupitishwa na Bunge. Katika kipindi hicho, kulikuwa na jumla ya vituo vya redio 152 na luninga 35. Takwimu zinabainisha kuwa mwaka 2017, vituo vya redio 6 na luninga 3 vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo vya redio 23 na luninga 6 vilivyopata usajili mwaka 2016. Kupungua kwa usajili wa vituo kulitokana na upungufu wa masafa ya kutangazia katika maeneo ya miji mikubwa hasa katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Dar es Salaam.

Jedwali 16.8: Idadi ya Vituo vya Radio na Televisheni Vilivyosajiliwa

Mwaka	Idadi ya Magazeti/Majarida	Idadi ya Vituo vya Redio	Idadi ya Vituo vya Televisheni
2010	8	14	1
2011	41	12	0
2012	29	12	0
2013	36	4	0
2014	23	8	3
2015	39	22	1
2016	26	23	6
2017	161	6	3

Chanzo: Idara ya Habari-MAELEZO, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Sekta ya Maendeleo ya Sanaa

296. Mwaka 2016/2017 Serikali kupitia Bodi ya Filamu Tanzania ilitoa vibali 153 vya utengenezaji wa filamu, makala za filamu na picha jongevu kwa kampuni za ndani na nje ya nchi ikilinganishwa na vibali 168 vilivyotolewa mwaka 2015/2016, sawa na upungufu wa asilimia 8.9. Upungufu huu ulitokana na ukuaji wa haraka wa teknolojia unaowezesha filamu kuchukuliwa na vifaa vyepesi pamoja na baadhi ya waombaji kutokidhi vigezo.

Jedwali 16.9: Idadi ya Vibali vya Kutengeneza Filamu Vilivyotolewa Nchini

Mwaka	Vibali vya Wageni	Vibali vya Watanzania	Jumla
2011/12	84	21	105
2012/13	123	30	153
2013/14	125	33	158
2014/15	133	36	169
2015/16	137	31	168
2016/17	123	30	153

Chanzo: Bodi ya Filamu Tanzania.

Huduma Zitolewazo na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)

297. Katika kipindi cha mwaka 2016/17, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lilirusha jumla ya vipindi 87 kupitia radio na television ikilinganishwa na vipindi 110 vilivyorushwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 20.9. Aidha, Baraza lilitoa ithibati ya lugha kwa vitabu vinavyokusudiwa kutumika shuleni ambapo mwaka 2016/17 lilipitia miswada 61 ikilinganishwa na miswada 60 iliyopitiwa mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia 1.7. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa mwamko wa waandishi na wachapishaji wanaohitaji huduma hii.

298. Mwaka 2016/17, BAKITA lilitafsiri nyaraka 268, na kuhariri nyaraka 10 ikilinganishwa na nyaraka 350 (tafsiri) na nyaraka 20 (uhariri) mwaka 2015/2016, sawa na upungufu wa asilimia 23 na 50 kwa mtiririko huo. Upungufu huu ulitokana na idadi ndogo ya wateja waliojitokeza kwa ajili ya huduma hizi. Aidha, huduma ya ukalimani iliongezeka kufikia tatu mwaka 2016/17 ikilinganishwa na mbili zilizofanyika mwaka 2015/16 sawa na ongezeko la asilimia 50. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa wateja wanaohitaji huduma hii kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa ubainishaji makosa yanayofanywa na vyombo mbalimbali vya habari, jumla ya makosa 805 yalibainishwa mwaka 2016/17 ikilinganishwa na makosa 1,048 yaliyobainishwa mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 23.2. Mafanikio haya yanatokana na jitihada za utoaji elimu mara kwa mara kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya maneno ya lugha ya Kiswahili.

Jedwali Na. 16.10: Idadi ya Huduma Zilizotolewa

Mwaka	Vipindi vya redio na televisheni	Huduma ya Ithibati	Huduma ya Tafsiri	Huduma ya Ukalimani	Huduma ya Uhariri	Makosa yaliyobainika kutumiwa katika vyombo vya habari.
2010	156	24	300	3	9	1,300
2011	156	27	350	4	10	1,248
2012	156	25	280	5	9	1,248
2013	156	30	400	5	10	1,120
2014	156	24	410	3	7	1,010
2015	118	121	320	3	8	1,200
2016	110	60	350	2	20	1,048
2017	87	61	268	3	10	805

Chanzo: Baraza la Kiswahili la Taifa

Maendeleo ya Michezo

Usajili wa Vilabu vya Michezo

299. Mwaka 2017, kulikuwa na jumla ya vilabu vya michezo vilivyosajiliwa 288 ikilinganishwa na vilabu 331 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 13. Upungufu huu ulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo vilabu vingi ambavyo awali havikuwa na usajili kujitokeza kwa wingi kusajiliwa mwaka 2016. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya vyama vya michezo 29 vilisajiliwa ikilinganishwa na vyama 9 vilivyosajiliwa mwaka 2016. Ongezeko hili lilitokana na uzingatiaji wa takwa la Sheria ya Vyama vya Michezo kutoruhusiwa kuandaa mashindano bila kuwa na usajili. Vile vile, jumla ya vituo 13 vya michezo vilisajiliwa ikilinganishwa na vituo 15 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 13. Aidha, mwaka 2017, Serikali ilianza usajili mpya wa wakuzaji/mawakala wa michezo ambapo jumla ya wakuzaji/mawakala wa michezo 14 walisajiliwa.

Jedwali Na. 16.11: Mwenendo wa Vilabu, Vyama, na Vituo vya Michezo Vilivyosajiliwa

Mwaka	Vilabu vya Michezo	Vyama vya Michezo	Vituo vya Michezo	Wakuzaji /Mawakala wa Michezo
2010	272	9	9	
2011	168	5	2	
2012	339	26	5	
2013	285	37	12	
2014	464	17	7	
2015	224	15	12	
2016	331	9	15	
2017	288	29	13	14

Chanzo: Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 67

Maelezo	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Urefu wa Reli	KM	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707	2707
Magari ya Moshi:	Namba	45	43	25	22	20	45	45	30	44	44
Mvuke	Namba	1	1	0	0	0	0	0	0	0	0
Dizeli	Namba	45	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Mainlain		5	5	21	19	16	38	38	21	40	40
Shunting		40	38	4	3	4	7	7	9	4	4
Jumla ya mabehewa:	Namba	1648	1357	1071	1326	1162	1200	1214	1155	426	426
Abiria	Namba	45	68	50	53	36	91	91	56	56	56
Mizigo ya kawaida	Namba	1190	1093	648	658	635	681	590	561	22	22
Mafuta	Namba	244	178	179	335	208	178	203	196	123	123
Mifugo	Namba	18	39	88	88	80	39	64	64	27	27
Mengineyo	Namba	151	105	106	192	203	211	266	278	198	198
Uchukuzi	Namba										
Abiria	000	392	285	284	227	339	373	170	196	1707	2150
Mizigo	Tani'000	429	237	265	138	154	185	127	283	102	170

Chanzo: Shirika la Reli Tanzania

RELI YA UHURU - TAZARA

Jedwali Na. 68

Maelezo	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Urefu wa Reli Kuu	Km	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860	1860
Magari ya Moshi	Namba	10	16	15	13	13	15	16	17	21	17
Reli Kuu	Namba	8	11	10	9	9	11	13	12	14	12
Ya kujongeza	Namba	2	5	5	4	5	4	3	6	7	7
Mabehewa ya abiria	Namba	62	53	36	36	35	52	50	51	56	49
Abiria	Namba	53	44	31	30	30	45	44	43	48	40
Chakula	Namba	4	3	2	3	2	3	3	3	4	4
Vifurushi	Namba	5	6	3	3	3	4	3	5	4	5
Mabehewa ya mizigo	Namba	1371	1412	1620	930	858	1391	1101	1142	1221	1033
Mizigo ya kawaida	Namba	1217	1174	1381	795	765	1229	966	1007	1077	972
Mifugo	Namba	0	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Mafuta	Namba	114	196	197	93	59	104	82	82	89	26
Barafu	Namba	4	7	7	7	0	5	5	5	5	0
Mengineyo	Namba	2	2	2	2	1	1	1	1	1	1
Breki	Namba	17	16	16	16	16	35	30	30	32	30
Ballast	Namba	17	17	17	17	17	17	17	17	17	4
Uchukuzi mizigo (Tani)	000	525	333	540	248	259	245	33	81	96	171
Abiria	000	1177	923	758	414	678	654	287	327	440	443

Chanzo: Mamlaka ya Reli ya Uhuru

+ Urefu ni km. 1860.54, km 974.814 zikiwa nchini Tanzania

USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 69

Maelezo	Kipimo	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Jumla ya meli	Namba	1842	1274	1232	1600	742	1426	1617	1684	1688
Uwezo wa kubeba mizigo	000	17472	18721	24240	24496	13359	23278	31614	31278	31287
Jumla ya abiria	000	141	228	312	375	347	1000	1612	1735	1874
Jumla ya bidhaa zote	000 Dwt	4946	4954	5432	10122	5547	9082	14601	13580	13761
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	4382	4559	4816	9018	3899	7998	11901	11260	11460
Za kawaida	000wt	2430	2159	2474	5021	2682	4495	6657	6087	6376
Saruji	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	1852	2400	2342	3997	1217	3489	4882	4772	4740
Mengineyo1	000wt	100	0	0	0	0	14	362	401	344
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	497	466	616	1105	414	808	2499	2031	2045
Za kawaida	000wt	466	419	557	1033	391	763	2137	1915	1986
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	24	47	59	72	23	45	362	116	59
Mengineyo1	000wt	7	0	0	0	0	0	0	0	0
Mabadilishano	000wt	68	0	32	15	0	275	201	289	256

Chanzo: Mamlaka ya Bandari

1 Kama vile mbolea, mollasses, tallow fats n.k

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Jumla ya meli	Namba	144	101	201	232	92	64	63	87	72
Uwezo wa kubeba mizigo	000	671	1059	1005	1378	700	990	1018	1258	1041
Jumla ya abiria	000	0	228	312	2865	0	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000wt	359	529	508	608	271	536	645	677	486
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	213	357	373	1051	5357	437	561	614	436
Za kawaida	000wt	147	313	365	436	3171	437	483	398	141
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	66	44	8	615	2186	0	78	216	295
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	145	171	507	166	912	100	83	63	50
Za kawaida	000wt	145	171	507	166	912	100	83	63	50
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-
Mabadilishano	000wt	-	-	-	-	-	-	-	-	-

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwali Na. 69 (linaendelea)

Maelezo	Kipimo	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Jumla ya meli	Namba	32	58	129	498	339	428	46	113	105
Uwezo wa kubeba mizigo	000	31	455	307	1557	1245	1343	593	460	457
Jumla ya abiria	000	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla ya bidhaa zote	000	95	107	112	178	144	248	248	375	378
Bidhaa zilizopakuliwa	000wt	23	39	44	309	894	149	109	158	91
Za kawaida	000wt	23	36	35	55	274	140	108	147	91
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	0	3	9	254	620	9	1	10	0
Bidhaa zilizopakiwa	000wt	72	68	71	123	70	100	139	218	286
Za kawaida	000wt	72	68	71	113	70	100	139	218	286
Mafuta (<i>Petroleum</i>)	000wt	-	0	0	10	0	0	0	0	0
Mabadilishano	000wt	-	0	0	0	0	0	0	0	0

Chanzo: Mamlaka ya Bandari Tanzania

- Takwimu hazikupatikana

HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 70

Maelezo	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Ofisi Ndogo Posta	Namba	167	202	171	105	65	74	74	65	65	66
Franchised Post Offices	Namba	113	81	81	151	112	89	89	90	90	87
Ofisi Kubwa	Namba	172	170	170	163	147	160	160	158	158	154
Jumla	Namba	452	453	422	419	324	323	323	313	313	307
Masanduku Binafsi	000	174	117		146	162	173	142	160	160	161
Masanduku Yaliokodishwa	000	130	87	120	130	140	148	128	138	138	143
Maombi Yasiotimizwa	000	5	4	0	21	28	25	18	4	1	1
Mifuko Pekee Iliyokodishwa	Namba	182	62	183	361	278	212	260	180	180	342
Barua Zilizotumwa bila Vifurushi	Mill.	15	14	29	27	15	26	15	10	4	5
Regista na Barua za Amana	000	307	377	480	347	397	568	455	402	297	269
Vifurushi Nchini	000	18	9	15	10	15	29	12	17	36	51
Vifurushi Nje	000	6	2	7	11	12	9	5	9	2	3
Leseni za kuuza stamp	Namba	6242	6256	25145	28257	33311	2637	3715	0	0	4635
Huduma za Haraka, barua na vifurushi	"										
Ndani ya Nchi	"	216762	493709	283711	501635	404453	620478	406732	416007	452827	560710
Nje ya Nchi	"	14650	4012	18766	16965	24347	17130	20564	308288	6364	9534
EMS Money Fax	"	366382	23165	82002	36357	2940	550	745	748	272	18
EMS Fax (Fax message received)	"	121901	103558	31594	1595	876187	544	1194	3844	2518	129
Overnight Mail Services	"					9963	115126	0	0	0	0
Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	85595	68912	76983	115403	50082	87051	46652	53639	57605	24966
Vifurushi vya magazeti vilivyosafirishwa	"	12754	13934	2752	12040	10652	18784	8700	9130	113448	2120
Huduma za gari ndogo											
Idadi ya Mifuko ya Barua Iliyosafirishwa	"	4328	268	0	193	24095	849	714	9576	-	-
Amna za Haraka Zilizotolewa	"	0	20057	8169	4717	3087	2034	845	58423	272	127
Amna za Haraka Zilizolipwa	"	93508	23069	11881	17397	516	555	0	0	0	0
Amna za Haraka za Nje ya Nchi											
Zilizotumwa	"	1354	1030	1027	998	369	478	325	221	220	8
Zilizopokelewa	"	671	150	150	217	77	83	227	283	116	43
Amna za Posta zilizouzwa	"	8062	8831	1924	633	414	684	261	251	107	45
Amna za Posta Zilizolipwa	"	5709	5490	3262	1662	252	166	67	25	18	8
Benki ya Akiba (Transaction)											
Uwekaji Amana (Deposit)	"	24574	9535	18863	13438	6260	21491	12732	21541	261423	59249
Uchukuaji Amana (Withdrawal)	"	21122	11663	23025	72358	17527	37556	12807	18098	45449	76926

Chanzo: Shirika la Posta

IDADI YA WANAOTUMIA SIMU ZA MEZANI NA VIGANJANI

Jedwali Na. 71

Kampuni	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017	Badiliko (%)
A. Simu za Kiganjani										
Mobitel/Tigo	4178089	4477510	5450766	6370796	6297288	8624638	11115991	11677344	11062852	-5.3
Vodacom	6883661	8670536	11625773	9357672	10288972	11810064	12714297	12419425	12866059	3.6
Airtel	4910359	6021091	6993418	8356095	8995824	9551977	11047505	10456117	10855955	3.8
Zantel	1378595	1715985	1524601	3083889	1814444	1730105	1839391	1085642	935076	-13.9
Benson	3101	2396	1558	725	528	528	1560343	803251	131501	-83.6
TTCL Mobile	115681	246019	225578	221663	210766	296618	304214	293495	302726	3.1
Sasatel		24827	5824	4810	0	0	0	0	0	
Hallotel							1226678	3438509	3799691	10.5
Jumla Ndogo	17469486	21158364	25827518	27395650	27607822	32013930	38581741	40173783	39953860	-0.5
B. Simu za Mezani										
TTCL	157321	159054	159364	166148	158935	140391	138754	127112	127009	-0.1
Zantel	15601	15457	1699	10219	6064	10883	4065	2485	85	-96.6
Jumla Ndogo	172922	174511	161063	176367	164999	151274	142819	129597	127094	-1.9
Jumla Kuu	17642408	21332875	25988581	27572017	27772821	32165204	38724560	40303380	40080954	-0.6

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA (ATCL)*

Jedwali Na.73

Maelezo	Kipimo	2008	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Tani-Kilometa:											
Zilizokuwepo	000	-	5313	9482	1662	1932	6154	3052	60042	3937	863107
Zilizotumika	000	-	1508	2888	268	815	2503	117	30889	1756	89092
Matumizi	%	-	28.4	30.5	16.0	42.0	40.7	3.8	54.4	46.9	10.3
Viti-kilometa:											
Vilivyokuwepo	000	469426	41396	59724	7140	15131	54665	3680	21693	37877	225259
Vilivyotumika	000	129000	16469	30527	2946	10209	27279	946	11472	20692	122532
Matumizi	%	27.5	39.8	51.1	41.0	67.0	50.0	25.7	52.8	56.0	54.4
Abiria **	000	188	27	41	9	11	35	56	31	28	129
Mizigo ya ziada	Tani	30	9	8	2	0	45	0	53	1	41
Mizigo mingine	Tani	1044	54	145	4	5	35	45	42	7	50
Shehena za Posta	Tani	162	11	30	0	0	25	405	4 -		32

Chanzo: Shirika la Ndege Tanzania

- + Zinahusu "scheduled traffic" tu
- ++ Abiria waliolipa nauli kamili
- Takwimu hazikupatikana

SURA YA 17

NISHATI

Ufuaji wa Umeme

300. Mwaka 2017, uwezo wa uzalishaji wa umeme ulifikia MW 1,424.60 kutoka MW 1,469.39 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 3.0. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa umeme kupitia mitambo ya IPTL yenye uwezo wa kuzalisha MW 100 ulisitishwa na uwezo wa uzalishaji umeme kwa mitambo ya Kinyerezi II uliongezeka kwa MW 55.94 baada ya ujenzi wa mitambo hiyo kukamilika. Mahitaji ya juu ya umeme yalifikia MW 1,051.27 mwaka 2017 kama ilivyokuwa mwaka 2016. Aidha, umeme uliozalishwa kutoka vyanzo mbalimbali ulifikia saa za gigawati 7,115.32 ikilinganishwa na saa za gigawati 7,092.13 zilizozalishwa mwaka 2016, ikiwa ni ongezeko la asilimia 0.3. Kati ya hizo, saa za gigawati 6,800.67 zilizalishwa kwenye gridi ya Taifa; saa za gigawati 208.86 zilizalishwa kwenye vituo nje ya gridi ya Taifa; na saa za gigawati 105.79 ziliingizwa kwenye gridi ya Taifa kutoka nje ya nchi.

301. Mchanganuo wa umeme uliozalishwa katika gridi ya Taifa mwaka 2017 unaonesha kuwa: umeme wa mitambo ya nguvu za maji ulikuwa saa za gigawati 2,349.91; gesi saa za gigawati 4,226.35 na mafuta mazito na dizeli saa za gigawati 224.41. Umeme uliozalishwa na mitambo inayomilikiwa na TANESCO ulikuwa saa za gigawati 5,469.57 mwaka 2017 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,153.07 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.1. Hii ilitokana na kuingizwa kwa MW 55.94 kutoka kituo cha kufua umeme cha Kinyerezi II. Kampuni binafsi kwa pamoja zilizalisha saa za gigawati 1,539.97 mwaka 2017 ikilinganishwa na saa za gigawati 1,795.46 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 14.2. Upungufu huo ulitokana na kuisha kwa muda wa leseni za makampuni binafsi ya kufua umeme wa dharura. Aidha, umeme ulionunuliwa kutoka nchi jirani za Kenya, Uganda na Zambia ulikuwa saa za gigawati 105.79 mwaka 2017 ikilinganishwa na saa za gigawati 101.54 mwaka 2016, sawa na asilimia 1.5 ya umeme wote uliozalishwa mwaka 2017.

302. Kwa upande wa mauzo, umeme uliouzwa kwa watumiaji mbalimbali ulikuwa saa za gigawati 5,956.18 mwaka 2017 ikilinganishwa na saa za gigawati 5,871.47 zilizouzwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.4. Umeme uliopotea kutokana na uchakavu wa mitambo ya kusafirisha na kusambaza

umeme ulikuwa saa za gigawati 1,159.10 sawa na asilimia 16.29 ya umeme uliozalishwa ikilinganishwa na saa za gigawati 1,220.66 sawa na asilimia 17.2 ya umeme uliozalishwa mwaka 2016. Aidha, taarifa kuhusu upatikanaji wa umeme kwa mwaka 2016 (Energy Access Situation Survey, 2016), inaonesha kuwa asilimia 32.8 ya kaya zote Tanzania Bara zimeunganishiwa umeme, ambapo kwa upande wa vijijini ni asilimia 16.9 na asilimia 65.3 kwa maeneo ya mijini.

**UWEZO WA MITAMBO YA UMEME NA KIASI CHA UMEME ULIOZALISHWA
KWA VITUO MWAKA 2017**

Jedwali Na. 74

Kituo	Uwezo (MW)	Umeme Uliozalishwa (GWh)
Kidatu	204.0	941.4
Kihansi	180.0	815.4
Mtera	80.0	276.4
New Pangani Falls	68.0	50.5
Hale	21.0	22.2
Nyumba ya Mungu	8.0	219.5
Uwemba	0.8	1.1
Mwenga Min Hydro	4.0	16.3
Yovi	1.0	4.9
Matembwe	0.6	0.3
Darakuta	0.3	1.9
Jumla Ndogo - Hydro	567.7	2349.9
Ubungo Gas Plant I	102.0	593.6
Tegeta Gas Plant	45.0	241.8
Ubungo Gas Plant II	129.0	959.0
Zuzu	7.4	0.7
Nyakato	63.0	148.1
Biharamuro	4.1	0.7
Kinyerezi I	150.0	951.3
Kinyerezi II	55.9	15.8
Jumla Thermal	556.5	2910.8
IPTL	-	52.1
Songas	189.0	1465.0
Imports from SPPs	10.5	22.8
Jumla Wazalishaji Binafsi	199.5	1540.0
Jumla Grid	1323.7	6800.7
MATAWI MENGINE (ISOLATED STATIONS)		
Kigoma	6.3	27.7
Songea	8.2	9.2
Mpanda	5.7	10.5
Mbinga	2.0	5.3
Ngara	2.5	5.6
Mafia	2.2	5.0
Tunduru	2.1	6.5
Ludewa	1.3	1.4
Liwale	0.9	2.7
Somanga	7.5	13.9
Sumbawanga	5.0	3.4
Kasulu	2.5	7.2
Kibondo	2.5	4.8
Loliondo	5.0	1.2
Namtumbo	0.3	1.2
Mtwara	17.9	81.8
Inyonga	0.5	0.1
Madaba	0.5	0.0
Bukoba	2.6	0.4
Ngombeni	1.2	0.0
Tulila	5.0	18.4
Andoya	0.5	2.6
Umeme kutoka nchi jirani	19.0	105.8
Jumla Nje ya Gridi	100.9	314.7
Jumla Kuu ya Umeme – Nchi Nzima	1424.6	7115.3

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

MAUZO YA UMEME KWA WATUMIAJI MBALIMBALI

Jedwali Na. 75

GWH

Mwaka	Tanzania Bara			Zanzibar	Jumla	Umeme uliopotea	Jumla ya umeme uliotengenezwa
	Wateja wadogo (D1)	Wateja wa Kati (T1)	Wateja Wakubwa (T2, T3 & T8)	T5			
2011	328.8	1270.8	2118.0	277.2	3994.7	1158.7	5153.5
2012	320.8	1480.1	2301.8	298.6	4401.4	1048.3	5449.6
2013	280.6	1747.0	2560.4	218.7	4806.7	1139.5	5946.2
2014	217.0	1891.0	2595.0	348.5	5051.5	1135.3	6186.8
2015	148.8	2082.7	2721.1	344.6	5297.1	1119.7	6416.9
2016	345.3	2263.4	2887.2	375.6	5871.5	1220.7	7092.2
2017	301.5	2371.0	2893.3	390.4	5956.2	1159.1	7115.3

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MAUZO YA UMEME KWA MIKOA

Jedwali Na. 76

Mkoa	2009	2010	2011	2012	2013	2014	2015	2016	2017
Dodoma	79	83	86	94	105	111	116	137	150
Arusha	236	269	240	286	316	326	311	357	366
Manyara	17	19	20	23	24	25	26	29	32
Kilimanjaro	88	124	118	138	144	154	151	182	179
Tanga	166	209	219	245	264	266	300	322	330
Morogoro	121	179	163	207	221	232	212	240	243
Coast	94	106	116	142	171	199	220	260	302
Dar-es-Salaam	1014	1615	1387	1548	1932	2118	2229	2398	2413
Lindi	11	13	14	15	18	23	22	24	23
Mtwara	29	27	30	34	35	9	51	49	48
Ruvuma	15	21	21	24	27	28	31	34	35
Iringa	85	101	92	102	105	107	112	107	98
Mbeya	125	139	132	150	153	170	164	177	178
Singida	26	26	23	29	32	35	47	43	44
Tabora	84	97	95	103	109	60	52	57	56
Rukwa	12	17	19	19	20	22	23	28	27
Kigoma	12	16	18	21	23	25	28	29	35
Shinyanga	253	313	310	279	280	359	417	428	372
Kagera	33	44	29	55	53	54	60	72	77
Mwanza	192	215	200	224	231	241	236	262	283
Mara	52	110	109	108	125	134	135	142	157
Njombe								69	36
Katavi								4	11
Geita								34	43
Simyu								8	18
Songwe						6.4	11.4	5	10
Jumla Tanzania Bara	2744.0	3743.0	3440.5	3845.5	4388.0	4702.8	4952.6	5495.9	5565.8
Zanzibar	186.0	174.0	277.2	298.6	218.7	348.5	344.6	375.6	390.4
JUMLA	2930.0	3917.0	3717.8	4144.1	4606.7	5051.3	5297.1	5871.5	5956.2

Chanzo: Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

MW Megawatt

GWH GigaWatt-Hour (Saa za GigaWatt) = Million KWH

Utafutaji Mafuta na Gesi

Gesi Asilia

303. Mwaka 2017, uzalishaji wa gesi asilia katika visima vya Songosongo na Mnazi Bay ulifikia futi za ujazo bilioni 47.46 ikilinganishwa na futi za ujazo bilioni 48.32 zilizozalishwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 1.8. Hii ilitokana na kisima cha Kiliwani North kutoendelea kuzalisha gesi asilia katika kipindi cha mwaka 2017. Aidha, kukamilika kwa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam kuliongeza matumizi ya gesi asilia hadi kufikia wastani wa futi za ujazo milioni 175 kwa siku kwa mwaka 2017 kutoka futi za ujazo milioni 145 kwa siku kwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 20.7.

304. Mapato kutokana na mauzo ya gesi asilia yalipungua kwa asilimia 18.7 hadi kufikia dola za Marekani 42,261,263 mwaka 2017 ikilinganishwa na dola za Marekani 51,991,433 mwaka 2016. Upungufu huo ulitokana na kisima cha Kiliwani North kutoendelea kuzalisha gesi asilia na hivyo kupungua kwa kiasi cha gesi kilichouzwa.

305. Hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya futi za ujazo trilioni 57.55 zilikuwa zimegunduliwa ambapo kati ya hizo, futi za ujazo trilioni 10.41 zipo nchi kavu na sehemu yake ndio inayotumika kuzalisha gesi inayotumika hivi sasa nchini kwa matumizi ya kuzalisha umeme na matumizi ya viwandani. Kiasi kilichobaki cha futi za ujazo trilioni 47.13 zimegunduliwa katika kina kirefu cha maji baharini. Kwa upande mwingine, mwaka 2017, Serikali ilianza maandalizi ya Awamu ya Pili ya Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia Nchini ambao unahusisha usambazaji wa gesi asilia katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza na Mbeya. Upelekaji wa gesi asilia katika mikoa hiyo utaongeza kasi ya uendelezaji wa viwanda nchini pamoja na kuongeza matumizi ya nishati ya uhakika na yenye gharama nafuu katika taasisi na majumbani.

306. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa gesi iliyopatikana baharini inaendelezwa na kuuzwa katika soko la kimataifa ikiwa katika muundo wa gesi kimiminika (Liquefied Natural Gas, LNG) na sehemu kuuzwa katika soko la ndani. Aidha, kazi mbalimbali ziliendelea kutekelezwa katika mradi wa LNG ikiwa ni pamoja na: kukamilika kwa tafiti mbalimbali za kiufundi zilizopelekea uchaguzi wa teknolojia ya kuzalishia gesi baharini ; upembuzi wa awali wa kihandisi (Pre-FEED) kwa upande wa vitalu vya baharini ; na upatikanaji wa

eneo la mradi. Aidha, majadiliano kati ya nchi yenye rasilimali na wawekezaji (Host Government Agreement - HGA) yenye lengo la kuainisha haki na wajibu wa wawekezaji na Serikali katika uzalishaji wa gesi, ujenzi na uendeshaji wa mradi yaliendelea kufanyika ambapo pindi yatakapokamilika, yataruhusu mradi kuendelea katika hatua nyingine. Vile vile, Serikali iliendelea kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Timu ya Majadiliano ya Serikali (Government Negotiation Team, GNT) pamoja na wataalamu wengine wanaoendeleza mradi.

Jedwali Na. 17.1:Uzalishaji wa Gesi Asilia ya Songo Songo na Mnazi Bay

Mwaka	Futi za Ujazo (SCF)			
	Songosongo	Mnazibay	Kiliwani North	Jumla
2017	29,496,560,000	17,960,300,000	-	47,456,860,000
2016	29,747,400,000	5,792,141,976	2,783,497,46	48,323,024,922
2015	31,384,100,000	783,595,488	-	37,176,241,976
2014	33,061,500,000	715,942,883	-	33,845,095,488
2013	35,217,410,590	673,870,408	-	35,933,353,479
2012	36,233,010,000	664,980,487	-	36,906,880,408
2011	30,970,500,000	454,123,320	-	31,635,480,487
2010	27,633,000,000	323,686,310	-	28,087,123,320
2009	23,593,000,000	321,239,550	-	23,916,686,310
2008	20,084,000,000	258,186,803	-	20,405,239,550
2007	19,705,000,000	-	-	19,963,186,803
2006	17,907,000,000	-	-	17,907,000,000
2005	14,704,000,000	-	-	14,704,000,000
Jumla	246,901,960,000	27,948,067,225	2,783,497,46	396,260,172,743

Chanzo:Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania-TPDC

Jedwali Na. 17.2: Mapato Yaliyotokana na Mauzo ya Gesi ya Songo Songo na Mnazi Bay (Dola za Marekani)

Mwaka	Songo Songo	Mnazi Bay	Jumla
2017	22,795,142	19,466,121	42,261,263
2016	38,172,718	13,818,715	51,991,433
2015	43,854,236	1,921,965	45,776,201
2014	58,761,119	1,762,977	60,524,096
2013	50,582,385	1,592,879	52,175,264
2012	35,026,145	1,525,251	36,551,396
2011	38,337,903	1,444,856	39,782,759
2010	25,607,621	1,080,131	26,687,753
2009	21,403,804	396,109	21,799,913
2008	19,521,646	388,449	19,910,095
2007	16,861,492	305,236	17,166,727
2006	14,966,409	-	14,966,409
2005	9,019,384	-	9,019,384
Jumla	394,910,004	43,702,689	438,612,693

Chanzo : Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)

Uagizaji na Mwenendo wa Bei za Mafuta

307. Mafuta yaliyoingizwa nchini yalipungua kwa asilimia 2.3 hadi kufikia lita za ujazo milioni 5,361.5 mwaka 2017 kutoka lita za ujazo milioni 5,486.9 mwaka 2016. Hii ilitokana na kupungua kwa mafuta yaliyoagizwa kwa matumizi ya ndani. Katika kipindi hicho, mafuta yaliyoagizwa kwa ajili ya matumizi ya ndani yalipungua kwa asilimia 3.3 kutoka lita za ujazo milioni 3,302.3 mwaka 2016 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 3,193.2 mwaka 2017. Aidha, lita za ujazo milioni 2,168.2 zilisafirishwa kwenda nchi jirani mwaka 2017 ikilinganishwa na lita za ujazo milioni 2,185.1 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 0.8.

Jedwali Na. 17.3 Mafuta Yaliyoingizwa Nchini Mwaka 2017

Mwezi	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Taa	Mafuta ya Ndege	Mafuta Mazito (HFO)	Jumla
Januari	123,866,676	39,192,399	2,272,969	12,999,188		178,331,232
Februari	112,648,188	75,344,036	794,877	18,859,311	-	207,646,411
Machi	93,370,625	82,451,785		12,135,008	22,188,529	210,145,948
Aprili	92,420,003	53,812,639	1,128,246	15,394,035		162,754,924
Mei	75,443,928	54,823,939	978,551	16,936,649		148,183,067
Juni	105,529,141	78,930,449	1,001,413	15,907,399	-	201,368,403
Julai	116,048,620	59,145,683	1,553,372	9,791,418		186,539,093
Agosti	165,889,892	66,809,164	3,851,902	14,695,790		251,246,748
Septemba	99,308,313	110,742,113	3,167,355	18,616,925	5,606,778	237,441,483
Oktoba	243,605,222	105,366,218	3,471,079	24,395,144		376,837,662
Novemba	139,317,287	116,782,919	3,244,495	20,379,300		279,724,001
Desemba	139,646,419	100,413,504	4,559,062	14,338,368	17,305,832	276,263,185
Mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit)	236,662,193	234,619,617	4,641,442	847,351	-	476,770,603
Jumla Kuu	1,743,756,506	1,178,434,465	30,664,762	195,295,886	45,101,139	3,193,252,759

Chanzo: EWURA

**Jedwali Na. 17.4 Mafuta Yaliyopitishwa Nchini kwenda Nje ya Nchi
Mwaka 2017**

Mwezi	Dizeli	Petroli	Mafuta ya Taa/Ndege	Mafuta Mazito (HFO)	Jumla
Januari	146,195,172	60,061,434	5,656,000	-	211,912,607
Februari	109,586,649	94,968,844	6,012,897		210,568,390
Machi	97,048,367	110,500,219	7,480,297	11,263,101	226,291,984
Aprili	82,944,292	66,254,251	8,105,290	-	157,303,833
Mei	99,190,465	86,458,565	10,910,208	-	196,559,238
Juni	80,084,228	56,838,131	13,466,185	-	150,388,544
Julai	75,349,067	49,307,094	15,604,913		140,261,074
Agosti	199,210,277	103,460,773	15,401,415		318,072,465
Septemba	168,136,720	118,725,056	11,479,615	2,038,828	300,380,219
Oktoba	219,488,667	63,332,311	12,583,913		295,404,891
Novemba	131,700,500	93,947,644	14,406,707		240,054,851
Desemba	119,240,155	66,296,769	12,228,457		197,765,381
Ondoa mafuta ya nje yaliyouzwa ndani ya nchi (Localized Transit)	236,662,193	234,619,617	5,488,793		476,770,603
Jumla Kuu	1,291,512,366	735,531,474	127,847,104	13,301,930	2,168,192,874

Chanzo: EWURA

Bei za Mafuta

308. Mwaka 2017, wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia uliongezeka. Katika kipindi hicho, wastani wa bei ya mafuta ya petroli ulifikia dola za Marekani 540 kwa tani, mafuta ya dizeli dola za Marekani 484, na mafuta ya taa dola za Marekani 503 ikilinganishwa na dola za Marekani 462, dola za Marekani, 380 na dola za Marekani 407 mwaka 2016 kwa mtiririko huo. Bei hizi zilikuwa sawa na ongezeko la asilimia 16.9 kwa mafuta ya petroli, asilimia 27.4 kwa mafuta ya dizeli na asilimia 23.6 kwa mafuta ya taa. Kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia kulitokana na ongezeko la bei ya mafuta ghafi

kwa asilimia 24 mwaka 2017. Aidha, mwezi Desemba 2017 ulikuwa na kiwango cha juu cha wastani wa bei ya mafuta ikilinganishwa na miezi mingine. Katika kipindi hicho cha mwezi Desemba, wastani wa bei ya mafuta ya petroli kwa tani ulifikia dola za Marekani 599, mafuta ya dizeli dola za Marekani 549 na mafuta ya taa dola za Marekani 587.

Jedwali Na. 17.5: Bei za Mafuta katika Soko la Dunia (FOB) – Dola za Marekani kwa Tani za Ujazo (Metric Tons)

Aina ya Mafuta	Petroli			Dizeli			Mafuta ya Taa		
	2015	2016	2017	2015	2016	2017	2015	2016	2017
Januari	449	398	497	468	258	421	495	284	442
Februari	539	357	502	573	280	468	576	312	499
Machi	509	431	542	593	333	485	540	361	504
Aprili	529	467	557	622	352	505	553	381	510
Mei	594	497	531	669	401	470	597	425	476
Juni	562	498	555	689	429	480	577	451	497
Julai	495	440	521	643	397	455	509	419	474
Agosti	442	464	503	539	389	454	457	411	464
Septemba	449	478	510	503	399	462	467	425	485
Oktoba	433	512	560	485	449	516	455	473	529
Novemba	407	471	600	469	417	546	435	440	570
Desemba	329	532	599	438	461	549	363	498	587
Wastani wa Bei (USD/MT)	478	462	540	558	380	484	502	407	503
Wastani wa Ongezeko kwa mwaka (%)		-3.3	17		-32	28		-19	23

Chanzo: EWURA

309. Mwaka 2017, wastani wa bei za mafuta katika soko la ndani ulipanda ikilinganishwa na wastani wa bei kwa mwaka 2016. Wastani wa bei za ukomo za mafuta katika soko la ndani mwaka 2017 uliongezeka na kuwa shilingi 2,004 kwa lita moja ya mafuta ya petroli; shilingi 1,873 kwa mafuta ya dizeli; na shilingi 1,832 kwa mafuta ya taa ikilinganishwa na shilingi 1,845; shilingi 1,673; na shilingi 1,644 mwaka 2016 kwa mtiririko huo. Hii ni sawa na

ongezeko la wastani wa asilimia 8.6, 12.0 na 11.4 kwa mafuta ya petroli, dizeli, na mafuta ya taa kwa mtiririko huo. Ongezeko hilo la wastani wa bei lilitokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la nje mwaka 2017.

Jedwali Na.17.6: Mwenendo wa Bei za Mafuta kwa Dar es Salaam

Mwezi / Mwaka 2016	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/Lita)	Mafuta ya Taa (Sh/Lita)	Mwezi / Mwaka 2017	Petroli (Sh/Lita)	Dizeli (Sh/Lita)	Mafuta ya Taa (Sh/Lita)
Januari	1,898	1,747	1,699	Januari	1,890	1,732	1,700
Februari	1,842	1,600	1,699	Februari	1,959	1,861	1,852
Machi	1,811	1,486	1,465	Machi	2,060	1,913	1,852
Aprili	1,728	1,516	1,501	Aprili	2,057	1,925	1,858
Mei	1,785	1,602	1,578	Mei	2,027	1,844	1,842
Juni	1,867	1,633	1,607	Juni	2,052	1,888	1,825
Julai	1,888	1,720	1,687	Julai	1,978	1,830	1,830
Agosti	1,905	1,811	1,759	Agosti	1,867	1,719	1,719
Septemba	1,840	1,747	1,673	Septemba	1,989	1,887	1,811
Octoba	1,827	1,699	1,658	October	1,993	1,897	1,810
Novemba	1,860	1,720	1,669	Novemba	2,014	1,999	1,938
Desemba	1,890	1,798	1,737	Desemba	2,160	1,984	1,942
Wastani mwaka 2016	1,845	1,673	1,644	Wastani mwaka 2017	2,004	1,873	1,832
Wastani mwaka 2015	1,973	1,808	1,739	Wastani mwaka 2016	1,845	1,673	1,644
Mabadiliko (%)	-6.5	-7.5	-5.5	Mabadiliko (%)	8.6	12.0	11.4

Chanzo: EWURA

Nishati Jadidifu

Maporomoko Madogo ya Maji

310. Mwaka 2017, kiwango cha uzalishaji wa umeme kupitia maporomoko madogo ya maji kilifikia megawati 55.0 kutoka megawati 36.74 zilizozalishwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 49.7. Ongezeko hili lilitokana na kukamilika kwa miradi ya maporomoko ya maji ya *Kiliflower* megawati 1.5 (Arusha), Darukuta megawati 2 (Manyara) na Luponde megawati 3.5 (Njombe).

Aidha, kiasi cha Kilowati 0.6 kutoka mradi wa Darukuta ziliunganishwa kwenye gridi ya Taifa. Umeme uliotokana na maporomoko hayo ulitumika katika shughuli mbalimbali zikiwemo za umwagiliaji mashamba ya maua na chai, matumizi ya majumbani kwa wananchi katika maeneo hayo na katika taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo shule na zahanati.

Tungamotaka, Bayogesi na LPG

311. Mwaka 2017, uzalishaji wa umeme uliotokana na tungamotaka ulifikia megawati 42.0 ikilinganishwa na megawati 38.0 zilizozalishwa mwaka 2016. Kati ya kiasi hicho, megawati 10.5 ziliingizwa kwenye gridi ya Taifa na megawati 31.5 zilitumika kwa matumizi ya viwanda vya kuzalisha sukari na mazao ya misitu. Aidha, Serikali iliendelea kuweka msukumo mkubwa wa matumizi ya nishati ya bayogesi ili kupunguza matumizi makubwa ya mkaa na kuni ambapo hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya mitambo 30,000 ilijengwa ikilinganishwa na mitambo 28,000 iliyojengwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kwa upande mwingine, matumizi ya gesi ya mitungi (LPG) majumbani yaliendelea kuongezeka hasa katika sehemu za mijini na baadhi ya maeneo ya vijijini. Hii ilitokana na kuongezeka kwa muamko wa matumizi ya gesi badala ya mkaa na kuni pamoja na makampuni ya usambazaji na uuzaji wa nishati hii kuongeza vituo vya mauzo hadi vijijini.

Nishati ya Mionzi ya Jua

312. Mwaka 2017, matumizi ya nishati ya jua yaliongezeka ambapo kupitia teknolojia ya mifumo ya umeme wa jua majumbani (*Solar Home Systems*) zaidi ya megawati 15 zilipatikana. Aidha, upatikanaji wa umeme kupitia mifumo midogo ya umeme wa jua (*Solar min grid*) katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya Taifa uliongezeka ambapo takribani megawati 5 zilizalishwa kupitia teknolojia hii.

SURA YA 18

MAJI

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji

313. Mwaka 2017, Serikali iliendelea na mikakati ya kuhifadhi vyanzo vya maji ambapo vyanzo 261 vilitambuliwa kuwa katika hatari ya kuharibiwa na kuathiriwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ongezeko la shughuli za kibinadamu ikilinganishwa na vyanzo 269 mwaka 2016. Kati ya hivyo, vyanzo 85 viliwekewa mipaka na vipo katika mchakato wa kutangazwa kuwa maeneo tengefu ikilinganishwa na vyanzo 59 mwaka 2016. Aidha, maeneo 18 yalitangazwa kwenye gazeti la Serikali kuwa maeneo tengefu. Katika kipindi hicho, vituo vya kupima wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi vilifikia 694. Vile vile, Serikali ilishirikiana na wadau mbalimbali kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji na mitandao ya usambazaji maji.

314. Hadi Desemba 2017, jumla ya sampuli 3,471 za majisafi zilikusanywa na kuchunguzwa ambapo sampuli 2,844 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maji majumbani. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli 2,174 sawa na asilimia 76.4 zilikidhi viwango vinavyokubalika na sampuli 670 sawa na asilimia 23.6 hazikukidhi viwango. Kutokukidhi kwa viwango, kulitokana na uwepo wa viwango vikubwa vya madini ya chuma, manganese, chumvichumvi na vijidudu kwenye sampuli zilizochukuliwa katika wilaya za Tunduru, Pangani, Handeni na Mbeya.

315. Mwaka 2017, sampuli za maji 318 zilikusanywa na kuchunguzwa ili kuhakiki ubora wa maji yanayotumika kwa ajili ya shughuli za viwandani, ujenzi, umwagiliaji na utafiti. Kati ya hizo, sampuli 268 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya viwandani, sampuli 10 (ujenzi), sampuli 8 (umwagiliaji) na sampuli 32 kwa ajili ya shughuli za utafiti. Matokeo ya uchunguzi yalionesha kuwa sampuli zote zilikidhi viwango vya ubora kwa matumizi husika. Aidha, hadi Desemba 2017, jumla ya sampuli 256 za majitaka yanayorudishwa kwenye mazingira zilihakikiwa na kubainika kuwa sampuli 167 sawa na asilimia 65.2 hazikukidhi viwango vya ubora unaokubalika.

Huduma ya Maji Vijijini

316. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini kupitia programu ya kuendeleza sekta ya maji kwa lengo la kuongeza kiwango cha

upatikanaji wa maji vijijini. Hadi kufikia Desemba 2017, ujenzi wa miundombinu ya miradi 1,493 ulikamilika na miradi 366 ujenzi unaendelea kutekelezwa na umefikia hatua mbalimbali. Miradi hiyo inahusu ujenzi wa miradi ya vijiji 10 kwa kila halmashauri, miradi ya kimkakati, miradi ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji pamoja na miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo. Katika kipindi hicho, miundombinu ya maji iliyojengwa ilikuwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji 123,888 vyenye uwezo wa kuhudumia watu 30,972,000 sawa na asilimia 85.2 ya wananchi waishio vijijini. Kati ya hivyo, vituo 85,286 vinafanya kazi na kutoa huduma kwa watu 21,321,500 sawa na asilimia 58.7. Hii ilichangiwa na uwezo mdogo katika kusimamia na kuendesha miradi ya maji katika ngazi ya halmashauri.

Huduma za Maji Mijini

317. Mwaka 2017, mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira katika miji mikuu ya mikoa zilitoa huduma ya maji kwa wakazi takribani milioni 4.8 kwa wastani wa kiwango cha asilimia 78 ikilinganishwa na wakazi takribani milioni 4.5 kwa wastani wa kiwango cha asilimia 86 mwaka 2016. Upungufu huo ulitokana na kuongezeka kwa eneo la utoaji wa huduma baada ya upanuzi wa mipaka ya baadhi ya miji, kuanzishwa kwa miji mipya pamoja na uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji. Kwa upande mwingine, uzalishaji wa maji katika miji mikuu ya mikoa uliongezeka hadi kufikia mita za ujazo milioni 148.82 kutoka mita za ujazo milioni 147.11 mwaka 2016. Aidha, idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji iliongezeka kufikia wateja 462,790 kutoka wateja 428,435 mwaka 2016. Makusanyo yaliyopatikana yaliongezeka kwa asilimia 21.1 kutoka shilingi bilioni 110.68 mwaka 2016 hadi kufikia shilingi bilioni 134.04 mwaka 2017. Kwa upande wa miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa, utoaji wa huduma ya maji ulifikia wastani wa asilimia 60 ya wakazi wanaopata maji. Vile vile, uzalishaji wa maji uliongezeka hadi mita za ujazo milioni 62 mwaka 2017 kutoka mita za ujazo milioni 59 mwaka 2016. Halikadhalika, idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji iliongezeka hadi kufikia wateja 161,925 mwaka 2017 kutoka wateja 147,163 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 10.

318. Wastani wa upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa Jiji la Dar es Salaam uliongezeka kutoka asilimia 72 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 75 mwaka 2017 kwa wateja wapatao milioni 3 waliounganishiwa huduma ya maji. Aidha, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam

pamoja na maeneo ya miji ya Kibaha na Bagamoyo iliimarika baada ya kukamilika kwa miradi ya uzalishaji wa maji na ukarabati wa mabomba chakavu. Uzalishaji wa maji katika Miji Mikuu ya Mikoa uliongezeka kwa asilimia 1.2 kutoka mita za ujazo milioni 147.11 mwaka 2016 hadi kufikia mita za ujazo milioni 148.82 mwaka 2017. Aidha, idadi ya wateja wanaopata huduma ya maji iliongezeka kutoka wateja 428,435 mwaka 2016 hadi kufikia wateja 462,790 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 8.

Hali ya Sekta ya Umwagiliaji

319. Hadi kufikia Desemba 2017, jumla ya hekta 468,338 zilikuwa zinamwagiliwa. Eneo hilo la umwagiliaji linachangia asilimia 24 ya mahitaji ya chakula nchini. Katika kipindi hicho, Mradi wa Kuongeza Uzalishaji wa Zao la Mpunga ulikamilisha usanifu wa miundombinu ya skimu za Njage na Msolwa Ujamaa (Kilombero), Mvumi (Kilosa), Kigugu na Mbogo (Mvomero). Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wakulima viongozi 50 wa kamati za uendeshaji na utatuzi wa migogoro ya ndani na ya nje ya skimu. Halikadhalika, katika mradi wa kujenga uwezo kwa wataalam wa kanda za umwagiliaji, halmashauri za wilaya na wakulima, jumla ya wataalam 35 kutoka kanda 7 za umwagiliaji, wataalam 30 kutoka halmashauri za wilaya na wakulima 300 walinufaika na mafunzo kuhusu Mwongozo Yakinifu wa Umwagiliaji.

UZALISHAJI WA MAJI NA MAPATO YATOKANAYO NA MAJI MIJINI

Jedwali Na. 77

Mamlaka	Uzalishaji wa Maji (Mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Uzalishaji wa Maji (mita za ujazo)	Mapato (TShs)	Wastani wa Upatikanji wa Huduma ya Maji 2017 (%)
	2015		2016		2017		
Arusha	15267200	9189207260	15267200	11385681743	16063140	13266008384	48%
Babati	1565467	1210094769	1565467	1443980929	2197237	1996989394	78%
Bukoba	3111505	1354793498	12038250	1879612507	2579696	2402314859	9%
Dodoma	12038250	10473029627	5384053	12222417151	14342862	15784277531	56%
Iringa	5384053	4402847990	481226	5726246072	5064617	8253626402	87%
Kigoma	2693846	1411612380	15680862	1495898490	2340622	1727740848	24%
Lindi	481226	256676508	11642401	198582859	391293	229473270	86%
Mbeya	15680862	8099457867	10771035	8789113162	14874398	10109520093	29%
Morogoro	11642401	6586853102	3093413	7726217100	10678558	8192719085	18%
Moshi	10771035	6142186713	3391420	7616200285	11851809	8346772210	84%
Mtwara	3093413	2037164193	3818506	2652851020	2990362	3350692910	64%
Musoma	3391420	2256894510	2515028	2377423671	5368089	3028380267	81%
Mwanza	27140398	16882598795	2851497	21047423562	28943933	24442226082	29%
Shinyanga	3818506	3554969593	4786207	4416379733	3964787	5319707891	69%
Singida	2515028	1658438213	10288619	2137392972	2415323	2500977359	62%
Songea	2851497	2109228289	1342230	2352913720	2926061	2550495722	67%
Sumbawanga	1598912	776913969	192467	940707565	3574900	2452594849	40%
Tabora	4786207	3153920080	1237511	3906149905	4462058	6587593839	63%
Tanga	10288619	9453232952	91479	10752460576	10135778	11552081699	62%
Mpanda	1342230	321938674	27140398	399069657	1020865	515082997	59%
Bariadi	192467	97084376	3111502	113235333	185375	143533808	75%
Njombe	1237511	444136912	1598912	918031280	1174500	822846568	44%
Geita	91479	55062750	2693846	184353437	1272343	461359520	93%
Jumla	140983532	91928343020	140983528.7	1.10682E+11	148818606	1.34037E+11	

Chanzo: Wizara ya Maji na Umwagiliaji

MAHITAJI NA UPATIKANAJI WA MAJI KATIKA MIJI KWA MWAKA 2017

Jedwali Na. 78

Mamlaka	Mahitaji ya Maji kwza mwaka (Mita za Ujazo)	Wateja waliopo kwenye Mtandao wa Majisafi	Wateja wenye dira za Maji (Idadi)	Wateja wenye dira za Maji (%)	Wateja waliopo kwenye Mtandao wa Majitaka (idadi)	Upotevu wa maji (%)	Wastani wa Saa za kupata Huduma (Masaa)
Arusha	33544800	47819	47819	100	5201	46	15
Babati	2821500	6894	6894	100	0	42	18
Bariadi	2049024	899	617	69	0	28	20
Bukoba	4630439	9394	8815	94	0	59	21
Dodoma	16560000	37949	37620	99	5659	28	23
Geita	5366340	3900	3160	94	0	24	15
Iringa	5888000	20129	20129	100	1975	28	10
Kigoma	7949784	10411	10072	97	0	29	14
Lindi	2185506	2691	2202	82	0	38	6
Mbeya	17616000	52046	52046	100	2166	34	23
Morogoro	16570832	29302	26010	89	1780	37	6
Moshi	14682960	31556	31556	100	2731	23	24
Mpanda	3515000	4571	3587	78	0	23	11
Mtwara	4346910	11836	11836	100	0	30	20
Musoma	8640000	12584	10377	82	0	61	20
Mwanza	43191734	70946	70946	100	4063	36	3
Njombe	2955701	6519	5045	77	0	27	10
Shinyanga	6281509	18955	18949	100	0	18	23
Singida	3905730	10586	10586	100	0	19	16
Songea	4971510	14297	14035	98	1338	23	23
Sumbawanga	4769780	7373	5377	73	0	31	20
Tabora	10159794	15824	15824	100	385	27	16
Tanga	10899425	36837	36837	100	2769	26	23
Jumla	233502278	463318	450339	97	28067	32	17

Chanzo: Wizara ya Maji na Umwagiliaji

SURA YA 19

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

Elimu ya Awali

320. Mwaka 2017, wanafunzi 1,517,670 waliandikishwa katika elimu ya awali ikilinganishwa na wanafunzi 1,562,770 walioandikishwa mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 2.9. Kati ya hao, wasichana walikuwa 751,774, sawa na asilimia 49.5 ya wanafunzi wote na wavulana walikuwa 765,896. Wanafunzi katika shule za Serikali walikuwa 1,436,322 mwaka 2017 ikilinganishwa na wanafunzi 1,488,439 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 3.5. Kati ya hao, wasichana walikuwa 712,022 na wavulana walikuwa 724,300. Aidha, katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 81,348 ikilinganishwa na wanafunzi 74,331 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 9.4. Uwiano wa mwalimu mwenye sifa kwa wanafunzi katika shule za awali za Serikali ulikuwa 1:183 mwaka 2017 ikilinganishwa na 1:169 mwaka 2016 wakati kiwango halisi cha uwiano unaokubalika ni 1:25. Kufuatia hali hiyo, Serikali inaendelea kuongeza jitihada za kuimarisha mafunzo ya ualimu wa elimu ya awali katika vyuo vya ualimu vya Serikali ili kufikia uwiano unaokubalika.

Elimu ya Msingi

321. Mwaka 2017, idadi ya shule za msingi ilikuwa 17,357 ikilinganishwa na shule 17,174 mwaka 2016. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 16,140 ikilinganishwa na shule 16,109 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Aidha, idadi ya shule zisizo za serikali iliongezeka kutoka 1,065 mwaka 2016 hadi shule 1,217 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 14.3.

322. Mwaka 2017, idadi ya wanafunzi katika elimu ya msingi iliongezeka kwa asilimia 7.9 kufikia wanafunzi 9,317,791 kutoka wanafunzi 8,639,202 mwaka 2016. Kati ya hao, wavulana walikuwa 4,629,215 na wasichana walikuwa 4,688,576, sawa na asilimia 50.3 ya wanafunzi wote. Aidha, idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali iliongezeka kutoka wanafunzi 8,342,284 mwaka 2016 hadi wanafunzi 8,969,110 mwaka 2017, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Katika ongezeko hilo, wasichana walikuwa 337,575 na wavulana 289,251. Idadi ya wanafunzi katika shule zisizo za Serikali ilikuwa 348,681 ikilinganishwa na

wanafunzi 296,918 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 17.4. Kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kilipungua kutoka wanafunzi 2,120,667 mwaka 2016 hadi wanafunzi 2,078,377 mwaka 2017, sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Vilevile, kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi wa rika lengwa (miaka 7-13) kilipungua kutoka asilimia 85.6 mwaka 2016 hadi asilimia 84 mwaka 2017.

323. Mwaka 2017, wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walikua 909,950 ikilinganishwa na wanafunzi 789,479 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 15.3. Kati ya hao, wasichana walikuwa 480,784, sawa na asilimia 52.8 na wavulana walikuwa 429,166. Kiwango cha ufaulu kiliongezeka kutoka asilimia 70.4 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 72.8 mwaka 2017.

324. Mwaka 2017, idadi ya walimu wenye sifa katika shule za Serikali ilikuwa 176,876 ikilinganishwa na walimu 188,668 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 6.3. Mwaka 2017, uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi ulikuwa 1:47 ikilinganishwa na uwiano wa 1:42 mwaka 2016. Uwiano stahiki wa mwalimu kwa mwanafunzi kwa mujibu wa vigezo vya kimataifa ni 1:40. Upungufu huu ulitokana na kuondolewa kwa walimu wasiokuwa na sifa kwenye utumishi wa umma.

Elimu ya Sekondari

325. Mwaka 2017, kulikuwa na shule za sekondari 4,796 ikilinganishwa na shule 4,773 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 0.5. Kati ya hizo, shule za Serikali zilikuwa 3,604 na shule za watu binafsi zilikuwa 1,192. Aidha, mwaka 2017, kulikuwa na wanafunzi 1,908,857 wa kidato cha kwanza hadi cha sita katika shule za Sekondari ikilinganishwa na wanafunzi 1,806,955 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Vile vile, wanafunzi waliojiunga na elimu ya sekondari kwa kidato cha kwanza hadi cha nne katika mwaka 2017 walikuwa 1,767,890 ikilinganishwa na wanafunzi 1,675,593 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 5.5. Idadi ya walimu katika shule za Sekondari mwaka 2017 ilikuwa 110,163 ikilinganishwa na walimu 108,596 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 1.4.

326. Mwaka 2017, watahiniwa 374,950 walifanya mtihani wa kidato cha nne ambapo watahiniwa 287,713 walifaulu kwa kiwango cha ufaulu cha asilimia 76.7 ikilinganishwa na kiwango cha ufaulu cha asilimia 69.8 mwaka 2016.

Aidha, jumla ya watahiniwa 62,233 walifanya mtihani wa kidato cha sita ambapo wanafunzi 58,556, sawa na asilimia 94.1 walifaulu ikilinganishwa na watahiniwa 64,861 waliofanya mtihani mwaka 2016 ambapo wanafunzi 63,499 walifaulu, sawa na ufaulu wa asilimia 97.9.

Elimu ya Ualimu

327. Mwaka 2016/17, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu ilikuwa 20,324 ikilinganishwa na wanachuo 19,825 mwaka 2015/16. Kati ya hao, wanaume walikuwa 14,204 na wanawake 6,120. Aidha, vyuo vya ualimu vya Serikali vilikuwa na wanachuo 16,861 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na wanachuo 14,057 mwaka 2015/16, sawa na ongezeko la asilimia 19.9. Kati ya hao, wanawake walikuwa 4,380 (asilimia 26.0) na wanaume walikuwa 12,481. Vile vile, idadi ya wanachuo katika vyuo vya ualimu visivyo vya Serikali ilikuwa 3,463 mwaka 2016/17 ikilinganishwa na wanachuo 5,768 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 40.0. Upungufu huo ulitokana na kukosekana kwa wanafunzi wenye sifa stahiki sambamba na gharama ya kujiunga katika vyuo.

Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu

328. Mwaka 2016/17, Serikali ilikagua taasisi 12,389 za elimu ikiwa ni sawa na asilimia 59.8 ikilinganishwa na malengo ya kukagua taasisi 20,718 katika kipindi hicho. Lengo la ukaguzi ni kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa katika ngazi zote inakuwa na ubora na viwango vinavyostahili.

Jedwali 19.1: Ukaguzi wa Taasisi za Elimu Hadi kufikia Machi, 2017

Taasisi/Shule/ Vituo/Vyuo	Idadi iliyolengwa kukaguliwa (2016/17)	Idadi halisi iliyokaguliwa (2016/17)	Kiwango cha utekelezaji (% ya idadi iliyokaguliwa)
Shule za Awali	8,095	5,007	61.9
Shule za Msingi	1,482	709	47.8
Shule za kiujuzi baada ya Msingi” <i>Post Primary Vocational Centres</i> ”	5,264	3,611	68.6
Shule/Vituo vya Elimu Maalum	1,353	945	69.8
Vituo vya Elimu ya Watu Wazima	211	64	30.3
Shule za Sekondari	2,966	1,443	48.7
Vyuo vya Ualimu	1,347	610	45.3
Jumla	20,718	12,389	59.8

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Elimu ya Ufundi na Mafunzo

329. Mwaka 2016/17, idadi ya wanafunzi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo iliongezeka kwa asilimia 9.4 hadi wanafunzi 128,121 kutoka wanafunzi 117,067 mwaka 2015/16. Kati ya hao, wanaume walikuwa 70,665 (asilimia 55.2) na wanawake walikuwa 57,456. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilianzisha ofisi 8 za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi za kanda.

Elimu ya Ufundi Stadi

330. Mwaka 2016/17, idadi ya wanafunzi waliojiunga na vyuo vya ufundi stadi ilikuwa 130,079 ikilinganishwa na wanafunzi 196,091 mwaka 2015/16, sawa na upungufu wa asilimia 33.7. Kati yao, wanaume walikuwa 80,135 na wanawake walikuwa 49,944 (asilimia 38.4). Upungufu huu ulitokana na wanafunzi wengi kujiunga na elimu ya sekondari kufuatia utekelezaji wa Sera ya Serikali ya elimumsingi bila malipo.

Elimu ya Juu

331. Idadi ya wanafunzi katika vyuo vikuu nchini ilipungua kwa asilimia 30.0 hadi wanafunzi 132,833 mwaka 2016/17 kutoka wanafunzi 189,857 mwaka 2015/16. Kati ya hao, wanawake walikuwa 49,280, sawa na asilimia 37.1 na wanaume walikuwa 83,553. Upungufu huu ulitokana na baadhi ya vyuo kufungiwa na Tume ya Vyuo Vikuu nchini kutoa programu ambazo zilikuwa hazina wanataaluma wenye uwezo wa kufundisha programu hizo.

332. Aidha, idadi ya wanafunzi walionufaika na mikopo iliongezeka kutoka wanafunzi 116,706 mwaka 2016/17 hadi kufikia wanafunzi 122,623 mwaka 2017/18. Kati ya hao, wavulana walikua 80,953 na wasichana walikua 41,670.

SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 80

(Namba)

Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2000	43643	36734	31132	25456	6654	6143	149762
2001	47204	45078	30531	29188	7198	6601	165800
2002	56101	50371	36989	29045	7711	7126	187343
2003	52863	60643	36906	35653	7780	6885	200730
2004	98738	67294	46546	36385	8353	7572	264888
2005	134963	109398	46188	46489	9710	8444	355192
2006	196391	151448	72167	42584	18211	9691	490492
2007	401011	218060	105770	70796	21789	11668	829094
2008	395930	332393	175353	95214	25240	11743	1035873
2009	480529	308131	159789	167355	31201	12695	1159700
2010	382207	398870	293519	279995	26065	20674	1401330
2011	403873	396724	380528	279117	30265	25164	1515671
2012	457321	386250	355740	343376	31206	28859	1602752
2013	444532	506036	193901	302963	30581	26698	1504711
2014	479089	506170	356787	178246	33619	26899	1580810
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	467982	366396	263981	278690	45533	47007	1469589
2017	491535	443614	296034	236775	53749	43494	1565201
Badiliko (%)							
2016 - 2017	5.0	21.1	12.1	-15.0	18.0	-7.5	6.5

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

IDADI YA WANAFUNZI NA WALIMU KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI KWA JINSIA

Jedwali Na.80A

	2017		
	Waume	Wake	Jumla
Elimu ya msingi			
Jumla ya wanafunzi wote walioandikishwa Darasa la I-VII	4629215	4688576	9317791
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za Serikali Darasa la I-VII	4453570	4515540	8969110
Jumla ya wanafunzi wanaosoma shule za binafsi Darasa la I-VII	175645	173036	348681
Jumla ya walimu katika shule za msingi	96387	101176	197563
Jumla ya walimu katika shule za msingi za Serikali	85908	93383	179291
Jumla ya walimu katika shule za msingi za binafsi	10479	7793	18272
Elimu ya Sekondari			
Jumla ya wanafunzi wote Kidato I-VI	947407	961450	1908857
Wanafunzi wanaosoma katika shule za Serikali, kidato I-VI	781077	784124	1565201
Wanafunzi wanaosoma katika shule za binafsi, kidato I-VI	166330	177326	343656
Idadi ya walimu katika shule za Serikali	71707	38456	110163
Idadi ya walimu katika shule za binafsi	55333	34142	89475
Jumla ya Walimu katika shule za Sekondari	16374	4314	20688

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

IDADI YA TAASISI ZA ELIMU

Jedwali Na. 80 B

Aina ya Taasisi	2016			2017		
	Serikali	Binafsi	Jumla	Serikali	Binafsi	Jumla
Shule za Msingi	16109	1065	17174	16140	1217	17357
Shule za Sekondari	3614	1145	4759	3604	1192	4796
Vyuo vya Ualimu (Msingi na Sekondari)	-	-	-	-	-	-
Elimu ya Ufundi na Mafunzo	-	-	-	-	-	-
Jumla	19723	2210	21933	19744	2409	22153

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

- Takwimu hazikupatikana

MAFUNZO YA WALIMU KATIKA VYUO VYA UALIMU KWA MWAKA 2017

Jedwali 80C

Ngazi ya Elimu	2017					
	Serikali			Binafsi		
	ME	KE	Jumla	ME	KE	Jumla
Stashahada (Pre-Service))	9,604	2,708	12,312	602	800	1,402
Stashahada (In service)	1,043	631	1,674	407	391	798
Daraja A (Certificate Pre service)	1,834	1,041	2,875	714	549	1,263
Elimu maalum	-	-	-	-	-	-
Mafunzo Kazini B/C-A	-	-	-	-	-	-
Jumla	12,481	4,380	16,861	1,723	1,740	3,463

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WANAFUNZI WANAOSOMA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU KWA JINSI KWA MWAKA 2016/2017

Jedwali Na.80 D

Jina la Chuo	Idadi ya Wanafunzi			Idadi ya Walimu		
	Me	Ke	Jumla	Me	Ke	Jumla
UNIVERSITY OF DAR-ES-SALAAM (UDSM)	17600	9209	26809	1929	584	2513
SOKOINE UNIVERSITY (SUA)	5280	2218	7498	-	-	517
DAR-ES-SALAAM INSTITUTE OF TECHNOLOGY (DIT)	3603	623	4226	165	27	192
MBEYA INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	3454	655	4109	204	29	233
INTERNATIONAL MEDICAL AND TECHNOLOGICAL UNIVERSITY (IMTU)	468	277	745	65	10	75
WELL BUGANDO UNIVERSITY COLLEGE OF HEALTH SCIENCES (WBUCHS)	1564	1054	2618	110	35	145
SAINT AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA (SAUT)	4492	2989	7481	181	96	277
MWENGE UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION (MWUCE)	2990	1348	4338	64	43	107
MOSHI UNIVERSITY COLLEGE OF COOPERATION AND BUSSINESS STUDIES	1880	1626	3506	111	36	147
STEFANO MOSHI MEMORIAL UNIVERSITY COLLEGE	295	275	570	30	17	47
RUAHA UNIVERSITY COLLEGE	3016	1932	4948	109	39	148
IRINGA UNIVERSITY	2022	1676	3698	81	28	109
MKWAWA UNIVERSITY OF COLLEGE EDUCATION	2897	1041	3938	113	64	177
THE AGAKHAN UNIVERSITY	99	101	200	32	13	45
JORDANI UNIVERSITY COLLEGE	1472	1026	2498	73	39	112
MZUMBE UNIIVERSITY	5687	2609	8296	212	81	293
COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION-DAR	2940	2807	5747	127	31	158
UNIVERSITY OF DODOMA INSTITUTE OF RURAL DEVELOPMENT PLANNING	2302	2315	4617	73	22	95
MADINI INSTITUTE- DODOMA	445	84	529	43	7	50
DODOMA UNIVERSITY (UDOM)	15898	7099	22997	528	226	754
ARUSHA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY	1975	1722	3697	76	18	94
HUBERT KAIRUKI MEMORIAL UNIVERSITY (HKMU)	675	720	1395	34	22	56
ECKERNFORDE TANGA UNIVERSITY	957	568	1525	28	3	31
ARDHI UNIVERSITY (UCLAS)	2471	1669	4140	170	71	241
INSTITUTE OF SOCIAL WORK	761	1593	2354	43	17	60
ST. JOHN COLLEGE OF ENGINEERING & TECHNOLOGY	741	898	1639	11	30	41
ARUSHA UNIVERSITY	839	734	1573	10	47	57
ST. JOSEPH UNIVERSITY COLLEGE OF ENGINEERING AND TECHNOLOGY	3051	828	3879	73	26	99
ARUSHA TECHNICAL COLLEGE	1242	375	1617	69	12	81
MUHIMBILI HEALTH ALLIED SCIENCES UNIVERSITY (MUHAS)	2053	1008	3061	163	141	304
INSTITUTE OF ADULT EDUCATION	1205	1496	2701	70	30	100
DARES SALAAM UNIVERSITY COLLEGE OF EDUCATION	3818	1850	5668	74	132	206
MWL. NYERERE MEMORIAL UNIVERSITY	2048	2204	4252	75	108	183
MARIAN UNIVERSITY	562	248	810	23	5	28
MUSLIM UNIVERSITY	1467	926	2393	49	13	62
EASTERN AFRICA STATISTICS TRAINING CENTRE	241	104	345	18	9	27
ST. JOHN UNIVERSITY OF TANZANIA	1791	1317	3108	72	32	104
COLLEGE OF BUSINESS EDUCATION-DODOMA	901	871	1772	34	8	42
LOCAL GOVERNMENT TRAINING INSTITUTE (LGTI)	1927	1153	3080	59	17	76
KILIMANJARO CHRISTIAN MEDICAL UNIVERSITY COLLEGE (KCMC)	1234	858	2092	106	53	159
CENTRE FOR EDUCATION DEVELOPMENT IN HEALTH ARUSHA (CEDHA)	14	17	31	7	4	11
LIVESTOCK TRAINING (LITA TENGERU)	263	203	466	18	4	22
HORTICULTURE RESEARCH AND TRAINING INSTITUTE (TENGERU)	29	35	64	11	6	17
ST. AUGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA-ARUSHA BRANCH	652	440	1092	24	14	38
TENGERU INSTITUTE OF COMMUNITY DEVELOPMENT (TICD)	378	699	1077	22	10	32
TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA	1659	1167	2826	37	14	51
MOUNT MERU UNIVERSITY	621	429	1050	48	12	60
NELSON MANDELA AFRICAN INSTITUTION OF SCIENCE AND TECHNOLOGY	157	81	238	38	19	57
JOMO KENYATTA UNIVERSITY OF AGRICULTURE AND TECHNOLOGY	200	159	359	4	1	5
DAR ES SALAAM MARIRIME INSTITUTE (DMI) UNIVERSITY	461	51	512	33	5	38
SEBASTIAN KOLOWA UNIVERSITY	768	415	1183	56	18	74
TANZANIA INSTITUTE OF ACCOUNTANCY UNIVERSITY (TIA)	2876	3712	6588	39	4	43
THE OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA	29107	17834	46941	199	120	319
SAINT AUGUST UNIVERSITY OF TANZANIA (SAUT)-Mbeya branch	1233	748	1981	38	15	53
TEOFILO KISANJI UNIVERSITY-Mbeya	870	468	1338	35	12	47
INSTITUTE OF FINANCE MANAGEMENT UNIVERSITY	4842	3386	8228	122	33	155
MZUMBE UNIIVERSITY-DAR CAMPUS	758	792	1550	18	9	27
TUMAINI UNIVERSITY -DAR	862	1110	1972	36	17	53
TEOFILO KISANJI UNIVERSITY-DAR	210	207	417	17	6	23
JUMLA	154323	94059	248382	6309	2544	9370

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu
- Takwimu hazikupatikana

SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA KIDATO

Jedwali Na. 81	(Namba)						
Mwaka	I	II	III	IV	V	VI	Jumla
2000	30789	26601	23469	20430	5894	5011	112194
2001	36305	30820	25004	20762	5892	5116	123899
2002	41593	34209	27540	20681	6418	5534	135975
2003	46891	38506	26385	21650	6430	4859	144721
2004	48752	46167	33240	24476	8847	6229	167711
2005	45276	46321	32063	29248	9183	7046	169137
2006	46968	48013	42878	29796	9569	7956	185180
2007	47437	46927	41340	35746	11299	8667	191416
2008	42971	43232	43177	35980	12576	8594	186530
2009	44255	36384	37064	34061	11851	9096	172711
2010	56620	57876	50778	46820	12269	13006	237369
2011	63282	67205	65859	54521	11083	11926	273876
2012	65058	69403	64453	61209	9684	11713	281520
2013	70060	77407	67998	65637	8592	9651	299345
2014	109784	96732	76574	66898	8865	7686	366539
2015	-	-	-	-	-	-	-
2016	70844	81499	72970	73231	21091	17731	337366
2017	71160	79548	77168	72056	24146	19578	343656
Badiliko (%)							
2016 - 2017	0.4	-2.4	5.8	-1.6	14.5	10.4	1.9

Chanzo: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

- Takwimu Hazikupatikana

SURA YA 20

AFYA NA MAENDELEO YA JAMII

AFYA

Vituo vya Kutolea Huduma za Afya

333. Katika juhudi za Serikali kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya iliongezeka kufikia vituo 7,678 mwaka 2017 kutoka vituo 7,400 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Katika kipindi hicho, jumla ya watu 35,082,840 walihudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na watu 32,463,458 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 8.1. Hii ilitokana na kuongezeka kwa vituo vya afya na kuwa karibu na jamii, kuboreshwa kwa huduma zinazotolewa katika vituo hivyo na kuhamasishwa kwa matumizi ya bima za afya. Aidha, idadi ya wagonjwa waliolazwa ilipungua kwa asilimia 7.1 kufikia wagonjwa 1,650,224 kutoka wagonjwa 1,775,835 waliolazwa mwaka 2016. Idadi ya vitanda vya wagonjwa iliongezeka na kufikia vitanda 60,952 mwaka 2017 kutoka vitanda 59,757 mwaka 2016.

Huduma ya Chanjo

334. Mwaka 2017, Serikali ilinunua na kuratibu matumizi ya chanjo mbalimbali zikiwemo BCG, Rota, PCV, bOPV, Measles Rubella na TT. Mchanganuo wa chanjo zilizounuliwa mwaka 2017 ni kama ifuatavyo: Rota dozi 2,383,700 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara kwa watoto; PCV 13 dozi 1,000,000 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa nimonia; Measles Rubella dozi 3,326,200 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa surua na rubella; bOPV dozi 3,966,000 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio); pentavalenti dozi 1,179,000; TT dozi 2,000,000 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa pepopunda; BCG dozi 2,000 za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa kifua kikuu; na IPV dozi 999,600 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa ulemavu wa ghafla.

Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba

335. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa unaboreshwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili kuondoa kero ya kukosa huduma ya dawa kwa wananchi wanapokwenda kutibiwa katika vituo vya umma. Katika kupunguza gharama za ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba, na kuongeza upatikanaji wake, Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

iliingia mikataba ya muda mrefu (Framework Agreement) na wazalishaji 110 wa dawa na kati ya hao, 10 ni viwanda vya ndani. Hii ilisababisha kupungua kwa bei ya dawa kwa wastani wa asilimia 40 ikilinganishwa na utaratibu wa zamani wa kununua dawa kutoka kwa mawakala.

336. Hali ya upatikanaji wa aina 135 za dawa muhimu katika Bohari Kuu ya Dawa iliendelea kuimarika kwa kiwango cha wastani wa asilimia 81 katika kipindi cha hadi Desemba 2017. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya ilifikia wastani wa asilimia 89.6 katika kipindi hicho.

Afya ya Uzazi na Mtoto

337. Mwaka 2017, Serikali ilitekeleza mipango mbalimbali ya kuboresha afya ya uzazi na mtoto kwa lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Utekelezaji wa mipango hiyo ulihamasisha wajawazito wengi kuhudhuria kliniki ambapo idadi ya wajawazito wanaohudhuria kliniki mpaka hudhurio la nne iliongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 2016 hadi asilimia 46 mwaka 2017 na wajawazito waliopatiwa dawa ya IPT2 ili kujikinga na malaria iliongezeka kutoka asilimia 60.4 mwaka 2016 hadi asilimia 65.9 mwaka 2017. Aidha, Serikali ilinunua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango katika vituo vya huduma za afya nchini, kama ifuatavyo: Depo-provera chupa 2,986,853; dawa ya kidonge yenye kichocheo kimoja (Microval) mizunguko 19,357; vipandikizi 227,976; vitanzi 61,599; dawa ya dharura (emergency contraceptives) 28,953; vipandikizi vya Jadelle 209,050; Microgynon mizunguko 1,500,000; kondomu za kiume 6,902,646; na kondomu za kike 61,599.

338. Katika kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto, Serikali ilinunua na kusambaza dawa za sindano aina ya Oxytocin chupa 1,141,208 kwa ajili ya kuzuia mama mjamzito kutokwa na damu; Magnesium Sulphate chupa 76,219 kwa ajili ya kuzuia kifafa cha mimba; Fefol vidonge 55,888,500 kwa ajili ya kuongeza wingi wa damu; vidonge 4,086,946 vya Amoxicillin myeyuko; na Zinc/ORS 1,084,780. Jumla ya wajawazito 952,484 walifikia kwa kutumia ujumbe kwa njia ya simu kuwahasisha kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuwaelimisha umuhimu wa kuhudhuria kliniki katika kipindi chote cha ujauzito na baada ya kujifungua hadi mtoto anapotimiza miaka mitano. Lengo ni kufikia wajawazito 1,800,000 kwa mwaka.

339. Hadi kufikia Desemba 2017, Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo ilipeleka vifaa kwenye vituo vya afya 8 ili viweze kutoa huduma ya upasuaji wa kutoa mtoto tumboni. Aidha, Serikali ilibainisha vituo 203 kutoka Halmashauri mbalimbali nchini vitakavyofanyiwa ukarabati mkubwa ili viweze kufanya upasuaji wa kutoa mtoto tumboni (CEmoNC). Kati ya vituo hivyo, vilivyopatiwa fedha vilikuwa 173 ambavyo havikua vinatoa huduma hii na vingine vilikua vinatoa huduma ya upasuaji lakini vinahitaji maboresho.

Lishe

340. Mwaka 2017, Serikali ilizindua mradi wa “Mtoto Mwerevu” wenye lengo la kutokomeza udumavu wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Udumavu ni hali ya kutokukua kwa viungo vya mtoto ukiwemo ubongo kwa kiwango kinachotakiwa kutokana na lishe duni ya mama wakati mtoto akiwa tumboni hadi anapofikisha umri wa miaka miwili. Mtoto wa aina hii huandamwa na magonjwa ya mara kwa mara, huwa dhaifu na mbaya zaidi maendeleo yake darasani huwa siyo mazuri. Mradi wa “Mtoto Mwerevu” unatokana na ukweli kwamba mtoto asiyekuwa na udumavu anakua vizuri kimwili, kiakili na kufanya afundishike vizuri. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa TDHS wa mwaka 2015/16, tatizo hili bado ni kubwa hapa nchini ambapo asilimia 34 ya watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano (zaidi ya watoto milioni 2.7) wana udumavu. Mradi huu unajielekeza katika kuhakikisha kuwa siku 1,000 tangu mimba ya mtoto kutungwa hadi anapofikisha miaka miwili zinaeleweka na akina mama wanakula lishe bora pamoja na kunyonyesha maziwa yake pekee kwa miezi sita ya mwanzo.

Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa

341. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, moja ya jukumu la kipaumbele kwa Wizara ilikuwa ni kuendelea kuboresha na kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa zitolewazo nchini. Maboresho hayo, yanalenga katika kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi ili kupunguza gharama kubwa kwa Serikali katika kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari 2018, idadi ya wagonjwa waliopewa rufaa ya matibabu nje ya nchi ilipungua na kufikia wagonjwa 103 ikilinganishwa na wagonjwa 304 mwaka 2016/17. Mafanikio haya ni kutokana na maboresho yaliyofanyika katika Hospitali za Serikali ambazo kwa hivi sasa zimeongeza uwezo wa kutoa huduma za kibingwa ambazo awali hazikuwa zikitolewa hapa nchini na hivyo kulazimu wagonjwa kupatiwa rufaa nje ya nchi.

Udhibiti wa Malaria

342. Maambukizi mapya ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano yalipungua na kufikia chini ya wastani wa asilimia 10 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 15 mwaka 2016. Hii ni kufuatia jitihada za Serikali za kusambaza vyandarua kwa wananchi na kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kutibu malaria. Mwaka 2017, Serikali ilisambaza jumla ya vyandarua 1,175,671 kwa ajili ya wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja na vyandarua 2,396,732 kwa wanafunzi shuleni. Aidha, Serikali ilitekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusambaza viuadudu jumla ya lita 236,420 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Vile vile, Serikali kupitia MSD, ilisambaza vitendanishi vya malaria (mRDT) vipimo 21,428,725, dawa ya mseto ya malaria (ALU) dozi 11,300,880 kwa ajili ya malaria isiyo kali, na SP dozi 5,928,700 kwa ajili ya kinga-tiba kwa wajawazito dhidi ya athari ya malaria.

343. Mwaka 2017, Serikali kwa kushirikiana na Taasisi ya Afya Ifakara (IHI); Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS); Chuo Kikuu Kishiriki cha Matibabu Kilimanjaro (KCMUCo); na Chuo Kikuu cha Sayansi ya Afya na Tiba - Bugando (CUHAS-Bugando) zikiongozwa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) walifanya ufuatiliaji wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa ya mseto, ambapo matokeo yalionesha kuwa dawa hii inatibu malaria kwa zaidi ya asilimia 96.

Mapambano Dhidi ya VVU na UKIMWI

344. Mwaka 2017, Serikali iliendelea na juhudi za kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI ambapo huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (PMTCT) ziliendelea kutolewa. Katika kipindi hicho, jumla ya akina mama wajawazito 1,967,260 sawa na asilimia 98.7 ya akina mama 1,993,639 walipatiwa huduma za ushauri nasaha na upimaji wa VVU. Kati yao, akina mama 79,242 sawa na asilimia 4 waligundulika kuwa wanaishi na VVU. Akina mama 79,240 sawa na asilimia 99.9 ya akina mama wenye maambukizi ya VVU, walipatiwa dawa (ARV) ya kufubaza virusi vya UKIMWI. Aidha jumla ya watoto 72,960 sawa na asilimia 92 walipata kipimo cha awali cha utambuzi wa maambukizi ya VVU ambapo watoto 2,918 sawa na asilimia 4.0 walikutwa na maambukizi. Kiwango hicho kinaashiria kuendelea kupungua kwa maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, na hivyo kuiwezesha nchi kufikia malengo ya Kimataifa ya kutokomeza kabisa maambukizi ya VVU kwa watoto. Kwa ujumla inakadiriwa kuwa, maambukizi

ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yalipungua hadi asilimia 4.9 mwaka 2017 kutoka asilimia 12 mwaka 2011.

Mapambano Dhidi ya Ugonjwa wa Kifua Kikuu

345. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza afua mbalimbali katika kuongeza wigo wa utambuzi, ambapo huduma mpya za ugunduzi wa ugonjwa wa kifua kikuu kwa kutumia vipimo vya vinasaba (genexpert) ilianzishwa katika wilaya mbalimbali nchini. Mwaka 2017, Serikali ilinunua na kusambaza mashine za genexpert 189 ikilinganishwa na mashine 66 zilizokuwepo mwaka 2016. Vile vile, Serikali iliendelea kupanua wigo wa huduma za matibabu ya wagonjwa wa kifua kikuu sugu ambapo vituo vya kutolea huduma hiyo viliongezeka kutoka kituo kimoja mwaka 2015 na kufikia vituo 60 katika mikoa 17 nchini.

Mafunzo kwa Watumishi wa Kada ya Afya

346. Mwaka 2017, Serikali ilifanya udahili wa wanafunzi 16,214 kujiunga na vyuo vya Afya. Kati ya hao, wanafunzi 6,564 walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali na wanafunzi 9,650 kwenye vyuo binafsi katika program za uuguzi na ukunga, sayansi shirikishi za afya na wahudumu wa afya ya jamii. Aidha, jumla ya wanafunzi 23,098 walifanya mitihani ya kuhitimu mafunzo katika ngazi mbalimbali. Kati yao, wanafunzi 10,669 walikuwa wa sayansi shirikishi za afya, wanafunzi 7,300 wa uuguzi na ukunga na wahudumu afya ya jamii 5,129.

MAENDELEO YA JAMII

Mafunzo ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

347. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya maendeleo ya jamii katika ngazi za cheti, diploma na shahada kwenye vyuo vya maendeleo ya jamii. Katika kipindi hicho, jumla ya wanafunzi 2,450 walidahiliwa, ikijumuisha wanawake 1,587 na wanaume 863 ikilinganishwa na wanafunzi 2,201 waliidahiliwa mwaka 2016 ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.3. Aidha, jumla ya wanafunzi 3,847 walihitimu katika vyuo vya maendeleo ya jamii, ambapo wanaume walikuwa 1,431 na wanawake walikuwa 2,416 ikilinganishwa na wahitimu 4,502 mwaka 2016, sawa na upungufu wa asilimia 14.5. Vile vile, jumla ya wanafunzi 1,295 (wanawake 884 na wanaume 411) walidahiliwa katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii – Kijitonyama ikilinganishwa na wanafunzi 1,277 waliidahiliwa mwaka 2016. Kati yao, wanafunzi 423 walidahiliwa katika ngazi za Cheti, 409 Diploma, 28 Stashahada ya Uzamili, 398 Shahada na 37 Shahada ya Uzamili. Aidha, jumla ya wanafunzi 1,122

(wanawake 722 na wanaume 400) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 1,164 (wanawake 783 na wanaume 381) waliohitimu mwaka 2016.

348. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa haki na huduma za ustawi wa jamii kwa wazee 514 wasiojiweza (wanaume 267 na wanawake 247) wanaoishi katika makazi ya wazee ya Serikali. Aidha, Serikali iliwezesha upatikanaji wa vifaa ikiwa ni pamoja na bajaji 10, vifaa vya jikoni na vifaa vya huduma ya kwanza katika makazi 17 ya wazee ya Serikali. Vile vile, Serikali iliwezesha wazee 518,453 kupata kadi za bima ya afya ambapo wanaume walikuwa 263,660 na wanawake walikuwa 254,793. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 31.4 ya wazee 1,653,331 waliotambuliwa.

Huduma za Ustawi na Maendeleo ya Watoto

349. Mwaka 2017, Serikali ilianza utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Katika hatua za awali za utekelezaji wa Mpango huo, Serikali ilitoa mafunzo kwa watu wa kada mbalimbali wakiwemo watoto kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni. Aidha, Serikali iliendelea kukuza ushiriki wa watoto katika maendeleo yao kwa kuwezesha kuundwa kwa mabaraza 15 ya watoto kwa mikoa 15 ambayo iliyofanya uchaguzi mwaka 2017 ikilinganishwa na mabaraza 19 mwaka 2016. Lengo la mabaraza haya ni kutoa fursa kwa watoto kujadili masuala mbalimbali yanayohusu haki na ustawi wao.

350. Mwaka 2017, jumla ya watoto 61 (wavulana 27 na wasichana 34) walio katika mazingira hatarishi walipata huduma za unasihi na malezi ya kambo. Lengo likiwa ni kuwezesha watoto kuishi na kuendelezwa wakiwa ndani ya familia kulingana na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, leseni 18 za maombi ya makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi zilitolewa ili kuwezesha wadau kuchangia katika upatikanaji wa huduma za msingi kwa watoto walio katika mazingira hatarishi. Serikali pia iliendelea kutoa huduma za msingi pamoja na huduma za msaada wa kisheria kwa watoto 291 (wavulana 278 na wasichana 13) waliokuwa katika mkinzano na sheria na wanaolelewa katika mahabusu za watoto.

351. Mwaka 2017, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana. Aidha, jumla ya vituo 47 vya kulelea watoto wadogo mchana vilisajiliwa na kufikia vituo 888

nchini ikilinganishwa na vituo 841 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Vile vile, Serikali iliendelea kuratibu utoaji wa elimu ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika vyuo 23 ambapo jumla ya wanafunzi 850 walidahiliwa katika vyuo hivyo.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

352. Mwaka 2017, mashirika 158 yalisajiliwa chini ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 24 ya mwaka 2002, kama ilivyorekebisha mwaka 2005, ikilinganishwa na mashirika 570 yaliyosajiliwa mwaka 2016. Aidha, mwaka 2017 Serikali ilifanya uhakiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 3,363 kwa lengo la kuboresha kanzidata ya mashirika hayo, kutambua mashirika yaliyosajiliwa chini ya Sheria nyingine nchini na kuwezesha utambuzi wa mashirika yaliyo hai kiutendaji. Vile vile, Serikali ilipokea na kuchambua taarifa za kazi na fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 80 ikilinganishwa na mashirika 699 mwaka 2016. Lengo ni kutambua mchango wa mashirika hayo katika ajenda ya maendeleo ya jamii.

IDADI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 84

Aina ya Vituo	2014			2015			2016			2017		
	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla	Binafsi	Serikali	Jumla
Zahanati	1390	4523	5913	1419	4724	6143	1421	4789	6210	1435	4925	6360
Vituo vya Afya	208	505	713	211	507	718	259	508	767	277	527	804
Hospitali	130	124	254	128	124	252	146	119	265	150	123	273
Nyinginezo*	79	10	89	133	3	136	39	15	54	182	8	190
Maternity Homes									50	50	1	51
Jumla	1807	5162	6969	1891	5358	7249	1865	5431	7346	2094	5584	7678

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

* Ni pamoja na kliniki

HUDUMA ZA AFYA : WANAFUNZI WALIOFAULU MAFUNZO YA AFYA

Jedwali Na.85

Aina ya Mafunzo	2011/12	2012/13	2013/14	2014/15	2015/16	2016/17
Doctor of Medicine (MO)	278	174	-	204	869	1072
Advanced Diploma in AMO Anaesthesia	4	2	-	3	3	8
Advanced Diploma in Clinical Dentistry	-	1	-	7	7	1
Advanced Diploma in Clinical Medicine	207	189	59	130	36	56
Advanced Diploma in Ophthalmology	6	6	-	10	4	2
Advanced Diploma in Vector Control	14	20	7	12	3	-
Diploma in Clinical Medicine	444	185	-	700	440	394
Diploma in Dental Laboratory Technology	4	4	4	4	4	3
Diploma in Dental Therapy	50	51	-	47	26	53
Diploma in Diagnostic Radiography	41	45	-	55	55	91
Diploma in Environmental Health Science	159	204	116	136	75	35
Diploma in Health Laboratory Sciences	148	188	44	120	194	223
Diploma in Health Personnel Education	37	38	23	29	21	29
Diploma in Medical Laboratory Sciences	133	174	44	194	40	64
Diploma in Nursing and Midwifery	878	1052	508	1804	1060	623
Diploma in Occupational Therapy	6	14	-	12	-	-
Diploma in Optometry	13	16	-	11	10	15
Diploma in Pharmaceutical Sciences	130	118	40	184	137	88
Diploma in Physiotherapy	19	22	26	20	7	13
Certificate in Clinical Medicine	-	-	-	830	110	138
Certificate in Medical Laboratory Sciences	-	-	-	506	271	217
Certificate in Health Record Technology	-	-	-	48	16	50
Certificate in Pharmaceutical Sciences	-	-	-	150	150	132
Certificate in Nursing	-	-	-	2740	3288	1645
	2571	2503	871	7956	6826	4952

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

- Takwimu hazikupatikana

IDADI YA WAGONJWA KATIKA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Jedwali Na. 86

Mwaka	Wagonjwa wa Nje			Jumla ya Wagonjwa waliolazwa
	Hospitali	Zahanati	Vituo vya Afya	
1995	355483	6785925	545921	240707
1996	604023	9530361	927606	541781
1997	711222	10003245	1052326	559949
1998	750465	10112305	1134242	-
1999	812891	10321654	1242354	626700
2000	989101	13697988	1874346	626700
2001	1167139	17218371	2511624	680263
2002	1328395	19695356	3258520	701568
2003	1491909	22935688	3659615	1390273
2004	1532028	23552460	3758027	2125388
2005	1619700	24900276	3973085	2237146
2006	1754925	26979136	4304787	2837252
2007	1842671	28328093	4520026	2979115
2008	1934805	29744498	4746027	3128071
2009	2128286	32718948	5220630	3440870
2010	2341114	35990843	5742693	3784957
2011	2622048	39917117	6431816	4239152
2012	2815529	41333522	6657817	4388108
2013	2903275	42682479	6873056	4529971
2014	5910725	14008692	475295	1665935
2015	4480781	25072487	6006466	1858956
2016	4984645	20859281	6515219	1775835
2017	5266252	21115639	7050725	1650224

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

IDADI YA VITANDA KATIKA HOSPITALI ZOTE NCHINI

Jedwali Na. 87

Aina ya Huduma	2016				Jumla	2017				Jumla
	Serikali	Shirika la Umma	Shirika la Kujitolea/Dini	Binafsi		Serikali	Shirika la Umma	Shirika la Kujitolea/Dini	Binafsi	
Hospital za Mkoa	5158	260	0	0	5418	6931	260	0	0	7191
Hospitali za Wilaya	8693	0	6618	0	15311	6683	0	6618	0	13301
Hospitali nyingine	935	154	2705	462	4256	224	97	2705	529	3555
Vituo vya Afya	8933	672	3993	1506	15104	9429	258	3820	2185	15692
Zahanati	12166	790	4127	2585	19668	13299	250	4110	3554	21213
Jumla	35885	1876	17443	4553	59757	36566	865	17253	6268	60952

Chanzo: Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto